Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Saba – Tarehe 21 APRILI, 2010**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

Spika (*Mhe. Samuel J. Sitta*) Alisoma Dua

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Taarifa ya Mwaka ya Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Nishati na Maji kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2009 *[The Annual Report and Accounts of the Energy and Water Utilities Regulatory Authority for Year ended 30th June, 2009]*.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MANTUMU B. MAHIZA):**

Taarifa ya Mwaka ya shughuli za Chuo Kikuu Huria Tanzania kwa Mwaka 2007/2008 *[The Annual Report on the Activities of the Open University of Tanzania for the year 2007/2008]*.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSUF MZEE):**

Taarifa ya Mwaka ya Upimaji wa Utekelezaji wa Mamlaka ya Ununuzi wa Umma kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 *[The Annual Perfomance Evaluation Report of the Public Procurement Regulatory Authority for the Year 2008/2009]*.

**KAIMU MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (MHE. MOHAMED R.ABDALLAH):**

Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali kwa Mwaka 2009/2010.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa Mwaka 2009/2010.

**KAIMU MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA (MHE. DR. RAPHAEL M.CHEGENI):**

Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma kwa mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2008.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 80

**Ruzuku katika Mpango wa Taifa wa Usafirishaji Vijijini(*LGTP*)**

**MHE. MBARUK K. MWANDORO** aliuliza:-

Kwa kuwa, kwa muda mrefu sasa Serikali haijatoa fedha za ruzuku kwa Halmashauri nyingi, ikiwemo Mkinga kwa ajili ya Mpango wa Taifa wa Usafirishaji Vijijini(*LGTP*) na hivyo wananchi kukata tamaa na kupoteza imani na Halmashari zao kushindwa kuondoa kero hiyo:-

(a) Je, ni sababu zipi zinaifanya Serikali kushindwa kufikisha ruzuku hiyo kwa Halmashauri licha ya kasma husika kuidhinishwa na kuwekwa katika Bajeti kila mwaka?

(b) Je, ni lini Serikali itafikisha ruzuku hizo kwa Halmashauri husika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbarouk Kassim Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika Bajeti yake Serikali hutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Barabara chini ya programu ya usafiri katika Serikali za Mitaa. Programu hii ilianza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2007/2008 na inahisaniwa na Serikali za Norway na Denmark.

Katika mwaka wa fedha 2008/2009 Serikali ya Norway ilibadilisha utaratibu wa kutoa fedha zake, badala ya kupeleka fedha moja kwa moja kwenye miradi sasa fedha hizo zinapatia kwenye Mfuko wa kusaidia Serikali yaani(*General Budget Support).* Kutokana na hatua hii, hata fedha za programu hii nazo zinatumia utaratibu huu. Mabadiliko haya yamesababisha fedha za mpango wa Taifa wa usafirishaji Vijijini kutokuelekezwa katika programu kama ilivyotarajiwa na hivyo kuathiri utekelezaji wa programu.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kupitisha fedha za wahisani katika Mfuko wa kusaidia Serikali yaani (*General Budget Support)* ni utaratibu ambao Serikali imekubaliana na Wahisani na wadau wa Maendeleo. Utaratibu huu husaidia Serikali kuelekeza rasilimali kwa kuzingatia vipaumbele vya Taifa ikiwemo sekta husika ya barabara.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na kuhakiki, kulipa, pamoja na kuhakikisha kwamba Wakandarasi wote waliofanyakazi wanalipwa fedha zao. Aidha, kwa sekta ya barabara Halmashauri zihakikishe kwamba zinaandaa mipango yao ya maendeleo kwa mwaka 2010/2011 kwa kutoa vipaumbele kwa miradi ya barabara ambayo haijakamilika badala ya kuanza miradi mipya kama ilivyoelekezwa katika mwongozo wa maandalizi ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:**Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri; kwa kuwa, fedha hizi ambazo zilikuwa zimetengwa katika kasma hizi ziliidhinishwa na Bunge na Halmashauri mbalimbali zilikuwa zikitazamia kupata fedha hizi kwa ajili ya utekelezaji:-

(a) Je, mabadiliko haya yaliyofanyika, Serikali ilichukua hatua za kulifahamisha Bunge ipasavyo, na kuzifahamisha Halmashauri ipasavyo ili Halmashauri hizo zisiendelee kuwa na matumaini ya kuzipata fedha hizo?

(b) Je, yale maeneo ambayo fedha zilikuwa zimetengwa na fedha hizo hazikupelekwa, Serikali itatoa fedha zingine au utaratibu utakuwaje?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, labda nieleze kidogo hapa na Mheshimiwa Mwandoro aweze kunielewa kwamba ninazungumza nini, Fedha hizi kama nilivyosema zimebadilisha mkondo wake, kwa maana ya kwenda kwenye *General Budget support*, pesa hizi zilifika mahali ambapo zilipoteza utambulisho wake maana yake ni kwamba zimepoteza ile *identity* yake.

Mheshimiwa Spika, kilichofanyika hapa ni kwamba hela za mfuko wa barabara ziliazimwa kwa ajili ya kupeleka katika Halmashauri zile ambazo zilikuwa zimeshaji-*commit* tayari, tulipokwenda ku-*check* katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga kuangalia kama na wao walishaji-*commit*, tutakuta kwamba hapakuwa na *commitment* yeyote ambayo ilikuwa imefanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga.

Mheshimiwa Spika, ninatambua kwamba Halmashauri hii ni mpya. Kwa hiyo, inahitaji msaada, ninamwomba Mheshimiwa Mwandoro kama kuna *commitment* yeyote ambayo ilikuwa imeshafanyika cha kwanza ambacho tumeelekeza hapa ni kwamba wahakikishe kwamba wanapoingia katika Bajeti ya mwaka 2010/2011, wasianzishe jambo jingine jipya bali waelekeze kila kitu katika miradi ambayo walikuwa wameshaji-*commit.*

Na. 81

**Kuchelewa kwa Malipo ya Walimu Wapya**

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH (K.n.y. MHE. BENITO W. MALANGALILA)** aliuliza**:-**

Kwa kuwa, mishahara ya walimu wapya ikicheleweshwa sana huwasababishia kero walimu hao wapya wanapoajiriwa:-

(a) Je, ni kwa nini mishahara ya Walimu hao imekuwa inacheleweshwa sana wakati mwingine hata kufikia miezi sita au zaidi?

(b) Kwa kuwa, tatizo hili limekuwa ni la muda mrefu hasa kwa kuzingatia maisha duni ya huko Vijijini. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa walimu hao wa vijijini wanahamasishwa kuishi huko kwa kuwaongezea vivutio vya kimapato.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benito William Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kabla ya mwaka wa fedha 2008/2009 Watumishi wapya walitakiwa kuanza kufika vituo vya kazi na Mwajiri kujaza fomu ya kuthibitisha uhalali wa ajira ikiwa ni pamoja na walimu. Utaratibu huu ulisababisha kuwepo kwa usumbufu kwa watumishi ikiwa ni pamoja na walimu kutopata mishahara kwa muda mrefu baada ya kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali yetu ni sikivu, baada ya kuangalia tatizo hili OWM-TAMISEMI, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Wizara ya Fedha na Uchumi kwa pamoja, tumekubaliana kwamba sasa mishahara kwa ajili ya waajiriwa wapya wakiwemo walimu itafika katika vituo vya kazi mwezi huo huo baada ya kuajiriwa. Utaratibu huu umeanza kutumika tarehe 1 Septemba 2009 ambapo Walimu walipata mishahara yao katika mwezi huo huo baada ya kuajiriwa. Aidha, Ofisi yangu imetoa maelekezo kuwa Halmashauri

zote nchini ziwalipe walimu posho ya kujikimu ya siku saba mara tu Mwalimu anapofika kuanza kazi. Zoezi hili limefanyika kwa mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba kwa mwaka 2009/2010 hakuna mwalimu ambaye anadai mshahara wake wa mwezi au posho ya kujikimu. Na kama kuna Mtumishi anayedai mshahara wa kwanza kuanzia mwaka 2009/2010, Mtumishi au mwalimu huyo hakwenda kwenye kituo alichopangiwa, hivyo mshahara wake kwenda kwingine na yeye kujipangia kituo tofauti. Watumizi ambao hawafiki katika vituo vyao vya kazi mishahara yao hurudishwa Hazina.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika sehemu (a) hakuna mwalimu aliyeajiriwa katika mwaka 2009/2010 ambaye anadai mshahara wake baada ya kuanzishwa kwa utaratibu huo. Hata hivyo, kuhusu vivutio katika maeneo ya kazi hii ni changamoto kwa Serikali.

Aidha, kwa sababu shule hizi ni sehemu ya Jamii, itakuwa vema kama jamii itaona umuhimu wa kupata walimu hawa na hivyo kubuni mbinu mbalimbali ili kuwa na mvuto kwa walimu kupenda kufanya kazi katika jamii husika.

Mheshimiwa Spika, ziko baadhi ya Halmashauri ambazo jamii imeanza kuchukua jukumu kama hili na mfano mzuri ni Mkoa wa Rukwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga ambapo wameweza kuwapokea watumishi na kujaribu kanuni na utaratibu ambao unasaidia kuwapa watumishi motisha na kuishi katika mazingira hayo.

Taarifa tulizonazo, maeneo hayo yamefanikiwa kuwafanya watumishi wabaki na kufanya kazi katika maeneo hayo. Tunaomba Waheshimiwa Wabunge ambao ni sehemu ya Baraza la Madiwani watusaidie kutafuta vivutio na kuhakikisha watumishi wanaopangwa huko kwenye Wilaya wanaridhika na mazingira ya kazi.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Naomba niipongeze Serikali kwa hatua ambazo inazichukua sasa hivi kuhakikisha kwamba misharaha ya Walimu inafika kwa wakati, lakini utaratibu mishahara ya Walimu au wafanyakazi wa Halmashauri, cheki zao kupitia kwa Katibu Tawala wa Mkoa ambaye yeye hahusiki moja kwa moja na mishahara hiyo isipokluwa ni Mkurugenzi wa Halmashauri na hatimaye *Audit Query* inakwenda kwa Katibu Tawala wa Mkoa.

Je, Serikali haioni kwamba inambebesha mzigo Katibu Tawala wa Mkoa kwa fedha ambazo yeye mwenyewe wala hazigusi, wala hana mamlaka nazo?

Serikali ina utaratibu gani wa kulitizama hilo na kumpa majukumu hayo Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, huu utaratibu anaouzungumza Mheshimiwa Rished ni utaratibu ambao ulitumika kwa sababu ya malimbikizo ya mishahara ya Walimu.

Kwa hiyo, ilikuwa ni utaratibu maalum na mtu wa kwetu wa karibu kabisa ambaye ni wa Serikali Kuu ambaye unaweza ukamtegemea pale ni *RAS*, lakini kama nilivyoeleza hapa ni kwamba hii habari inayozungumzwa hapa ni habari ya hapo zamani za kale, kwa sababu hela sasa hivi zinakwenda moja kwa moja mpaka kwenye Halmshauri zinazohusika.

Kwa hiyo Mwalimu anapoondoka hapa anapofika kwenye Halmashauri anaanza kujaza zile fomu zake *retrospectively* mpaka anapokuwa amekamilisha ule utaratibu mzima. Kwa hiyo suala la kwamba Mwalimu sasa atakwenda kwenye kituo chake cha kazi au Mtumishi atakwenda kwenye kituo cha kazi asipate mshahara wake halipo tena sasa, kwa sababu sisi wadau wote tumeshakubaliana na hapa nazungumzia 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, kule nyuma kunaweza kukawa kuna matatizo na kama kuna matatizo tunaomba tuletewe hayo matatizo, lakini nataka nirudie tena habari ya kwamba Watumishi watakuwa wanakosa mishahara yao inatokana na kama alipangwa kwenda Magu akaenda Newala mshahara wake utakwenda Magu. Akienda kule Newala yeye hatakuambia kwamba unajua mimi nilipangwa kule Magu, atakuambia kwamba mimi niko Newala hapa nataka mshahara wangu, tatizo hilo limetokana na hali hiyo. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, kwa zaidi ya asilimia themanini na tano tumeshafanikiwa kupunguza au kumaliza kero za Walimu:-

Je, Serikali sasa itakuwa tayari kurudi kwa watumishi wengine kama vile Watendaji wa Vijiji, Kata na Wakuu wa Idara ili nao wapate malipo yao kama Walimu ambao walilipwa madai yao yote?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kazi inayofanyika sasa hivi ni ya kushughulikia Watumishi wengine ambao siyo Walimu, ninapenda kukiambia kikao chako cha Bunge kwamba kwa upande wa TAMISEMI mimi nilitumwa na Ofisi ya Waziri Mkuu nilikwenda Morogoro tumekaa na wadau wote wanaohusika na maeneo mengine kwa upande wa TAMISEMI na kuangalia jinsi ambavyo tutahakiki madeni haya kama ilivyofanyika kwa upande wa Walimu.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jitihada hizi kwa maana ya watendaji wa Kata na wale watendaji wengine wa vijiji na wale wengine wote wanaohusika zinaendelea na kazi inayofanyika kubwa hapa ni kuhakiki madeni ili baadaye tuweze kuwalipa bila kuwa tumepotoshwa kwamba kiasi ni hiki kumbe sicho.

Na. 82

**Fedha za Mfuko wa Kuwasaidia Wajasiriamali Mkoa wa Kusini Pemba**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKARI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imetekeleza vizuri Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2005-2010, na kwa kudhihirisha hilo Serikali pamoja na mambo mengine imeandaa Mfuko wa Kuwapatia Mikopo wananchi wake unaotambulika kwa jina la mfuko wa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Aman Karume:-

(a) Kwa kutekeleza azma hiyo ya utoaji mikopo kwa wananchi. Je, ni vikundi vingapi vya wajasiriamali Wanawake wa Mkoa wa Kusini Pemba wamepatiwa mikopo hiyo?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetolewa?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakari, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Faida Mohamed Bakari, Mbunge wa Viti Maalum, kwa kuipongeza Serikali ya CCM kwa kutekeleza vizuri Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005-2010 ya kuendelea kuondoa umasikini kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuondoa umasikini Serikali kwa idhini ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ilitoa kiasi cha shilingi bilioni 21 kwa mikoa 21 ya Tanzania Bara.

Aidha Rais Kikwete aliagiza shilingi 600,000,000/= ziende kwenye Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mheshimiwa Aman Abeid Karume, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar naye alitoa kiasi cha shilingi 600,000,000/=, hivyo kufanya jumla ya fedha zilizotolewa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufikia Shilingi 1,200,000,000/=. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mpango huo kwa upande wa Tanzania Visiwani ulianza rasmi mwezi Machi,2009. Hadi kufikia Septemba, 2009 jumla ya shilingi 861.97 milioni zilikuwa zimetolewa kwa wajasiriamali 414.

Katika kutekeleza azma ya utoaji mikopo kwa wananchi, Mkoa wa Kusini Pemba unaojumuisha Wilaya ya Chakechake na Mkoani, ulipewa jumla ya shilingi 191 milioni. Kati ya wakopaji 68 waliopata mikopo ya uwezeshaji wananchi yenye thamani ya shilingi 191 milioni katika Mkoa wa Kusini Pemba, wapo wajasiriamali wanawake 22 waliopata mikopo ya mtu mmoja mmoja yenye thamani ya shilingi 44 milioni na kikundi kimoja tu cha wanawake kilichopata shilingi milioni 3.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameongea hapa kwamba wakopaji 68 wa Mkoa wa Kusini Pemba wakiwemo wanawake 22 wamepatiwa mikopo ya mtu mmoja mmoja. Lakini naamini hii ni *SACCOS* kikundi kimoja tu cha wanawake ambacho kimepewa mkopo huu.

(a) Je, Serikali haioni kwamba kuwapatia mtu mmoja mmoja mikopo inakuwa ngumu kufuatilia kuliko kutoa kwa *SACCOS* ama vikundi vya Ushirika?

(b) Kwa kuwa elimu ya kuendesha biashara ni muhimu sana katika ukopaji na urejeshaji mikopo kwa sababu kama haijatolewa elimu fedha zitatolewa lakini mikopo hii haiwezi kurejeshwa na Serikali itapata hasara.

Je, Serikali imechukua hatua gani ya kuweka mfumo wa kuelimisha wananchi wake kabla ya kuwapa mikopo? Ahsante sana. (*Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, napenda nikubaliane na Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, kwamba kwa kweli ukopeshaji wa mtu mmoja mmoja una matatizo. Niseme wazi hapa kwamba hata mabenki yaliyoshiriki ya *NMB* na *CRDB* pale ambapo mikopo haijarudishwa mpaka leo mingi ya mikopo hiyo ni ile iliyokopeshwa kwa mtu mmoja mmoja. Lakini mikopo inayokopeshwa kwa vikundi na hasa *SACCOS* ufuatiliaji wake kwanza ni wa uhakika na ni mzuri.

Lakini kwa sababu mikopo hii ilikuwa imedhamiriwa kwenda kwa wajasiriamali mmoja mmoja na wale walioko kwenye vikundi kwa sababu siyo kila mmoja atakuwa mwanachama wa *SACCOS* au kikundi ndiyo maana Serikali iliamua kwamba na yule mmoja mmoja ambaye Benki itathibitisha kwamba anayo biashara na anaweza akarudisha basi na wenyewe wakopeshwe kwa sababu na wenyewe wanataka kuondoa umaskini wao.

Lakini kwa kweli tatizo lipo na ningeshauri huku tunakokwenda mbele ya safari ni vema wengi wa wajasiriamali wakaungana kwenye vikundi au *SACCOS* ili ufuatiliaji uwe mzuri.

Kuhusu suala la elimu ya wajasiriamali nikubaliane naye tena kwamba ni jambo la msingi lakini nina hakika kwa vile vikundi na hasa *SACCOS* ambao wanakopa kama vikundi kwa kawaida wanakuwa na mafunzo. Lakini hata wajasiriamali mmoja mmoja ni vema wakafanya mafunzo ili kupata elimu ya ujasiriamali kabla ya kukopa. Ni jukumu ambalo ni la kwao.

Lakini Serikali inaweza kusaidia lakini vigumu sana ukajua mmoja mmoja tukawafanyia mafunzo. Lakini Wizara ya Kazi, Ajira, Maendeleo ya Vijana imekuwa ikiendelea na kutoa mafunzo maeneo mbalimbali kwa wajasiriamali ambao baadaye wanakwenda mmoja mmoja akakopa. Lakini nakubaliana naye kwamba elimu ya ujasiriamali ni muhimu na sisi tutaendelea kutoa na *SACCOS* na vikundi viendelee kutoa elimu hiyo. (*Makofi*)

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Spika, swali langu linataka kufanana na alilouliza Mbunge aliyekaa. Kwa kuwa katika Mkoa wangu wa Kaskazini Pemba ni vikundi vingapi vya wajasiriamali waliopata kusaidiwa hasa hususani ikiwemo Wilaya yangu ya Micheweni?

**SPIKA:** Nadhani hili ni la takwimu itabidi lifanyiwe utaratibu mwingine. Basi tunaendelea na Wizara ianyofuata.

Waheshimiwa Wabunge, swali namba 83 limeondolewa kwa ridhaa ya mwenye swali, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis. Kwa hiyo, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Na. 84

**Elimu ya Usalama Barabarani kwa Vijana Wafanyakazi**

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA** aliuliza:-

Kwa kuwa, vijana wengi mijini wameamua kujiajiri katika kazi ya kubeba mizigo kwa kutumia marikwama/mikokoteni na maguta na kwa kuwa vyombo hivyo vimekuwa vingi mijini na vinatumia barabara sambamba na magari jambo ambalo wakati mwignine linaweza kusababisha ajali.

(a)Je, Serikali inaweza kulieleza Bunge hili iwapo hawa vijana wanapata elimu mahususi inayohusu usalama barabarani kabla ya kujiajiri katika kazi hiyo?

(b)Kama bado, Serikali litakubaliana nami kwamba ni muhimu kwa vijana hawa kupatiwa elimu hiyo ili kupunguza uwezekano wa kuongeza ajali za barabarani?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shehe Almutalam Mwadini Abbas Jecha, Mbunge wa Wete, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, elimu ya usalama barabarani imekuwa ikitolewa na inaendelea kutolewa kwa makundi mbalimbali ya watumiaji wa barabara wakiwemo vijana waliojiajiri katika kazi ya kubeba mizigo kama malikwama yaani Mikokotoni, waendesha mikokoteni na waendesha maguta kupitia Redio *TBC* na *Uhuru FM* katika Jiji la Dar  es Salaam na Mikoani kupitia vituo vya *FM Radio* zilizopo huko.

Aidha, Jeshi la Polisi limekuwa likandaa vipeperushi mbalimbali vya elimu ya usalama barabarani na kuvigawa kwa watumiaji wote wa barabara wakati wa maonyesho ya sababa, nanenane na wakati wa maadhimisho ya wiki ya nenda kwa usalama barabarani.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu   ilizindua kitabu cha kanuni za barabara mwezi Oktoba, 2008 Mkoani Morogoro, ambapo kitabu hicho kimeelezea wajibu wa kila mtumiaji wa barabara afanye nini na nini asifanye.

Wito wetu kwa Wasukuma mikokoteni (Malikwama) waendesha maguta na watumiaji wengine wote wa barabara wafahamu kuwepo kwa kitabu hiki katika maduka ya vitabu vya Serikali au maduka makubwa yaliyoidhinishwa wakipate ili waweze kujifunza wajibu wao wanapokuwa barabarani.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutoa elimu ya usalama barabarani ili kupunguza uwezekano wa kuongezeka kwa ajali za barabarani kwa watumiaji wote wakiwemo kundi alilolielezea Mheshimiwa Mbunge.

**MHE.  MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri Alhaji Shehe Imam Khamis   Kagasheki.

Kwa kuwa wasukuma Mikokoteni  mara nyingi wanafanya shughuli zao katika sehemu za misongamano na za biashara na kwa kuwa mikokoteni hii mara nyingi haina viwango maalum vya urefu wala upana.

(a)Je, Serikali sasa iko tayari kuweka viwango maalum vya urefu na upana kwenye mikokoteni hii ili kupunguza adha katika sehemu za biashara?

(b) Kwa kuwa kumewahi kutokea *incidence* mbili/tatu hivi au zaidi za wasukuma mikokoteni kukimbia na mizigo ya wateja wao wasiowaaminifu.   Na kwa kuwa alama

pekee wanayoitumia wateja wa mikokoteni hii ni alama ya nguo ambayo anaivaa msukuma mikokoteni na kwa bahati mbaya mara nyingi hawavai shati. Je, Serikali sasa iko tayari kuvisajili vyombo hivi na kuviwekea namba maalum ili iwe ni kielelezo cha mkokoteni upi ni mteja yupi amekodi? Ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, hakika kwa mujibu wa maswali yake hayo mawili naona umuhimu wake. Lakini nafikiri Mheshimiwa Mbunge atakubaliana na mimi kwamba Serikali Kuu kwa kweli haitakuwa barabara kusema kwamba itaweza kuingilia utaratibu wa kutengeneza maeneo maalum ya wapi hawa watu wataweka biashara zao na kadhalika.

Pia hata hizo taratibu anazosema kwamba watu wengine ambao wanachukua hii mizigo wanapotea maana yake hawana alama maalum na kadhalika. Mimi nashauri kwamba hizi ni kazi ambazo zinaweza kufanywa na Halmashauri na ziko ndani ya uwezo wa Halmashauri katika kutengeneza maeneo ya wapi hawa watu watafanyiakazi na taratibu gani ambazo watazitumia. Niseme tu kwamba wazo ni zuri na tumelipokea na nadhani Wizara husika wenzangu tutazungumza nao kuona kwamba wanahimiza vipi Halmashauri iweze kuzingatia hoja ya Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ongezeko kubwa sana la ajali na watu wengi ambao wamelazwa katika hospitali mbalimbali, waliojaza wodi wanatokana na waendesha pikipiki ambazo zimekuwa nyingi sana. Na kwa kuwa waendesha pikipiki hizi wengi wao hawatumii kofia maalum ambazo zingeweza kuokoa maisha yao. Naomba Serikali itoe tamko jinsi gani itadhibiti tatizo hili ambalo linaelekea kuwa janga kubwa sana la kitaifa nchi nzima?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa mujibu wa takwimu ambazo tunazipata kumekuwa na ongezeko kubwa la ajali za waendesha pikipiki katika Wilaya na Mikoa mbalimbali ya nchi yetu. Lakini tumekuwa tunahimiza na tunaendelea kuhimiza kwamba kabla hizi pikipiki hazijaanza shughuli za biashara ambazo wamepata kibali cha kufanya hivyo ambacho kilitoka katika Bunge lako Tukufu baada ya kurejea ile sheria mwaka jana tumehimiza kwamba yapo masharti ya muhimu ambayo lazima yazingatiwe katika kufanya shughuli hii ambayo wanaifanya ya kibiashara kuweza kuwapatia kipato. Miongoni mwa hayo imekuwa siyo kwamba tu yule mwendesha pikipiki ndiyo anavaa kofia ya kumkinga na ajali lakini imeainisha kusema kwamba na yule abiria ambaye anabebwa katika pikipiki lazima pia avae ile kofia kwa sababu ajali inapotokea wote wawili yule abilia na anayeendesha pikipiki wote wanaweza kuumia. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kusema kwamba tunawekea mkazo na tunarejea tena kwamba hiyo sheria ipo, utekelezaji wake unafuatiliwa kwa makini na askari *traffic* ambao wako barabarani katika kusimamia sheria hii tunasema kwamba waisimamie kwa nguvu zote ili kuhakikisha kwamba waendesha pikipiki na abiria ambao wanaendeshwa katika pikipiki hizo wanakuwa wamevaa hizo kofia za kuzuia ajali.

Na. 85

## Kujenga Kituo cha Polisi Kata ya Kipatimu

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara inayounganisha Kata ya Kipatimu na Nambunju ni mbaya sana na ina matukio mengi ya ujambazi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi wa kujenga kituo kidogo cha polisi kwenye Kata ya Kipatimu ili kunusuru maisha ya wananchi na mali zao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Samson F. Mpanda, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua umuhimu wa kusogeza huduma za Ulinzi na Usalama katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, ikiwemo Kata ya Kipatimu kwa kujenga vituo na Ofisi za Polisi ili kuwawezesha wananchi kufanya shughuli zao za kiuchumi na kijamii pasipokuwa na hofu ya uhalifu.

Hata hivyo Serikali inashindwa kufanya hivyo kwa sababu ambayo tunaizungumzia mara kwa mara kwamba Bajeti yetu kidogo inakuwa haitoshelezi kufuatana na mahitaji ambayo yanakuwepo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo Jeshi la Polisi litaendelea kutumia mpango wa Polisi Kata na Ulinzi Shirikishi kwa Wananchi wa Kipatimu. Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau kama vile TAMISEMI na wananchi itaendelea kujenga vituo vya polisi katika maeneo yenye uhitaji mkubwa wa huduma hizo ili kuimarisha ulinzi na usalama. Aidha, Wananchi wa Kipatimu wataendelea kupata huduma ya kipolisi kutoka Kilwa Masoko palipo na Kituo cha Polisi. *(Makofi)*

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kipatimu iko km kama 80 kutoka Kituo cha Kilwa Masoko na hii ndiyo inayosababisha wahalifu waweze kupata mpenyo wa kuweza kutoroka maana kutoka Kilwa Masoko mpaka Kilwa Kivinje gari lenyewe *Land Rover* halafu wakifika kule wanapotea.

(a)Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kunisaidia kuwashinikiza watu wa TAMISEMI waweze kutujengea kituo hicho haraka iwezekanavyo?

(b)Kwa kuwa tangu tunapata Uhuru viongozi wakuu kama Spika, au Rais hawajawahi kufika Kipatimu. Je, hii ndiyo sababu kuu inayofanya viongozi hawa wasifike Kipatimu? *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, hukutafuta wengine unasema juu ya Maspika tu? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli alivyosema umbali kati ya hivi vituo viwili ni kilomita 80, hilo kweli tunalizingatia.

Lakini pia ningependa tu nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa mujibu wa takwimu sisi tulizokuwa nazo ni kwamba hali kwa kweli si mbaya kiasi hicho maana yake tunatazama matukio yale ambayo yametokea. Lakini hiyo siyo sababu ya kusema kwamba kituo cha Polisi kisiwepo.

Lakini niseme kwamba hilo tumelichukua na tutazungumza na wenzetu wa TAMISEMI na ningependa nichukue fursa hii niseme kwamba kwa kweli tusiwe na utegemezi mkubwa sana katika Serikali Kuu. Lakini yako mambo mengine ambayo yanaweza yakafanywa na Halmashauri zetu na inategemea Halmashauri zinajipanga namna gani na humo tukawa na suala zima la Polisi Jamii na Ulinzi Shirikishi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la pili, sidhani kwamba viongozi wakuu hawajawahi kufika Kipatimu kwa sababu hakuna kituo cha polisi pale. Nasema kwamba tutajitahidi kuona kwamba hata na sisi wengine maana yake nchi yetu ni kubwa na kwa kweli tunakwenda kila mahali tunakokwenda na tumefika katika maeneo mbali mbali.

Lakini nizingatie tu hilo kwamba Mheshimiwa Mbunge amelitaja. Kwa hiyo, tutaliweka katika program zetu ili tuweze kukutembelea huko. *(Makofi)*

Na. 86

**Kuboresha Silaha Wanazotumia Askari Polisi**

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, baadhi ya Majambazi hutumia silaha za kisasa zaidi kuliko walizonazo polisi vituoni mwao na hivyo kushidwa kupambana nao ipasavyo wakati wa matukio ya uhalifu:-

(a)Je, Serikali ina mikakati gani ya kulipatia ufumbuzi tatizo hilo kwa kuwapatia Polisi Silaha bora na mafunzo ya ziada hasa kwa askari waliopo maeneo ya mpakani mwa Rwanda, Burundi na kadhalika?

(b) Je, Serikali haioni kuwa ni vema kuweka kambi za kudumu za JWTZ katika maeneo ya mapori wanamojificha majambazi na vibaka hasa kwenye Wilaya za Bukombe, Chato, Geita na Biharamulo?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuna ukweli kwamba maeneo yanayopakana na baadhi ya nchi jirani kumekuwa na matukio ya ujambazi wa kutumia silaha kubwa.

Mheshimiwa Spika, vyombo vya Ulinzi na Usalama vimekuwa vinafanya juhudi kubwa kukabiliana na uhalifu huo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba askari wetu wanazo silaha za kisasa kuweza kukabiliana na matishio ya ujambazi katika maeneo yote nchini.

Askari wameweza kupambana vizuri na uhalifu katika maeneo ya mipakani, lakini pia hata silaha wanazokamatwa nazo baadhi ya majambazi hazizidi ubora wa silaha wanazotumia askari wetu. Hata hivyo Serikali itaendelea kuboresha vitendea kazi katika majeshi yetu ili waweze kufanyakazi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa inatoa mafunzo ya mbinu za medani na mafunzo ya darasani kwa askari wanapokuwa katika mafunzo ya awali *(Recruit Course)*, lakini pia wamekuwa wanapewa *course* wakiwa kazini na wengine wanapewa mafunzo nje ya nchi ili kupambana na uhalifu na wahalifu.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi limekuwa likishirikiana na Vyombo vingine vya Dola likiwemo JWTZ katika maeneo ya mipaka, maeneo ya mapori na majini kwa kufanya doria, operesheni na misako kwa pamoja ili kuhakikisha maeneo yetu yanakuwa salama. Hivyo ndiyo kusema kwamba, Askari wa JWTZ wapo sehemu hizo.

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA:** Mheshimiwa Spika, na mimi niungane na Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwapongeza askari wetu kwa kazi nzuri wanayofanya pamoja na kwamba wanakumbana na matatizo.

Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Ninataka kujua silaha hizo wanazipata wapi hawa wahalifu wakati Serikali imechukua juhudi ya kuzichoma na kuziangamiza?

(b) Kwa kuwa suala la uharibifu limekuwa likiongezeka hasa hili la kutumia silaha kali; je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kuchukua hatua mahususi ya kuwaongezea silaha bora askari wetu hasa polisi; kwa sababu kuna wakati majambazi wanaposhambulia maeneo fulani hata polisi wanashindwa kujibu mashambulizi hayo kutokana na udhaifu wa silaha walizonazo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu maswali

ya nyongeza ya Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu, kama ifuatavyo:-

Swali lake la kwanza anauliza kama Serikali ama Jeshi letu la Polisi linaweza kudhibiti hizi silaha basi hawa wahalifu hizi silaha wanazipata wapi?

Mheshimiwa Spika, tulichonacho hapa ni matukio ambayo yametokea makubwa makubwa na tumekuwa tunaeleza bayana, hakuna siri ndani yake; watu wengi ambao wamekuwa wakikamatwa kwenye matukio ya ujambazi wanatoka nje ya nchi ya Tanzania. Hiyo inaeleweka na wanakotoka wanakuja na hizo silaha, lakini kubwa ni kwamba, tumeweza kupambana nao, tumeweza kuwanyang'anya hizo silaha na tumeweza kudhibiti wimbi la ujambazi.

Sina haja hapa ya kuwakumbusha Wabunge; mtakumbuka mwaka 2006 hali ya Dar es Salaam mathalani hata Arusha kule katika Taasisi za Fedha, Mabenki na *Bureau de Change*, ilikuwa mbaya sana. Lilikuwa ni wimbi ambalo linatisha, wizi na ujambazi, ulikuwa unafanyika mchana wa kupora mapesa na kuuwa watu. Tuliweza kudhibiti silaha walizokuwa wanakuja nazo kutoka nje. Kwa hiyo, niseme tu kwamba, hatuwezi tuka-*control* hiyo ya watu kuja ingawa tunafanya kila jitihada, lakini siyo kwamba silaha zinapatikana humu ndani, zinatoka huko nje.

Mheshimiwa Spika, la pili, askari wetu wanazo hizo silaha siyo kwamba hawana, isipokuwa wakati mwingine matukio yanapotokea yanakuwa ni ya ghafla, tunapoanza kuyashughulikia hatujasema kwamba tumeshindwa. Kwa hiyo, niseme kwamba, silaha zenyewe na anavyofahamu Mheshimiwa Mbunge na najua kwamba anafahamu ni soko ambalo kuna ubora kila mahali na ni teknolojia ambayo inakuwa *improved* mara kwa mara.

Kwa hiyo, silaha ambazo zimetengenezwa miaka mitano iliyopita, siyo sawa na silaha ambazo zinatengenezwa sasa ama zitakazotengenezwa miaka kumi ijayo. Ndiyo maana katika *terms* ambazo wanazitumia za kitaalamu wanasema kwamba, kuna *new generation* ya vifaa kama hivi.

Kwa hiyo, niseme tu kwamba, tunazo silaha na wala hatutishiki kwa ujambazi na niwahakikishie Watanzania kwamba, hali ya Tanzania ni shwari na itaendelea kuwa shwari na Watanzania wataendelea kuwa salama na mali zao zitaendelea kulindwa na Jeshi letu la Polisi. *(Makofi)*

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa Naibu Waziri amekiri uwepo wa matukio ya ujambazi kwenye maeneo ya mapori kwa Wilaya zilizo mipakani; na kwa kuwa Jeshi letu la Kujenga Taifa muundo wake unatoa fursa ya sisi kama nchi kupata faida kiuchumi na kijamii kwa kuwapa vijana ajira; je, Wizara iko tayari kushirikiana na Wizara ya Ulinzi kuona uwezekano wa kuweka Kambi

za Jeshi la Kujenga Taifa kwenye maeneo ili ziwe na *detachment* ambazo zitasaidia ulinzi kwenye njia zenye mapori?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Oscar Mukasa, kama ifuatavyo:-

Swali kama hili limewahi kujitokeza na tumewahi kulijibu mara kwa mara hapa Bungeni; ni kwamba, sijui dhana hii inatoka wapi maana ushirikiano katika vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ni mkubwa na pale ambapo tunaona kwamba ipo haja ya kushirikiana na Jeshi la Wananchi, hatujasita kufanya hivyo na wao hawajasita kufanya hivyo.

Mpaka sasa yapo maeneo katika nchi yetu na siyo vizuri kiusalama kuyasema, nina hofu, lakini usalama wa nchi yetu uko sawa sawa. Siyo vizuri kwenda kwa undani zaidi wa mambo mengi ambayo tunayafanya kiusalama, kwa sababu tukifanya hivyo inakuwa hatujitendei sisi wenyewe haki na tunatoa taarifa kwa maadui ambao shabaha yetu ni kupambana nao.

Niseme tu kwamba, hoja yake tumeipokea na kwa sababu upo ushirikiano, tutafanya kila jitihada kuhakikisha kwamba, matukio ya ujambazi ambayo yamekuwa yanatokea katika mapori, kwa mfano, sehemu za Biharamulo kule anakotoka Mheshimiwa, athari na hatari hizi zitachukuliwa hatua. Ushirikiano kati ya Jeshi la Polisi na Jeshi la Wananchi upo na ni mzuri sana.

Na. 87

**Mpango Mahususi wa Kulipendelea Zao la Tumbaku**

**MHE. JANET Z. MBENE (K.n.y. MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Zao la Tumbaku ni zao pekee ambalo halijaathirika na mtikisiko wa uchumi duniani; na kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Nne iliahidi kulikuza zao hili kutoka tani 47,000 mwaka 2005 hadi tani 100,000 mwaka 2010:-

(a) Je, ahadi ya Serikali ya tani 100,000 itatimia?

(b) Je, Serikali ina mpango gani mahususi wa kulipendelea zao hili kwa hali ilivyo sasa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

(a) Mheshimiwa Spika**,** kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Serikali katika kikao chake cha tarehe 17 Mei, 2006 kati ya Waziri Mkuu na Wadau wa Sekta Ndogo ya Tumbaku, iliagiza Programu ya Kuendeleza Sekta Ndogo ya Tumbaku iandaliwe ili kuongeza uzalishaji wa tumbaku toka tani 50,000 mwaka 2005/2006 hadi kufikia tani 100,000 mwaka 2009/2010.

Katika kipindi cha miaka mitatu tangu agizo hilo kutolewa, uzalishaji wa tumbaku umeongezeka kwa wastani wa asilimia 20 toka tani 50,618 mwaka 2005/2006 hadi kufikia tani 60,741 mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kasi ya ongezeko la uzalishaji tumbaku ya wastani wa asilimia tisa kila mwaka tangu 2005/2006, lengo la kufikia tani 100,000 mwaka 2009/2010 halitafikiwa. Sababu kuu ya kutofikiwa lengo hilo ni wadau kutowekeza rasilimali za kutosha ili kufikia tija ya tani 1.5 za tumbaku kwa hekta moja toka wastani wa sasa wa tani 1.0 kwa hekta.

Aidha, kutotumika kwa maeneo mapya ya ardhi inayofaa kwa kilimo cha tumbaku katika mikoa 10 nchini yenye wastani wa hekta milioni nane zinazofaa kwa kilimo cha tumbaku, kunachangia kutofikiwa kwa lengo tulilojiwekea. Kwa sasa eneo la uzalishaji wa tumbaku ni wastani wa hekta 55,000 tu kwa mwaka.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na mchango mkubwa wa Zao la Tumbaku katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa nchi yetu, mkutano wa wadau wa tumbaku uliofanyika tarehe 17 hadi 18 Machi, 2010 Mjini Tabora, ulishauri kuwa lengo la kuzalisha tani 100,000 kwa mwaka lisogezwe hadi mwaka 2013/2014 ili kuendana na hali halisi ya kiwango cha kuongezeka kwa uzalishaji cha wastani wa asilimia tisa kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza Zao la Tumbaku, hatua zinazochukuliwa ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(i) Kupanua maeneo ya kilimo cha tumbaku kwa kufungua maeneo mapya ili hekta milioni nane zinazofaa kwa kilimo cha tumbaku katika mikoa 10 yenye fursa ya kuzalisha zao hilo zitumike;

(ii) Kuimarisha miundombinu katika kukaushia tumbaku ili kupunguza upotevu wa majani ya tumbaku unaofikia hadi asilimia 40 kwa sasa;

(iii) Halmashauri za Wilaya linakolimwa Zao la Tumbaku kutenga asilimia 10 ya makusanyo ya ushuru kutokana na mauzo ya tumbaku kwa ajili ya kuendeleza uzalishaji wa zao hilo;

(iv) Kuimarisha usimamizi wa shughuli za kilimo na masoko katika ngazi mbalimbali hususan katika Vyama vya Msingi, Uongozi wa Wilaya na Bodi ya Tumbaku ili kuwapa moyo wakulima kuongeza uzalishaji; na

(v) Kuimarisha huduma za ugani na utafiti katika maeneo yanayozalisha tumbaku.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona. Kwa kuwa Serikali kwa kuona umuhimu wa Zao hili la Tumbaku katika Bajeti ya 2009/2010 iliahidi kulipa madeni ya nyuma waliyokuwa wanadai wakulima katika Vyama vya Msingi na Bunge lako Tukufu likaidhinisha shilingi bilioni 2.2; na kwa kuwa msimu wa soko 2010/20111 unaanza hivi karibuni na fedha hizi mpaka sasa hazijalipwa, jambo ambalo linawafanya wakulima wetu wapate hofu kwamba watakatwa fedha zao za msimu huu kulipia deni hilo. Je, Serikali inasema nini juu ya kuhakikisha kwamba fedha zile zinalipwa mapema kabla ya msimu wa soko kuanza?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Nkumba, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kabisa Serikali katika bajeti ilitenga shilingi bilioni 2.2 kwa ajili ya kulipa madeni ya Vyama vya Ushirika kwa wakulima wa tumbaku.

Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu na wakulima wa tumbaku kwamba, *commitment* ya Serikali ipo pale pale na fedha hizi zitalipwa katika bajeti ya mwaka huu, yaani huu tunaoendelea nao, kabla hatujafikia mwezi wa saba watakuwa wameshalipwa.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nilikuwa na swali moja la nyongeza. Kwa kuwa muda wa kufikia malengo unataka kuongezwa mpaka kufikia mwaka 2012/2013 lakini kwa staili hii ambayo pembejeo zinashindwa kuwafikia wakulima kwa wakati; Serikali imejipanga vipi ili kuhakikisha kwamba pembejeo zinawafikia wakulima bila usumbufu kama msimu uliopita?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, kama ifuatavyo:-

Kucheleweshwa kwa pembejeo za kilimo cha tumbaku kulitokana na mfumo ule ambapo makampuni binafsi ndiyo yalikuwa yanatoa pembejeo na sasa hivi vyama vya ushirika katika kilimo cha tumbaku ndiyo vinavyohusika. Kwa hiyo, kwa ujumla ni kwamba, kwa sababu tulikuwa kwenye *transition period*, lazima kuwe na matatizo madogomadogo kama haya. Kwa sasa Serikali itahakikisha kwamba, vyama hivi vinajipanga mapema ili pembejeo ziweze kuwafikia wakulima mapema zaidi.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ninataka nikiri kwamba, swali nililotaka kuuliza ni kama alilouliza Mheshimiwa Said Amour Arfi. Ahsante sana.

**MHE. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Bunge lako Tukufu liliridhia mkataba kuhusiana na uvutaji wa tumbaku; na kwa kuwa kuridhia huko tulizungumzia umuhimu wa kutoa tahadhari kwa wavutaji wa

tumbaku; na kwa kuwa Wizara hii inahamasisha kilimo cha tumbaku hususan katika maeneo ambayo mojawapo ni Mkoa wa Ruvuma, Namtubo; je, Wizara ina mpango gani wa kutenga kiasi cha pesa katika bajeti yake ili kuwaelimisha wananchi hao juu ya athari ya zao hili la tumbaku ?

**SPIKA:** Wewe mama vipi tena; wenzio tunategemea tumbaku wewe unaipiga vita! Mheshimiwa Waziri wa Kilimo. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Stella Manyanya, kama ifuatavyo:-

Swali la msingi lilikuwa linazungumzia juu ya kilimo cha tumbaku na alilouliza sasa ni athari ya kuvuta tumbaku; wanaolima tumbaku siyo lazima wavute, lakini athari na elimu inayohusiana na athari zinazotokana na kuvuta zinatolewa zaidi na Wizara ya Afya, sisi tunashughulika na kilimo cha tumbaku. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, wewe mtu unatufaa sana. Swali linalofuata.

Na. 88

**Soko la Ununuzi wa Chakula cha *SGR***

**MHE. VITA R. KAWAWA (NAMTUMBO**) aliuliza:-

Kwa kuwa mvua nzuri iliyonyesha imefanya upatikanaji mzuri wa mazao ya chakula kwenye mikoa minne *"the big four":-*

Je, Serikali inaweza kufungua mapema soko la ununuzi wa chakula la Kitengo cha Hifadhi ya Chakula katika mikoa hiyo na kusogeza soko hilo karibu na wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika**,** kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kila mwaka wakati wa msimu wa ununuzi wa mazao ya chakula, Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa, hununua nafaka kutoka kwa wananchi katika maeneo mbalimbali ya nchi yenye ziada yakiwemo maeneo ya Mikoa ya Iringa, Mbeya, Rukwa na Ruvuma ili kuhifadhi ziada ya chakula kwa ajili ya kukabiliana na dharura wakati wa upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mvua zilizonyesha vizuri katika maeneo ya mikoa ya *"the big four"* kama alivyoainisha Mheshimiwa Mbunge, Wakala wa Hifadhi ya Chakula, inalenga kufungua vituo vya ununuzi mapema mwezi Julai, 2010.

Mheshimiwa Spika, Mikoa ya Iringa, Mbeya, Rukwa na Ruvuma ina vituo vikuu vitatu vya ununuzi wa nafaka vilivyoko Makambako, Songea na Sumbawanga.

Aidha, Kanda ya Makambako ina vituo vidogo vya Makambako, Vwawa, Mlangali, Ludewa na Mundindi. Kanda ya Songea ina Vituo vidogo vya Songea, Mgazini, Kigonsera, Hanga, Mgalula, Rwanda, Namtumbo na Madaba. Kanda ya Sumbwanga ina vituo vidogo vya Sumbawanga, Laela, Matai, Namanyere na Mtenga. Lengo la kuwa na vituo hivyo katika maeneo haya ni kusogeza huduma hiyo ya ununuzi wa nafaka karibu na wananchi.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa katika msimu huu wa kilimo Serikali imefikisha mbolea katika kila ghala la kijiji na mvua zilikuwa nzuri hivyo mazao ya mahindi yamezalishwa kwa wingi na wakulima katika Mikoa hiyo hasa Mkoa wa Ruvuma wanategemea sana soko hili la Kitengo cha Hifadhi ya Chakula. Je, Serikali imeiongezea fedha za kununulia mahindi zaidi ya tani 120,000 zilizokuwa zinatengwa katika misimu ya nyuma ili wakulima wengi zaidi wauze katika soko hili?

(ii) Kwa kuwa wakulima wa Namtumbo wamejaliwa kuzalisha mahindi mengi mwaka huu. Je, Serikali inaweza kukielekeza Kitengo cha Hifadhi ya Chakula kutuongezea vituo viwili zaidi katika Makao Makuu ya Tarafa ya Mkongo na Sasawala?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza kuhusu Serikali kutenga fedha nyingi kwa ajili ya ununuzi wa chakula; hilo ndiyo lengo letu kwamba, ikiwezekana bajeti inayokuja mtupitishie fedha za kutosha ili tuweze kununua chakula cha kutosha kwa ajili ya hifadhi ya chakula kwa vile kumetokea upungufu wa chakula mara kwa mara kutokana na mabadiliko ya tabianchi na mambo mengine.

Suala lake la kuongeza vituo, napenda kusema kwamba, tutaangalia umbali uliopo kati ya vituo vilivyopo na maeneo haya ya ununuzi kusudi kama inawezekana, tuweze kuongeza vituo ili tuweze kusogeza huduma hii karibu na wakulima wenye mahindi.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa ni kweli kwamba mwaka huu kutakuwa na ziada kubwa sana ya mahindi hasa katika Wilaya za Mbozi na Mbeya Vijijini Mkoani Mbeya, ambayo naamini kabisa siyo yote yatakayonunuliwa na SGR; na kwa kuwa Waziri Mkuu aliahidi wiki iliyopita hapa mbele ya Mbunge kwamba anaweza akafikiria kuruhusu wakulima wenye ziada ya zao la mpunga kuuza nje; je, Serikali inawapa matumaini gani wakulima

hawa wa mahindi ambao watakuwa na ziada nao wataruhusiwa kuuza nchi za nje? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Hilda Ngoye, kwa kulieleza Bunge lako Tukufu, lakini pia kwa kuwajulisha wananchi kwamba, nafaka iliyoruhusiwa kuuzwa kwa kuomba kibali ni mpunga peke yake na siyo nafaka kwa ujumla kwa sababu ndiyo umezalishwa kwa wingi na sasa hivi wakulima wako karibu kuvuna mpunga mpya, kwa hiyo, wanaruhusiwa kuuza ile ziada. Mpunga peke yake kuuza ile ziada, mahindi hayajaruhusiwa.

Sasa naomba nijibu swali lake kama ifuatavyo:-

Tathmini itafanyika, ikionesha kwamba, kutakuwa na utoshelevu wa chakula kwa nchi nzima kwamba, mahitaji yetu ni tani milioni 10.6, kama tutakuwa na kiasi hicho cha chakula basi ruhusa itatolewa kwa sababu kusimamisha kwa muda kuuza nje ya nchi ni kutokana na kuangalia usalama wa chakula ndani ya nchi. Sera yetu ni kuwapa wananchi ili waweze kupata masoko, lakini pale chakula kinapopungua ni sharti tuzuie. Kwa hiyo, tutaangalia kama kiasi tutakachozalisha kitaruhusu kuuza, basi tutaruhusu kama tulivyoruhusu mpunga.

Na. 89

**Kupeleka Umeme Katika Miji Midogo ya Mbinga**

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Wilaya ya Mbinga ni eneo la Mbinga Mjini tu ndilo lina umeme na ambao hautumiki wote:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika Miji Midogo ya Maguu, Litembo, Matiri na Ruanda ili kutumia umeme huu kikamilifu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mhshimiwa Spika, naomba nitambue hapa kwamba, Mheshimiwa Kayombo, alishazungumzia suala hili wakati akichangia kwenye hotuba ya bajeti ya Wizara yangu na tatizo la kuupatia umeme Mji wa Mbinga na Miji Midogo ya Maguu, Litembo, Matiri na Ruanda lilizungumzwa. Mbinga imeshapata uzalishaji wa umeme wa jenereta mbili zenye uwezo wa kuzalisha jumla ya MW 2.5, ingawa kwa sasa matumizi ya juu hayazidi

MW 1. Hata hivyo, maeneo yote ya Mbinga yametathminiwa kuwa na mahitaji makubwa zaidi ya matumizi ya hivi sasa kulingana shughuli zake za kiuchumi na kijamii na hasa zile za wakulima wa kahawa, ambao kwa sasa bado hawajafikiwa na mtandao huu wa umeme, wanatumia nishati ya umeme kwa gharama kubwa ya jenereta za dizeli.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo haya, naomba ieleweke kwamba, Serikai inatambua kuwa Miji Midogo ya Maguu, Litembo, Matiri na Ruanda, inahitaji kupelekewa ujenzi wa njia ya umeme ili kutumia kikamilifu uwezo wa mashine za kuzalisha umeme zilizofungwa Mbinga. Tatizo linalokwamisha upelekaji umeme maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge ni uwezo mdogo wa Serikali kwa hivi sasa kutekeleza miradi ya kusambaza umeme nchini, yote kwa pamoja kwa wakati mmoja kulingana na uwezo wa kifedha.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kuzingatia kwamba Mji wa Mbinga wenyewe unahitaji usambazaji ili kuongeza matumizi ya umeme unaozalishwa, katika bajeti ya mwaka 2009, *TANESCO* wamepanga kuongeza mtandao wa umeme Mjini Mbinga kama ifuatavyo:-

Kwanza, ujenzi wa km 1.0 ya njia ya msongo wa kV 11, kufunga *transformer* yenye uwezo wa kVa 100 na ujenzi wa njia ndogo ya umeme yenye urefu wa km 2.0 ili kusambaza umeme maeneo ya Makita na Tanki la Maji, Mjini Mbinga.

Pili, kufunga *transformer* yenye uwezo wa kVa 100 na kujenga njia ndogo ya umeme yenye urefu wa km 2.0 ili kusambaza umeme maeneo ya Matarawe - Ruhuwiko.

Tatu, ujenzi wa njia ndogo ya umeme yenye urefu wa km 1.5 ili kusambaza umeme maeneo ya Kiwandani - Mbambi.

Mheshimiwa Spika, upanuzi mkubwa wa mtandao wa umeme katika Wilaya ya Mbinga umejumuishwa kwenye mradi wa kV 132 wa kupeleka umeme Songea kutoka Makambako. Ni vyema nitumie nafasi hii, kutambua ufuatiliaji wa karibu sana na wa makini wa Waheshimiwa Wabunge; Gaudence Kayombo na John Komba wa Wilaya ya Mbinga, ambao umechangia mafanikio yaliyofikiwa. Naomba niwaahidi Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwamba, Serikali itaendelea na juhudi za kutafuta fedha za kufikisha umeme kwa viwango bora zaidi kuliko ilivyo hivi sasa. Kwa maana hii, namhakikishia Mheshimiwa Kayomba kwamba, Serikali itaendelea kulifanyia kazi suala la kupeleka umeme Maguu, Litembo, Matiri na Ruanda.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwanza, nitoe shukrani zangu kwa Serikali kwa mipango mizuri sana juu ya usambazaji wa umeme katika Mji wa Mbinga ingawa kwa upande wa Miji Midogo ya Ruanda, Litembo, Maguu na Matiri mipango hiyo haijioneshi vizuri. Ninaishukuru pia Serikali kwa kupeleka umeme Peramiho, Jimbo la Mheshimiwa Jenista Mhagama na nimpongeze Mheshimiwa Mhagama, kwa kazi nzuri sana aliyoifanya. *(Makofi)*

(i) Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia hapa wakati Serikali ikijibu masuala ya umeme jinsi ambavyo Serikali yetu imekuwa ikipeleka umeme katika vijiji mbalimbali

katika nchi yetu. Katika Mkoa wa Ruvuma, pengine ni Peramiho tu ndiyo kijiji ambacho kina umeme. Sasa nachukua nafasi hii kumualika Mheshimiwa Waziri afike Mbinga aitembelee miji hiyo, aone *potential* iliyoko kule. Wakati huu ninapoongelea juu ya Kilimo Kwanza na maeneo yenye uzalishaji mzuri sana wa kahawa; je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kupokea mwaliko huo?

(ii) Kwa vile iko Kampuni ya *Tancol* ambayo imeingia ubia kati ya Serikali ya Tanzania kupitia *NDC* na *Pacific Cooperation* ya Australia ambao wamekubali kuendeleza uchimbaji wa makaa ya mawe ya Ngaka katika Kijiji cha Liyombo, Kata ya Ruanda, Wilaya ya Mbinga. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kukaa na hawa wawekezaji ambao wako tayari kujenga mtambo wa kuzalisha umeme wa MW 400 lakini pia wako tayari kuanza kujenga mtambo mdogo wa MW 10 ambao utamaliza tatizo la Mji wa Ruanda na Matiri pamoja na Mbinga? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Kayombo kwamba, katika Mkoa wa Ruvuma siyo Mji wa Peramiho tu ambao pana mikakati ya kupeleka umeme au pana umeme. Kwa Mkoa mzima wa Ruvuma, tuna mikakati sasa hivi ya kupeleka umeme Namtumbo, Songea yenyewe, kuboresha upatikanaji umeme kwenda mpaka Mbinga.

Mradi wa Makambako-Songea ambao umechelewa kwa sababu ya majadiliano yanayoendelea na Wafadhili wa Sweden, unahitaji zaidi ya dola milioni 70. Upatikanaji wa umeme wa gridi kwa Mkoa mzima wa Ruvuma utakuwa wa uhakika tutakapokamilisha mazungumzo.

Pale Songea pia pana mradi wa kununua jenereta mpya litakaofungwa pale, ambao utaboresha sana umeme kwenye Jimbo la Mheshimiwa Emmanuel Nchimbi na Jimbo la Mheshimiwa Mhagama. Kwa hiyo, hiyo yote ni mikakati ya Serikali ya kuboresha umeme kwenye Mji wa Ruvuma na vitongoji vyake.

Hili la pili la Mbinga, naomba niridhie kabisa mwaliko alionipa Mheshimiwa Kayombo na kati yangu au Mheshimiwa Waziri Ngeleja, mmoja wetu atakuja na kusema hili jambo la Ngaka, tayari utafiti wa viwango vya makaa ya mawe ya Ngaka umefanyiwa kazi na umeonekana kuwa ni mzuri sana kwa kuzalisha umeme.

Kwa hiyo, ninachosema, kama unafahamu sasa hivi matatizo ya uzalishaji wa kutumia makaa ya mawe yana kelele kelele hizi kidogo za mazingira za wakubwa wenzetu huko juu. Kwa sisi ambao tuna mikakati ya maendeleo, lazima tuangalie mbele mikakati yetu ya maendeleo na kusema kweli mradi huu wa Ngaka ni mradi ambao utekelezaji wake uko katika kipaumbele. Tutazungumza na wawekezaji hao na wewe umesema MW 10, lakini mimi nilipokuja Songea mwaka jana wao walisema wangeweza kuanza hata na 50.

Mheshimiwa Spika, kusema kweli kwa kiwango chochote ambacho mradi huu unaweza kuanza, sisi tutaufanyia kazi na tutashirikiana na wawezezaji ili mradi huu upate utekelezaji wa haraka. *(Makofi)*

Na. 90

**Kupeleka Umeme Vijiji vya Jimbo la Tarime**

**MHE. SAID A. ARFI (K.n.y. MHE. CHARLES N. MWERA)** aliuliza:-

Kwa kuwa vijiji vingi vya Jimbo la Tarime havina umeme na kwa kuwa kwenye bajeti ya mwaka 2009/2010 Serikali iliahidi kupeleka umeme vijijini kutoka Tarime - Itiryo:-

Je, ni lini utekelezaji utaanza ili wananchi katika Vijiji vya Nyamwigura, Rosana, Kemakorere, Nyarero, Nyamwaga, Keisongora, Muriba, Bungurure, Kabori, Itiryo, Kegonga, Masanga pamoja na vijiji vya jirani wapate huduma hiyo ya umeme ili kuboresha maisha ya wananchi katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Nyanguru Mwera, Mbunge wa Tarime, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2008/2009, Wakala wa Nishati Vijijini *(REA),* ilitenga shilingi milioni 120 kwa ajili ya kuanza Mradi wa Umeme Itiryo. Hata hivyo, *TANESCO* katika bajeti yake ya ndani pia ilitarajiwa kuchangia shilingi milioni 50 katika mradi huu kama gharama za usimamizi. Vijiji karibu vyote alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge vimo katika orodha ya miradi inayofadhiliwa na Wakala wa Nishati Vijijini chini ya mradi wa kupeleka umeme Itiryo kutoka Kituo cha Nyamongo, ambapo njia kuu ya msongo wa kV 33 umbali wa km 37 itajengwa. Mradi pia utahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa 0.4 kV na ufungaji wa *transformer* nane.

Mheshimiwa Spika, zabuni ya kuwapata wakandarasi wa kutekeleza mradi huu ilitangazwa mwishoni mwa Julai, 2009, ufunguzi wa zabuni hizo ulifanyika Novemba, 2009, majadiliano na mkandarasi aliyeshinda zabuni *M/S Namis Cooperative Limited* ya Tanzania yalikamilika mwezi uliopita Machi, 2010 na mkataba na mkandarasi unatarajiwa kusainiwa mwezi huu wa Aprili, 2010. Hivyo basi, kazi za ujenzi zinatarajiwa kuanza Mei, 2010 na kukamilika Aprili, 2011. Vijiji vinavyotarajiwa kunufaika ni pamoja na Itiryo, Nyamwigura, Kemakorere, Nyarero, Nyamwaga, Keisangora, Muriba na Tagagire.

Mheshimiwa Spika, umeme unaofika Jimbo la Tarime ni Gridi ya Taifa; hivyo basi, naomba nimshauri Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Tarime, wavute subira katika kipindi hiki ambacho Serikali inaboresha mtandao wote ili kukarabati mfumo wa usafirishaji na usambazaji wa umeme katika Kanda ya Ziwa. Tumeshazungumzia suala hili hivi karibuni wakati tukijibu maswali ya Mheshimiwa Richard Ndassa na

Mheshimiwa Chitalilo na tumerejea kutoa maelezo ya mipango ya kununua jenereta ya MW 60 kwa ajili ya Mji wa Mwanza itakayoboresha upatikanaji wa umeme Kanda hii yote ya Ziwa. Hivyo basi, naomba niwasihi wadau wote, sote kwa pamoja tunahimiza kukamilika kwa mipango hii yote kwa pamoja ili kuwapatia wananchi wa kanda hii umeme kwa viwango stahili.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa niaba ya Mheshimiwa Mwera, naishukuru Serikali kwa jitihada zinazofanywa na ninaamini kwamba, utekelezaji utakuwa kama jinsi ambavyo Mheshimiwa Waziri ametoa maelezo hivi sasa pamoja na ujenzi wa mradi huu.

(i) Kwa mujibu wa majibu ya Mheshimiwa Waziri, Jimbo la Tarime linapata umeme wa Gridi ya Taifa. Je, katika mpango wa ukarabati wa mradi huo watashirikisha Vijiji vya Kibaso, Jemkuru, Nyamwaga, Kiwanja, Morito, Kirembe na Nyakunguru katika mradi ambao sasa unashughulikiwa?

(ii) Kwa kuwa tatizo la Tarime linafanana sana na tatizo lililopo katika Mji wa Mpanda, Mitaa ya Ilembo, Shanwe, Kawajense na Semulwa; haipati umeme kwa sababu uwezo wa *TANESCO* kupeleka huduma katika maeneo hayo ni mdogo. Je, sasa Serikali itasaidia jitihada za *TANESCO* ili kuhakikisha mitaa inayozunguka Mji wa Mpanda inapata umeme? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nishukuru kwa pongezi alizozitoa Mheshimiwa Arfi, kwa kutambua kwamba Serikali inafanya kazi nzuri na kubwa ya kuongeza boresho ya upatikanaji wa umeme Jimbo la Tarime na maeneo yanayozunguka Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Spika, nimepokea maombi ya vijiji alivyoongeza Mheshimiwa Arfi kwa niaba ya Mheshimiwa Mwera. Labda niseme tu kwamba, tayari kazi ambayo imepangwa kufanyika hapa, gharama yake ni shilingi bilioni 1.6 kwa vijiji ambavyo tunakusudia kuvishughulikia hivi sasa. Kwa hiyo, kwa hivyo vijiji vilivyoongezeka, labda niseme tu kwamba, nimevipokea, naenda kuangalia jiografia yake nione kama utekelezaji wa mradi huu mkubwa unaweza ukaongeza vijiji hivyo. Vinginevyo, itakuwa ni utekelezaji wa mpango mpya na tutauzingatia kadiri fedha na uwezo wa Serikali utakavyokuwa.

Mheshimiwa Spika, amesema tatizo la Tarime linafanana na tatizo la Mpanda; nadhani siyo kweli japo katika kujibu suala la Mpanda naomba niwe mwangalifu kidogo. Tatizo la Mpanda ni la jenereta; majenereta yaliyokuwepo pale ni makuukuu kidogo. Sasa katika haya majenereta 12 ambayo tumekuwa tukiyazungumzia kwamba, yamefanyiwa ulipaji mwezi Desemba mwaka jana; kati ya hayo manne yanakwenda Sumbawanga, mawili nadhani yatakuwa Mji wa Sumbawanga na mawili yatakuwa Mpanda.

Kwa hiyo, nadhani mpaka kufikia mwisho wa mwaka huu, patakuwa na upatikanaji na umeme wa uhakika zaidi katika Mji wa Mpanda. Katika hatua hiyo, pia

tutafanya kazi ya usambazaji wa umeme huo baada ya uzalishaji wa uhakika kupatikana kwenye Vijiji vya Ilembo, Shamsa, Kwajeusi na Mpanda yenyewe.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kuniona. Kwa kuwa ahadi ya Serikali iliyotolewa kupeleka umeme vijijini kutoka Tarime mpaka Itiryo ni sawa sawa na ahadi iliyotolewa na Serikali mwaka 2009/2010 kuwa itapeleka umeme katika Vijiji vya Pahi, Nemya, Kolo na King'ang'a na mpaka sasa hakuna utekelezaji wowote ambao umechukuliwa. Wananchi wa vijiji hivi wengi wao wamejizatiti, wamenunua *television*, wamenunua simu na pasi wakiwa mategemeo kwamba umeme unawafikia.

Je, Serikali inawaambia nini wananchi hawa na hasa tukizingatia Mheshimiwa Malima ni mdau wa Kondoa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, huna haja ya kufafanua kwa nini wewe ni mdau; wewe jibu swali tu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zabein Mhita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nikifafanua itanipatia usalama zaidi nyumbani nikirejea jioni. Mimi nimeoa Kondoa na nimezaa Kondoa, kwa hiyo ni wakwe zangu na hivi vijiji vinanihusu moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme tu kwamba, tatizo la Kondoa ni kweli linataka kufanana kidogo na tatizo la Itirio, kwa sababu upatikanaji wa umeme wa gridi Kondoa pia una matatizo kwa sababu ya ule umbali wa usafirishaji wa umeme wenyewe unaokwenda pale. Kwa hiyo, mikakati iliyopo ni kwamba, kweli Serikali imeweka ahadi kwenye Vijiji vya Pahi, Mnunia, Kolo na Kinganga; na umeme wake kama alivyosema Mheshimiwa Zabein, unatokea Kingale.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tumeboresha mtandao mkuu wa *transmission* unaotoka Kusini kwenda Kaskazini kuja mpaka Singida. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Zabein Mhita kwamba, utekelezaji wa miradi hii bado uko palepale unaendelea, lakini sasa hivi pamoja na kupeleka umeme Pahi, Mnunia, Kolo na Kinganga, kazi kubwa inayotakiwa iende sambamba ni utekelezaji wa miundombinu ya usafirishaji ambayo ndiyo kazi tunayoifanya kwa hivi sasa. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie yeye na wananchi wote wa maeneo haya na wakwe zangu pia kwamba, utekelezaji wa mradi huu unakwenda vizuri.

Na. 91

**Ujenzi wa Barabara ya Mtwara – Mbamba Bay**

**MHE. RAYNALD A. MROPE** aliuliza:-

Kwa kuwa upo mpango wa kujenga Barabara ya lami kutoka Mtwara mpaka Mbamba Bay kupitia Mpango wa Maendeleo wa Kusini, yaani *Mtwara Development Corridor*:-

(a) Kwa kuwa lami inayowekwa ni hafifu ikilinganishwa na ile iliyowekwa kati ya Nangurukuru na Mingoyo; je, Serikali haioni kuwa gharama zitakuwa kubwa kwa ukarabati wa mara kwa mara?

(b) Je, hakuna viwango maalum vilivyowekwa katika ujenzi wa barabara hiyo ili iweze kudumu kwa miaka mingi?

(c) Je, gharama zilizotumika zinalingana na kazi iliyofanyika hasa kwenye barabara kati ya Mtwara na Mingoyo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba niseme kwamba, hakuna ujenzi mpya unaofanyika katika Barabara ya Mtwara – Masasi yenye urefu wa kilometa 201. Kinachofanyika ni matengenezo ya muda maalum katika baadhi ya sehemu zilizoharibika sana. Sehemu inayohusisha ujenzi mpya wa barabara ni kati ya Masasi na Mangaka – kilometa 54 na ujenzi wake umezingatia viwango kulingana na usanifu. Tatizo lililokuwepo katika sehemu ya Masasi – Mangaka awamu ya kwanza na ya pili ya ujenzi ni la mifereji ya maji. Tatizo hili lilitokana na Mfadhili kutotoa fedha za kujenga mifereji ya maji. Hata hivyo, Serikali imeliona hilo na tayari mifereji ya maji katika sehemu hiyo ya barabara inaendelea kujengwa kwa kutumia fedha za ndani.

(b) Mheshimiwa Spika, viwango vinavyotumika katika kujenga Barabara za lami vipo kwenye mwongozo *(specifications)* wa mwaka 2000 wa Wizara ya Miundombinu, ambao ndiyo unaotumika nchi nzima.

(c) Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mtwara – Mingoyo, ilijengwa mwaka wa 1976 ikiwa ni miaka 34 tangu ijengwe na pia ikiwa ni takriban miaka 20 zaidi ya muda wa uhai wa barabara hiyo, yaani *design life*, ambayo ni miaka 15. Kutokana na umri huo, barabara hii imechakaa na inahitaji matengenezo makubwa, yaani *rehabilitation*, kwa barabara nzima. Kutokana na uwezo mdogo wa fedha, kwa sasa sehemu zilizochakaa sana ndizo zimekuwa zikifanyiwa matengenezo ili ziendelee kupitika hadi hapo uwezo wa kifedha utakaporuhusu kuifanyia matengenezo makubwa barabara yote. Aidha, gharama iliyotumika kwa matengenezo inalingana na kazi zilizofanyika.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninawashukuru na kuwapongeza Waziri pamoja na Naibu wake, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kusimamia barabara zetu hapa nchini. Kwa kuwa matengenezo yanayofanyika ni ya muda maalum *(periodic maintainance)* na swali langu la msingi lilihusu ubora ama viwango vya barabara hizo za lami. Je, kwa nini Wizara katika kufanya matengenezo hayo hawasisitizi hasa kuwepo kwa ubora au viwango hivyo wanavyovisema ili barabara hizi ziwe nzuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatoa mifano; hata hapa nje ya Bunge hili Tukufu, barabara ilijengwa mwaka jana na mkandarasi, lakini hebu angalia tayari ina mashimo; inakuwaje?

(ii) Serikali imefanya kazi nzuri sana ya kujenga barabara kati ya Dar es Salaam – Kibiti – Lindi na sisi tunawapongeza sana kwa kazi hiyo. Sasa kwa kazi hii nzuri waliyoifanya; je, kipande kati ya Daraja la Mkapa na Somanga kitakamilika lini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mrope, Mbunge wa Masasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda nipokee pongezi alizotupa mimi pamoja na Mheshimiwa Waziri na kusema kweli hizi ni pongezi za Serikali kwa ujumla, kwa sababu tumewekwa pale ili kutekeleza shughuli hizi kwa niaba ya Serikali; kwa hiyo tunakushukuru sana. Pia na mimi nimpongeze tu kwa kujali matatizo ya wananchi wake, kwa sababu ya kufuatilia barabara zinazopita katika maeneo ya nchi hii mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, napenda sasa nijibu maswali yake mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hii habari ya viwango tumeieleza hapa kwamba, viwango vimewekwa maalum kutoka mwaka 2000 ambavyo vinatakiwa vifuatwe. Sasa namna ya kusimamia na ndiyo maana katika ujenzi wa barabara kunakuwa na msimamizi ambaye anafuatilia mara kwa mara kuona viwango hivi vinatimizwa. Inapotokea kwamba viwango hivyo vinakuwa havijatimizwa, mkandarasi anawajibika, kabla hajaikabidhi hiyo barabara aweze kufanya marekebisho yanayohusika ili barabara hiyo iweze kukidhi hivyo viwango vinavyohusika.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, katika Barabara ya Kusini ya Nangurukuru – Mbwemkuru, ujenzi wake haukufuata viwango. Kwa hiyo, baada ya Serikali kugundua hilo, ilimlazimisha mkandarasi ambaye alikuwa anajenga barabara hiyo kuhakikisha kwamba, anafanya marekebisho yanayohusika kabla haijakabidhiwa. Sasa hivi mkandarasi huyo ameshaingia mkataba wa kufanya marekebisho hayo ambayo kazi yake itaanza mwezi Mei, 2010. Hii yote ni kuhakikisha kwamba, usimamizi ndiyo kitu kinachofanya tuweze kujua ubora wa viwango vya barabara unatumika.

Mheshimiwa Spika, la pili kuhusu Barabara ya Ndundu – Somanga ambayo ujenzi wake hivi sasa unaendelea; ninataka niseme tu kwamba, mkandarasi sasa hivi

yuko *site* na sisi tuko karibu sana kufuatilia utekelezaji na ujenzi wa barabara hii ili iweze kukamilika kwa mujibu wa mkataba ambao huyu mkandarasi amewekewa.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Spika, mimi nataka kuuliza kuhusu kipande cha Ndundu – Somanga. Je, Wizara haiwezi kumshawishi mkandarasi anayejenga kipande hicho akaanza kujenga kutoka pale Malendego, Somanga na Muhoro halafu akaendelea na sehemu nyingine? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Samson Mpanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mkandarasi wa barabara hii ya Ndundu – Somanga tayari yuko *site* ameanza ujenzi. Kwa utaratibu wa kuingia mikataba ya ujenzi, mkandarasi anakuwa amejipangia kazi ambayo itakuwa imekubalika kwenye mkataba na kwa hiyo atakuwa anaifanya kazi hiyo kutegemeana na mipango aliyonayo. Niseme tu kwamba, kwa sababu maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge yana kero hizo, mimi naomba awe na subira kwa sababu barabara yote hii itakamilika muda si mrefu. Kwa hiyo, sisi tutahakikisha kwamba, maeneo yote yaliyotajwa hapa yatafikiwa na barabara hii iweze kupitika kwa ukamilifu wake.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, itabidi tufidie ule muda uliotumika katika kuwasilisha taarifa nyingi sana leo. Kwa hiyo, tutaendelea ingawa muda wa maswali umepita. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mbunge wa Lushoto.

Na. 92

**Barabara za Korogwe Kusimamiwa na *TANROADS***

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilikubali sehemu ya Mlalo – Mng'aro katika Barabara ya Lushoto – Mlalo – Mng'aro isimamiwe na *TANROADS* Mkoa wa Tanga:-

Je, Serikali iko tayari kuamua hivyo hivyo kwa sehemu za Mlalo – Ngwelo na Mlalo – Makanya kwa hoja zilezile na vigezo vile vile?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika ziara ya Mheshimiwa Rais, aliyoifanya Mkoani Tanga, mwezi Julai, 2008 alipoitembelea Wilaya ya Lushoto, aliagiza kuwa Barabara ya Mlalo –

Mng'aro, yenye urefu wa kilometa 25, ambayo iko chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto, itengenezwe na *TANROADS.* Agizo hili la Mheshimiwa Rais, lilitolewa kwa kuzingatia kuwa, Barabara ya Mlalo – Mng'aro, inapaswa kuwa iwe sehemu ya Barabara ya Mkomazi – Lushoto – Mlalo – Mng'aro. Barabara hii ilivyo hivi sasa, hukatwa vipande vipande na kuhudumiwa na *TANROADS* na sehemu nyingine kuhudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto.

Mheshimiwa Spika, Barabara za Mlalo – Muhero na Mlalo – Makanya, hazipo kwenye mazingira yanayofanana na yale ya sehemu ya Malalo – Mng'aro. Barabara hizi mbili zinajitegemea na siyo mwendelezo wa barabara nyingine kama ilivyokuwa kwa sehemu ya Mlalo – Mng'aro. Kwa sababu hizo, barabara hizi zitaendelea kuhudumiwa na Halmashauri ya Wilaya inayohusika.

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Spika, leo asubuhi nilimkabidhi Mheshimiwa Waziri ramani ya barabara hizo, inayoonesha kwamba, Barabara ya Mlela – Makanya ni mwendelezo wa barabara hiyo yenye urefu wa kilometa 15; na kwamba, Barabara ya Mlalo – Ngwelo ni mwendelezo wa Barabara hiyo ya Mng'aro kwa maana hiyo, Barabara ya Ngwelo ni tawi. Barabara hizi ni barabara kubwa, yanapita mabasi yanayotoka huko kwenda Tanga, Arusha na Dar es Salaam.

(i) Je, kwa sababu hizo Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuziingiza barabara hizo katika mtandao huo?

(ii) Kama haamini kwamba ni mwendelezo; yuko tayari kuongozana na mimi tukakague barabara hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja nikiri kwamba, amenipatia mchoro wa barabara hizo leo asubuhi. Ningependa kujibu kwamba, Sheria ya Barabara ya Mwaka 2007, imeweka vigezo vya kupangia hadhi barabara mbalimbali nchini. Ni bahati mbaya sana kwamba, barabara hizi ambazo anazitaja; Mlalo – Kwabranchi; ile ya kwenda Ngwelo; na Mlola – Kwabranchi; Makanya au Kolasi; hazikidhi vigezo vya kuwa Barabara ya Mkoa au Barabara Kuu ambazo zinakuwa chini ya usimamizi wa *TANROADS.* Kama katika maeneo mengine nchini, barabara ambazo zinahudumiwa na Halmashauri, panapotokea changamoto maalum, tungependa kuikaribisha Halmashauri ya Lushoto iwasiliane na Serikali Kuu, kwa maana ya Wizara yangu, tuone kama kuna changamoto maalum ambayo Serikali Kuu inaweza ikasaidia, tutakuwa tayari kuwasaidia ili kuwahakikishia usafiri mzuri. Ahsante sana.

Na. 93

**Wizara ya Maji na Umwagiliaji Kukosa Uwakilishi Wilayani**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA (K.n.y. MHE. STEPHEN J. GALINOMA)** aliuliza:-

Kwa kuwa kabla ya mabadiliko ya mwisho ya Baraza la Mawaziri, usimamizi wa umwagiliaji ulikuwa chini ya Idara ya Kilimo Wilayani; na kwa kuwa baada ya mabadiliko hayo Wilaya zimeachwa bila Uongozi wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji ikizingatiwa kwamba Idara ya Maji inahusika tu na maji ya kunywa na siyo umwagiliaji:-

Je, Serikali inaweza kueleza msimamo wake kuhusiana na upungufu huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Jones Galinoma, Mbunge wa Kalenga, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, fani ya umwagiliaji inahitaji wataalamu wenye taaluma mbalimbali ambao hufanya kazi pamoja kama timu ili kuweza kufanikisha uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji kwa tija na ufanisi unaohitajika. Taaluma hizo za wataalamu zinajumuisha uhandisi, haidrolojia, upimaji wa ardhi, udongo, vipando, sayansi ya jamii na uchumi wa kilimo. Kutokana na uhaba wa wataalamu hao kwa ajili ya kukidhi mahitaji katika ngazi ya Taifa na ngazi ya Halmashauri nchini, Serikali katika mwaka 1982, ilibuni muundo wa Vituo vya Kanda na kuanzisha Vituo vya Kanda saba za umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, huko nyuma masuala ya umwagiliaji katika ngazi ya Halmashauri yalikuwa yanaratibiwa na Afisa Maendeleo wa Kilimo na Mifugo wa Wilaya *(DALDO)*, ambapo chini yake alikuwepo Afisa Ugani wa Wilaya *(DEO)*, ambaye alikuwa na Kitengo cha Umwagiliaji. Muundo huu ulionekana kumnyima Mtaalamu wa Umwagiliaji, uhuru wa utendaji kazi. Hali hii iliangaliwa pia wakati wa kutathmini mahitaji ya rasilimali watu katika utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo, ambayo inaupa kipaumbele umwagiliaji. Tathmini hiyo ilipendekeza kuiongezea hadhi Ofisi ya Umwagiliaji ya Wilaya ili iweze kutimiza majukumu yake kikamilifu kwa kuifanya kuwa Idara kamili inayosimamiwa na Afisa au Mhandisi wa Umwagiliaji wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Galinoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshatambua upungufu wa kimuundo na uhaba wa wataalamu wa umwagiliaji uliopo, siyo tu katika ngazi ya Wilaya isipokuwa hata katika ngazi ya Taifa na inaendelea kuchukua hatua kurekebisha tatizo hili. Kwa mfano, mwaka 2008, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alifanya mabadiliko ya kimuundo kwa kuunda Wizara mpya ya Maji na Umwagiliaji. Muundo huu unatoa fursa kwa wahandisi wa umwagiliaji, kujihusisha na ujenzi wa

miundombinu ya umwagiliaji na kuacha huduma za ugani, yaani *Agricultural Extension Services,* zikisimamiwa na Wizara yenye dhamana ya kilimo.

Kinachofanyika sasa ni kuendelea kujenga uwezo katika ngazi ya Wilaya kwa kuajiri wataalamu wenye sifa zinazotakiwa na kuwapa vitendea kazi. Idadi ya chini ya wataalamu wa umwagiliaji inayopendekezwa katika kila Halmashauri ni wataalamu watano wanaojumuisha mhandisi mmoja wa umwagiliaji, mafundi sanifu watatu na mpima ardhi mmoja.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaendelea kushirikiana na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kujenga uwezo wa huduma za maji na umwagiliaji kwa kuajiri wataalamu na kuwapa vitendea kazi ili kuongeza ufanisi wa utendaji. Wakati utaratibu huu unaendelea, Halmashauri zitaendelea kupata ushauri wa kitaalamu katika fani ya umwagiliaji kutoka katika Ofisi za Kanda saba za Umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara yangu inaangalia uwezekano wa kuimarisha Ofisi za Umwagiliaji za Kanda ikiwa ni pamoja na kuongeza Kanda hizo kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma. Aidha, kwa kuanzia, Mikoa sita ya Mbeya, Rukwa, Kigoma, Morogoro, Iringa na Ruvuma, yenye uwezekano mkubwa wa kuzalisha mazao, itapewa kipaumbele katika uwezeshwaji wa rasilimali katika fani hii ya umwagiliaji.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, katika majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri, amekiri kwamba kuna upungufu na kwamba muundo wa sasa wa Idara ya Kilimo na Mifugo, hauruhusu suala la umwagiliaji kupewa kipaumbele na amependekeza kwamba, Serikali ina wazo la kuunda Idara ya Umwagiliaji katika ngazi ya Halmashauri.

Je, ni lini katika mipango ya Serikali hiyo Idara itaundwa ili iweze kuwezesha umwagiliaji uweze kufanyika katika ngazi ya Wilaya?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kama sote tunavyojua, katika ngazi ya Wilaya, TAMISEMI ndiyo hasa yenye jukumu hilo la kusimamia muundo ulioko pale. Ndiyo maana katika jibu la msingi nimesema Wizara yangu inashirikiana na TAMISEMI, kuhakikisha kwamba katika ngazi ile huduma hii ya umwagiliaji nayo inapata kasi inayotakiwa.

Sitaki kusema ni lini idara hii itaundwa kwa sababu mambo ya muundo pia yanahitaji mipango na fedha. Ninataka niseme tu kwamba, upungufu huu tumekwishauona na tunaufanyia kazi kwa kushirikiana na TAMISEMI. Muda ukifika, basi idara hiyo itaundwa kama Wizara ya Maji na Umwagiliaji mwaka huo wa 2008.

Na. 94

## Ufufuaji wa Viwanda Nchini

**MHE. LUCY F. OWENYA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilipokuwa ikijibu swali namba 43 kwenye Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge ilisema kuwa ipo kwenye mkakati wa kutafuta wawekezaji ili waweze kufufua viwanda na pindi watakapopata wawekezaji viwanda hivyo vitaanza kufanya kazi:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuvifufua viwanda hivyo na kutafuta wazawa kununua hisa katika viwanda hivyo ili viweze kuwanufaisha?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Bisahara na Masoko, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu swali namba 43, tarehe 24 Aprili, 2009; Serikali imeweka umuhimu mkubwa katika ufufuaji wa viwanda. Juhudi za ufufuaji wa viwanda nchini zimekuwa zikienda sambamba na ubinafsishaji wa mashirika na viwanda vilivyokuwa vya umma, ambapo kwa sasa 97% ya viwanda vyote iko chini ya sekta binafsi. Vingi vimefufuliwa na vinafanya kazi, ikiwa ni pamoja na viwanda vya saruji, bia, sigara, vya kusaga unga *(NMC)*, vya nguo, majani ya chai na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika kuhamasisha Watanzania kumiliki mali za umma, Serikali imekuwa ikishikilia hisa chache za mashirika yanayobinafsishwa ili baadaye hisa hizo ziuzwe kwa Watanzania kupitia Soko la Hisa la Dar es Salaam punde mashirkka na viwanda hivyo vitakapofufuliwa na kuzalisha kwa faida. Ili kuwezesha Watanzania wenye kipato kidogo kumiliki hisa za Serikali katika mashirika na viwanda vilivyofufuliwa, Serikali huuza hisa hizo kwa bei ndogo kuliko bei ya soko na Watanzania wengi sasa wanamiliki hisa katika viwanda vilivyofufuliwa.

Hadi sasa makampuni ambayo yameuza hisa zake kwa Umma wa Watanzania kupitia Soko la Hisa la Dar es Salaam ni pamoja na Kiwanda cha Saruji cha Wazo *(TPCC)*, Kiwanda cha Saruji cha Tanga, Kiwanda cha Bia cha *TBL*, Kiwanda cha Sigara *(TCC)*, Kiwanda cha Gesi *(TOL)*, Kiwanda cha Kufungasha Chai cha *TATEPA*, Kampuni ya *DAHACO na* vingine ambavyo baadaye Serikali itauza hisa zake.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Kilimo Kwanza kwa kiasi kikubwa utawezesha wazawa kushiriki kikamilifu katika Sekta ya Viwanda na Biashara na kumiliki uchumi wa taifa. *(Makofi*)

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza, lakini nasikitika swali langu

halikujibiwa kama nilivyouliza. Jana wakati tukijadili Sheria ya Mifugo, Waziri wa Mifugo na Uvuvi alilieleza Bunge hili kwamba, wafugaji wanashindwa kuuza nyama zao nje kwa sababu hatuna viwanda vya ku-*process* nyama.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na Kiwanda cha Tanganyika Packers ambacho kilikuwa kinafanya kazi kikabinafsishwa, lakini kwa sasa hivi inasemekana kwamba, imebadilisha matumizi na itakuwa inategemea kuwa ni shule au godauni. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwashughulikia hao ambao wamebadilisha matumizi badala ya kufanya kuwa kiwanda yanatumika kwa shughuli tofauti?

Mheshimiwa Spika, jibu la Serikali katika swali namba 43 lilieleza kwamba, Serikali ina mikakati ya kufufua na kutafuta wawekezaji ili waweze kufufua viwanda vilivyobinafsishwa. Je, endapo wawekezaji hawatapatikana Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba viwanda vile vinafanya kazi ukizingatia sasa hivi tuna kaulimbiu ya Kilimo Kwanza na sasa hivi tunaingia katika soko la pamoja ambalo wenzetu wa Kenya tayari wana viwanda vingi sana na inabidi sisi tuwe katika ushindani tuweze kuwa na viwanda vya kuweza ku-*process* vitu hapa hapa Tanzania? *(Makofi*)

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Lucy Owenya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimejitahidi sana kujibu swali la Mheshimiwa Owenya, kwa kadiri *situation* ilivyo au hali ilivyo, pengine sijajibu kama anavyopenda yeye kwa sababu hali yenyewe sivyo ilivyo.

Mheshimiwa Spika, uchumi wa sasa hivi ni uchumi wa soko huru, ambao huwezi ukashurutisha uwekezaji pale ambapo mwekezaji haoni kuna faida. Ndiyo maana kuna sababu pale ambapo sekta binafsi haiwezi kuwekeza, Serikali kupitia mashirika kama NDC inawekeza.

La pili, viwanda vilivyouzwa au mashirika yaliyouzwa yameuzwa kwa namna mbalimbali siyo kwa namna moja; vya kwanza ambavyo vinaendesha shughuli zake kwa kawaida kama *ongoing concern* au biashara inayoendelea viliuzwa. Viwanda vingine vimeuzwa kama *asset-stripping* kama vile kuuza mali zao moja moja.

Kwa hiyo, inategemea kwa kiwanda ambacho kimeuzwa kama *ongoing concern*, Serikali inaweza kumfuatilia yule mwekezaji na kuona kama anatekeleza mkataba wake. Kwa kiwanda kama Tanganyika Packers, ambavyo vimeuzwa kama *asset-stripping*, Serikali haiwezi kufuatilia zile asset zinatumiwa vipi kwa sababu atazitumia mali zile kulingana na jinsi biashara inavyokwenda. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Owenya aelewe kwamba, wakati wa *command economy* umepita, wakati ambapo Serikali inaweza ikashurutishwa kiwanda kujengwa mahali au kuwekezwa mahali. Sasa hivi ni nguvu ya soko ndiyo inayowafanya wawekezaji waweze kuwekeza mahali ambapo pana faida. Kwa hiyo, Serikali haiwezi kuwashurutisha wawekezaji kuwekeza mahali ambapo wao wanafikiria kwamba hakuna faida.

Sasa kuhusu kutafuta wawekezaji, Mheshimiwa Lucy Owenya ni shahidi kwamba, Serikali kupitia Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri na kupitia hili Bunge, tumehamasisha sana wawekezaji kuja kuwekeza na ni kweli kwamba, lazima Watanzania tujifunze kujisifu wenyewe badala ya kungojea watu wa nje. Ukweli ni kwamba, sasa hivi uwekezaji wa viwanda uko mwingi zaidi Tanzania kuliko Kenya na kwa hiyo sioni kwa nini Mheshimiwa Mbunge, aisifie Kenya na asisifie juhudi au jitihada ambazo zinachukuliwa Tanzania. *(Makofi*)

**SPIKA**: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umepita, sasa ni matangazo; nitaanza na wageni wetu.

Wapo wageni wa Mheshimiwa Waziri Mwantumu Mahiza ni wanafunzi 34 wa Chuo Kikuu cha Dodoma, ambao ni wenyeji wa Mkinga Tanga. Wale wanafunzi kutoka Mkinga ambao wako UDOM, tunawatakia mafanikio katika masomo yenu, mfanye vizuri ili nchi iendelee kupata wataalam walio bora; karibuni sana. *(Makofi*)

Wapo wageni wanane wa Mheshimiwa Felix Kijiko na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Christopher Chiza, wakiwemo Viongozi wa CCM Jumuiya ya Wazazi, wote wanaongozwa na Mchungaji Mstaafu Naftal Bikaka, Askofu wa Kanisa la Anglikana Kibondo. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), Mheshimiwa Philipo Marmo, ambao ni wanafunzi 23 kutoka *St. John's University of Tanzania*, Wilaya ya Mbulu. Nanyi tunawatakia mafanikio katika masomo ili nchi iendelee kuwa na wataalam bora; karibuni sana. *(Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Ruth Msafiri ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM),* ambao ni Ndugu Mathias Antidius; naomba asimame pale alipo. Ndugu Adoroph Kibi; Ndugu Ezron Rwenamba; na Ndugu Mutungi Ngemera; naona labda wana udhuru.

Wapo wageni 15 wa Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib na Mheshimiwa Ali Haroon Suleiman, ambao ni Viongozi wa CCM Wadi ya Kazimkazi, Jimbo la Makunduchi, wakiongozwa na Mheshimiwa Abdulaziz Hamad, Mheshimiwa Diwani wa huko. Wageni wetu kutoka Zanzibar Kazimkazi karibuni sana; kila mara ni furaha kubwa kukuoneni ndugu zetu kutoka Zanzibar. *(Makofi*)

Wanafunzi 20 na walimu watatu kutoka Shule ya Msingi Sir John Tanga ni wageni wa Shule ya Martin Luther ya Dodoma. Wale wanafunzi 20 na walimu watatu kutoka Shule ya Msingi Sir John. *(Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Castor Ligallama, ambao ni wafuatao; Ndugu Pelegrin Kifyoga, Katibu Mwenezi wa CCM Wilaya ya Kilombero pamoja na Ndugu David

Ligazio, Diwani wa Kata ya Sanje na Ndugu Ali Kikulo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Msolwa Ujamaa; asante sana na karibuni sana kutoka Kilombero.

Wageni wa Mheshimiwa Mussa Azan Zungu ni vijana kutoka Kamati inayoitwa Kamati ya Ilala; sijui ndiyo Kamati yake yeye mwenyewe au Kamati ya chama; basi ni Ndugu Shela Ashiki na Ndugu Sania Kimji; karibuni sana kutoka Ilala.

Tunao pia wanafunzi 30 kutoka Chuo cha Biashara CBE Dodoma, naomba wasimame pale walipo; asante sana wataalam wetu, tunawatakia mafanikio katika mafunzo yenu tunawahitaji sana. *(Makofi*)

Mwisho, wapo wageni sita wa Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mbunge wa Igalula, ambao ni Viongozi wa CUF kutoka Jimbo la Igalula, wakiongozwa na Ndugu Magella Salum Magella, Mkurugenzi wa Haki za Binadamu Jimbo la Igalula. *(Makofi*)

Unajua huu mwaka wa uchaguzi tunaona mambo mengi; uhusiano wa Mbunge wa CCM na Viongozi wa CUF kwenye Jimbo; basi ndiyo mambo yalivyo! *(Kicheko*)

Matangazo ya kazi; Mheshimiwa Alhaj Mohamed Missanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, anaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Miundombinu, mkutane saa saba mchana Ukumbi Namba 231.

Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, anaomba Wajumbe wote na nimetoa ridhaa kulingana na Muswada wa Sheria ya Madini, wakutane leo saa tano asubuhi katika Ukumbi wa *Basement* hapa ndani ya jengo jipya la Bunge.

Vivyo hivyo Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Dkt. Haji Mwita Haji, nimewaruhusu saa tano hii asubuhi wakutane kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa, kuzingatia Muswada wa Sheria ya *Pharmacy*.

Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mwenyekiti wa Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama, anaomba Wajumbe wote wa Kamati hiyo mkutane kwa kikao kifupi, saa saba mchana, Ukumbi Namba 219, Jengo la Utawala.

Mheshimiwa Abdisalaam Khatib, Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo, wakutane saa saba mchana katika Ukumbi Namba 227.

Mheshimiwa Elietta Switi, Katibu wa Chama cha Wabunge Wanawake *(TWPG)*, anawaomba Wabunge wote Wanawake wakutane leo saa saba mchana katika Ukumbi wa *Basement B*.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, anaomba Wajumbe wote mkutane leo saa saba mchana kwenye Ukumbi wa *Basement*.

Tangazo la Ofisi; nakala za Sera ya Madini zimewekwa kwenye visanduku vya nyaraka vya Waheshimiwa Wabunge wote, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnaombwa mkachukue nakala zenu ili mchango katika Muswada wa Sheria ya Madini uweze kukamilika.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Kaimu Katibu wa Wabunge wa CCM, anatangaza kwamba, Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi, wakutane leo saa mbili usiku, Ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la Mkurugenzi wa Idara ya Shughuli za Bunge; mgao wa *CBCF* umekwishawekwa vizuri. Kwa hiyo, Wenyeviti wote wa Wabunge wa kila mkoa, tunafahamu tuna vyama vyetu vya kimkoa, sasa Wenyeviti wote 26 waende Ofisi Namba 402, kuanzia saa tano. Kuna Waraka huo muhimu unaoonesha mgao wa fedha wa *CDCF* kwa kila jimbo ili Wenyeviti sasa waitishe vikao vya Wabunge kila mkoa ili kuweza kutambua hali hiyo.

Kuna makosa madogo madogo inabidi yarekebishwe, mimi nimeuona huo Waraka itabidi ufanyiwe marekebisho, lakini hayo ni masuala ya kujadiliana tena baadaye na TAMISEMI ili kurekebisha.

Huo ndiyo mwisho wa matangazo, sasa namwita Katibu kwa shughuli inayofuata.

## HOJA ZA KAMATI

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, leo tutapokea Taarifa za Kamati zetu za *Oversight;* Kamati za mahesabu zote tatu na kila Mwenyekiti anapewa muda usiozidi dakika 30 kuwasilisha na ili tuweze kwenda vizuri, badala ya kuwa na taarifa moja halafu tunaijadili, nadhani ni vyema taarifa zote za Wenyeviti wetu hawa ziwasilishwe moja baada ya nyingine kwa nusu saa, nusu saa, halafu ndiyo tuweze kuwa na mjadala ya kijumla. Ahsante sana. *(Makofi*)

Kwa tangazo hilo, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa John Cheyo, awasilishe taarifa yake. *(Makofi*)

**MHE. JOHN M. CHEYO - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza ni utangulizi. Kwa mujibu wa Kifungu Na. 114 (15) cha Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, naomba kuwasilisha taarifa ya kazi za Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa kipindi kilichoanzia Aprili 2009 mpaka Aprili, 2010. Katika kipindi hicho Kamati ilijadili Hesabu za Serikali za Mwaka wa bajeti wa 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, kabla sijawasilisha taarifa ya Kamati, naomba kutoa salamu za pongezi kwa niaba ya Kamati kwa Mheshimiwa Janet Mbenne na Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu kwa kuteuliwa na Rais kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania. Kamati inawatakia kila la kheri katika utendaji wao katika Bunge hili na Mungu awajaalie wawepo katika Bunge lijalo pia.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuwapongeza wajumbe wa Kamati hii kwa ushirikiano wao na kwa kazi nzuri waliyoifanya Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yaliyoainishwa hapo juu. Michango yao imesaidia kuboresha na kujenga dhana ya kuwepo nidhamu ya matumizi ya fedha na mali za Serikali kulingana na sheria, taratibu na Kanuni zilizopo. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa John M. Cheyo, Mwenyekiti; Mheshimiwa Zubeir A. Maulid, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Mohammed R. Abdallah, Mjumbe; Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mjumbe; Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mjumbe; Mheshimiwa Hasnain G. Dewji, Mjumbe; Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mjumbe; Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, Mjumbe; Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami, Mjumbe; Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mjumbe; Mheshimiwa Sevelina S. Mwijage, Mjumbe; Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Alhaji Ali Haji Ali, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mjumbe; Mheshimiwa Manju S. Msambya, Mjumbe na Mheshimiwa Lucy Owenya, Mjumbe.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye taarifa ya Kamati ya mwaka uliopita, Kamati nyingi za Hesabu za Serikali katika Mabunge ya nchi zinazoendelea zinashughulika na kazi ya kuangalia Taarifa na vitabu vya mahesabu (*financial statements*) mezani. Kazi muhimu ni kuhakikisha kwamba fedha zilizotolewa na Bunge zimeleta matokeo yaliyotarajiwa *value for money*. Suala hili linawezekana tu kama Kamati zinawezeshwa kusafiri na kuangalia miradi inayotekelezwa na Serikali. Hata Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pia imepanua shughuli zake ambapo sasa inajikita katika ukaguzi wa thamani. Kamati inampongeza kwa dhati Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kuwasilisha katika Bunge lako Tukufu taarifa nne kwa mwaka za thamani ya fedha inayoidhinishwa na Bunge kwa matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, changamoto mbele ya Bunge na Kamati za Hesabu (*Oversight*) ni uwezo wetu wa kutumia taarifa hizi kwa sababu mwelekeo huu ni mpya. Kamati inaendelea kujenga uwezo na Mwezi Mei mwaka huu tutakuwa na mafunzo elekezi yatakayojumuisha Kamati zingine kiulimwengu ili kubadilishana uzoefu *(international conference on VFM Dar es salaam)*. Tunamshukuru sana Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Benki ya Dunia kwa kuwezesha mafunzo haya kwa Kamati.

Mheshimiwa Spika, misingi inayoongoza utendaji wa kazi za Kamati. Naomba kurejea sehemu ya taarifa ya Kamati hii kwa mwaka 2008 na 2009 kwa kutaja misingi muhimu inayoongoza Kamati wakati wa utendaji wa kazi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, msingi wa kwanza ni Katiba ya Tanzania Ibara ya 63, nanukuu: "Sehemu ya Pili ya Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka, kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii".

Mheshimiwa Spika, moja ya majukumu makuu ya Serikali ni kukusanya kodi na fedha kutoka vyanzo mbalimbali vya walipa Kodi na kutumia fedha hizo kama vile Bunge lako Tukufu lilivyoidhinishwa. Kazi yetu kama Bunge ni kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kutumia Kamati mbalimbali. Kazi ya Kamati ya Hesabu za Serikali ni kukagua Hesabu za Serikali *(financial audit)* na utekelezaji wa malengo ya bajeti *(performance audit)* na kuishauri Serikali katika matumizi bora na endelevu ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tunashauri Bunge lako Tukufu lijielekeze kwenye Sura ya Saba ya Katiba, Ibara ya 133 mpaka 144 (Masharti kuhusu Fedha za Jamhuri ya Muungano) na kwa msisitizo mambo yafuatayo yaangaliwe kwa makini:-

a) Fedha za Serikali haziwezi kutumika bila Sheria iliyotungwa na Bunge (Ibara ya 136).

b) Hakuna Kodi ya aina yoyote itakayotozwa isipokuwa kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge (Ibara ya 138).

c) Majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (Ibara ya 143) ambayo ni pamoja na kuhakikisha kwamba fedha zitatoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa matumizi yaliyoidhinishwa na Bunge na angalau mara moja kwa mwaka kukagua mahesabu yote ya Serikali na kupeleka taarifa ya Ukaguzi kwa Rais. Aidha, Rais anawajibika kuwaagiza watu wanaohusika wawasilishe taarifa hiyo kwenye kikao cha kwanza cha Bunge kitakachofuata baada ya Rais kupokea taarifa hiyo na itabidi iwasilishwe katika kikao hicho kabla ya kupita siku saba tangu siku ile kikao kilipoanza.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Fedha. Utekelezaji wa Katiba katika eneo hili umepewa nguvu ya kisheria katika Sheria ya fedha *(Public Finance Act No.6)* kama ilivyorekebishwa Mwaka 2004. Sheria inasisitiza kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu anafanya kazi yake ya Ukaguzi kwa niaba ya Bunge.

Nanukuu kifungu 31(1) : *"The Controller and Auditor General shall on behalf of the National Assembly examine, inquire into and audit the accounts submitted to him under section 25 of this Act and perform any other functions which he is authorized to perform by or under this Act."*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ukaguzi wa Umma (*The Public Audit Act*, 2008) pia inatoa madaraka kwa Kamati za Bunge na hatimaye kwa Bunge zima kushughulikia masuala ya fedha za Serikali. Nanukuu: *"39 (1) The Public Accounts Committee, Local Authority Accounts Committee, Parastatal Organisations Committee and any other*

*Parliamentary Sectoral Committee as the case may be, shall discuss the reports of the Controller and Auditor General after they have been tabled in the National Assembly."*

*(2) Upon the completion of hearing the Parliamentary Oversight Committees shall prepare and submit to the National Assembly reports which may include comments and recommendations".*

Mheshimiwa Spika, Kanuni zilizotengenezwa na Waziri wa Fedha chini ya Sheria ya Fedha *(Public Finance Act, No.6 of 2001),* Sehemu ya Pili zimeeleza uwajibikaji wa Maafisa Wahasibu kwa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (*PAC*), nanukuu: *"Every Accounting Officer shall be personally and pecuniarly responsible and accountable for the collection and receipt of all revenue or for all disbursements of expenditure in his vote, and shall be answerable to the Public Accounts Committee (PAC)."*

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kamati ya Hesabu za Serikali yameainishwa katika Kanuni za Bunge (2007) Nyongeza ya Nane (8) Kifungu cha 10 kama ifuatavyo:-

a) Kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara za Serikali yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

b) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwisha kutolewa na Kamati hiyo yenye lengo la kuondoa matatizo hayo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara za Serikali; na

c) Kutoa mapendekezo na ushauri kwa Wizara za Serikali kuhusu matumizi ya fedha za Umma.

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hii kila Afisa Mhasibu anawajibika kufika mbele ya Kamati ya Bunge na kutetea utekelezaji wa bajeti ya fungu lake na anaweza kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Mheshimiwa Spika**,** taarifa hii ina sehemu saba yaani, sehemu ya kwanza utangulizi, sehemu ya pili masuala ya ujumla, sehemu ya tatu utekelezwaji wa maagizo ya Kamati, sehemu ya nne matokeo ya ukaguzi, sehemu ya tano ziara za Kamati, sehemu ya sita maoni na mapendekezo ya Kamati na sehemu ya saba hitimisho.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ni kuhusu masuala ya jumla, mzunguko wa uwajibikaji (*Accountability Loop*). Mara baada ya kuwasilisha taarifa ya kazi za Kamati kwa kipindi kilichoishia Machi, 2009, Kamati yangu iliendelea na mzunguko wa uwajibikaji kama ilivyo kawaida ya Kamati za Uchunguzi. Kamati ilitoa maoni na mapendekezo Serikalini ambayo yalilenga katika kuboresha uwajibikaji wa Fedha za Umma. Serikali kwa mara ya kwanza ilijibu rasmi hoja za Kamati za kiuchunguzi kama inavyohitajika kisheria. Hongera sana kwa jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, hatua ya Serikali kujibu mapendekezo ya Kamati na *CAG* ndiyo inakamilisha mzunguko wa uwajibikaji. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii

muhimu. Hata hivyo, kwa kuwa matakwa ya kujibu hoja za Kamati ambazo huridhiwa na Bunge ni la kisheria, Kamati inasisitiza kuwa ni lazima utekelezwaji wake ufanyike mara moja, isipokuwa pale inapoonekana ipo haja ya suala hilo kurejeshwa tena mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilishauri kuwa, mzunguko huu wa uwajibikaji hauna budi kufuatwa na wote wanaohusika ili kuweza kuhakikisha matumizi sahihi ya fedha za umma. Tuliikumbusha Serikali ianzishe utaratibu wa kujibu mapendekezo ya *CAG* na Kamati katika mfumo wa *treasury notes* ndani ya muda maalum kama inavyohitajika kisheria *(Public Audit Act, 2008)*. Kamati imefarijika kuwa utaratibu huu sasa umeanza kufuatwa.

Mheshimiwa Spika , kuhusu Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*). Kamati yangu imeendelea kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi katika kufanya shughuli zake. Kwa namna ya pekee, Ofisi hii imeendelea kupanua wigo wa ukaguzi wake, hatua ambayo inapongezwa sana na Kamati. Hivi karibuni tumeshuhudia taarifa za ukaguzi wa ufanisi (*perfomance audit*) katika sekta ya afya na elimu. Kamati inampongeza sana Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na timu yake nzima kwa kazi nzuri wanayoifanya mpaka sasa. Ni matumaini ya Kamati kuwa Taarifa za kaguzi hizo zitaisaidia Serikali kuboresha huduma zake katika maeneo yenye upungufu.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya *CAG* inaikagua Serikali kwa niaba ya Bunge kama ilivyoelezwa katika Sheria ya fedha *(Public Audit 2008 )*. Sheria inasisitiza kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anafanya kazi yake ya Ukaguzi kwa niaba ya Bunge. Hivyo, Bunge halina budi kumpa ushirikiano wa kutosha ili aweze kufanya kazi yake kikamilifu. Kama inavyohitajika kisheria, bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi hujadiliwa katika kikao cha mashauriano (*consultative meeting*) kati ya Kamati ya Hesabu za Serikali (*PAC*), Waziri wa Fedha na Uchumi na *CAG*. Tayari Kamati yangu imeshaitisha na kufanya kikao hicho tarehe 11 Februari, 2010 ambapo kwa pamoja tulikubaliana kuhusu bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa Fedha 2010/2011. Bajeti hiyo imelenga kuongeza uwezo wa Ofisi hii muhimu ili kutekeleza majukumu yake. Aidha, Kamati inampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuonesha dhamira ya kuiwezesha Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa kuwaongezea nguvu kazi, kuboresha mishahara na mazingira ya Kazi.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani. Katika vikao mbalimbali kati ya Kamati yangu na maafisa Masuuli mbalimbali, Kamati ilishuhudia hoja nyingi za kikaguzi ambazo zinazuilika kabisa. Katika vikao hivyo, Kamati imekuwa ikiagiza kuimarishwa kwa mifumo ya ukaguzi wa ndani wa mafungu mbalimbali. Pamoja na yote haya, ilijitokeza hoja ya kuwa na mfumo huru wa ukaguzi wa ndani. Kamati yangu inaipongeza sana Serikali kwa kuona umuhimu wa kutenganisha shughuli za ukaguzi wa ndani toka kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali na kuwa Idara inayojitegemea ambayo itawajibika moja kwa moja kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali. Kamati inaamini idara hii itasaidia sana kuboresha mfumo wa ukaguzi wa ndani ambao utapunguza sana hoja za kikaguzi na hivyo kubadili sura ya vitabu vyetu vya fedha.

Msheshimiwa Spika, kuanzia Aprili 2009 mpaka Aprili 2010 Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali ilifanya kazi zifuatazo:-

Kujadili Hesabu za Serikali Kuu zilizokaguliwa za mwaka 2007/2008; Kamati ilijadili Hesabu za Serikali zilizokaguliwa zilizoishia tarehe 30 Juni, 2008. Hesabu hizo ni za Serikali Kuu, Mikoa na Vitengo vya Serikali vinavyojitegemea. Kamati imetekeleza jukumu hili kwa kadri ilivyoweza.

Mheshimiwa Spika, kufanya ziara ya kukagua thamani ya kazi zilizofanywa kwa fedha za Serikali kwa mwaka 2007/2008. Katika kipindi cha kuanzia April 2009 hadi Aprili mwaka huu Kamati yangu imefanya ziara za kikaguzi katika maeneo yafuatayo:-

- Barabara ya Marangu-Rombo Mkuu-Tarakea.
- Bandari ya Dar es Salaam.
- Bohari za MSD.
- Shirika la Nyumbu Kibaha.
- Shirika la Mzinga.
- Mradi wa upanuzi wa Hospitali ya Mkoa wa Morogoro.
- Hospitali ya Mkoa wa Arusha.
- Hospitali ya Mkoa wa Kilimanjaro na KCMC.
- Mradi wa Ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Makao Makuu ya Wilaya ya Mvomero na Ilemela.
- Hospitali za Bugando na Sekou Toure.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupata semina za mafunzo. Katika kipindi hicho Kamati pia ilipata Semina mbalimbali zilizokusudia kujenga uwezo kwa wajumbe. Semina hizi ziliendeshwa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali na Mradi wa *Deepening Democracy*.

Mheshimiwa Spika, kujadili maazimio. Kamati pia ilijadili Azimio la Bunge kuhusu Azma ya Kufuta Madeni na Upotevu wa Vifaa vya Serikali kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2008 na maoni yake yaliwasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu katika Mkutano wa 16 wa Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, Kuteua Mkaguzi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Kama inavyohitajika kisheria (*Public Audit Act*, 2008), Kamati yangu ilifanya kazi ya kuteua Mkaguzi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, ambapo kampuni ya *SBC Consultancy Services* iliongezewa muda wa mwaka mmoja kuendelea na kazi hiyo, muda ambao unaishia mwezi Mei, mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, kuchambua na kuidhinisha Bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Kamati yangu pia ilipitia na kuchambua bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2010/2011, ambapo Kamati iliipitisha bila mabadiliko. Kikao hicho pia kilihudhuriwa na Waziri wa Fedha na Uchumi. Utaratibu huu ni kwa mujibu wa Sheria ya Ukaguzi ya mwaka 2008. Hizo ndizo kazi ambazo tumefanya mpaka sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ni kuhusu utekelezwaji wa maagizo ya Kamati. Moja ya mambo muhimu ambayo Kamati yangu huyafanya katika vikao vyake, ni kujadiliana na Afisa Masuuli kuhusu hali ya taarifa ya hesabu zake kama inavyoripotiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kamati huangalia kwa pamoja sababu zilizopelekea Afisa Masuuli kupata hati aliyonayo, kisha hupanga mikakati ya kuondokana na hati chafu katika mahesabu yanayofuata. Kwa wale wenye hati safi, Kamati hupongeza na kutoa rai ya kuendelea kuwa na hati safi.

Mheshimiwa Spika, nina furaha kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, majadiliano haya yamekuwa na matokeo ya kuridhisha kwa asilimia kubwa miongoni mwa Maafisa Masuuli. Idadi ya hati chafu imekuwa ikipungua mwaka hadi mwaka, hoja za kikaguzi zinazotokana na uzembe zimepungua na juhudi zinaonekana katika matumizi ya fedha za umma yanayofuata taratibu. Hii ni hatua nzuri sana katika uwajibikaji kwa fedha za umma. Hata hivyo, bado Serikali haijafikia hatua ya kujivunia katika suala zima la matumizi ya fedha za umma. Bado kuna kasoro kadhaa ambazo Serikali inabidi izirekebishe. Kamati yangu bado inayo azma ya kushirikiana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kuhakikisha kuwa fedha za umma zinatumika si kwa kufuata taratibu tu, bali kwa matumizi sahihi, yenye tija na yanayolingana na thamani ya fedha.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ukaguzi ya mwaka 2008 inamtaka Mlipaji Mkuu wa Serikali kutoa majibu kwa hoja zinazotolewa na Kamati za uchunguzi ndani ya kipindi cha miezi mitatu. Napenda kuchukua nafasi hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa Serikali kwa mara ya kwanza kujibu rasmi taarifa za Kamati za kiuchunguzi kwa kuwasilisha majibu hayo Bungeni. Kamati yangu imeyapitia majibu hayo kwa undani kabisa ikishirikiana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Pamoja na jitihada hizo nzuri zilizooneshwa na Serikali katika kujibu hoja za Kamati, bado maeneo kadhaa katika majibu hayo, hayakutolewa majibu ya kuridhisha na kwa sababu hiyo, Kamati inalazimika kutaka maelezo zaidi na utekelezaji toka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya Kamati yangu iliyotolewa hapa Bungeni mwezi Aprili, mwaka jana, Kamati ilitoa pendekezo kwa Serikali kupunguza matumizi yasiyo ya lazima sana. Kamati inapongeza jitihada za Serikali katika kutekeleza agizo hili kwa kupunguza idadi ya Semina, makongamano na warsha ambazo zilikuwa zikifanyika kwa wingi sana. Hata hivyo, bado Kamati yangu inaamini kuwa, Bunge lako Tukufu linahitaji kujua Serikali ina mikakati gani ya kutumia hatua hizi katika kusaidia kuongeza bajeti ya maendeleo ambayo kwa kiasi kikubwa imeendelea kutegemea fedha za wahisani.

Aidha, Kamati yangu ilipendekeza Serikali ipunguze gharama kwa kupunguza manunuzi ya magari ya kifahari pasipo ulazima wowote, ilihali bado ina magari mazuri na mazima. Kamati inahoji kama kweli upo ulazima wa kila kiongozi anayeteuliwa kushika wadhifa unaostahili gari la Serikali, anunuliwe gari jipya, ikiwa gari la aliyemtangulia halijamaliza muda wake wa matumizi kwa mujibu wa taratibu za Serikali. Aidha, Kamati imekemea mtindo uliozuka wa kutumia samani za kutoka nje badala ya

kununua samani za mninga wetu zitakazodumu muda mrefu na kuleta ajira kwa viwanda vyetu vya samani. Kamati inasitiza tena jambo hili litekelezwe na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu pia iliagiza Maafisa Masuuli kufanya makisio sahihi ya matumizi yao, ili waweze kupewa bajeti inayokidhi pale inapowezekana. Serikali katika majibu yake imeihakikishia Kamati kuwa inawasisitiza Maafisa Masuuli kufuata utaratibu huu. Hata hivyo bado Kamati inaona utaratibu huu hautaweza kuisaidia Serikali kama itaendelea na utaratibu uliopo sasa wa kulimbikiza mno madeni. Madeni haya hulazimika kulipwa katika miaka mingine ya fedha na hivyo kuharibu kabisa mipango ya kibajeti. Hivyo Kamati inaikumbusha tena Serikali kuhakikisha kuwa madeni yote ya Serikali yanalipwa ndani ya miaka ya fedha husika ili kuondoa kasoro hizi.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya mwaka jana, Kamati yangu ilihoji madeni yasiyolipwa ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi yaliyofikia kiasi cha shilingi 18,525,429,295. Katika majibu yake, Serikali iliiambia Kamati kuwa ilikuwa na mpango wa kulipa madeni haya ndani ya mwaka wa fedha 2007/2008. Ahadi hii haikutekelezeka kwani, katika Hesabu za mwaka 2007/2008, deni hili limeonekana kuongezeka mpaka kufikia kiasi cha shilingi bilioni 26. Kamati hairidhishwi hata kidogo na kuongezeka kwa madeni haya. Ili kupunguza tatizo hili Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha madeni haya yanawekwa kwenye bajeti na kulipwa mapema iwezekanavyo ili kuinua ari ya watumishi wake.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilihoji utaratibu mzima wa kubakiza fedha katika maeneo ya makusanyo *(Retention scheme)* na udhibiti wake. Serikali imejibu vyema kwamba fedha zote za makusanyo hulazimika kurudi kwanza kwenye mfuko mkuu, kabla ya kurejeshwa kwa sehemu husika. Kamati haina kipingamizi na hili. Hata hivyo, Kamati inaona ipo haja ya kuongeza usimamizi wa zoezi hili katika balozi zetu. Pamoja na ukweli kwamba mapato katika balozi zetu yanatofautiana nchi hadi nchi, utaratibu wa kuhamisha fedha moja kwa moja toka balozi moja kwenda nyingine usitishwe. Kamati inaona ipo haja ya fedha hizo kurudi kwanza kwa Afisa Masuuli ambaye ndiye atakayepeleka fedha hizo katika balozi husika. Utaratibu huu utasaidia kuzuia uhamishaji fedha holela na kuzuia matumizi zaidi ya ilivyokasimiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Kamati yangu inaiomba Serikali kuzingatia maoni, mapendekezo na maagizo ya Kamati za kichunguzi katika maeneo mbalimbali yaliyotolewa katika taarifa zilizopita. Ni vyema pale penye ugumu wa kutekeleza agizo ama pendekezo fulani, Serikali ishauriane na Kamati husika juu ya njia mbadala ya kufikia malengo husika.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne ni matokeo ya hesabu. Shahada za Usahihi wa Hesabu. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, mwaka ambao Kamati yangu imeufanyia kazi, kulikuwa na jumla ya hati chafu tano, tatu toka kwenye *MDAs* na mbili kutoka katika balozi zetu. Aidha, kulikuwa na hati safi 71 na hati zenye shaka 26. *(*Kiambatisho i) Kamati yangu imekutana na Maafisa Masuuli wote wenye hati chafu na zenye shaka na baadhi ya Maafisa Masuuli wenye hati safi. Katika vikao vyetu tulijadiliana kuhusu hoja zilizopelekea kupata hati chafu na kuweka mikakati ya kurekebisha hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imeendelea kukutana na hoja za kikaguzi ambazo zinatokana na uzembe ambao unaepukika. Mafungu mengi yamepata hati zisizo safi kwa mambo madogo madogo kama vile kutotunza nyaraka za manunuzi, kutofuata taratibu na Sheria za Ununuzi, uvivu wa kurekebisha kasoro za Kihesabu kwa wakati na umahiri wa kujibu hoja, badala ya kuzuia hoja.

Mheshimiwa Spika, katika kurekebisha hali hiyo, Kamati yangu ilitoa maagizo mbalimbali kwa mafungu haya ambayo yalilenga kuboresha hali hii. Kamati ina imani kuwa kwa Hesabu za miaka ijayo, kasoro hizi zitaendelea kupungua na hatimaye kuisha kabisa.

Mheshimiwa Spika, Hoja za Ukaguzi. Katika Hesabu za Mwaka wa Fedha 2007/2008 ambazo Kamati ilizifanyia kazi, hoja kadhaa za kikaguzi zilijitokeza, nyingi zikiwa zinajirudia rudia. Hata hivyo, kumekuwepo na maboresho kidogo katika baadhi ya hoja, ikilinganishwa na mwaka uliotangulia. Baadhi ya hoja kubwa za Kikaguzi zilizojitokeza katika Hesabu za mwaka 2007/2008 ambazo Kamati ilizifanyia kazi ni hizi zifuatazo:-

Masurufu yasiyorejeshwa. Bado kumekuwepo na tatizo la kutorejesha masurufu kwa wakati katika matumizi ya fedha za umma. Takwimu zinaonesha kuwa tatizo hili limenza kupungua ukilinganisha na mwaka wa fedha 2006/2007, ambapo mpaka kufikia kipindi cha kuandikwa taarifa ya Ukaguzi kwa hesabu za mwaka 2006/2007 kiasi cha shilingi 3,138,942,669 kilikuwa hakijarejeshwa na kwa mwaka wa fedha 2007/2008 kiasi cha shilingi 976,045,660 kilikuwa hakijarejeshwa. Pamoja na kupungua kwa masurufu yasiyorejeshwa, bado Kamati inaitaka Serikali kudhibiti hali hii kama sheria inavyotaka (Reg. 103 (1) of PFR 2001). Kamati ilibaini kuwa, Maafisa Masuuli walio wengi hawakuwa wakali katika kufuatilia suala hili.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitoa maagizo kwa Maafisa Masuuli kufuata sheria inayoelekeza utoaji wa masurufu, ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua kwa wale watakaozembea. Kamati inaamini hali hii itaendelea kuboreka kwa hesabu zijazo, kama maafisa Masuuli watatekeleza maagizo ya Kamati juu ya suala hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu malipo yenye Shaka. Matokeo ya ukaguzi kwa mwaka 2007/2008 yaliibua hoja nyingine ya malipo yenye shaka ya kiasi cha jumla ya shilingi 10,056,706,649**.** Ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliotangulia, malipo haya yamepungua, ambapo kwa mwaka 2006/2007 kiasi cha shilingi 82,820,848,330 kilihojiwa. Malipo haya ni yale yasiyo na viambatanisho, kuhalalisha aina ya malipo yaliyofanywa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa pamoja na ujanja unaofanyika katika aina hii ya malipo, zaidi upo uzembe katika utunzaji wa kumbukumbu sahihi za malipo.

Baadhi ya nyaraka za malipo yaliyohojiwa zilipatikana baada ya kuhojiwa na wakaguzi na kabla ya kuja mbele ya Kamati ya Hesabu za Serikali. Katika hili Kamati ina shaka kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kughushi nyaraka ili kuhalalisha malipo. Kamati yangu imekemea vikali suala hili, na kuagiza kuwa pale inapobainika kuwa viambatanisho vya malipo ni vya kugushi, basi hatua za kisheria zichukuliwe mara moja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madeni ya Serikali. Matokeo ya kaguzi yamebaini pia uwepo wa madeni mengi sana ya Serikali, yakijumuisha *commitments* na *liabilities* mbalimbali ambazo Serikali huwekeana na wadau wake. Wizara na Idara nyingi za Serikali zimekuwa zikitumia huduma mbalimbali bila kulipa gharama za madeni hayo kwa wakati. Aidha, kumekuwepo na madai mbalimbali kwa Serikali toka kwa watumishi wake. Kwa mfano, Jeshi la Polisi, linadaiwa jumla ya Shilingi za Kitanzania bilioni 31 ambalo sasa limepungua hadi kufikia bilioni 26, Jeshi la Magereza shilingi bilioni 10,966,651,514 ambalo mpaka sasa limepungua kufikia shilingi 8,001,681,290.

Mheshimiwa Spika, madeni mengine ni yale ya Wizara ya Elimu na mafunzo ya Ufundi. Madeni hayo yalifikia jumla ya shilingi 26,075,448,333 ikiwa ni madai mbalimbali ya walimu wa shule za sekondari nchini. Madai hayo yalihusu tofauti za mishahara kutokana na kupandishwa vyeo, madai ya likizo, gharama za uhamisho na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla wake, madeni haya na mengine mengi ambayo hayajatajwa kwenye Taarifa hii yanatokana na ufinyu wa bajeti ya Serikali, ikilinganishwa na mahitaji. Tatizo hili husababisha mapungufu pia katika miaka ya fedha inayofuata kwa sababu madeni haya inabidi yalipwe. Suala hili linakwamisha jitihada za maendeleo, kwa kuwa fedha nyingi zatumika kwa madeni na kwa zile taasisi zinazoidai Serikali zinaathirika kwa kukosa fedha zinazodai.

Mheshimiwa Spika, Matengenezo ya magari yasiyofuata taratibu. Kanuni za ununuzi wa umma namba 59(1) na (2) ya mwaka 2005 inaeleza kuwa matengenezo ya magari ya Serikali ni lazima yafanywe katika karakana zilizoidhinishwa. Idhini hii hutolewa na Wakala wa Ufundi na Umeme wa Serikali (*TEMESA*). Mafungu kadhaa yamekutwa na hoja za ukaguzi zilizotokana na sheria hii.

Mheshimiwa Spika, kimsingi Kamati yangu haina pingamizi na sheria hii. Hata hivyo, Kamati inaona ipo haja ya kuimarisha karakana za *TEMESA* kwa kuzipatia vipuri vya kutosha, mafundi na vifaa vya kazi. Baada ya kusikiliza maelezo ya Maafisa Masuuli, Kamati imeshawishika kuwa sheria hii kwa namna moja au nyingine hukwaza sana hasa kama yakitokea mahitaji ya dharura. Karibu kila mkoa hapa nchini, karakana za *TEMESA* hazina kazi zaidi ya kutoa vibali vya kupeleka magari katika karakana za mitaani. Ni muhimu Wizara husika ilichukue suala hili kwa uzito unaostahili ili kuboresha utendaji wa wakala hii na kuondoa hoja za kikaguzi zinazotokana na kasoro hizi.

Mheshimiwa Spika, katika kupitia hesabu za mafungu mbalimbali, Kamati iliona tatizo kubwa la utegemezi wa bajeti yetu ambao umekuwa ni kikwazo kikubwa katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo. Serikali imekuwa ikibajeti shughuli za maendeleo

kwa kutegemea fedha za wahisani ambazo upatikanaji wake umekuwa wa kusuasua sana na ni mara chache mno ambapo fedha za kigeni zinazoahidiwa, zinatolewa kikamilifu. Hii imekuwa ikisababisha Maafisa Masuuli wengi kushindwa kutekeleza mipango ya maendeleo kikamilifu na hivyo kukwamisha juhudi za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mfano mdogo ni kwa Wizara nyeti kama vile Nishati. Kwa mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara ilitengewa fedha za maendeleo (*foreign component*) shilingi 306,254,884,900. Fedha iliyotolewa mpaka kufikia mwisho wa mwaka ilikuwa shilingi 23,294,826,786 sawa na asilimia7.6. Kwa mwaka wa fedha 2008/2009 fedha iliyoahidiwa ilikuwa shilingi 221,879,710,000, fedha iliyotolewa ilikuwa shilingi 24,436,238,883 sawa na asilimia 11. Hali kadhalika, kwa mwaka wa fedha 2009/2010 Wizara ilikasimia kiasi cha shilingi 75,047,778,000. Mpaka kufikia tarehe 31 Desemba, Wizara ilikwisha pokea kiasi cha shilingi 169,500,000 sawa na asilimia 0.23.

Mheshimiwa Spika, hali hii imejionesha si tu kwa Wizara hii, bali Wizara nyingine nyingi. Kamati haifurahishwi na mwenendo huu, kwani umekuwa ukijirudiarudia na kuleta picha isiyo sahihi kwa wananchi. Bajeti inaposomwa hapa Bungeni, wananchi na Wabunge wao hupata matumaini kuwa kuongezeka kwa bajeti ya maendeleo kutaboresha maisha yao, matumaini ambayo kiuhalisia hayatekelezeki kwa mwenendo huu wa bajeti. Ni vyema Serikali ikajihakikishia uhakika wa ahadi kabla ya kuziingiza katika bajeti ili kuwapa wananchi picha halisi ya bajeti yao.

Mheshimiwa Spika, utaratibu uliopo sasa wa kununua magari kupitia Wizara ya Miundombinu ulifanywa kwa nia njema kabisa ya kudhibiti manunuzi holela na kuhakikisha magari yanayonunuliwa yanakidhi viwango na ubora uliowekwa na Serikali. Utekelezaji wa utaratibu huu umekuwa ukileta malalamiko mengi miongoni mwa Maafisa Masuuli kuwa una urasimu (mchakato mrefu) na pia unaongeza gharama za manunuzi ya magari, ikilinganishwa na kama Wizara ama idara itanunua moja kwa moja bila kupitia Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona iko haja ya utaratibu huu kuangaliwa upya na pale penye kasoro parekebishwe mara moja ili kuondoa malalamiko na hoja za kikaguzi. Kuna ulazima wa Serikali kuweka bayana sababu za kuongezeka kwa gharama za ununuzi wa magari kwa kutumia utaratibu huu wa Wizara ya Miundombinu ili zieleweke na kupunguza malalamiko. Aidha, ili kupunguza muda wa kusubiri, Wizara irahishishe masharti ya ruhusa ya kununua magari moja kwa moja ili basi Wizara na Idara nyingine za Serikali ziweze kununua magari haya moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na tatizo kubwa la Serikali kutokuwa na taarifa sahihi juu ya watumishi wanaostahili kulipwa mishahara. Ukaguzi wa *CAG* umebainisha kuwa, limekuwepo tatizo kubwa la Serikali kuwalipa watu waliostaafu, walioacha ama kuachishwa kazi na pia waliofariki. Tatizo hili limejitokeza zaidi katika Hesabu za Mikoa na Wizara zenye Idara pana. Ili kutatua tatizo hili, Kamati imewashauri Maafisa Masuuli kufuatilia mara kwa mara taarifa za watumishi wao ili kujua uhalali wa aina ya malipo husika.

Mheshimiwa Spika, fedha za Halmashauri kupitia kwa *RAS*. Fedha za matumizi katika mikoa huombwa katika bajeti ya Makatibu Tawala wa Mikoa (*RAS*) na hujumuishwa katika mafungu yao kimahesabu. Fedha hizi zinapotolewa kwa ajili ya matumizi, hupelekwa moja kwa moja kwa Halmashauri, bila kupitia kwa Katibu Tawala. Hata hivyo, Katibu Tawala hupelekewa mfano wa vocha ya malipo (*dummy voucher*) toka Hazina kumjulisha kiasi cha pesa kilichotolewa kwa Halmashauri. Katika hali halisi, mtumiaji wa fedha hizi za Halmashauri ni Mkurugenzi wa Halmashauri. Hata hivyo, sheria inambana Katibu Tawala wa Mkoa kuwajibika kwa fedha hizi kwa sababu ziko chini ya Fungu lake.

Mheshimiwa Spika, Kamati imekuwa ikihoji jambo hili kila inapokutana na Maafisa Masuuli. Pamoja na ukweli kwamba Maafisa Tawala wengi hawaonekani kuona tatizo juu ya suala hili, Kamati inaona ipo haja ya utaratibu huu kuangaliwa upya, ili *RAS* ahojiwe na *PAC* kwa fedha zile tu alizozitumia na si vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekekzo kwa baadhi ya mafungu. Kamati kwa kushirikiana na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ilipitia na kuchambua hesabu za Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali (Fungu 23) ambayo pia inahusika na Deni la Taifa (Fungu 22) na Majumuisho ya Hesabu za Kitaifa *(The National Consolidated Final Accounts).* Katika mijadala ya mafungu haya Kamati ilibaini mambo kadhaa ambayo Serikali inalazimika kuyafanyia kazi mara moja.

Mheshimiwa Spika, katika kupitia na kuchambua hesabu za Fungu 23 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Fungu 22- Deni la Taifa pamoja na Hesabu za Majumuisho ya Kitaifa, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali iliweza kuona changamoto zifuatazo:-

1. Udhibiti wa dhamana za Serikali (*Government guarantees*) na mikopo kwa Mashirika ya Umma na Taasisi binafsi haupo.

Kamati ilibaini kuwa Serikali imekuwa ikiyadhamini mashirika ya umma na taasisi binafsi kupata mikopo katika mabenki na taasisi mbalimbali za fedha kama vile Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Vilevile Serikali imekuwa ikizikopesha fedha taasisi mbalimbali binafsi au kukopa toka taasisi za fedha za Kimataifa kwa niaba ya mashirika mbalimbali. Yafuatayo yalijitokeza:-

(i) Kufikia tarehe 30 Juni 2008 dhamana za Serikali kwa taasisi binafsi na mashirika ya Umma zilifikia kiasi cha Shs. 529,772,316,000.

(ii) Kiasi cha Shs.20.58 bilioni zilichukuliwa na Taasisi binafsi toka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) lakini kumbukumbu zake hazikuwepo katika taarifa ya dhamana za Serikali inayoandaliwa na Msajili wa Hazina.

(iii) Dhamana nyingi zilitolewa bila kuwepo kwa poni (*Securities*) kama sheria ya Mikopo, Dhamana za Serikali na Misaada (*Revised 2004*) inavyohitaji.

(iv) Serikali imekopesha Taasisi kadhaa binafsi kupitia Benki ya Rasilimali kiasi cha Shs. 36,500,000,000 ili kuendeleza kilimo cha maua, ambapo urejeshwaji wake si wa kuridhisha.

(v) Dhamana nyingine zilichukuliwa juu ya kiwango cha 100% ya mkopo, na hapakuwepo kibali cha Waziri wa Fedha kama matakwa ya sheria hiyo yanavyohitaji.

(vi) Baadhi ya maamuzi ya kutoa dhamana yalifanywa na Baraza la Mawaziri bila kupitia Kamati Maalum za Kusimamia Deni la Taifa (*National &Technical Debt Management Committees).*

(vii) Taasisi kadhaa binafsi na Mashirika ya Umma kama *TFC*, Nyanza na kadhalika zimeshindwa kurejesha mikopo waliyochukua na hakuna hatua madhubuti zinazochukuliwa katika kufuatilia urejeshwaji wa mikopo hii.

(viii) Kukosekana kwa Taasisi moja ya usimamizi wa Deni la Taifa.

Kamati ilifahamishwa kuwa usimamizi wa Deni la Taifa unafanywa na Idara na taasisi tofauti ambazo zinafanya kazi tofauti. Idara hizi ni pamoja na Ofisi ya Mhasibu Mkuu, Idara ya Sera, Idara ya Kushughulikia Masuala ya Fedha za Nje (*External Finance*), Msajili wa Hazina, Idara ya Bajeti, Benki Kuu na kadhalika. Kamati ilibaini kuwa hakuna mawasiliano ya kutosha katika Idara na Taasisi hizi kiasi kwamba wakati mwingine malipo hufanywa kwa madeni yaliyokwishasamehewa ndio mwanzo wa *EPA* hapo.

Gharama za kuondoa ziada ya fedha katika mfumo wa Uchumi (*Mopping up of excess liquidity in the economy).* Kamati ilifahamishwa kuwa Serikali inachangia gharama za kuondoa kiasi cha fedha kinachozidi katika uchumi, zoezi ambalo hufanywa na Benki Kuu. Vile vile ilifahamishwa kwamba kuna makubaliano ya uchangiaji huo kati ya Serikali na Benki Kuu kwa kutumia kanuni iliyokubaliwa na pande zote mbili.

Kamati ilifahamishwa kuwa ziada hii ya fedha katika uchumi inachangiwa na fedha nyingi za wafadhili zinazoingia kuendesha miradi mbalimbali ya maendeleo. Kamati ilibaini kwamba Serikali inaingia gharama kubwa ya kulipia riba katika mikopo ya Wafadhili na kisha kulazimika kulipia tena gharama za kupunguza ziada ya fedha katika uchumi, gharama ambazo zingeweza kuepukika iwapo mfumo wa fedha na uchumi (*Monetary and Fiscal Policy*) wa nchi ungesimamiwa vema.

Pia ilibainika kuwa fedha nyingi za miradi zinazowekwa katika mabenki hutumiwa na mabenki hayo kununua ikitumia dhamana za Serikali (*Government Securities*) yaani '*liquidity papers*' zinazotolewa na Benki Kuu ili kupunguza ziada hiyo na hivyo Serikali kujikuta ikilipia riba kwa fedha zake ilizohifadhi katika mabenki.

Kamati ilihoji kwa nini Wizara ya Fedha na Uchumi pamoja na Benki Kuu wanashindwa kudhibiti ongezeko hili ambalo linasababisha gharama zisizo za lazima na

mzigo kwa Serikali. Kamati inasitiza jambo hili liangaliwe na maamuzi yafanywe na Serikali ili kupunguza gharama za kuondoa fedha katika mzunguko wa uchumi (*moping up excess liquidity).*

Kukosekana kwa mkataba wa kiutendaji (*Memorandum of Understanding*) kati ya Hazina na Benki Kuu. Kamati ilifahamishwa kuwa Benki Kuu inaongozwa na Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006 ilihali Hazina inaongozwa na Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001(iliyorejewa 2004).

Kulingana na kifungu cha 5(1) na 60(1) na (2) cha Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006, Benki Kuu inao wajibu wa kuishauri Serikali kwenye masuala ya fedha na uchumi. Vile vile, kifungu cha 32(2)(b) na (c) cha sheria hiyo kinatamka kuwa Benki Kuu itakuwa Wakala wa Serikali katika kushughulikia malipo ya Deni la Taifa la ndani na nje, ikiwa nia pamoja na kulipia riba kwa mikopo hiyo.

Kamati ilibaini kuwa mbali na sheria hizi ambazo bado hazipambanui majukumu ya kila upande, hakuna mkataba maaalum wa kiutendaji kati ya Benki Kuu na Hazina ambao unaweka mipaka ya majukumu kati ya taasisi hizi mbili. Tatizo ambalo limekuwa likisababisha migongano wakati wa kufanya maamuzi hasa yanayohusu usimamizi wa deni la Taifa. Kamati inasisitiza hali hii irekebishwe ili kuleta ufanisi.

Kamati iligundua kuwa deni la Taifa limekuwa likiongezeka kwa kasi kubwa ambapo kwa mwaka ulioishia Juni 2006 jumla ya Deni la Taifa lilikuwa Shs. 9,232,929,037,390, hata baada ya kusamehewa kiasi cha USD. 4,391,490,000 bado deni kufikia Juni 2008 deni lilikuwa Shs. 6,477,451,842,417.72. Ilibainika kuwa wakati wa kukopa, viwango vya juu *(ceiling*) vya kukopa havifuatwi kulingana na matakwa ya kifungu cha 3(a), (b) na 6 cha Sheria ya Mikopo, Dhamana za Serikali na Misaada (kama ilivyorekebiswa 2004).

Kamati ilifahamishwa na uongozi wa Hazina kuwa pamoja na kuongezeka kwa deni, Serikali bado iko ndani ya kiwango kilichokubalika cha kukopa (*sustainable level)* cha 70% ya pato la Taifa. Hata hivyo, ilibainika kuwa mchanganuo unaoonyesha kiwango cha kumudu deni (*debt sustainability analysis*) hakijumuishi dhamana za Serikali (*Government guarantees*) kwa mashirika na taasisi binafsi suala ambalo limeonekana ni mzigo mkubwa kwa Serikali kwa vile mashirika mengi ya umma na taasisi binafsi yameshindwa kulipia madeni yaliyokopa na hivyo kuilazimu Serikali kulipia mikopo hiyo kwa niaba ya taasisi na mashirika hayo.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) – *Vote* 50, Kamati inapongeza jitihada za *TRA* katika ukusanyaji wa mapato. Kuongezeka kwa kiasi cha makusanyo, ni dalili kuwa kazi nzuri inafanyika. Hata hivyo, Kamati ilipokutana na Afisa Masuuli anayesimamia Mamlaka hii, ilimshauri kuhakikisha kuwa vyanzo zaidi vya mapato vinabuniwa ili kuweza kuongeza makusanyo na kupunguza utegemezi.

Mheshimiwa Spika, mtiririko wa makusanyo ya Kodi unaonyesha kuwa *TRA* imekuwa ikiongeza kiasi cha makusanyo kadri miaka inavyokwenda. Taarifa ya ukaguzi iliyowasilishwa mbele ya Kamati inaonesha kuwa kwa miaka mitatu mfululizo toka

2005/2006, makusanyo yamekuwa yakiongezeka zaidi ya ilivyokadiriwa kwa miaka hiyo. Kwa mfano, kwa mwaka wa fedha 2007/2008, *TRA* ilikadiriwa kukusanya shilingi 1,583,792,800,000 lakini makusanyo halisi yalifikia shilingi 1,592,668,031,974. Tofauti ya makusanyo zaidi ya makadirio ni kiasi cha shilingi 8,875,231,974 sawa na asilimia moja.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imefurahishwa sana na mafanikio haya ya *TRA* na ni matumaini yetu kuwa, kazi hii nzuri itaendelezwa na kwamba makusanyo yataendelea kuongezeka kwa miaka inayofuata. Pamoja na mafanikio haya, Kamati inaamini bado *TRA* inao uwezo wa kukusanya zaidi ya inachokusanya sasa. Hili litafanikiwa endapo tu vyanzo zaidi vya kodi (*Tax Base*) vitabuniwa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa wote wanaostahili kulipa kodi, wanafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, katika hesabu za *TRA* kwa mwaka 2007/2008 imejitokeza tena suala la malimbikizo ya madeni ya wadaiwa wa *TRA*. Kwa namna ya pekee, Kamati ilielezwa kuwa madeni mengi ambayo *TRA* inadai, yanacheleweshwa na mlundikano wa Kesi za madai mahakamani. Taarifa ya Ukaguzi inaonesha kuwa jumla ya madai ya *TRA* ya shilingi 37,621,013,159 yaliyopelekwa mahakamani, shilingi 29,811,317,909 yalilipwa na shilingi 7,809,695,250 yaliwekewa vipingamizi.

Mheshimiwa Spika, takribani shilingi 6,013,085,311 ambayo ni sawa na asilimia 78 ya kiasi kilichowekewa pingamizi ni deni linalotokana na kampuni moja, *M/s TIOT Limited*, deni linalotokana na mafuta yaliyoingizwa nchini kati ya mwaka wa fedha 2001/2002 na 2006/2007. Kwa kuwa maamuzi ya mahakama juu ya suala hili yamechukua muda mrefu sana, kuna hatari ya Serikali kukosa fedha hii, hasa ukichukulia kuwa kampuni tajwa yaweza kuamua kufunga biashara kwa namna yeyote na hivyo kulifanya deni hili lisilipike. Huyu bwana ana kiburi sana. Kamati inataka kujua hiki kiburi anakipata wapi na kwa nini Serikali haishughulikii.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha ukusanyaji wa mapato na kupunguza utegemezi wa bajeti yetu, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa fedha zote zinazohitajika kukusanywa kisheria, zinakusanywa. Kufanikisha hili, ni Serikali haina budi kuhakikisha kuwa Idara ya Mahakama inaharakisha mashauri ya Kodi ili kutopoteza thamani ya fedha inayoshtakiwa. Aidha, hatua kali za kisheria zichukuliwe kwa watu binafsi, taasisi na makampuni yanayokwepa kulipa kodi kwa makusudi ili kujinufaisha. Huyu bwana ana kiburi sana. Kamati inataka kujua hiki kiburi anakipata wapi na kwa nini Serikali haishughulikii, Kamati inasisitiza kiburi cha kampuni ya *TIOT* kishugulikiwe na vyombo vyote vya dola. Aidha, suala la misamaha ya kodi hlijashugulikiwa vya kutosha na Serikali.

Mheshimiwa Spika, fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii katika kujadili hesabu za Fungu hili, Kamati ilishauriana mambo mengi na Afisa Masuuli yaliyolenga kuinua utalii wa nchi yetu. Katika mjadala huo, Kamati ilijulishwa mambo kadhaa ambayo ni vema Bunge lako likajulishwa na kuazimia.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu haijaridhishwa na mwenendo wa utalii katika nchi yetu. Tanzania inazo rasilimali nyingi sana ambazo kama tukiwekeza vizuri na kuweka sheria madhubuti, Utalii waweza kuwa moja ya sekta zinazoongoza katika kuchangia pato la Taifa. Pamoja na kwamba takwimu zinaonesha kuwa utalii unachangia takriban asilimia 17 ya Pato la Taifa (*GDP*), bado mchango huo unaweza kuongezwa kama msukumo wa kutosha utawekwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuwekeza katika kufunza watumishi katika sekta hii ili kuweza kumudu ushindani na nchi zingine. Ukweli ni kwamba, huduma katika sekta ya utalii bado si ya kuridhisha. Kamati ilijulishwa kuwa Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa, inajenga chuo kikubwa cha utalii, kitakacholenga kuwafunza watumishi wa sekta ya utalii. Ni matumaini ya Kamati kuwa Chuo hicho kitasaidia kuboresha huduma za utalii nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uhifadhi na uendelezaji wa mapori ya akiba, Kamati yangu haikuridhishwa sana na mwenendo wa uendelezaji wa pori la akiba la Selous. Mapori haya yanaiingizia nchi mapato kwa njia ya uwindaji. Sheria inaruhusu mapori haya kubakiza kiasi cha makusanyo yake (50%) ili kuweza kujiendeleza. Hata hivyo, kiasi kinachobakizwa kimekuwa kikipungua mwaka hadi mwaka (*Kiambatisho i*). Kamati inaliomba Bunge lako kuona umuhimu wa kuishawishi Serikali kufanya jitihada za makusudi kuhakikisha kuwa mapori ya akiba yanaendelezwa na kupatiwa fedha kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ziara za Kamati. Katika kipindi cha kuanzia Aprili mwaka jana hadi Machi mwaka huu, Kamati yangu imefanya ziara mbalimbali za kikazi ndani na nje ya nchi. Ziara za ndani ya nchi zilikuwa ni za kikaguzi ambapo Kamati iliweza kufanya ukaguzi katika sehemu mbalimbali ambapo fedha za umma zimetumika.

Mheshimiwa Spika, ziara ya Kimafunzo nchini Uganda, Kamati yangu ilifanya ziara ya Kimafunzo ya siku nne nchini Uganda mwezi Oktoba Mwaka jana, ziara ambayo iliandaliwa na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ya Tanzania. Ziara hii ililenga kuwaelimisha Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yangu juu ya utaratibu Mpya wa uhamishaji wa pesa kwa njia ya kielectroniki (*electronic money transfers*) ambao Serikali inakusudia kuutumia hapa nchini ili kurahisisha mawasiliano ya kifedha. Nchi ya Uganda ilikwishaanza kutumia utaratibu huu na umekuwa na mafanikio makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, katika ziara hii, Kamati ilishawishika kuwa ipo haja kwa Serikali kuanza kutumia utaratibu huu katika ngazi zote ili kuepukana na utaratibu wa sasa wa kufanya malipo kwa hundi. Kwa kutumia utaratibu huu, Serikali itaweza kurahisisha na kuharakisha malipo baina yake na wateja wake wote na itapunguza sana matumizi ya karatasi na urasimu usio wa lazima. Kamati yangu ina maoni yafuatayo kuhusu Serikali ya Tanzania kuanza kutumia utaratibu wa kutuma Fedha kielektroniki:-

(i) Kwa kuwa *electronic money transfer* ni teknolojia mpya hapa nchini na kwamba inahitaji utaalam wa hali ya juu katika matumizi yake, Kamati inaikumbusha Serikali kuwa ipo haja ya kuandaa na kuendeleza mpango kabambe wa kuwaelimisha

wadau wote wa fedha kuhusu matumizi sahihi ya teknolojia hii. Aidha, ili kuweza kudhibiti hasara zozote na potevu zinazoweza kutokea kutokana na ugeni wa teknolojia hii katika nchi yetu, Serikali haina budi kuuanzisha mpango huu kwa awamu *(in phases*) ili kupima utekelezaji wake na kudhibiti kasoro zinazojitokeza kabla ya kuendelea na sehemu zingine.

(ii) Kwa kuwa teknolojia hii inatumia zaidi mifumo ya Kompyuta na kwa kuwa katika teknolojia ya kompyuta kuna wizi wa kisayansi ambao unaweza kufanyika, Kamati inashauri kuwa, Serikali ihakikishe na kujiridhisha kuwa ipo mifumo madhubuti ya kuzuia wizi unaoweza kufanyika kwa kuidanganya mifumo ya Kompyuta.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ziara ya Kamati Kukagua Ujenzi wa Barabara. Kamati yangu pia ilipata fursa ya kutembelea mradi wa ujenzi wa Barabara ya Marangu hadi Rombo Mkuu na Mwika hadi Kilacha yenye jumla ya Kilometa 96. Mradi huu ni kati ya Miradi kadhaa ya barabara ambayo imekumbwa na migogoro kati ya wakandarasi na Serikali na hivyo kusababisha gharama za ujenzi na muda wa kukamilisha ujenzi kuongezeka kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, Rombo Mkuu – Tarakea kipande hiki chenye urefu wa kilometa 29 kilijengwa kwa Ushirikiano kati ya *BADEA* (85%) na Serikali ya Tanzania (15%). Lengo la mradi huu ilikuwa kuinua kiwango cha barabara hii kutoka changarawe kwenda lami, katika ujenzi huu, *TANROADS* ilisaini mkataba na kampuni ya *M/S Prismo Badr JV (PBJV)* kwa ajili ya kujenga barabara hiyo lakini mkataba huu ulilazimika kukatishwa katika hatua za mwanzo kabisa za ujenzi kutokana na mkandarasi huyu kuvunja masharti ya mkataba. Gharama ya mradi mzima mpaka kumalizika kwake ilikisiwa kuwa shilingi 15,782,582,754. Mpaka siku mkataba na *PBJV* unakatishwa, Serikali ilikuwa imeshailipa kampuni hiyo Fedha za mwanzo shilingi 3,778,046,601. *TANROADS* iliingia mkataba na kampuni nyingine ijulikanayo kama *M/S General Nile Company for Roads and Bridges* (*GNRB*) ambayo ilikuwa na ubia na kampuni ya *DOTT Services,* Mkataba huu ulianza tarehe 26 Machi, 2008.

Mheshimiwa Spika, Marangu-Rombo Mkuu na Mwika Kilacha. Kipande hiki chenye urefu wa kilometa 32 kimefadhiliwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Norway (kupitia *NORAD*) na Serikali ya Tanzania. Kama ilivyo kwa kipande cha Tarakea-Rombo Mkuu, Mkataba kati ya *TANROADS* na mkandarasi (*PBJV*) ulikatishwa katika hatua za mwanzo na badala yake *GNRB* ikishirikiana na *DOTT Services* walipewa kazi hiyo. Katika ujenzi huu, mchango wa Tanzania upo katika usimamizi na ule wa kazi za ujenzi uligharamiwa na Serikali ya Norway (*Based on Payment Certificate*). Mpaka kufikia kipindi mkataba unasitishwa, *TANROADS* ilikwishailipa kampuni ya *PBJV* shilingi 3,778,046,601 kama malipo ya awali, gharama ya ujenzi katika barabara hii ilikadiriwa kuwa shilingi 23,292,981,752.98.

Mheshimiwa Spika, Tarakea-Rongai-Kamwanga, kipande hiki kilijengwa kwa fedha za ndani na hadi Kamati inatembelea eneo la Mradi, Kipande hiki kilikuwa kimekamilika. Jumla ya fedha zilizotumika katika mradi huu zilikuwa shilingi 14,418,430,562. Lengo la Mradi huu pia ilikuwa ni kuinua kiwango cha barabara kufikia kiwango cha lami. Mkandarasi katika ujenzi huu ilikuwa ni kampuni ya *M/S SIETCO* ya

China na Mhandisi Mshauri ikiwa ni kampuni ya *MS NORCONSULT A.S* ya Norway, kazi hii ilimalizika tarehe 30 Septemba, 2009.

Mheshimiwa Spika, yaliyojiri katika ziara ya kukagua mradi huu wa barabara, Kamati ilipata fursa ya kukutana na wataalam wa *TANROADS* Mkoani Kilimanjaro, Wakaguzi kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Wakandarasi waliopewa kazi hizi na baadhi ya wananchi wa sehemu za Miradi, Kamati yangu ilipokea maelezo kutoka pande zote hizi kuhusu hali ya miradi hii. Kutokana na maelezo ya pande zote hizi, Kamati ilibaini yafuatayo:-

(i) Kulikuwa na kasoro ndogo ndogo katika mkataba wa ujenzi hasa katika kuweka wazi baadhi ya mambo ambayo yangerahisisha ufuatiliaji wa mwenendo wa mradi. Kwa mfano Kampuni ya Prismo-Badr Joint Venture iliwasilisha mpango wake wa kazi kwa Mhandisi Mshauri ikionesha kuwa kazi zitaanza tarehe 3 Mei, 2007 na kwamba mpaka kufikia 20 Aprili, 2007 vifaa vya ujenzi vingekuwa eneo la mradi. Hata hivyo, program hiyo haikuonesha ni wapi hasa vifaa hivyo vingekusanywa, suala ambalo limepelekea ugumu katika kuhakiki mwenendo wa mradi. Mkataba haukumbana Mkandarasi kueleza ni wapi hasa vifaa vyake vitakusanywa.

(ii) Katika utendaji wa kiufundi katika miradi hii, imedhihirika kuwa kulikuwa na ucheleweshwaji katika kufikisha vifaa vya ujenzi eneo la mradi na pia upatikanaji wa wafanyakazi wenye sifa kama inavyotakikana katika mkataba. Kwa mujibu wa Mhandisi Mshauri, mpaka kufikia Februari, 2008 Mkandarasi alikuwa nyuma ya muda katika maeneo kadhaa kama ifuatavyo:-

(a) Watendaji muhimu katika mradi kama mhandisi wa vifaa, mhandisi wa barabara, Mhandisi wa mifumo ya maji na *surveyor* walikuwa bado hawajafika eneo la mradi kinyume na mpango wa kazi.

(b) Ukusanyaji wa vifaa ulikuwa nyuma kwa asilimia 67.

(c) Upatikanaji wa huduma kwa wahandisi hasa vifaa vya kazi, nyumba, maabara na magari ulilegalega kwa asilimia hamsini.

(iii) Hoja nyingine zilizohojiwa katika mradi huu ni kama ifuatavyo:-

(a) Malipo ya ziada ya Tshs 368,099,335 yaliyolipwa na *TANROADS* kwa kampuni ya *Prismo* kwa sababu ya kutumia *exchange rate* tofauti na ile ya kwenye mkataba.

(b) Malipo yasiyoidhinishwa kwa walinzi wa mitambo iliyozuiliwa ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri katika maeneo ya kambi za Mengwe na Mwika

(c) Malipo yasiyorejeshwa yaliyolipwa kwa Kampuni ya *Prismo*.

Kwa ujumla hali ya maendeleo ya mradi mpaka kufikia Februari, 2008 ilikuwa si ya kuridhisha sana. Mradi ulikuwa uko nyuma ya wakati na gharama za Mradi zilizidi makisio *(Cost Overrun*).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea mradi huu kwa nia ya kupata picha halisi ya mradi huu. Mkaguzi aliripoti kuongezeka sana kwa gharama za mradi huu, ikilinganishwa na ilivyokadiriwa awali. Sababu za wazi za kuongezeka kwa gharama hizi ni Mkandarasi kutofuata makubaliano ya mkataba, Serikali kuchelewa kutimiza majukumu yake ya kimkataba na makadirio ya gharama yasiyo na picha halisi ya kiasi cha kazi. Kamati ilitoa maelekezo kwa Mkaguzi wa *CAG* kufanya ukaguzi wa mkataba na kutoa taarifa kwa Kamati. Ukaguzi huo ulifanyika na mapendekezo yake yamekwishawasilishwa Serikalini kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, ziara ya Kamati katika Vikosi na Miradi ya Jeshi. Katika vipindi mbalimbali, Kamati yangu ilitembelea maeneo ya Vikosi vya Jeshi na Miradi iliyo chini ya Jeshi la Kujenga Taifa. Ziara hizi zilitokana na majadiliano na hoja za ukaguzi wakati wa Vikao vya Kamati na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na pia kati ya Kamati na Afisa Masuuli wa Mafungu ya Jeshi. Kamati ilitembelea Kikosi cha Jeshi la Maji Kigamboni, Miradi ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Shirika la Nyumbu na Shirika la Mzinga.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali, Wizara ya Ulinzi na JKT pamoja na mafungu ya majeshi yetu yamekuwa yakifanya vizuri katika hesabu zake. Hata hivyo, kumekuwa na matatizo makubwa ya kifedha katika mashirika yaliyo chini ya Jeshi hili kiasi cha kuyafanya yafanye kazi chini ya kiwango. Kamati inaamini kwa utaalam unaojionesha katika mashirika haya, yakiwezeshwa, yatatoa mchango mkubwa sana katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipotembelea Shirika la Mzinga, ilijionea jinsi shirika linavyotumia teknolojia ya magari katika kuhaulisha teknolojia za msingi za uhandisi wa mitambo na umeme. Katika kufanya hivyo, miradi mitatu ilibuniwa ikiwa ni pamoja na mradi wa gari la Nyumbu, mradi wa magari ya kivita na mradi wa magari ya zimamoto. Mabadiliko ya Sera za nchi hususan ya Serikali kujiondoa katika uendeshaji wa viwanda vya uzalishaji yaliilazimu mzinga kutafuta wawekezaji, juhudi ambazo zinaendelea mpaka hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa, Nyumbu imekuwa ikipokea ruzuku toka Serikalini kwa kiwango tofauti ambapo mwaka wa fedha 2003/04 ilipewa Ths 240 milioni na mwaka wa fedha 2008/09 ilipata Tshs 600 milioni. Mapato ya Mauzo ya Huduma kwa miaka hii miwili kwa mfano yalikuwa 2003/04, Tsh 180 milioni na 2008/09, Tsh 405 milioni. Ukilinganisha ruzuku na mapato, ni wazi kuwa Shirika bado halifanyi vizuri. Katika hili Kamati ililishauri shirika kuongeza jitihada katika kujitangaza na kufanya kazi kibiashara ili kuweza kujiendesha kibiashara. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuona uwezekano wa kuyawekea dhamana mashirika haya ya Jeshi ili yaweze kukopa na kufanya shughuli zake kibiashara. Zana zinazotengenezwa katika mashirika haya, hususan Nyumbu, yanaweza sana kusaidia katika kukuza kilimo.

Mheshimiwa Spika, ikiwa katika Shirika la Mzinga, Kamati pia ilifurahishwa sana na utaalam na kujituma kwa wanashirika. Kama ilivyo kwa Nyumbu, Shirika hili pia linahitaji sana msaada wa Serikali katika kujiendesha. Kamati inaamini, kama Serikali itafanya jitihada za makusudi kuwekeza katika mashirika ya Kijeshi kama ilivyo kwa nchi zingine, mchango wa mashirika haya katika uchumi utakuwa mkubwa sana. Hivyo Serikali ilione hili kama changamoto katika mipango yake.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilifanya ziara za kikaguzi katika baadhi ya Hospitali za hapa nchini ili kuweza kujionea miradi mbalimbali inayotekelezwa na *RAS* kwa mafungu wanayopewa. Vilevile Kamati ilitembelea baadhi ya Hospitali za Taasisi mbalimbali ili kuweza kulinganisha utendaji katika sekta hii. Hii ni katika kuunga mkono juhudi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) katika kufanya ukaguzi wa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, katika Hospitali ya Mkoa wa Morogoro, Kamati iliridhishwa na jitihada zinazofanywa na Uongozi wa Mkoa pamoja na ule wa Hospitali. Kwa sasa kuna mradi Mkubwa wa Upanuzi wa Hospitali unaendelea na mpaka Kamati ilipotembelea Hospitali, mradi ulikuwa umefikia hali ya kuridhisha sana. Hata hivyo, bado Hospitali hii kama zilivyo Hospitali nyingi nchini ina tatizo kubwa la kifedha. Kamati ilijulishwa kuwa Watumishi pekee wanaidai Serikali jumla ya Tshs 287,183,659.00 zikijumuisha madeni ya likizo, matibabu, uhamisho, mafunzo, posho na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia hairidhishwi na mwenendo wa Ununuzi Dawa toka MSD. Pamoja na kazi na jitihada nyingi zinazofanywa na MSD katika utendaji wake, bado imeripotiwa kuwa kikwazo sana karibu katika hospitali zote yaliyotembelewa na Kamati. Fedha nyingi zimekuwa zikipelekwa *MSD* toka vyanzo mbalimbali lakini upatikanaji wa Dawa na vifaa umekuwa unalegalega. Ni vema Serikali ikakaa na *MSD* kuona ni jinsi gani wanaweza kutatua kero hizi toka katika mahospitali yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Hospitali Binafsi, Kamati yangu ilitembelea Hospitali inayoendeshwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na Kanisa Katoliki, Hospitali ya Bugando. Katika Hospitali hii, Kamati ilijionea miradi mbalimbali ya upanuzi inayoendeshwa kwa ushirika kati ya Kanisa na Serikali. Kamati yangu ilifurahishwa sana. Suala la Msingi linalohitaji kuchukuliwa na Serikali ni suala la ruzuku. Kumekuwa na tatizo la ruzuku ya matumizi ya Kawaida (*OC*). Kiasi kinachohitajika na kinachotolewa ni tofauti sana. Kwa mfano, kwa mwaka wa Fedha 2008/2009, fedha zilizoombwa zilikuwa Tshs 2,213,695,000, fedha iliyotolewa ilikuwa Tshs 984,090,000 sawa na takriban asilimia 44.5. Kwa mwaka huu wa fedha, fedha iliyoombwa ilikuwa Tshs 3,686,768,600 na fedha zilizotolewa ni Tshs 984,090,000 sawa na asilimia 26.7.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo pia na tatizo la watumishi kutolipwa mishahara inayostahili kulingana na vyeo vyao. Kamati ilipotembelea Hospitali hii, kulikuwa na kesi za madai ya mapunjo yanayofikia Tshs 60.3 Milioni kwa kipindi cha kuanzia Julai hadi Machi 2009. Aidha, Uongozi wa Hospitali uliijulisha Kamati kuwa Hospitali

inakabiliwa na tatizo kubwa la wadaiwa sugu ambapo baadhi ya Taasisi za Serikali zimekuwa zikipata Huduma ya Hospitali hii bila kulipa madeni kikamilifu. Madeni hayo na wadeni wake kwenye mabano ni Jeshi la Wananchi (Tshs 80,600,000), Jeshi la magereza (Tshs 29,600,000) na pia iliyokuwa Kampuni ya Simu za Mikononi ya *TRITEL* (Kiasi cha Tshs 31.6 Bn). Kamati inaishauri Serikali kujipanga ili kuweza kulipa madeni hayo, ili kuipunguzia matatizo ya hospitali hii ambayo inasaidia sana wananchi wa Kanda ya Ziwa takribani mill 15.

Mheshimiwa Spika, tuliweza pia kutembelea Hospitali ya Mkoa wa Mwanza, Sekou Toure. Katika Hospitali hii Kamati ilikagua mradi wa upanuzi wa Hospitali hii unaofanywa kwa fedha za Mkoa. Kamati ilijulishwa kuwa katika mwaka wa fedha 2008/2009, Serikali ilitenga shilingi 600 milioni kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kuboresha huduma zitolewazo katika hospitali hiyo. Maeneo yaliyopangwa kushughulikiwa ni pamoja na kununua jenereta la umeme, kujenga wodi ya wagonjwa wa akili, kukarabati wodi za wagonjwa na kupanua Ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa. Wakati Kamati ilipotembelea eneo la mradi, kazi ilikuwa ikiendelea vizuri, ingawa ilikuwa nyuma ya muda uliotarajiwa kukamilika.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilishtushwa na taarifa iliyotolewa na uongozi wa Hospitali kuwa kuna upungufu mkubwa sana wa Madaktari na Madaktari Bingwa katika hospitali hii. Tatizo hili linatokana na maslahi duni ambayo madaktari wetu wanapata na hivyo kulazimika kuhamia Hospitali binafsi. Kamati ilijulishwa kuwa kuna uhaba mkubwa wa Nyumba za makazi ya madaktari na kiwango cha posho ya makazi wanayopewa hakikidhi mahitaji ya soko la nyumba hivi sasa. Kamati inaiomba Serikali kufanya jukumu la makusudi kurekebisha kasoro hii.

Mheshimiwa Spika, katika kikao chake na Afisa Masuuli wa Wizara ya Afya, Kamati ilijulishwa kuwa wapo Madaktari waliofudhu hivi karibuni ambao wanatarajiwa kusambazwa kwenye mahospitali yetu yote yenye upungufu. Kamati inapongeza jitihada hizi, lakini inaikumbusha Kamati kuwa, ili Madaktari hawa waendelee kuwepo katika vituo vyao vya kazi, Serikali haina budi kuwaboreshea maslahi yao, vinginevyo, wataondoka tena.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kukagua Hospitali ya Mawenzi-Moshi ya Mkoa wa Kilimanjaro. Katika hospitali hii, Kamati ilielezwa tatizo la ufinyu wa bajeti, ambapo kwa wastani hospitali inahitaji shilingi 120,000,000 kwa robo mwaka, lakini hospitali imekuwa ikipata takriban shilingi 94,000,000 kwa robo mwaka. Kama ilivyo hospitali nyingine nyingi za Serikali, hospitali hii pia ina upungufu wa vifaa tiba, majengo na madawa.

Mheshimiwa Spika, kiujumla bado nchi yetu haijawekeza vya kutosha katika sekta ya afya na Kamati inaamini kama fedha za kutosha zitatengwa katika kuhudumia sekta hii, sekta zingine zitaweza kuendelezwa na kuimarishwa vizuri zaidi na kwa uhakika. Bila afya njema wananchi watashindwa kufanya kazi za kilimo, maofisini, viwandani na hata watoto wetu mashuleni. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa sekta hii inapewa kipaumbele ili kuwezesha juhudi nyingine za maendeleo kama vile “kilimo kwanza” kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati baada ya kupitia Hesabu zilizokaguliwa za Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea, Kamati yangu imebaini mapungufu kadhaa katika baadhi ya mafungu, mafanikio katika mafungu mengine na changamoto kwa mafungu mengi. Kama nilivyoeleza katika sehemu iliyotangulia ya matokeo ya ukaguzi, bado Serikali ina changamoto kubwa katika kuhakikisha kuwa fedha za umma zinatumika vema, kwa matumizi yaliyokusudiwa lakini pia kwa kufuata sheria na taratibu zilizowekwa. Kamati yangu ina maoni na mapendekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Uchumi iongeze juhudi katika kusimamia dhamana inazotoa kwa taasisi mbalimbali ili kuhakikisha kwamba Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada inazingatiwa kabla na baada ya kutoa dhamana na kwamba taasisi hizo zilizowekewa dhamana zinalipa mikopo hiyo iliyodhaminiwa kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri pawepo na mawasiliano mazuri kati ya taasisi na idara zote zinazoshughulika na usimamizi wa Deni la Taifa. Kuna umuhimu pia wa kuwepo kwa taasisi moja inayoshughulikia usimamizi wa Deni la Taifa.

Mfumo wa fedha na uchumi (*Monetary and Fiscal Policy*) wa nchi inabidi usimamiwe vema mfano kwa kutumia fedha za ziada katika uchumi kugharimia pengo la matumizi ya Serikali (*Government budget deficits*) na hivyo kupunguza kiwango cha fedha zinazoingia nchini kwa njia ya mikopo ambayo inaongeza gharama za riba za mikopo hiyo na ile ya kupunguza ziada ya fedha katika mfumo wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu pawe na mkataba wa kiutendaji kati ya Hazina na Benki Kuu ambao utaainisha majukumu kati ya Hazina na Benki Kuu. Mkataba huo pia ni vema ukaweka wazi uhusiano wa kiuwakala kati ya Hazina na Benki Kuu ili kuifanya Benki Kuu iendelee na majukumu yake ya kuishauri Serikali na kuiacha Hazina kuchukua maamuzi ya kusimamia Deni la Taifa kwa uhuru zaidi.

Ili kudumisha maadili ya kiutendaji (*credibility)* ya pande hizi mbili, ni muhimu usimamizi wa Deni la Taifa ukawa nje ya Benki Kuu, vinginevyo, Benki Kuu na Hazina waaandae mpango madhubuti wa kuhakikisha kuwa shughuli za usimamizi wa Deni la Taifa ikiwa ni pamoja na kuendesha minada ya dhamana za Serikali unafanyika kwa umakini zaidi bila kuathiri majukumu ya msingi ya taasisi hizi mbili.

Ni muhimu sheria ya Mikopo, Dhamana za Serikali na Misaada (kama ilivyorejewa 2004) ikafuatwa ipasavyo katika mchakato mzima wa kukopa ili kuhakikisha kuwa Deni la Taifa linakuwa katika kiwango ambacho Serikali itaweza kumudu kulipa bila kuathiri huduma muhimu za jamii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza utaratibu wa kupitisha fedha za Halmashauri kwa *RAS* bila *RAS* kuwa na mamlaka nazo, ila wajibu nazo uangaliwe upya ili kuona kama kuna utaratibu mbadala. Kwa kuwa Wakurugenzi wa Halmashauri na Manispaa ndio hasa watumiaji wa fedha hizi, Kamati inashauri Katibu Tawala wa Mkoa awajibike kwa fedha zile tu zinazotumiwa na sekretarieti ya Mkoa na ndizo

atakazowajibika kuhojiwa akija mbele ya Kamati ya Hesabu za Serikali, kuliko ilivyo sasa kwamba anapata hoja za ukaguzi kwa fedha ambazo hajawahi kuziona.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu haijaridhishwa na mwenendo wa bajeti yetu hasa katika bajeti ya maendeleo. Katika mafungu mengi tuliyoyakagua, Hesabu zao zinaonesha kuwa bajeti ya maendeleo hasa zile zinazotegemea fedha za wahisani zimekuwa hazitekelezeki kwa sababu fedha hizo aidha, zinachelewa kufika, zinafika kidogo sana ama hazifiki kabisa. Kwa sababu hii miradi mingi imekuwa ikikwama, ikichelewa ama kutotekelezeka kabisa, kuliko kuwa na bajeti ambayo haina uhakika, Kamati inashauri kuwa masuala yote muhimu ya kimaendeleo yatengewe fedha za ndani ama zile za nje zenye uhakika. Aidha, Kamati pia inashauri serikali kutoingiza katika mahesabu ya bajeti zile ahadi ambazo hazijathibitishwa ili kuepuka kuwapa wananchi matumaini yasiyotekelezeka.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, Kamati yangu inaliomba Bunge lako Tukufu kukemea vikali matumizi ya Serikali yanayofanyika nje ya utaratibu wa kibajeti, isipokuwa pale unapofanyika kwa mujibu wa sheria. Kamati inapongeza hatua ya hivi karibuni ya Serikali kuleta mbele ya Bunge lako Tukufu bajeti ndogo ya Serikali (*supplementary budget*). Hii inaonesha kuwa Serikali inatambua nafasi ya Bunge katika nchi hii. Bunge hili ndilo lenye mamlaka ya kuidhinisha matumizi ya fedha na si vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu katika kazi zake, imejulishwa na kujionea hali halisi ilivyo kwa baadhi ya nyumba za makazi na pia Ofisi za Maafisa Waandamizi wa Serikali, hususan viongozi wa Mikoa. Pamoja na ukweli kwamba zoezi la uuzaji wa nyumba za Serikali limeleta usumbufu kiasi fulani kwa sehemu nyingi za nchi hii kwa maafisa waandamizi wanaohamishiwa katika mikoa isiyo na nyumba mbadala, Kamati yangu imebaini kuwa hakuna kiwango (*standard*) maalum kinachotumika kujenga majengo ya Serikali, hususan maofisi ya Wakuu wa Wilaya na Mikoa. Katika ziara zake Kamati haikuridhishwa na utofauti mkubwa uliopo katika majengo ya Ofisi za wakuu wa Wilaya Mpya za Mvomero na Ilemela. Pamoja na kwamba Kamati haiukuridhishwa na ubora wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, hali ilikuwa mbaya zaidi pale Kamati ilipotembelea majengo yaliyojengwa kwa ajili ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ilemela. Majengo haya yalikuwa ni tofauti kabisa kwa ukubwa na ubora.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na mfano huo mdogo, ambao unatoa picha ya jinsi hali ilivyo hata kwa sehemu nyingine, Kamati yangu inashauri Serikali iweke kiwango maalum ambacho kitatumika katika kujenga majengo haya. Hii itaepusha mambo mengi, ikiwa ni pamoja na gharama zisizo za lazima, ubora wa majengo na usawa pia. Aidha, Kamati inarejea rai iliyoitoa katika taarifa yake mwaka jana kuhusu umuhimu wa kutumia samani za hapa hapa nchini. Bado suala hili halijatekelezwa, pamoja na kuridhiwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kumekuwa na matatizo kadhaa katika sheria za fedha yanayokwamisha shughuli mbalimbali za miradi na maendeleo kwa ujumla na kwa

kuwa Serikali imeahidi kurekebisha sheria hizo ili kutatua tatizo hili, Kamati inashauri mchakato huo uharakishwe. Mabadiliko ya sheria hizi ni muhimu katika kuleta tija katika matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inarejea rai ya *CAG* kuwakumbusha Maafisa Masuuli wote kuhakikisha kuwa wanafuata Sheria ya Manunuzi Namba 21 ya mwaka 2004 katika shughuli zao. Hata hivyo, Kamati inapendekeza kuwa ipo haja ya kuiangalia upya sheria hii kwa kuwa inakwaza sana katika utekelezaji wake kwa baadhi ya maeneo. Hali kadhalika, Kamati inakumbusha haja ya kurejea kanuni za manunuzi kwa Balozi zetu (*Foreign Service regulations*) kwa sababu zinazotumika sasa zimepitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la dawa na vifaa vya afya, Kamati haijaridhishwa na utendaji wa *MSD* hasa katika kuhakikisha kuwa vifaa na dawa zinapatikana kwa wakati. Kamati inapendekeza kuwa utaratibu wa fedha za *OC* kwa ajili ya manunuzi ya dawa kupelekwa moja kwa moja MSD usitishwe mara moja ili mamlaka husika ziwe na uwezo wa kununua dawa toka vyanzo vingine pale dawa na vifaa vinapokosekana *MSD.*

Mheshimiwa Spika, Kamati haijaridhishwa na taratibu zilizopo sasa za utoaji, usimamizi na ufuatiliaji wa Dhamana za Serikali (*Government Guarantees*) kwa wanaostahili. Ushauri kwa Serikali kuhusu hili ni kwamba, sheria inayosimamia *guarantees* ifuatwe na uwekwe utaratibu mzuri wa kufuatilia utendaji wa yale mashirika, makampuni ama taasisi zilizo na *guarantee* ya Serikali ili kuhakikisha kuwa fedha za walipa kodi hazipotei. Kwa hali ilivyo sasa, inasikitisha kuona kwamba, fedha zinatolewa kama vile Hazina mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa imeonekana kuwa majeshi yetu yana ujuzi na utaalam mkubwa katika suala la uzalishaji vitu mbalimbali, Kamati inashauri jitihada za makusudi zifanyike katika kuyapatia mtaji mashirika yaliyo chini ya Jeshi la Wananchi kama vile Mzinga na Nyumbu ili kuweza kuinua utaalam wake kuyawezesha kufanya kazi kibiashara. Kamati inaamini kuwa, mashirika haya yakiwezeshwa, yatalisaidia Jeshi letu kupunguza utegemezi kwa Serikali na pia kuchangia katika kukua kwa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu suala la uagizaji wa Magari ya Serikali nje ya nchi, Kamati inashauri kurejewa kwa utaratibu wa zamani ambapo muagizaji mmoja anachaguliwa kuagiza kwa niaba ya Serikali kuliko ilivyo hivi sasa. Utaratibu wa sasa wa kutangaza zabuni kwa ajili ya uagizaji wa magari unaleta shida sana katika kuchagua aina ya magari yanayofaa kwa nchi yetu na pia upatikanaji wa vipuri kwa ajili ya magari hayo.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, napenda kutumia fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali kuhusu utekelezaji wa shughuli zake kwa mwaka 2009 na 2010.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine naomba kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika, Mheshimiwa Anne S. Makinda; Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, na Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, kwa

uongozi wenu wa pamoja. Nawatakia baraka za Mwenyezi Mungu katika kutekeleza kazi nzito na muhimu ya kuliongoza Bunge.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa kutekeleza majukumu mbalimbali yaliyoihusu Kamati hii kwa moyo na uadilifu mkubwa. Aidha, nawapongeza kwa kushiriki kikamilifu katika maandalizi ya Taarifa hii na kunipa heshima ya kuiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Kamati katika kutekeleza kazi zake ilikuwa ikisaidiwa na Maafisa Waandamizi kutoka Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Mhakiki Mkuu wa Mali za Serikali. Nawashukuru sana kwa mchango wao wa kitalaam.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dr. Thomas D. Kashillilah kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, nampongeza Katibu wa Kamati hii ndugu Michael Chikokoto kwa kuratibu shughuli zote za Kamati hii kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii na kuijadili na hatimaye ipitishe mapendekezo ya Kamati kama yalivyoandikwa naomba *Hansard* ichukue kama tulivyoandika kwenye taarifa yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Namwita sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa.

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kabla sijasema na kutoa maoni ya Kamati kuhusu Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa kazi za Kamati kwa mwaka 2009/2010 naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa, lakini pia niwashukuru sana wananchi wangu wa Wilaya ya Karatu ambao ndio walionipa heshima ya kuweza kusimama mbele ya Bunge lako hili Tukufu na hasa kwa kuendelea kuniunga mkono katika shughuli zetu za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, shughuli zetu zinaongozwa kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pamoja na sheria mbalimbali, lakini kwa sababu ya muda tuliiandaa hotuba yetu tukijua tunazo dakika 60

kama ilivyo Katiba kwa ajili ya muda ni nusu saa basi naomba taarifa yangu iandikwe katika *Hansard* jinsi ilivyo isipokuwa nitapita yale maeneo ambayo ni muhimu tu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 114 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2007, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa juu ya Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iliyowasilishwa Bungeni mwezi Machi, 2009 kuhusu Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha unaoishia 30 June, 2008.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Ibara ya 96 (1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, inayoipa Bunge idhini ya kuunda Kamati za namna mbalimbali kwa kadri litakavyoona inafaa katika utekelezaji bora wa madaraka yake na kutumia Kanuni za Bunge kufafanua muundo na shughuli za Kamati hizo, naomba nielezee kwa kifupi majukumu ya Kamati yangu kama yalivyoainishwa kwenye Nyongeza ya Nane, Kifungu Na.12 chini ya Kanuni ya 115 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2007 kama ifuatavyo:-

(a) Kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za Serikali za Mitaa yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

(b) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati kwa nia ya kuondoa matatizo hayo; na

(c) Kutoa mapendekezo na ushauri kwa Serikali za Mitaa kuhusu matumizi mazuri ya fedha ili kuhakikisha kwamba tatizo la matumizi mabaya ya fedha linapungua katika Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu hayo, Kamati ilifanya kazi zake katika namna kuu tatu (3) kama ifuatavyo:-

(a) Kukagua Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijadili na kuchunguza vitabu vya Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa za mwaka wa Fedha wa 2007/2008 zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Aidha, kazi hiyo imefanywa kwa Halmashauri zote 133 zilizokuwepo katika mwaka unaohusika na ukaguzi.

(b) Kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha ukaguzi wa miradi unafanywa kwa ufanisi, Hesabu za Halmashauri husika zilijadiliwa kwanza na ndipo miradi ya maendeleo ilikaguliwa bila kujali kama zimepata Hati inayoridhisha au isiyoridhisha na ilithibitika kuwa Halmashauri kupata Hati inayoridhisha, hakumaanishi kwamba hakuna matumizi mabaya ya fedha. Niseme tu, utaratibu huu unafaa zaidi kwani umeiwezesha Kamati

kuthibitisha usahihi wa kilichoandikwa vitabuni na hali halisi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka unaohusika na ukaguzi, Kamati iliweza kutembelea na kufanya ukaguzi wa thamani ya miradi ya maendeleo, katika Halmashauri za mikoa 17 kati ya 21, ambayo ni Mara, Arusha *(isipokuwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Longido)*, Manyara *(ilitembelea Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro tu)*, Mkoa wa Iringa *(isipokuwa Halmashauri za Wilaya za Ludewa na Mufindi)*, Kagera, Kigoma, Rukwa, Mbeya, Tanga, Shinyanga, Singida, Dodoma, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Pwani na Dar es Salaam. Hivyo, Kamati imeweza kukagua miradi ya maendeleo katika Halmashauri 93 ambazo ni sawa na asilimia 70% ya Halmashauri zote 133 zilizokuwepo katika Mwaka wa Fedha wa 2007/2008. Aidha, napenda kutoa shukurani na pongezi kwa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutembelea na kukagua miradi ya Halmashauri nyingi zaidi kwa mwaka huu ambazo ni sawa na ongezeko la asilimia 28.8% ukilinganisha na zilizotembelewa katika mwaka wa kazi uliopita.

(c) Kujenga uwezo wa Wajumbe kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Katika kuzingatia umuhimu wa Wajumbe wa Kamati kupata mafunzo mbalimbali kama nyenzo muhimu katika utekelezaji wa majukumu yao ipasavyo, Wajumbe walipata fursa mbalimbali za kuhudhuria mafunzo na warsha katika nyakati tofauti kama ifuatavyo:-

(i) Mafunzo yaliyoandaliwa na TAMISEMI kuhusu *International Public Sector Accounting Standards (IPSAS)*. Mafunzo hayo yalikuwa na lengo la kuwaelimisha Waheshimiwa Wajumbe kuhusu matumizi sahihi ya Kanuni za kihasibu za Kimataifa katika ufungaji wa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa na yalifanyika Dar es Salaam tarehe 17-18 Oktoba 2009;

(ii) Mafunzo yaliyoandaliwa na Wizara ya Fedha na Uchumi (*MOFEA*) kuhusu Maboresho katika Mfumo wa Ukaguzi wa Ndani katika Sekta ya Umma. Mafunzo haya yalikuwa na lengo la kuwaelewesha Wabunge kuhusu dhamira ya Serikali kuhusiana na maboresho hayo na vilevile kuwawezesha Wabunge kutoa ushauri wenye lengo la kuboresha mfumo husika. Aidha, mafunzo hayo yalifanyika kwa pamoja na Kamati za Hesabu za Serikali (*PAC*), Hesabu za Mashirika ya Umma (*POAC*) na Fedha na Uchumi, mnamo tarehe 11-12 Novemba 2009, Dar es Salaam; na

(iii) Mafunzo yaliyoandaliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (*CAG*) akishirikiana na Benki ya Dunia kuhusu Changamoto zinazoikabili Serikali katika Usimamizi na matumizi ya fedha za Umma *(Public Expenditure Forum)*. Mafunzo hayo yalihusisha Kamati za Bunge za Kiuchunguzi, Kamati ya Fedha na Uchumi, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge, Wafadhili toka Nje ya Nchi, Wawakilishi toka TAMISEMI na Benki ya Dunia, na ilifanyika Dodoma, tarehe 13 - 14 Februari 2010.

Mheshimiwa Spika, kila Halmashauri iliyofika mbele ya Kamati iliwasilisha Taarifa zifuatazo:-

(a) Taarifa ya Wilaya (*District Profile*) yenye Maelezo ya shughuli zote zilizomo katika Halmashauri ya Wilaya.

(b) Taarifa ya Mapato na Matumizi halisi inayoonyesha pamoja na Makisio kwa muda wa miaka mitatu,(2005/2006,2006/2007 na 2007/2008).

(c) Taarifa na michanganuo ya kina ya Mapato na Matumizi ya Miradi yote inayopata Ruzuku ya Serikali, Wahisani, Halmashauri na Wananchi (kama Mfuko wa Barabara (*Road Fund*), Mfuko wa Maendeleo (*Development Fund*), Mfuko wa Afya wa Pamoja (*Basket Fund*), *MMEM, Irish Fund, DANIDA, TASAF, PADEP* na kadhalika. Pamoja na Taarifa ya Uchambuzi wa Matumizi ya Miradi yote iliyomo kwenye Halmashauri ikionyesha salio anzia, fedha iliyopokelewa, fedha iliyotumika na salio ishia kwa mwaka husika.

(d) Majibu ya hoja za ukaguzi yaliyohakikiwa na Wakaguzi na Majibu ya hoja za Kamati ya *LAAC* yaliyowasilishwa kwa kila Halmashauri wakati wa vikao vya nyuma na kuhakikiwa na Wakaguzi.

*(e) Certificate of Balance, Bank Reconciliation* na *Bank Statement* kwa kila Akaunti ya Halmashauri iliyoko Benki.

*(f) Endorsed Bill of Quantities* (BOQs), *Engineers estimates*, Hati za malipo, *Certificates of Completion* na Mikataba yenye saini ya Mwenyekiti wa Halmashauri kwa mwaka unaohusika na Ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na taarifa hizo, Kamati imedhamiria kwa kaguzi zijazo kupitia na kujadili Taarifa za Wakaguzi wa Ndani wa Halmashauri zinazotolewa kila robo mwaka, hususan baada ya Wizara ya Fedha na Uchumi kukamilisha mchakato unaoendelea wa kuboresha mfumo wa Ukaguzi wa Ndani kwa lengo la kuimarisha usimamizi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha na mali za Umma.

Mheshimiwa Spika, yaliyojitokeza katika uchambuzi wa hesabu. Kabla sijaainisha yaliyojitokeza katika uchambuzi wa vitabu vya Hesabu vya Halmashauri, naomba nigusie kwa ufupi hali ya uwajibikaji na utendaji kazi katika Halmashauri zetu. Kwa ujumla, hali ya uwajibikaji na utendaji kazi inaridhisha, ikizingatiwa kuwa Watendaji wa Halmashauri wanatekeleza wajibu wao kwa kuzingatia taratibu, Kanuni na Sheria zilizowekwa, ingawa bado wapo baadhi wanaorudisha nyuma maendeleo ya Halmashauri kwa kutozingatia maadili ya kiutumishi na kuweka mbele maslahi yao.

Kwa mfano, matumizi mabaya ya fedha na utayarishaji wa taarifa za uongo uliofanywa na baadhi ya Watendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kwa muda mrefu mpaka Serikali ilipong'amua kufuatia ukaguzi maalum uliofanyika na kuwachukulia hatua za kisheria Watendaji waliohusika. Aidha, tunaipongeza Serikali kwa hatua kali ilizozichukua.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2007/2008, mwelekeo wa ufungaji na uwasilishaji wa Hesabu za Halmashauri kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali umezidi kuwa mzuri ukilinganisha na mwaka wa ukaguzi uliopita, kwa maana Halmashauri zote 133 (100%) ziliwasilisha taarifa za mwaka za fedha ilipofika tarehe 30 Septemba, 2008 ambalo ni hitaji la kisheria. Hata hivyo, Halmashauri 14 zilichomoa taarifa zao na kuwasilisha taarifa za fedha zilizorekebishwa kati ya Novemba, 2008 na Februari, 2009 na kuacha Halmashauri 118 ambazo ni sawa na asilimia 89% (ongezeko la 9%) zikizingatia uwasilishaji wa hesabu kwa mujibu wa Sheria.

Kamati inapongeza jitihada na juhudi zilizofanywa na Halmashauri katika ufungaji wa hesabu na kuwasilisha vitabu hivyo kwa Wakaguzi kwa wakati uliowekwa kwa mujibu wa Sheria. Aidha, Kamati inaikemea tabia ya baadhi ya Halmashauri kuwasilisha Taarifa na hatimaye kuziondoa kwa lengo la kufanya marekebisho nje ya muda uliowekwa kisheria, kwani kitendo hiki si tu kinakiuka sheria bali pia huifanya Ofisi ya Ukaguzi ya Taifa (*NAO*) kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kwa wakati unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, kufuatia vitabu vya hesabu vinavyotayarishwa na Halmashauri kwa ajili ya kujadiliwa na Kamati, ningependa kuipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu kwa kutayarisha Kitabu kizuri cha Hesabu katika mwaka husika wa ukaguzi. Ni vema Halmashauri zingine zikaiga mfano huo kwa lengo la kuboresha zaidi utayarishaji wa taarifa za Hesabu kwa kuzingatia maelekezo ya Kamati na Wakaguzi.

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi wa Hesabu za mwaka wa fedha wa 2007/2008, unaonyesha kushuka kwa matokeo ya Hati za Ukaguzi ukilinganisha na ukaguzi wa mwaka 2006/2007. Kati ya Halmashauri 133 zilizokuwepo katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, Halmashauri 72 sawa na asilimia hamsini na nne (54%) zilipata Hati inayoridhisha/Hati Safi ambapo katika mwaka wa fedha wa 2006/2007, Halmashauri 100 sawa na asilimia themanini na moja (81%) zilipata Hati inayoridhisha/Hati Safi. Aidha, kati ya Halmashauri 133 zilizokaguliwa, Halmashauri 61 sawa na asilimia arobaini na sita (46%) zilipata Hati isiyoridhisha/Hati zenye mashaka katika mwaka 2007/2008 ukilinganisha na Halmashauri 24 sawa na asilimia kumi na tisa (19%) tu katika mwaka 2006/2007. Hivyo, Kamati itaendelea kuzibana Halmashauri kwa njia ya kukagua Hesabu na miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa lengo la kuhakikisha zinapata Hati Safi kwa miaka ijayo.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa miradi ya maendeleo umedhihirisha kuwa matokeo ya hati za ukaguzi si kigezo toshelezi katika kupima hali ya matumizi ya fedha za umma katika Halmashauri. Serikali inabidi iendelee kukagua Hesabu na kutembelea

miradi husika kwa lengo la kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma. Kama nilivyoainisha hapo awali, baadhi ya Halmashauri zenye hati inayoridhisha zimetumia fedha vibaya na kuandaa Hesabu ambazo hazilingani na hali halisi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kila Halmashauri inapewa sababu zilizoifanya ipate hati isiyoridhisha. Hivyo ni imani ya Kamati kwamba, Halmashauri zote zilizotajwa kwenye Taarifa ya Mwaka 2007/2008 ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa zilipata Hati isiyoridhisha zitakuwa zimejirekebisha ipasavyo na zile zilizopata Hati Safi zitaendelea kudumisha umakini huo katika matumizi na utayarishaji wa Taarifa za matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, katika Hesabu za mwaka 2007/2008, mapendekezo na maoni mbalimbali yametolewa na Kamati pamoja na Wakaguzi kuhusu masuala muhimu yaliyojitokeza katika ukaguzi uliofanyika miaka iliyopita hususan yanayohusu usimamizi wa fedha za Halmashauri. Halmashauri nyingi zimeonyesha juhudi ya kutekeleza maoni ya Ukaguzi na Kamati. Hata hivyo, kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, hadi kufikia Juni, 2008 Halmashauri 112 zilikuwa hazijatekeleza masuala yanayotokana na ukaguzi wa miaka ya nyuma yanayofikia kiasi cha Sh. 32,903,395,306.

Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa ndiyo ilikuwa na kiwango kikubwa zaidi cha Sh. 6,813,262,872 ya masuala ambayo yalikuwa hayajajibiwa. Kamati yangu imekuwa ikitoa ushauri na maagizo mbalimbali kwa Halmashauri ili ziweze kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza haraka katika kuboresha mfumo wa udhibiti wa ndani na usimamizi wa rasilimali za Halmashauri. Hulka ya kutoshughulikia taarifa au mapendekezo ya Kamati inaweza kusababisha kujirudia kwa dosari zilizojitokeza miaka ya nyuma. Aidha, hali hii ni kiashiria cha kutokuwepo kwa umakini na uwajibikaji kwa Menejimenti za Halmashauri husika, hivyo Serikali haina budi kuchukua hatua kali kwa Watendaji wanaoshindwa kushughulikia masuala ya ukaguzi yaliyojitokeza katika miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi umebaini kuwa bado kuna mapungufu katika mfumo wa ulipaji wa mishahara wa Serikali Kuu na wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwani kwa mwaka unaohusika na ukaguzi, jumla ya Sh. 178,066,130 toka Serikalini zililipwa kwa Watumishi hewa ambao aidha wameshafariki dunia, wamefukuzwa kazi, wameacha kazi au hata kutoroka kazini. Sambamba na hilo, kwa mujibu ya Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, imebainika kuwa baadhi ya Watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa hula njama na wale wa Serikali Kuu katika kujiongezea mishahara isivyo rasmi kwa kujipandisha vyeo isivyo halali.

Aidha, kufuatia ukaguzi uliofanyika jumla ya Sh. 881,996,748 za mishahara isiyolipwa hazikurudishwa Hazina na Halmashauri husika jambo ambalo ni kinyume na matakwa ya Sheria ya Fedha. Kufuatia kuthibitika kwa mapungufu hayo, ni kielelezo kuwa juhudi za makusudi zinabidi zielekezwe kwenye kuimarisha udhibiti wa matumizi ya mishahara ya watumishi wa umma kwani kinyume na hivyo Mamlaka ya Serikali za

Mitaa na Serikali kwa ujumla itaendelea kupoteza fedha nyingi ambazo zingeweza kutumika katika shughuli nyinginezo za maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kufuatia ukaguzi uliofanywa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa imebainika kuwepo kwa utofauti wa utayarishaji na utoaji wa taarifa za fedha miongoni mwa Halmashauri jambo ambalo ni kinyume na Kifungu Na. 40(2) cha Sheria ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) ambayo inazitaka Halmashauri zote kuwa na mfumo unaofanana wa utengenezaji na utoaji wa taarifa za fedha. Utofauti huo ulisababishwa na kuwepo kwa miongozo mbalimbali inayokinzana juu ya namna ya utayarishaji na utoaji wa taarifa za fedha kwa mwaka wa fedha 2007/08.

Aidha, Sheria ya fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) haiko wazi kuhusu ni nani kwa upande wa Serikali za Mitaa atakuwa na madaraka sawa na yale ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, ambayo ni pamoja na kusimamia fedha na uhasibu katika Mamlaka hizo. Kuwepo kwa mamlaka hiyo kwa upande wa Serikali za Mitaa kutasaidia sana katika uwekaji wa mfumo wa kisheria unaoendana na wakati, ikiwa ni pamoja na kuwa na miongozo inayofanana juu utoaji wa taarifa za fedha katika Mamlaka hizo.

Mheshimiwa Spika, katika utayarishaji na utoaji wa Taarifa za fedha, Halmashauri hazina budi kutoa taarifa sahihi na kukwepa tabia ya kutoa taarifa za uongo au za kugushi au zinazotofautiana kwa lengo la kuficha hali ya matumizi ya fedha kwa wale wanaozisoma au wanaozikagua. Mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Muleba iliwasilisha mbele ya Kamati Muhtasari wa kugushi kuhusu kufanyika kwa kikao cha Baraza la Madiwani tarehe 11/7/2009 katika ukumbi wa Halmashauri, kilichokuwa na *agenda* moja tu ya kujadili hoja za ukaguzi zilizotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2007/2008 na Maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa yaliyotolewa kwenye kikao kilichokaa kwenye Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kagera. Kufuatia uchunguzi uliofanywa na Kamati, ilibainika kuwa kikao hicho hakikufanyika katika tarehe tajwa, isipokuwa Kikao kilichofanyika ni cha tarehe 11/08/2009 ambacho kilikuwa na agenda 10.

Mheshimiwa Spika, vivyo hivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Mafia iliwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, taarifa ya mapato na matumizi katika miradi ya *TASAF* inayotofautiana na ile iliyowasilishwa Makao Mkuu ya *TASAF* na hivyo kuleta mkanganyiko katika kuthibitisha taarifa ipi ni sahihi, wakati Kamati ilipokwenda kufanya ukaguzi wa miradi katika Halmashauri hiyo. Kufuatia suala hili ambalo ni sawa na kulidanganya Bunge, Kamati iliagiza hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa Maafisa walioandaa Taarifa hizo na tabia hiyo isijirudie tena.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mpango mzuri wa Serikali wa kuhakikisha Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatumia mifumo ya kompyuta ya uhasibu, mafunzo juu ya

matumizi ya mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha (*IFMS*) kwa kutumia Programu aina ya *EPICOR* yalitolewa kwa Watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa miaka mingi iliyopita. Pamoja na utoaji wa mafunzo hayo, Kamati imebaini kuwa hakuna hata Halmashauri moja ambayo inatumia kwa kiwango cha juu mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha (*IFMS*) kwa kutumia Programu hiyo aina ya *EPICOR*. Hali hii inaashiria kupotea kwa fedha ambazo zilitumika katika kuhakikisha mfumo huo wa kompyuta unatumika kama ilivyokusudiwa, lakini matokeo ya mpango mzima yamekuwa ni mfumo huo kutotumika kabisa au kutumika kwa kiasi kidogo kwenye baadhi ya Halmashauri.

Aidha, sababu zilizopelekea matumizi ya mfumo huo kutofikia malengo ni pamoja na mfumo huo kutokidhi matakwa ya Halmashauri na vilevile kuhamishwa kwa Watumishi waliopewa mafunzo kutoka Halmashauri moja kwenda nyingine. Hivyo, ni vema Serikali ikaliangalia suala hili kuwa umakini kwa lengo la kupatikana kwa mfumo utakaokidhi matakwa ya Halmashauri ili kufanikisha juhudi za Serikali katika kuboresha mifumo ya Taifa ya uhasibu na ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa hesabu hutegemea sana uwepo wa nyaraka muhimu zinazoonyesha jinsi fedha zilivyotumika kwa kuzingatia kanuni na Sheria ya fedha. Kufuatia ukaguzi uliofanyika, imebainika kuwa Halmashauri nyingi hazina utaratibu mzuri wa kutunza kumbukumbu. Imekuwa ni mazoea kwa Afisa anayehusika na mradi kutunza kumbukumbu zote na iwapo ikatokea anahamishwa, Halmashauri hupoteza kumbukumbu na nyaraka zote muhimu. Tunaiomba Serikali hasa TAMISEMI itoe miongozo sahihi kuhusu utaratibu wa kutunza miongozo. Hali hii ya utunzaji mbaya wa kumbukumbu na nyaraka muhimu husababisha ukaguzi wa hesabu kuwa mgumu.

Mheshimiwa Spika, aidha, kupotea kwa nyaraka kama *BOQs* pamoja na makadirio ya awali ya Mhandisi *(Engineer's estimates)* husababisha miradi ya ujenzi kutekelezwa bila kuwa na mwongozo wa vipimo vya kitaalam, hali ambayo si tu husababisha kutokuwepo kwa uwiano baina ya ukubwa wa kazi na gharama iliyokadiriwa bali pia husababisha ujenzi kuwa na ubora hafifu. Hivyo, ni vema Halmashauri zikaimarisha kitengo cha manunuzi kwa kutenga chumba maalum cha kuhifadhi nyaraka za manunuzi ili kukomesha kasoro ya kutopatikana kwa nyaraka au kumbukumbu zinapohitajika.

Vivyo hivyo, ni vema Halmashauri zikaunda *Contract Management Team* ili kuimarisha usimamizi wa miradi kwa kupitia mikataba na hali halisi ya utekelezaji wa miradi husika kabla ya kufanya malipo. Kamati inaamini kuwa, kwa kufanya hivi Halmashauri zitaweza kurudisha nidhamu ya kutunza kumbukumbu na nyaraka muhimu tayari kwa kutumika pale zinapohitajika.

Mheshimiwa Spika, uwezo wa Halmashauri zetu wa kijitegemea kifedha kupitia mapato ya ndani umezidi kushuka katika mwaka wa fedha wa 2007/2008. Ulinganisho uliofanywa kati ya mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani vya Halmashauri, ruzuku za Serikali Kuu na fedha za Wahisani kwa mwaka 2007/2008 umeonyesha kuwa mapato kutoka vyanzo vya ndani vya Halmashauri yalikuwa ni wastani wa asilimia 7.57% ya

mapato yote ya Halmashauri ambapo kwa mwaka 2006/2007 yalikuwa ni wastani wa asilimia 7.8%.

Mheshimiwa Spika, hii haina maana hakuna viwango ambavyo ni chini kwa Halmashauri moja moja na kuna Halmashauri zina viwango vya 1.5%, hali hii ni mbaya sana kwa utegemezi. Aidha, mapato ya ndani yalikuwa Sh. 93,545,987,812 *(*ambalo ni ongezeko la asilimia *21%* toka *Sh.77,310,930,607* zilizokusanywa *2006/2007)* na mapato toka ruzuku ya Serikali Kuu na Wahisani yalikuwa Sh. 1,140,847,566,087 *(*Angalia Kiamb.B*).* Hali hii inaashiria kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika uendeshaji wa shughuli zake, zinazidi kutegemea kwa kiasi kikubwa ruzuku toka Serikali Kuu na fedha za Wahisani. Tuseme tu, hali hii ikiendelea itakuwa ni ngumu kwa Serikali ya Tanzania kufikia malengo iliyojiwekea kwenye MKUKUTA na *Vision 2025.*

Hata hivyo, Kamati inatambua kuwa hali hii kimsingi imetokana na Serikali Kuu kuchukua vyanzo vingi vya mapato na kiziachia Halmashauri vyanzo vichache na wakati huo huo ruzuku ya Serikali Kuu imeongezeka kwa kiwango kikubwa, hasa sehemu ya Mishahara ya Watumishi, jambo ambalo limeshusha kwa kiwango kikubwa uwiano huo wa makusanyo. Kufuatia hali hiyo, Kamati imezitaka Halmashauri kuwa na ubunifu zaidi, kwani nchi itaacha tu utegemezi kwa wahisani, iwapo tutakuwa na vyanzo vingi zaidi vya ndani vya mapato, angalau kutosheleza matumizi ya kawaida ya uendeshaji wa Halmashauri zetu zenyewe.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zetu bado hazijaweka mipango mizuri na endelevu katika uibuaji wa vyanzo vipya vya mapato na udhibiti katika usimamizi wa makusanyo. Kufuatia Taarifa za Halmashauri zinazowasilishwa kwenye Kamati yangu, ni wazi kuwa kuna mapato mengi ambayo hayakusanywi au hupotea na mpaka sasa bado haijawekwa mikakati madhubuti ya ukusanyaji *(*Angalia Kiamb.C*).* Aidha, kwa mwaka wa fedha wa 2007/2008, utaratibu wa kuwatumia mawakala kama wakusanyaji wa mapato ya Halmashauri umeishia kuwanufaisha mawakala hao kuliko Halmashauri zenyewe, kwani nyingi ziliingia mikataba kabla ya kufanya uchambuzi yakinifu juu ya mapato yake halisi.

Vivyo Hivyo, Mawakala wa ukusanyaji mapato wamekuwa hawazingatii mikataba ya ukusanyaji wa mapato na Halmashauri husika zimeshindwa kuwachukulia hatua za kisheria mawakala wanaoshindwa kuwasilisha makusanyo yaliyokubalika kwenye mikataba. Hivyo, Kamati yangu inaendelea kuziagiza Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwa makini katika kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani, lakini pia kuwa wabunifu katika kutafuta mbinu mbadala ambazo zitaongeza wigo wa vyanzo vya mapato ya ndani.

Hatua hii ni ya muhimu sana katika kulitoa Taifa letu kwenye utegemezi mkubwa tulionao toka kwa Wahisani na vyanzo vingine vya nje. Aidha, karibu Halmashauri zote sasa zimeajiri Wanasheria, hivyo hakuna tena sababu ya Halmashauri

kuingia mikataba mibovu kama awali. Kamati imewataka Wanasheria hao kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zetu zinakabiliwa na tatizo sugu la upungufu wa watumishi wa sekta karibu zote kwa muda mrefu. Katika kila Halmashauri ambayo Kamati yangu imehoji suala la watumishi, imebainika kuwa bado tatizo hilo halijapatiwa ufumbuzi wa kudumu. Serikali kupitia TAMISEMI imekuwa ikijitahidi kuwapanga Watumishi katika Halmashauri mbalimbali lakini baadhi ya watumishi wamekuwa hawaripoti kwenye maeneo waliyopangiwa na badala yake huomba na kupokelewa kwenye Halmashauri zingine.

Suala hili limejitokeza sana kwenye Halmashauri za mikoa ya Rukwa, Lindi, Manyara na Tabora na maeneo yaliyo na jiografia ngumu kama Wilaya ya Mafia. Mpango wa Mikoa na Halmashauri kupewa mamlaka ya kuajiri zenyewe bado haujafanikiwa kwani sababu zinazoathiri hazijapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, sababu hizo kwa ujumla ni pamoja na ubovu wa miundombinu ya barabara, usafiri na mawasiliano magumu, mazingira magumu ya kazi, imani potofu za ushirikina, jiografia za mikoa na tabia ya Serikali kuwasahau watumishi wanaofanya kazi katika maeneo hayo. Tunaomba Serikali iangalie mambo hayo ili tatizo la utumishi lipungue kwa sababu maisha bora kwa kila Mtanzania yatapatikana kama fedha zinapelekwa na kuna watumishi wa kutosha wa kutumia fedha hizo vizuri. Hivyo, Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa lazima iweke mikakati ya makusudi yenye lengo la kutatua tatizo la upungufu wa watumishi na juhudi kubwa zielekezwe katika kuboresha mazingira ya kazi ili watumishi waweze kufanya kazi sehemu walizopangiwa.

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri zetu bado lipo tatizo la Maafisa kukaimu nafasi zilizo wazi kwa muda mrefu bila kuthibitishwa katika nafasi hizo. Kamati yangu inaendelea kuisisitizia TAMISEMI kuhusu umuhimu wa kuchukua hatua za haraka na za makusudi pale ambapo Wakuu wa Idara wamekaimu kwa muda mrefu na wanazo sifa stahiki, ni vema wakathibitishwa mapema iwezekanavyo ili kuongeza uwajibikaji na usimamizi katika utekelezaji wa majukumu yao. Ikiwa hawajafikia vigezo hitajika basi watafutwe wenye sifa kujaza nafasi zilizokaimishwa kwa muda mrefu.

Aidha, Kamati imebaini kuwa karibu Halmashauri zote za Kigoma, Ruvuma, Mara na Halmashauri ya Wilaya ya Mafia zina Maafisa wengi wanaokaimu Ukuu wa Idara bila kuthibitishwa, kutokana na kutotimiza miaka saba katika utumishi wa Umma. Kanuni hii ni vyema ikaangaliwa upya hasa katika ngazi ya Halmashauri kwani inazisababishia kupoteza Watumishi wenye sifa na uwezo unaohitajika, kwa kushindwa kuwathibitisha hasa wale wenye muda mfupi katika utumishi wa Umma, japo wanazo sifa zingine zote zinazohitajika.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imeendelea kuchukua hatua kali kwa mujibu wa Kanuni za Fedha, ikiwa ni pamoja na kupiga tozo Wakuu wa Idara ambao wameonyesha uzembe katika utekelezaji wa majukumu yao. Kamati ililazimika kutoa tozo kwa Watendaji wa Halmashauri au kuirudisha Halmashauri ikaandae upya Hesabu zake au kuomba ufanyike ukaguzi maalum pale ilipogundua kuwa kuna walakini katika taarifa za fedha walizoziwasilisha mbele yake kwa ajili ya kuzijadili na kuzichambua.

Katika kutilia mkazo suala la uwajibikaji, Kamati ilitoa adhabu ya tozo ya asilimia 15% ya mshahara kwa Watendaji wa Halmashauri za Wilaya za Mafia, Muleba, Kilosa, Bunda, Korogwe, Longido na Muheza, kwa kushindwa kutekeleza majukumu na maelekezo ipasavyo au kwa kutoa taarifa za fedha za uongo au kwa kuidanganya Kamati kwa namna yoyote.

Aidha, katika kuhakikisha hesabu zinatayarishwa vizuri, Kamati ililazimika kuzirudisha Halmashauri zifuatazo kwenda kuandaa upya vitabu vyake kwa Hesabu za mwaka 2007/2008 na kisha kurudi mbele ya Kamati, Halmashauri za Wilaya za Sikonge, Muheza, Kongwa, Muleba, Kilosa, Babati, Morogoro, Mvomero, Korogwe, Lushoto, Pangani na Mkinga. Kwa Halmashauri ambazo Kamati iliona kuna hali ya ubadhirifu wa fedha za umma, ilikubaliana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kufanya ukaguzi maalum kwa lengo la kufanya uchunguzi yakinifu. Halmashauri zifuatazo zilifanyiwa ukaguzi maalum uliohusisha matumizi yaliyofanyika katika mwaka wa fedha husika, Halmashauri za Wilaya ya Tarime, Morogoro, Bunda, Songea, Sumbawanga, Monduli, Bagamoyo na Jiji la Dar es Salaam.

Aidha, matokeo ya Ukaguzi huo maalum yameonyesha upotevu mkubwa wa fedha na hivyo kupelekea Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kutoa malekezo mbalimbali ikiwa ni pamoja na wahusika kulipa sehemu ya hasara ambayo wameiingizia Serikali, wahusika kuchukuliwa hatua za kinidhamu na wengine kufikishwa mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, uwezo wa Halmashauri nyingi katika kusimamia miradi bado unatia shaka hasa katika kufikia malengo waliyojiwekea likiwemo la kuwaletea maendeleo wananchi wake. Ukaguzi wa hesabu wa mwaka 2007/2008, umebaini kuwa, pamoja na kiasi kikubwa cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali, miradi mingi haikukamilika kwa wakati uliopangwa (mfano miradi ya elimu, maji, masoko na machinjio katika Halmashauri zote za Kigoma, Mara na Dar es Salaam, Halmashauri za Wilaya ya Mbinga na Muheza), baadhi ya miradi imetekelezwa chini ya kiwango (mathalan miradi elimu na kilimo katika Halmashauri za wilaya ya Bagamoyo, Korogwe na Mkuranga).

Pia, na kumekuwa na usimamizi usioridhisha wa miradi na kiasi kikubwa cha fedha za miradi hakikutumika kabisa (mfano, Halmashauri za Mikoa ya Lindi, Ruvuma, Pwani na Kagera zilikuwa na bakaa kubwa), Halmashauri za Muheza na Bagamoyo kwa kweli zimeleta tatizo kubwa sana, Kamati yetu imetembelea miradi ikakuta miradi hewa na tunashukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu aliingilia akachukua hatua baada ya taarifa hiyo pia kutolewa na mdhibiti na Mkaguzi Mkuu.

Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo imekuwa na udanganyifu mkubwa kwa kuonyesha matumizi katika baadhi ya miradi ambapo Kamati ilipotembelea miradi hiyo haikuwepo kabisa. Sambamba na niliyoeleza, ni vema Serikali katika upelekaji wa fedha za miradi kwenye Halmashauri kama Wilaya ya Mafia ikazingatia vilevile hali ya kijiografia ambayo husababisha fedha nyingi kutumika katika usafirishaji na ununuzi wa vifaa vya ujenzi kwa gharama kubwa kutoka Dar es Salaam. Ni vema kiasi cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi kikazingatia changamoto hiyo ya kijiografia.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka husika jumla ya Halmashauri 111 zilipata ruzuku ya Serikali jumla ya Sh. 270,547,629,434 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hata hivyo, ilipofika tarehe 30 Juni 2008, kiasi cha Sh.171,791,488,611 tu ndio kilikuwa kimetumika na kubakia Sh.99,114,082,540 au 37%. Hali hii inaashiria usimamizi mbaya wa miradi ambao umesababisha kutotekelezwa au kutokamilika kwa baadhi ya miradi iliyotengewa fedha na hatimaye kulazimisha marudio ya bajeti ili kuweza kufidia mapungufu yaliyojitokeza kutokana na mfumuko wa bei. Aidha, ucheleweshaji huu kwa upande mwingine umesababishwa na Serikali kutokupeleka mapema fedha kwenye Halmashauri, au fedha nyingi kupelekwa mwishoni mwa mwaka wa Fedha, jambo ambalo linafanya Halmashauri husika isiweze kuzitumia kwa wakati uliokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, suala la Halmashauri kupeleka kwenye Akaunti za Vijiji asilimia 20% ya ruzuku inayotolewa na Serikali kama fidia ya mapato, bado ni tatizo kwani Kamati imeendelea kukutana na Halmashauri ambazo bado zinadaiwa deni la miaka ya nyuma au zimepeleka fedha pungufu kutoka kwenye fidia wanayopata na kuendelea kutumia zilizobaki kwa shughuli nyingine au hazikupeleka kabisa fedha hiyo katika miaka ya hivi karibuni ingawa Kamati iliagiza deni hilo lilipwe na Halmashauri ziendelee kupeleka fedha hiyo kwa kiwango ambacho Serikali imekipanga.

Kamati yangu inaendelea kusisitiza umuhimu wa Halmashauri zote kuweka mikakati ya kulipa madeni yatokanayo na kutotimiza maelekezo hayo ya Serikali kwani kutofanya hivyo sasa kutasababisha madeni hayo kuwa makubwa kiasi cha kushindwa kuyalipa. Hata hivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro ni Halmashauri pekee ambayo imepeleka fedha hizo, lakini badala ya kufanya kazi za maendeleo kama ilivyokusudiwa fedha hizo zote zimetumika kuwalipa Wenyeviti wa vijiji, jambo ambalo ni kinyume na sheria na maelekezo ya Serikali. Kwa hiyo tunakemea Halmashauri zote ambazo hazipeleki lakini pia zitumike kwa ajili ya matumizi kwa ajili ya shughuli za maendeleo kama ilivyokusudiwa na miongozo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ziara za Ukaguzi wa Miradi. Kamati ilifanya ziara katika Halmashauri za Mikoa kumi na saba (17) na kufanikiwa kuona Miradi ipatayo mia nne na moja (401) ya sekta mbalimbali kama ifuatavyo;

(i) Sekta ya Elimu: Miradi iliyotembelewa ni mia moja thelathini na tisa (139) ikiwemo Ujenzi, Ukamilishaji na Ukarabati wa Nyumba za Walimu, Madarasa,

majengo ya Utawala, Matundu ya Vyoo, Mabweni na ununuzi wa viti na meza katika Shule za Sekondari na Msingi, ambapo fedha zilizotumika ni za MMEM, MMES, *TASAF*, Nguvu za Wananchi na Halmashauri yenyewe. Kwa ujumla miradi iliyojengwa katika sekta hii inaridhisha ingawa mingi imejengwa bila kuzingatia miongozo na ramani zilizotolewa na Serikali. Halmashauri ya Muheza imetumia fedha za *TASAF* vibaya katika ujenzi wa madarasa ya Sekondari.

Vivyo hivyo, kumekuwa na ubadhirifu katika ujenzi wa Karakana katika Halmashauri ya Wilaya ya Monduli. Aidha, Sekta ya Elimu inakabiliwa na Upungufu wa Walimu, vifaa vya kufundishia na kujifunzia, matundu ya vyoo na Nyumba za Walimu, utoro wa wanafunzi na wanafunzi wa kike kupewa mimba. Kutokana na mapungufu hayo, agizo la jumla kwa Wakurugenzi wote limekuwa kwamba Shule zitakazojengwa sasa zizingatie michoro wa MMEM na MMES ambayo ndio michoro mipya iliyotolewa na Wizara kwa madarasa yote, Nyumba za Walimu zitakazojengwa ziwe na vyumba vitatu vya kulala na yajengwe mabweni ya wanafunzi wa kike ili kupunguza idadi ya mimba za wanafunzi.

(ii) Sekta ya Afya: Miradi iliyotembelewa ni sabini na saba (77) ikiwemo Ujenzi na Ukarabati wa Hospitali, Zahanati, Vituo vya Afya, Kliniki ya Wanawake na Watoto, Kituo cha Ushauri Nasaha (*VCT*), Ofisi na Wodi mbalimbali, Ujenzi wa Bohari la Madawa, majengo ya *X-ray* katika Hospitali za Wilaya na Matundu ya Vyoo, kwa kutumia fedha kutoka *Basket Fund, TASAF*, *Capital Development Grant*, Nguvu za Wananchi na fedha toka vyanzo vya Halmashauri na fedha za Wahisani.Kwa ujumla miradi mingi ya Afya imekamilika na thamani ya matumizi ya fedha imeonekana. Halmashauri ya Wilaya ya Muheza siyo tu imekuwa na ubadhirifu mkubwa, bali hata nyumba ya daktari iliyoonyeshwa kwenye vitabu kujengwa kwa fedha za Serikali, imejengwa kwa nguvu za Wananchi bila kutumia hata senti moja ya Serikali.

Vivyo hivyo, kwa Wilaya ya Mafia ambapo kuna upotevu mkubwa wa Fedha katika ujenzi wa Zahanati. Aidha, Sekta hii inakabiliwa na tatizo la upungufu wa Watumishi na suala la ukosefu wa madawa na vitendea kazi kutoka *MSD*. Aidha, Waganga wa Wilaya wamethibitisha kukosa baadhi ya huduma muhimu kutoka *MSD* pale zipohitajika wakati fedha zipo na hawana uwezo wa kuzihamisha ili mahitaji muhimu yaweze kupatikana kutoka kwa vyanzo vingine. Kamati inaendelea kuliona hili kama ni tatizo linalohitaji kutafutiwa ufumbuzi wa haraka iwezekanavyo.

(iii) Sekta ya Maji: Miradi iliyotembelewa ni arobaini na sita (46) ikiwemo ya Ujenzi wa Visima na matanki ya maji kwa kutumia fedha za Halmashauri, Serikali Kuu na Wahisani. Kwa ujumla miradi ya sekta ya maji imetekelezwa vizuri ingawa baadhi imeonekana kushindwa kuendelea kutoa huduma kutokana na usimamizi hafifu au kutofanyika kwa *feasibility study* kabla ya kuanzisha utekelezaji wa mradi. Baadhi ya miradi inayosimamiwa na Kitengo cha Umwagiliaji imeonekana kuwa na gharama kubwa kuliko gharama halisi, kama ilivyoonekana kwenye mradi wa umwagiliaji katika Wilaya ya Rungwe. Vivyo hivyo, katika Manispaa ya Arusha umebainika udanganyifu

katika matumizi ya fedha za mradi wa visima, hali ambayo imejitokeza pia kwenye utekelezaji wa visima 17 vya Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe.

(iv) Sekta ya Kilimo na Mifugo: Miradi iliyotembelewa ni sitini na tano (65) ikiwemo Ufugaji wa nyuki, ng'ombe, mbuzi na kuku, Mashamba darasa ya mazao mbalimbali, Ujenzi wa Majosho, skimu za umwagiliaji, mabwawa ya kunyweshea mifugo, Maghala ya nafaka, Masoko na Machinjio kwa kutumia fedha toka *DADPS, LGCDG* na *PADEP*. Hata hivyo, katika maeneo mengi, Kamati imebaini kuwa fedha nyingi zinatumika katika "Kujenga uwezo" na kwa bahati mbaya wanaojengewa uwezo ni wale wale kila mara. Fedha nyingi zinazopelekwa Wilayani, zinatumika kwenye mambo ambayo hayamlengi mwananchi mmoja kwa mmoja, iwapo hali hii haitabadilika, malengo ya Kilimo Kwanza itakuwa ngumu kuyafikia.

Kwa mfano, Shamba darasa ambalo Kamati ilitembelea katika Halmashauri ya Wilaya ya Mafia ni kielelezo cha wazi kuwa dhana ya Kilimo Kwanza haijaeleweka bado na matokeo yake ni fedha nyingi za umma kutumika mahali ambapo hazina tija ya moja kwa moja kwa walengwa yaani wakulima tunaolenga kuwatoa kwenye umaskini. Aidha, hali hii ipo katika maeneo mengi ambayo Kamati ilitembea na kukagua miradi ya kilimo.

(v) Sekta ya Uvuvi: Kamati ilitembelea vikundi viwili vya uvuvi vilivyofadhiliwa na Mfuko wa Jamii wa *TASAF* katika Halmashauri ya Wilaya ya Mafia. Kamati imegundua kuwa hakuna usimamizi mzuri wa miradi hii na imedhihirika kuwa hakuna uwajibikaji wa kutosha katika idara inayosimamia masuala ya uvuvi.

(vi) Sekta ya Miundombinu: Miradi iliyotembelewa ni ishirini na tatu (23) ikiwemo ujenzi na ukarabati wa barabara, makalvati, madaraja na Stendi za Basi kwa kutumia fedha toka *Road Fund* na *TASAF*. Kwa ujumla miumbombinu iliyotengenezwa katika Halmashauri zetu inakidhi viwango vinavyokubalika na kuonyesha thamani halisi ya matumizi yaliyoonyeshwa kwenye taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati.

Aidha, Kamati ilitembelea daraja ililopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru, ambalo halitumiki tangu lijengwe, kwani limejengwa kwenye kona ya mlima mkali wa mawe na kwa upande wa pili kuna mashamba ya Kahawa ya wananchi. Daraja hilo limegharimu jumla ya Sh. 60,000,000 na halijatumika kwa zaidi ya miaka miwili na hakuna mwelekeo wa kutumika ndani ya miaka mitano ijayo.

Ni wazi kuwa fedha zimetumika katika mradi usio na tija kwa wananchi ikizingatiwa wakulima hawakuhusishwa wakati wa ujenzi huo.

Hata hivyo, Kamati iliridhishwa na viwango vya utengenezaji wa barabara na madaraja, ingawa katika baadhi ya maeneo kama Halmashauri za Mkoa wa Kigoma, miundombinu ya barabara inahitaji matengenezo makubwa kutokana na kuharibiwa na mvua kubwa zinazonyesha wakati na baada ya matengenezo. Aidha, barabara nyingi

hazikuwa na Kalvati za kutosha kuweza kuzilinda ili zidumu kwa muda mrefu lakini pia baadhi hazikujengewa mifereji *(drainage system)* au kama imejengwa haisafishwi mara kwa mara hivyo, kusababisha maji kukwama kutokana na mrundikano wa uchafu na baadhi ya Madaraja hayakuwa na kingo *(guide rails).*

Hali hii inasababisha Serikali kutumia fedha nyingi kila mwaka kwa ajili ya matengenezo ya Barabara, ingawa kama ushauri wa kitaalam ungetolewa na kutumika vizuri, fedha nyingi zingeokolewa kwa kuongeza muda wa uhai wa barabara. Hivyo, Kamati imeendelea kuziagiza Halmashauri kuhakikisha zinatenga fedha kwenye bajeti za kila mwaka kwa ajili ya kuzifanyia barabara matengenezo ya mara kwa mara *(Routine Maintanance)* ili kuokoa barabara hizi zisiharibike na Wahandisi wawe makini katika utoaji wa *Certificates* kwani husababisha Makandarasi kulipwa wakati kazi iliyofanyika haina ubora.

(vii) Miradi ya Utawala: Miradi iliyotembelewa ni arobaini na tisa (49) ikiwemo ujenzi na ukarabati wa majengo ya Ofisi za Halmashauri, Ofisi za Wabunge na Ofisi za Serikali za Mitaa. Kwa ujumla miradi mingi ya utawala haijakamilika kutokana na tatizo la kukosa fedha na mara nyingi kuwepo na mapungufu katika mchakato wa kuwapata Makandarasi wenye uwezo wa kukamilisha miradi bila ya kutegemea malipo ya haraka toka kwa Halmashauri. Kamati imeshuhudia miradi mingi ambayo haijakamilika kutokana na Makandarasi kukosa fedha za kukamilisha ujenzi na hivyo kutelekeza miradi. Ni vema Serikali ikaweka mikakati ya makusudi kuhakikisha Makandarasi wanaoshinda zabuni wana uwezo na utaalam wa kutosha wa kukamilisha miradi kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kufuatia ukaguzi wa miradi uliofanyika, Kamati inatoa Taarifa hii kama mifano ya miradi ambayo Kamati imebaini haijakamilika au utekelezaji wake umesitishwa kutokana na matumizi mabaya ya fedha na uzembe wa kiutendaji katika Halmashauri zetu:-

(i) Ujenzi wa Madarasa mawili katika Shule ya Sekondari ya Lowassa Makuyuni iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Monduli – Ujenzi ulianza katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 na kugharimu jumla ya Sh.21m kutoka mfuko wa miradi ya maendeleo wa *LGDG*. Kamati ilipotembelea majengo hayo haikuridhika na utekelezaji wake kutokana na kuwa na sura ya kiwango cha chini, sakafu kubomoka, *ficherboards* kuoza na kuwepo kwa mabati chakavu. Hivyo, Kamati iliagiza Halmashauri kuchanganua upya gharama za mradi ikionyesha mchango wa wananchi na Wakaguzi kukagua matumizi ya fedha za mradi na endapo kutakuwepo na ubadhirifu hatua za kisheria zichukuliwe kwa Wahusika.

(ii) Ujenzi wa Nyumba ya Mwalimu katika Shule ya Msingi ya Mlongo iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mafia - Ujenzi wa nyumba hiyo ulianza katika mwaka wa fedha wa 2007/8 na kugharimu jumla ya Tshs 7.2m toka *MMEM*. Ujenzi wa

nyumba hiyo uko katika hatua ya msingi mpaka sasa na Kamati ilipohoji iliambiwa kuwa ujenzi wa jengo hilo umesitishwa kutokana na kujengwa bila kufuata utaalam na hivyo kutokuwa na ubora uliokusudiwa. Kufuatia ubadhirifu uliofanyika, *Afisa Elimu wa Wilaya* alimshusha cheo Mwalimu aliyehusika.

Aidha, Kamati iliagiza ujenzi wa nyumba hiyo ukamilike kwa kutumia fedha za *LGDG* kabla ya Septemba 2010 na Halmashauri imchukulie hatua za kinidhamu Mwalimu aliyesababisha hasara hiyo ikiwa ni pamoja na kukatwa mshahara pindi itakapothibitika kuwa ndiye aliyefanya ubadhirifu huo.

(iii) Ujenzi wa Machinjio ya Peramiho katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea - Kamati ilitembelea eneo ambalo wananchi waliomba ijengwe machinjio hiyo, ambapo ujenzi wake ulisitishwa ikiwa jumla ya Sh. 12,000,000 zilishatumika kati ya Sh. 30,000,000 zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Kamati ilihoji sababu ya kusitisha kwa mradi huo, ikizingatiwa baadhi ya fedha zilishatumika na kuelezwa kuwa Halmashauri ilipata msaada wa jumla ya Sh. 300,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa mradi mkubwa wa maji katika eneo hilo na ikaonekana kuwa mradi wa machinjio ungechafua maji, na hivyo mradi huo wa maji ungekosa tija.

Hivyo, Halmashauri kwa kuzingatia ushauri wa wataalam ilibomoa mradi wa machinjio na kuuza malighafi na kupata Sh.4,000,000 zilizotumika kwenye ujenzi wa madarasa katika Shule ya Sekondari ya Umoja na hivyo hasara iliyohesabika ni ya Sh. 8,000,000. Aidha, Sh.18,000,000 zilizobaki zilitumika katika utekelezaji wa miradi ya Kilimo. Kamati ilimuagiza Mkaguzi wa Ndani kukagua mchakato mzima wa kubadilisha matumizi ya fedha hizo na taarifa ipelekwe kwa Wakaguzi kisha Halmashauri ifanye taratibu za kufuta harasa ya Sh.12,000,000 katika vitabu vyake vya hesabu na taarifa ya utekelezaji ipelekwe kwa Wakaguzi.

(iv) Ujenzi wa Stendi ya Mabasi katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea - Kamati ilitembelea eneo ambalo limetengwa kwa ajili ya ujenzi wa stendi hiyo mnamo tarehe 4/08/2009 na kukuta jengo moja tu lililochakaa na hakuna dalili za kujengwa kwa Stendi ya Mabasi ingawa jumla ya Sh.17,000,000 zilishatumika kwa kazi ambayo haionekani. Kwa ujumla Kamati haikuridhiwa na utekelezaji wa mradi huu kwani utekelezaji wake ulianza tangu mwaka 2007.

Hivyo, Kamati iliagiza Halmashauri kuandaa Taarifa kamili ya utekelezaji wa mradi huo ikiambatishwa na nyaraka zote zinazohusu mradi huo na kuziwasilisha kwa Wakaguzi kwa uhakiki na ikionekana kuna ubadhirifu wa fedha, Wahusika wachukuliwe hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sheria. Tunaomba TAMISEMI itusaidie kwa sababu hatukuona mapendekezo ya Kamati na hawakuchukua hatua ambazo Kamati ilizipendekeza.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliweza kubaini miradi iliyokamilika lakini haitumiki kama ilivyokusudiwa yaani '*White elephant*' na mingine ambayo utelekezaji

wake hauendelei au hautoi huduma mara baada ya kuanzishwa. Aidha, ifuatayo ni miradi ambayo haitoi huduma iliyokusudiwa kutokana na uzembe uliofanyika ama katika uanzishwaji wake au katika usimamizi wa kila siku:-

(i) Mradi wa umwagiliaji wa Nangaramo uliopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu – Mradi haufanyi kazi kwa sasa kutokana na kukosekama kwa maji katika eneo ambalo limejengwa banio. Awali mradi ulikuwa wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi lakini ilipogawanyika mradi ukawa wa Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu, lakini ilidhihirika kuwa hapakufanyika upembuzi yakinifu kuhusu eneo zuri la kuanzisha mradi huo, kwani kwa sasa mradi hautumiki na ni hasara kwa Serikali kwani wanakijiji walioanzisha mradi wamependekeza yanunuliwe matrekta kwa ajili ya kilimo. Kufuatia hasara hiyo, Halmashauri iliomba Hazina kibali cha kununua matrekta na kukubaliwa. Aidha, Kamati imeagiza Halmashauri kufuata taratibu na sheria ya fedha katika mchakato wa kuomba kufuta hasara iliyotokea.

(ii) Ujenzi wa Ghala katika Kijiji cha Mabare kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo, ulianza katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 ambapo *DASIP* imetoa Sh. 16.8m, wananchi walichangia Sh.3.9m na Halmashauri ilitoa Sh.20.7m. Pamoja na matumizi ya jumla ya Sh.41.4m kwa ajili ya ujenzi wa ghala hilo Kamati ilikuta halitumiki. Hivyo, utekelezaji wa mradi husika hauna tija kwa wananchi.

(iii) Kituo cha Afya cha Mtisi kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda - Kituo kinamilikiwa na Kanisa la KKKT lakini kulingana na makubaliano ambayo yamefikiwa kati ya KKKT na Halmashauri ni kwamba kitakabidhiwa kwa Halmashauri kwa lengo la kukiendeleza ingawa mpaka sasa mkataba wa kukabidhiana rasmi bado haujaingiwa. Katika kuzingatia makubaliano hayo, Halmashauri ya Wilaya ilifanya ukarabati wa awali ambao uligharimu jumla ya Sh.17,000,000 kwa nia ya kuhakikisha wanakijiji cha Mtisi na vijiji vingine vya karibu wanapata huduma za afya. Ukarabati uliofanyika ni kuimarisha sakafu na kupaka rangi *ceiling board*.

Hata hivyo, baada ya kuanzisha utaratibu wa kuchangia gharama za matibabu (*Cost Sharing*), idadi ya wagonjwa wanaokwenda kwenye kituo hiko imepungua sana na kusababisha kituo kusimamisha utoaji wa huduma. Aidha, Halmashauri inashindwa kujenga nyumba ya Mganga katika eneo hilo kutokana na kutokamilika kwa makabidhiano na KKKT. Hivyo, Kamati iliagiza Halmashauri kuhakikisha inawasiliana na Kanisa la KKKT kwa ajili ya kukamilisha makabidhiano ya majengo ya Kituo hicho cha Afya na utoaji huduma uanze mara moja.

(iv) Ujenzi wa matanki ya kuhifadhia maji katika Kijiji cha Mkunya kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Newala – Ujenzi wa tanki hilo ni kati ya matanki 11 yaliyojengwa katika mradi mkubwa wa maji katika vijiji 11, uliogharimu jumla ya Sh.172.2m. Mradi huo mkubwa wa maji hautoi huduma iliyokusudiwa, kutokana na kukosekana kwa umeme katika Halmashauri hiyo. Hivyo, pamoja na fedha zote hizo kutumika, mradi haujaanza kutoa huduma mpaka sasa.

(v) Mradi wa Uvuvi kikundi cha Wazee ambao upo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mafia katika kijiji cha Kiegeani - Mradi ulianza katika mwaka wa fedha wa

2007/2008 ambapo kwa mujibu wa taarifa ya Halmashauri iliyowasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, *TASAF* ilitoa na zikatumika jumla ya Sh.10.8m lakini Kiongozi wa Kikundi alikiri kupokea kiasi cha Sh.10.1m tu. Kufuatia utofauti wa thamani ya mradi ulioonyeshwa kwenye tarifa hizo mbili, Kamati ilishindwa kuthibitisha thamani halisi ya mradi na kutilia shaka matumizi yaliyofanyika katika utekelezaji wa mradi huo. Aidha, kwa mujibu wa maelezo ya Kiongozi wa Kikundi, mradi umesimama na wako katika mchakato wa kuuza mashua bila kufuata taratibu za kisheria. Aidha, Kamati iliagiza Halmashauri kukagua thamani halisi ya mradi na kuweka mikakati ya kuhakikisha mradi huo na miradi mingine ya uvuvi inafanya kazi na iainishe matatizo yanayoikabili sekta ya uvuvi kwa lengo la kuyatatua.

(vi) Ujenzi wa mradi wa Josho la Nyamwaga katika Halmashauri ya Wilaya ya Tarime -Mradi ni mzuri na utekelezaji wake unaonyesha thamani halisi ya Sh.16,000,000 lakini tatizo hautumiki kutokana na kuwepo kwa tofauti baina ya koo za eneo husika.

(vii) Mradi wa ujenzi wa madarasa matatu katika Shule ya Sekondari ya Isoso iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu – Madarasa hayo matatu ambayo bado hayajakamilika yamekwishagharimu jumla ya Sh.27.95m kutoka *TASAF* na nguvu za wananchi Sh.5.55m. Ilibainika kuwa wakati wa bajeti ya utekelezaji wa mradi iliyopelekwa *TASAF*, haukujuimusha ununuzi wa madawati, hivyo madarasa hayo hayajaanza kutumika kutokana na Shule kukosa madawati. Aidha, kuna madarasa matatu mengine ambayo yalijengwa na wananchi ingawa mpaka sasa bado hayajapauliwa. Hivyo, Kamati iliagiza Halmashauri hiyo kupaua madarasa hayo ili mchango wa wananchi uwe na manufaa.

(viii) Ujenzi wa Josho katika Kijiji cha Nkuninkana kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida. Kamati ilikagua mradi wa josho lililojengwa kwa Sh.9.6m kutoka mfuko wa *PADEP* na wananchi walichangia Sh.2.6m ikiwa ni kwa ajili ya tanki la maji, sehemu ya kukusanyia ng'ombe (*collection pen*) na tanki la kuogeshea ng'ombe (*deep tank*). Kamati ilielezwa kuwa ng'ombe mmoja huogeshwa kwa gharama ya sh.100/= tu. Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa mradi kwani hautumiki kama ilivyokusudiwa kwa maelezo kuwa dawa ya kuoshea mifugo haipo kutokana na ukosefu wa fedha. Kuhusu fedha zilizopatikana kutokana na malipo ya kuogesha ngo'mbe, Halmashauri ilieleza kuwa fedha hizo wanakijiji wamezitumia katika ujenzi wa Ofisi ya Kijiji ambayo pia haijaanza kutumika kwani haijakamilika.

Aidha, Kamati ilibaini udhaifu wa uongozi wa Halmashauri kwa kushindwa kutoa ushauri wa kitaalam kwa wanakijiji hadi kufikia maamuzi yasiyo na tija ya kutumia mapato ya mradi kwa matumizi ambayo hayakuwa katika mipango ya Halmashauri kwa mwaka husika. Hivyo, Halmashauri iliagizwa kuhakikisha josho hilo linatoa huduma haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri nyingi hazifuatilii na kusimamia kwa karibu matumizi ya fedha zilizopelekwa katika ngazi ya vijiji kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya maendeleo inayoibuliwa katika vijiji husika na badala yake zimekuwa clearing house,

hivyo kusababisha miradi kutokamilika au kutumia gharama kubwa na mingine kujengwa katika kiwango cha chini. Ifuatayo ni miradi ya maendeleo ambayo imejengwa kwa gharama kubwa ingawa ni ya kiwango cha chini hasa kutokana na Halmashauri kutosimamia kwa karibu utekelezaji wake:-

(i) Ukarabati wa Wodi ya *JENA*, wodi ya Wazazi katika Hospitali ya Wilaya ya Muheza. Ukarabati ulihusisha kutoa bati chakavu aina ya *asbestos* na kuezeka kwa bati mpya za chuma. Aidha, Kamati ilibaini kuwa idadi ya bati zilizotumika ni chache ikilinganishwa na idadi iliyonukuliwa katika vitabu vya Halmashauri. Kufuatia udanganyifu huo, Kamati iliagiza Wakaguzi kukagua nyaraka zote zinazohusu ununuzi wa bati hizo na ikithibitika kuna ubadhirifu uliofanyika Wahusika wachukuliwe hatua za kinidhamu.

(ii) Ujenzi wa Zahanati ya Ndagoni iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mafia. Ujenzi wa Zahanati hiyo ulianza katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 na mpaka sasa bado haijakamilika ingawa imekwishatumia jumla ya Sh.29.2m kutoka *TASAF* kwa mujibu wa Taarifa iliyopelekwa *TASAF* na baadaye kuongezewa Sh.22.9m ambao mchanganuo wake wa matumizi haujaonyeshwa. Aidha, Taarifa iliyopelekwa *TASAF* Makao Makuu inakinzana na taarifa iliyofika mbele ya Kamati ambayo inaonyesha jumla ya Sh.22.26m zilitumika katika ujenzi huo.

Kwa ufupi taarifa zilizotolewa na Halmashauri yalikinzana na hivyo Kamati kushindwa kujua taarifa ipi ni sahihi. Hali hii inaonyesha Halmashauri imeandaa taarifa tofauti na nia ya kuziwasilisha kwa mamlaka tofauti. Hivyo, Kamati iliagiza Halmashauri kuhakikisha inakagua matumizi ya mradi huo kujua taarifa ipi ni sahihi na ikionekana kuna udanganyifu umefanyika hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa maafisa wanaohusika na utayarishaji wa hesabu hizo.

(iii) Kamati ilipotembelea Shule ya Sekondari ya Kimwanya iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ilikuta Nyumba za Walimu tatu (3) hazijakamilika na hazina dalili kabisa ya kukamilika ingawa ujenzi wa nyumba hizo ulianza tangu mwaka 2007. Aidha, Mkandarasi wa nyumba hizo ametelekeza mradi huo tangu mwaka 2008 na Halmashauri inashindwa kumpata ili wavunje mkataba. Kufuatia mgogoro huo, Kamati iliagiza Halmashauri kusitisha mkataba huo na kuangalia uwezekano wa kutafuta mkandarasi mwingine. Vilevile Ofisi ya ukaguzi ilipewa jukumu la kukagua matumizi yote yaliyofanyika katika ujenzi wa nyumba hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla bado kuna tatizo kubwa la kutofuata miongozo na ramani zinazotolewa na Serikali katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo hususan katika sekta ya Elimu, Afya na Miundombinu. Ujenzi wa majengo mengi umefanywa bila kuzingatia ushauri wa kitaalam ambao Halmashauri inapaswa kuzipatia Kamati za ujenzi na hivyo kusababisha miradi hiyo kutekelezwa chini ya kiwango au kuwa na ubora hafifu.

Kwa mfano, ujenzi wa baadhi ya madarasa ya shule za msingi haukuzingatia ramani iliyoko kwenye Mpango wa MMEM, Madarasa mengi yamejengwa kwa kutumia

ramani ya zamani ambayo kimsingi hatoi mwanga wa kutosha ndani na kuwa na madarasa madogo. Vivyo hivyo, ujenzi wa Nyumba nyingi za Walimu haukuzingatia ramani ya sasa, hivyo kufanya jengo liwe na vyumba vya kulala na sebule bila ya kuwa na choo, jiko, bafu na stoo. Aidha, majengo mengi yameezekwa kwa mabati ya geji 30 badala ya geji 28.

Mheshimiwa Spika, ifuatayo ni miradi ya ujenzi wa majengo ambayo Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wake kutokana na ujenzi wake kutozingatia matumizi mazuri ya fedha, miongozo na ramani zinazotolewa na Serikali katika utekelezaji wa miradi husika:-

(i) Ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kitagata kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ambao haujafuata kabisa ramani mpya iliyotolewa na Wizara ya Afya na hivyo kufanya jengo liwe fupi lenye madirisha madogo ambayo yanasababisha kuwepo na giza na kukosekana kwa hewa ya kutosha ndani ya vyumba.

(ii) Ujenzi wa Madarasa mawili katika Kijiji cha Mkuzi kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Muheza – Ujenzi wa madarasa hayo umegharimu jumla ya Sh. 18,000,000 chini ya Mpango wa *TASAF*. Kufuatia ukaguzi wa madarasa hayo, Kamati ilisikitishwa na ubora hafifu wa majengo hayo ikilinganishwa na kiasi cha fedha kilichotumika. Madarasa hayana madirisha, kuta hazikupigwa plasta, sakafu imepasuka, bati na vifaa vilivyotumika kujengea ni vya kiwango cha chini. Aidha, ujenzi bado haujakamilika tofauti na taarifa za utekelezaji zinazoonyesha kuwa ujenzi umekamilika.

Kamati haikuridhika na kudanganywa licha ya uongozi wa Halmashauri hiyo kufika mbele ya Kamati mara mbili kujadili taarifa zao za fedha. Hivyo, Kamati iliagiza Halmashauri kwa kushirikiana na Mkaguzi Mkazi kufanya uchunguzi wa kina juu ya matumizi ya fedha katika mradi huo na itakapobainika kuwepo kwa ubadhirifu wa fedha za mradi, hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya Afisa aliyehusika na utekelezaji wa mradi.

(iii) Ukarabati wa Soko la Musoma katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma haujakamilika na umejengwa kwa ramani isiyokubalika ingawa umetumia jumla ya Sh. 52,000,000 kwa ajili ya kufumua na kujenga meza za kuwekea bidhaa na kuweka zege katika sakafu. Aidha, thamani ya matumizi ya fedha haijaonekana kwani kazi iliyofanyika haijafuata kabisa miongozo ya kitaalam hivyo ni ya kiwango cha chini.

(iv) Ujenzi wa *drift* katika Halmashauri ya Wilaya ya Meatu. Kamati pia ilikagua ujenzi wa *drift* katika eneo la Mwananongu lililojengwa kwa gharama ya Sh.20.2m kutoka fedha za Mfuko wa Barabara yaani *Road Fund*. Aidha, Kamati haikufurahishwa na utekelezaji wa mradi huo kwani nguzo za usalama hazikukamilika ikiwa ni pamoja na kupaka rangi za kuonyesha kuwa eneo hilo lina *drift*. Hivyo, Kamati iliagiza kuwa kazi ya kuboresha hizo nguzo ikamilike kabla ya tarehe 31 Desemba, 2009. Mpaka sasa Kamati bado haijapata taarifa ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini pia miradi ambayo haijakamilika kutokana na kukosa fedha. Katika Halmashauri nyingi imedhihirika kuwa kukosekana kwa fedha za kukamilishia miradi husababababisha miradi hiyo kukamilishwa kwa gharama kubwa zaidi ya iliyokisiwa na wakati mwingine Wakandarasi hutelekeza miradi hiyo kwa hofu ya kutolipwa madai yao. Aidha, ifuatayo ni baadhi ya miradi iliyobainika kukosa fedha za ukamilishaji:-

(i) Ujenzi wa madarasa mawili na ununuzi wa madawati 80 na meza mbili katika Shule ya Sekondari ya Sangamwalugesha iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi – Mradi umegharimu jumla ya Sh. 24.2m. Katika shule hiyo ujenzi haujakamilika pamoja na kwamba ilielezwa kuwa vifaa vya ukamilishaji wa ujenzi vipo, tatizo ni kukosekana kwa fundi kwani aliyekuwepo aliondoka kabla ya kukamilisha ujenzi. Aidha, uchangiaji wa wananchi katika ujenzi huo haupo kwa sababu ya kukosa uhamasishaji. Hata hivyo wananchi wamejenga madarasa mawili, ofisi moja na nyumba ya mwalimu lakini majengo hayo hayajapauliwa kwa kukosekana kwa fedha. Watendaji wa Halmashauri walieleza kuwa wametenga kwenye bajeti jumla ya sh. 45,000,000 kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa maboma nane yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi.

(ii) Ujenzi wa Zahanati ya Mji Mpya iliyopo katika Halmashauri ya Kishapu. Ujenzi kwa sasa umesimama kutokana na Halmashauri kutoelewana na Mkandarasi kuhusu malipo na ukamilishaji wa mradi. Mpaka sasa mradi umekwishagharimu jumla ya Sh. 61,000,000 wakati gharama ya mradi mpaka kukamilika ni Sh. 250,000,000. Aidha, Halmashauri imetenga Sh. 40,000,000 kutoka katika mfuko wa *LGDG*, fedha ambayo haitoshi kukamilisha ujenzi huo. Kamati, inaishauri Serikali Kuu na Halmashauri husika kuhakikisha zahanati hiyo inakamilika kwani kutofanya hivyo ni kupoteza fedha za Serikali bure na ikizingatiwa huduma iliyokusudiwa kutolewa kwa wananchi haitolewi kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, ipo miradi ambayo utekelezaji wake umesimama au ni wa kusuasua kutokana na kuingiliwa na mipango ya Serikali Kuu, hali ambayo husababishwa na kutokuwepo kwa mawasiliano mazuri kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kufuatia utekelezaji wa mipango ya maendeleo. Ifuatayo ni miradi ambayo utekelezaji wake unakuwa mgumu kutokana na mipango iliyowekwa na Serikali Kuu.

(i) Katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, eneo ambalo kwa sasa ipo Shule ya Sekondari ya Kibada, limepimwa upya na Wizara ya Ardhi katika mpango wake wa kupima viwanja vya makazi na kumilikishwa kwa watu binafsi bila kuzingatia uwepo wa Shule hiyo. Hivyo, baadhi ya majengo ya shule yakiwemo madarasa yamewekewa alama ya X na kutakiwa kubomolewa ili kupisha uendelezaji wa wamiliki wapya.

Vivyo hivyo, mfumo wa barabara umepita kwenye eneo la shule na kuvuruga mpangilio wa baadhi ya madarasa. Aidha, kufuatia hali hii watoto wa Kata hiyo na zingine za karibu watakosa Shule na fedha zilizotumika kujengea majengo ya Shule zitapotea bure. Hivyo ni vema Wizara husika kwa kushirikiana na Manispaa ya Temeke wakaliangalia upya suala hili na kulitafutia ufumbuzi wa muda mrefu kwa manufaa ya walio wengi.

(ii) Ujenzi wa mradi wa Maji uliopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru - Kamati ilitembelea mradi huo wa maji wenye kisima chenye urefu wa mita 78 chenye uwezo wa kutoa lita 30,000 za maji kwa saa. Mradi huu ni mkubwa na una uwezo wa kutoa huduma ya maji kwa watu 10,000 kama utafanya kazi muda wote. Tatizo linaloukabili mradi huu ni kuwa chini ya Mamlaka ya maji ambayo haina uwezo wa kutosha wa kuendesha mradi. Mradi umekuwa ukisimama kutoa huduma kutokana na Mamlaka kushindwa kulipa gharama za umeme inaotumia.

Aidha, Halmashauri imekuwa ikilipa gharama za umeme ili wananchi wapate huduma ya maji suala ambalo liko nje ya bajeti ya mwaka husika. Hivyo, kufuatia kuwepo kwa hali hiyo, Halmashauri inaomba ufanyike utaratibu ambao utaruhusu baadhi ya miradi ya maji ambayo Mamlaka inashindwa kuiendesha irudishwe kwenye Halmashauri husika ili kuwapunguzia wananchi tatizo la ukosefu wa maji.

Mheshimiwa Spika, ipo miradi ambayo Kamati iliridhika na utekelezaji wake ambayo ilionyesha thamani halisi ya fedha iliyotumika. Aidha, ni miradi ambayo itaendelea kuwa na tija kwa miaka mingi. Ifuatayo ni miradi iliyotekelezwa vizuri kwa kuzingatia matumizi mazuri ya fedha za umma:-

(i) Ujenzi wa Nyumba ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo. Kamati ilitembelea nyumba ya Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo ambayo ujenzi wake ulianza katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 na kupendezeshwa nayo sana. Kwa ujumla nyumba imejengwa kisasa na inapendeza sana. Aidha, Kamati ilishauri Halmashauri zingine ziige mfano wa nyumba hiyo kwa ajili ya Wakurugenzi wao. Kufuatia kuridhika nayo, Kamati iliagiza Wakaguzi wakague thamani halisi ya nyumba hiyo ili Halmashauri zingine zishauriwe kujenga nyumba kama hiyo.

(ii) Ujenzi wa Soko la Kimataifa la Isunta lililopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi - Kamati ilishuhudia soko kubwa, zuri na lililojengwa katika hadhi ya Kimataifa. Soko hilo bado halijakamilika lakini mpaka hatua iliyofikiwa limekwishagharimu jumla ya Sh. 359,000,000. Aidha, Kamati inaipongeza sana Halmashauri ya Nkasi kwa kuweza kujenga soko zuri ambalo litatumika kwa muda mrefu kwa maana lina *facilities* zote zinazohitajika katika eneo la soko. Pamoja na hayo, Halmashauri iliagizwa kuzungushia uzio eneo la soko na ufanywe utaratibu wa kuweka mfumo wa kuvuna maji.

(iii) Mradi wa kutengeneza hariri kwa kutumia Viwavi, uliopo katika Kijiji cha Nyabihanga kilichopo kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi. Kamati ilitembelea mradi huu ambao umeibuliwa na wananchi na kufadhiliwa na Halmashauri ambao unaendeshwa na kikundi cha Jijenge.

Aidha, mradi ni mzuri, unaendelea vizuri na unawapatia faida nzuri wanakikundi. Kamati inapongeza ubunifu huo wa wanakikundi na Halmashauri kwa ujumla.

(iv) Ujenzi wa Kituo cha Afya cha Nanguruwe kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara. Ujenzi wa jengo hilo umekamilika vizuri na kugharimu jumla ya Sh. 30,000,000 kutoka Mfuko wa Maendeleo wa *LGDG*. Jengo limewekwa marumaru kwenye sakafu, madirisha ya vioo na *grill*. Aidha, Kamati ilivutiwa na uzuri na umadhubuti wa jengo la Zahanati hiyo.

(v) Kamati vilevile ilifanikiwa kutembelea maporomoko ya Tembwa ambayo yapo katika Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ambayo ni vema yakatumika kutengeneza umeme, nishati ambayo ni tatizo kubwa katika Halmashauri za Mkoa wa Rukwa hususan Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi. Aidha, maporomoko hayo yanaunganishwa na mito midogo minne ambayo ni Kisumbwa, Kokwe, Msuku na Mafinga.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla matatizo yote hayo tuliyoyatolea mfano ni kutokana na tatizo kubwa la kutofuata miongozo ya Kitaifa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo na hivyo kufanya miradi mingine kukosa fedha za utekelezaji, au kutekelezwa chini ya viwango vilivyokusudiwa.

Sambamba na tatizo hilo, pia utekelezaji wa miradi mingi hasa ile ya ujenzi katika ngazi ya Kata, haufuati ushauri wa kitaalam unaotakiwa kutolewa na Idara husika. Katika baadhi ya majengo, wahandisi hawajawahi kuonekana wala kutoa ushauri toka majengo hayo yaanze kujengwa mpaka yamepauliwa. Hali hii imechangia kwa kiasi kikubwa miradi kutokamilika katika muda uliokusudiwa ama kukamilika ikiwa katika kiwango cha chini. Kila sehemu yenye matatizo hayo Kamati ilikemea tabia hiyo na kushauri wahusika watekeleze wajibu wao mara moja la sivyo watahesabika kushindwa kuyamudu majukumu yao ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri zetu hakuna utamaduni endelevu wa kuyafanyia ukarabati wa mara kwa mara majengo ya Serikali ili yazidi kuwa imara. Hii imejidhihirisha katika majengo mbalimbali ya vituo vyetu vya afya, nyumba za walimu, masoko na madarasa ambapo majengo hayo kama si kwamba yanavuja, basi yana nyufa kubwa, yamepasuka na kutoboka sakafu au yameparuliwa rangi na kuonekana machakavu. Katika hili Kamati kila ilipopita iliwaagiza Wakuu wa Idara zenye miradi yenye kuhusika na uchakavu huo kutumia *OC* zao kuhakikisha wanafanya *routine maintanance* kwa miradi iliyo chini yao bila kusubiri Kamati iwakague ama kuwatolea karipio au maagizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kupongeza sana Watanzania wote kwa kukubali kwao kutoa michango pale inapohitajika kwa nguvu zao zote. Hata hivyo, nguvu na michango ya wananchi katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo havithaminishwi kupata uhalali wake kifedha, hivyo kutowatia moyo kabisa wananchi kujiingiza katika utekelezaji wa baadhi ya miradi katika baadhi ya maeneo. Lakini pia kutothaminishwa kwa nguvu hizo kunaweza kuhusishwa na ubadhirifu kwa fedha zinazotolewa na Serikali au kwamba zinatumika lakini kwa kiasi kidogo sana huku mzigo mkubwa wa utekelezaji ukiachwa kwa wananchi kujitolea.

Kutokuwepo kwa mchanganuo wa nguvu za wananchi ni hatari kwani kuna hatari ya kujua kama kweli ni wananchi walitoa mchango wao au ni fedha za Serikali ndizo zilizotumika katika ujenzi wa mradi husika. Lakini pia katika Halmashauri zetu bado hakuna uwazi wa kutosha katika kuwaonyesha wananchi na wadau wengine wa maendeleo kiasi cha mapato na matumizi katika kila mradi na katika baadhi ya zabuni. Jambo hili huwavunja moyo wananchi na wadau wengine wa maendeleo hasa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati. Pamoja na ushauri au mapendekezo tuliyotoa kwenye mambo ya jumla, Kamati inapenda kuongeza mapendekezo yafuatayo ambayo inaamini yataboresha utendaji kazi kwa Halmashauri zetu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kuendeleza jitihada za makusudi za kuiwezesha Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Kama tulivyopendekeza katika Taarifa yetu ya mwaka jana kuwa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi iwezeshwe katika kukabiliana na changamoto ya kupanuka kwa mawanda ya ukaguzi inayotokana na maboresho mbalimbali yanayofanywa na Serikali kwa lengo ka kupeleka madaraka katika ngazi za chini kupitia utaratibu wa *D by D*. Kamati yangu kwa kuelewa kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kuhakikisha maboresho na mabadiliko yanayofanywa na Serikali yanakuwa endelevu na kuleta tija na ni muhimu kwa wadau wote kuhakikishiwa kuhusu uwezo wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika kusimamia fedha na rasilimali nyinginezo za umma, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuweka juhudi za makusudi katika kuhakikisha Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inaimarishwa ili kutoa hali halisi ya usimamizi wa rasilimali za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ambayo itatumika kama kipimo cha mafanikio ya maboresho yanayofanywa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali ikamilishe mapema mchakato wa kuboresha mfumo wa ukaguzi wa ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali kilio cha *CAG* na Kamati kuhusu mfumo imara wa Ukaguzi wa Ndani kwa kuleta Bungeni Muswada wa Sheria wa kuunda mfumo huo. Mchakato wa maandalizi ya Sheria unaoendelea ni hatua nzuri na muhimu sana katika kuboresha mfumo wa Ukaguzi wa Ndani, kama sehemu ya kuimarisha usimamizi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha na mali za umma. Kamati inashauri kuwa ni vema basi maboresho hayo yakahusisha marekebisho katika Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na. 9 na Kanuni za Usimamizi wa Fedha na Mali za Umma yaani *Local Authorities Financial Memorandum* kama Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na Kamati ya *LAAC* ilivyosisitiza katika Taarifa ya mwaka 2006/2007, iliyowasilishwa Bungeni Aprili, 2009.

Aidha, uwepo wa mamlaka hiyo si tu utasaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha maslahi, uwajibikaji na kuondoa utegemezi wa kimaslahi wa Wakaguzi wa Ndani kutoka kwa Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, bali pia itaongeza kuaminika kwa Taarifa za Wakaguzi wa Ndani na udhibiti katika matumizi ya fedha za umma. Hivyo, Kamati inawaomba Waheshimiwa Wabunge kushiriki kikamilifu katika kupitisha Sheria

itakayosimamia maboresho ya mfumo wa Ukaguzi wa Ndani pindi Muswada wake utakapoletwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa Mhasibu Mkuu atakayesimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kama inavyoeleweka utaratibu wa *D by D* unalenga katika upelekaji wa madaraka katika ngazi za chini hususan Halmashauri zetu. Utaratibu huu unahitaji kuwepo kwa usimamizi wa hali ya juu wa ruzuku toka Serikali Kuu kwenda kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Hivyo kufuatia kuwepo kwa hitaji la mfumo ulio wazi katika utoaji na usimamizi wa ruzuku ya Serikali inayokwenda kwenye mamlaka hizo, Kamati yangu inaungana na moja kati ya mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ambalo ni kuwepo kwa Mhasibu Mkuu atayesimamia masuala yote ya fedha na uhasibu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, Kamati inasisitiza umuhimu wa kuanza mapema iwezekanavyo mchakato wa kuunda sheria itakayounda mamlaka hiyo na kumpa madaraka ya kuzisimamia mamlaka za Serikali za Mitaa kuondoa hali ya utata ambayo imekuwa ikijitokeza mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha ukusanyaji mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani. Kama nilivyosema awali, uwezo wa kujitegemea wa Halmashauri zetu kupitia mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani umezidi kushuka katika mwaka 2007/2008. Vivyo hivyo tumeshuhudia jinsi ambavyo utaratibu wa kutumia Mawakala kama wakusanyaji wa mapato ulivyowanufaisha Mawakala hao zaidi ya Halmashauri zenyewe. Hivyo, kufuatia mapungufu hayo Kamati inaziagiza Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha zinafanya uchambuzi yakinifu juu ya mapato yake halisi kabla ya kuingia mkataba na Mawakala hao.

Aidha, Mikataba yote itakayoingiwa na Halmashauri katika kutoa zabuni za ukusanyaji mapato lazima ipitiwe na Wanasheria wenye uwezo ili kuepuka mikataba inayoziletea hasara Halmashauri zetu. Sambamba na hilo, Halmashauri zenye vivutio vya uwekezaji ni vema ikavinadi kwa Wawekezaji kwa lengo la kuongeza mapato lakini zifanye hivyo kwa maslahi ya walio wengi (wananchi) na kwa kufuata sheria na taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeendelea kuona makadirio ya makusanyo ya mwaka yakipachikwa tu bila kufanyiwa uchambuzi wa kina kwa kuzingatia takwimu sahihi ambapo matokeo yake tunaona Halmashauri zinakusanya zaidi au pungufu ya makadirio ya makusanyo iliyojiwekea kwa vyanzo vya ndani. Aidha, tumeendelea kuona utegemezi kwa Wahisani unavyozidi kuongezeka wakati kila mdau wa maendeleo anafahamu kuwa utegemezi huu utakwisha tu iwapo kila Halmashauri itasimamia vizuri ukusanyaji wa mapato katika vyanzo vyake vya ndani na kubuni vyanzo mbalimbali ambavyo kwa sasa mapato yake hayakusanywi. Kwa kuzingatia hilo, Kamati imeendelea kuagiza Halmashauri zote kuandaa Mpango Mkakati wa muda mfupi na mrefu ambapo katika mpango mkakati wa muda mrefu, Halmashauri zizingatie kuweka jitihada za kuhakikisha ifikapo 2025, uwezo wa kujitegemea uwe ni asilimia 50.

Aidha, ni muhimu kuanzia sasa wananchi na Watendaji katika Halmashauri zetu kuwa makini katika kuondoa mianya yote ya ubadhirifu na udokozi ili tuweze kukamilisha ndoto yetu ya muda mrefu ya kujitegemea kama Taifa katika kuendesha shughuli za Serikali yetu kwa manufaa ya Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa Miaka iliyopita. Mapendekezo kadhaa yalitolewa na Kamati yangu pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi katika ukaguzi wa mwaka wa 2006/2007. Kamati yangu ilipokea majibu ya Serikali kupitia kwa Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI mnamo tarehe 18 Oktoba, 2009 ilipofanya Kikao na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI. Hata hivyo, majibu tuliyoyapokea yaligusia tu mchakato unaoendelea katika kutekeleza mapendekezo hayo pasipo kwenda kwa undani katika kutoa majibu yanayojitosheleza juu ya mikakati na juhudi za makusudi zilizowekwa kwa lengo la kutekeleza mapendekezo hayo kikamilifu.

Hii ni kinyume na matarajio ya Bunge ambalo linaitaka Serikali kuwasilisha nakala ya majibu na mpango kazi ukielezea namna ya kuyatekeleza mapendekezo ya ripoti za Kamati za Bunge za Kiuchunguzi pamoja na ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hili ni hitaji la kisheria. Kutotekelezwa kwa mapendekezo ya mamlaka hizi kunaweza kusababisha kujirudia kwa mapungufu yaliyobainika awali katika ripoti za kaguzi zilizopita na kurudisha nyuma jitihada za kuboresha usimamizi wa fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Hivyo, ni vema Serikali kwa kupitia vyombo vyake ikaweka mikakati ya makusudi ya kushughulikia kwa dhati mapendekezo ya Wakaguzi na Kamati za Bunge yenye lengo la kuboresha usimamizi wa fedha za umma na ikumbukwe kuwa fedha nyingi, juhudi kubwa na muda mwingi hutumiwa na vyombo hivi kwa lengo la kuchunguza matatizo kwenye mifumo ya fedha na kisha kutoa mapendekezo yenye lengo la kuondoa matatizo hayo.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri kuacha utaratibu wa kuwasilisha Nyaraka Muhimu kwa Wakaguzi mara baada ya Ukaguzi kumalizika ili zifanyiwe uthibitisho. Ili kuziba kabisa mianya ya ubadhirifu, Kamati yangu inaendelea kuzishauri Halmashauri kuacha utaratibu wa kuwasilisha nyaraka muhimu (mfano risiti, mikataba na kadhalika) kwa Wakaguzi mara baada ya ukaguzi kumalizika ili zifanyiwe uthibitisho. Utaratibu huu unatoa mwanya kwa Watumishi husika kutafuta nyaraka, mathalan *delivery note*, *cash receipts* na nyinginezo, kwa lengo la kuhalalisha matumizi yanayosemekana kufanyika. Hakuna sababu itakayomfanya Afisa Mhasibu tena mwenye cheti, kutokuwa na nyaraka zote zilizohitajika kabla ya malipo na kuzihifadhi katika *batch* tayari kwa kukaguliwa na Wakaguzi.

Mheshimiwa Spika, ushauri huu unalenga kupunguza ama kuondoa kabisa uwepo wa *unvouched or/and improperly vouched payments, missing receipts or/and books of accounts, items not in ledger* na nyinginezo. Kamati yangu inategemea kuwa ushauri huu wa Kamati utaungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge wote hasa wanapohudhuria vikao vya Kamati za Fedha katika Halmashauri zao na viongozi wote wenye majukumu ya kusimamia matumizi ya Fedha za Umma.

Aidha, Kamati inasisitiza, TAMISEMI kuunga mkono azimio la Kamati kuhusiana na kuwataka watendaji wawapatie Waheshimiwa Madiwani Taarifa ya kina katika vikao vyao hasa Kamati za Fedha, Uchumi na Mipango ili waweze kusimamia kikamilifu fedha za Umma na rasilimali zinazopelekwa na Taifa na kutumika katika ujenzi wa miradi mbalimbali katika Halmashauri zao. Bila kukubaliana na pendekezo hili na kuliingiza katika mfumo wetu wa usimamizi wa fedha, jitihada na kauli zote za maisha bora kwa kila Mtanzania zitabaki kuwa ndoto. Mfumo wa sasa hauwawezeshi Waheshimiwa Madiwani kusimamia matumizi ya fedha.

Mheshimiwa Spika, Serikali ihakikishe fedha za utekelezaji wa miradi zinapatikana na kuzifikia Halmashauri mapema kwa lengo la kukamilisha miradi kwa wakati. Kutokana na utegemezi mkubwa uliopo wa Mamlaka hizi kwa Serikali na wepesi wa wananchi katika uibuaji wa miradi ya maendeleo, ni vyema Serikali ikahakikisha kuwa fedha za miradi kama zilivyoidhinishwa kwenye bajeti zinapatikana na zinapelekwa kwenye Halmashauri mapema kama ilivyopangwa katika Bajeti ya mwaka husika ili zitumike kukamilisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wakati na kama ilivyokusudiwa. Aidha, si tu kuna umuhimu wa fedha hizo kutolewa mapema na kwa wakati muafaka bali hata kwa kiwango kilichokubalika na kuidhinishwa na Bunge ili utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyokusudiwa ufanyike kwa ufanisi na hatimaye miradi hiyo iwe na tija kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inasisitiza hili, kutokana na ukweli usiopingika kuwa kinachosababisha miradi mingi ya maendeleo kutokamilika kwa wakati au mingine kutokamilka kabisa, ukiachilia mbali uzembe unaoweza kujitokeza katika usimamizi wa miradi hiyo, ni suala zima la kutopatikana au kucheleweshwa kwa fedha za utekelezaji wa miradi kutoka Serikali Kuu kwenda kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hivyo ni vema Serikali ikajipanga katika kuweka mikakati ya makusudi itakayopunguza au kuondoa kabisa tatizo hili ambalo kwa kiasi kikubwa linachangia kurudisha nyuma maendeleo ya Halmashauri zetu. Ni muhimu kabla ya kupeleka Bungeni makisio ya mapato na matumizi, Serikali iwe imefikia makubaliano ya uhakika ili kuondoa tatizo la fedha za Wafadhili kuchelewa kutoka na pale zinapotoka fedha za Wahisani zisicheleweshwe na Serikali Kuu kupelekwa kule zilikokusudiwa kutumika.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa mipango ya maendeleo uzingatie bajeti ya mwaka husika. Kamati yangu inaendelea kusisitizia umuhimu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kupanga matumizi kwa kuzingatia fedha zilizotengwa kwenye bajeti ya mwaka husika kama ambavyo Kanuni ya 85(3) ya Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2001 pamoja na marekebisho yake inavyomtaka Afisa Masuhuli kupanga matumizi kwa kuzingatia Bajeti ya mwaka husika wa fedha. Utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya mamlaka za Serikali za Mitaa usipozingatia bajeti ya mwaka wa fedha husika, huisababishia Serikali kurudia zoezi la kupeleka fedha kwa ajili ya shughuli ambayo awali ilitengewa fedha vilevile husababisha Halmashauri kushindwa kutimiza majukumu yake ikiwemo kutokamilisha miradi kwa wakati au kuikamilisha katika kiwango cha chini.

Aidha, linaloshabihiana na hili ni suala la mamlaka hizi kubadili malengo ya matumizi ya fedha yaani bila kupima athari itakayotokea katika utekelezaji wa miradi mingine ya maendeleo na wakati mwingine hufanya hivyo bila kupitisha maombi katika vikao vya kisheria vya Baraza la Madiwani na Kamati ya Fedha na Mipango au kupata kibali cha Wizara ya Fedha (Hazina). Hivyo, kufuatia uwepo wa ukiukwaji wa Sheria unaoandaa mazingira ya ubadhirifu wa fedha za umma, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa utekelezaji wa mipango ya maendeleo uzingatie bajeti ya mwaka husika na utaratibu wa kubadili malengo ya matumizi ya fedha ufuate Sheria na Kanuni za fedha zilizopo.

Mheshimiwa Spika, kuongeza ufanisi katika utayarishaji na utoaji wa taarifa za fedha za Halmashauri. Kufuatia kuwepo kwa utofauti katika utayarishaji na utoaji wa taarifa za fedha miongoni mwa Halmashauri kulikosababishwa na kuwepo kwa miongozo mbalimbali inayokinzana juu ya namna ya utayarishaji na utoaji wa taarifa za fedha kwa mwaka wa fedha 2007/2008, Kamati yangu inashauri kuundwa kwa Mamlaka ambayo itakuwa na majukumu sawa kama yale ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ambayo ni kusimamia masuala ya fedha na uhasibu lakini yenyewe itasimamia masuala hayo kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, kama nilivyoeleza pia hapo juu. Uwepo wa Mamlaka hiyo si tu utasaidia kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma bali pia utaondoa tatizo la kuwepo kwa miongozo isiyofanana juu ya utoaji wa taarifa za fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kama ilivyojitokeza katika mwaka wa fedha wa 2007/2008.

Aidha, kufuatia utayarishaji usioridhisha wa taarifa za fedha unaofanya na Mamlaka za Seriakali za Mitaa,Kamati yangu inaendelea kusisitiza umuhimu wa Wakuu wa Idara kushirikiana katika utayarishaji wa Taarifa hizo na utaratibu wa kuandaa mchanganuo wa matumizi ya fedha katika kila mradi ikionyesha kila kilichonunuliwa uendelee kutumika kwa Taarifa za fedha zinazoletwa kwenye Kamati ya *LAAC* na utumike vilevile kwa Taarifa za fedha za kila mwezi zinazowasilishwa kwenye Kamati za Fedha na Mipango kwenye kila Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Serikali ihakikishe utekelezaji wa miradi unazingatia ushauri wa kitaalam, ubora na miongozo iliyowekwa. Miradi mingi ya maendeleo hususan miradi ya ujenzi inayotekelezwa katika ngazi ya vijiji haifuati miongozo na ramani zilizotolewa na Serikali. Ukaguzi wa thamani ya miradi umeendelea kubaini ujenzi wa majengo katika Halmashauri zetu usio na ubora na hivyo kuwepo kwa hatari ya majengo hayo kubomoka baada ya muda.

Aidha, yapo baadhi ya maeneo ambayo mazingira yake huathiri majengo kama maeneo ya Kanda ya Ziwa (Mikoa ya Mwanza, Kagera na Mara), majengo mengi yameathirika kwa popo wanaokaa kwenye dari na hivyo kusababisha majengo hayo kuwa hatarishi au kutotumika kabisa hali kadhalika maeneo ambayo yako kandokando ya bahari kama Dar es Salaam na Mafia, bati hushambuliwa na kutu itokanayo na maji ya bahari yenye madini mengi ya chumvi. Kufuatia hali hiyo, Kamati imekuwa ikishauri Halmashauri kutumia mabati yanayopitisha mwanga sehemu zenye popo wengi na sehemu za pwani mabati yapakwe rangi maalum inayozuia kutu. Aidha, ni vema Serikali

ikatoa miongozo itakayowezesha ujenzi wa majengo yote nchini ukazingatia mazingira ya eneo husika.

Mheshimiwa Spika, katika ujenzi wa majengo ya shule, baadhi ya Halmashauri hazifuati miongozo ya Serikali ya kuezeka kwa kutumia mabati ya geji 28 na kuhakikisha katika kila mfuko wa saruji unatoa matofali yasiozidi 28-30, bali Halmashauri zimekuwa zikiezeka majengo ya Shule kwa bati za geji 30 na kufyatua matofali zaidi ya 35 kwa mfuko mmoja wa Saruji. Huu ni utumiaji mbaya wa fedha za Umma na Michango ya Wananchi. Aidha, baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa hazitoi ushauri wa kitaalam kwa Kamati za Ujenzi za Vijiji, hivyo husababisha miradi ya ujenzi kutekelezwa chini ya kiwango pamoja na kuwa wahandisi ndio wanaotoa *Certificates* kabla ya malipo mbalimbali yanayohusiana na majengo hayo.

Ni muhimu Mamlaka za Serikali za mitaa zikatambua kuwa majengo haya yanajengwa kwa mategemeo kwamba yatadumu kwa muda mrefu, hivyo ni bora utekelezaji wake ukazingatia ushauri wa kitaalam, ubora na miongozo ya Serikali. Aidha, ni vema utaratibu ulioanzishwa wa kukagua utekelezaji wa miradi ukatiliwa mkazo zaidi ili kuondoa hasara ambayo Taifa inaingia kwa kuwa na majengo au miradi isiyo na ubora au isiyotumika.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha udhibiti katika mfumo wa ulipaji mishahara ya watumishi wa umma. Kufuatia kuwepo kwa udhibiti dhaifu katika mfumo wa ulipaji mishahara ya Watumishi wa umma ambao umepelekea Serikali kupoteza fedha nyingi, Kamati yangu inaunga mkono mapendekezo yaliyotolewa ma Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kuhusu umuhimu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, TAMISEMI, Ofisi ya Rais Menejimenti na Utumishi wa Umma na Wizara ya Fedha na Uchumi kuweka jitihada za pamoja za kiutendaji zenye lengo la kuhuisha kumbukumbu za mishahara ya watumishi wa umma.

Aidha, Kamati yangu ingependa kusisitiza kuwa ushirikiano huo wa kiutendaji wenye lengo la kuimarisha udhibiti wa mfumo wa ulipaji mishahara ya watumishi ni vema hatua zake za mwanzo zikakamilika mapema na kisha Mamlaka hizo zikaweka utaratibu endelevu ambao utadhibiti kabisa hasara zinazoweza kutokea kutokana na udhibiti hafifu katika mfumo wa ulipaji mishahara. Kamati yangu haioni sababu ya kuwepo kwa Watumishi hewa, wakati malipo yote yanafanywa katika ngazi ya Wilaya, ambapo Watumishi waliostaafu, waliofariki na waliofukuzwa kazi wanajulikana. Kila mwaka, Kamati inakutana na hoja inayohusu mishahara isiyorejeshwa Hazina, ni dhahiri kwamba kuna udanganyifu unaofanyika kwa muda mrefu.

Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuwa makini katika kusimamia mfumo wa ulipaji mishahara ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua kali za kinidhamu kwa Watendaji wanaojihusisha na udanganyifu huo na iwe desturi kwa Serikali kutoa maelezo ya hatua zilizochukuliwa kwa Watendaji hao mbele ya Bunge. Aidha, utaratibu wa kurejesha fedha hizo kupitia Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa (*RAS*) uangaliwe upya, kwani kuna uwezekano mkubwa wa *double accounting*, iwapo taarifa za fedha hazitahuishwa kikamilifu, hali ambayo itatoa mwanya mwingine wa ubadhirifu.

Mheshimiwa Spika, Serikali kuboresha mazingira ya kazi kwa lengo la kutatua tatizo la upungufu wa watumishi katika Halmashauri. Lengo la Serikali katika dhana yake ya *D by D* ni kupeleka madaraka katika ngazi za chini kwa nia ya kuzijengea uwezo mamlaka hizo wa kutoa huduma bora kwa wananchi ili kufikia malengo makuu ya MKUKUTA, *Millenia, Vision* 2025 na hata Kaulimbiu ya Kilimo Kwanza. Ni jambo lisilopingika kuwa utoaji wa huduma bora pamoja na mambo mengine hutegemea sana hali ya watoaji huduma wenyewe. Hivyo, Serikali haina budi kupeleka Watumishi wa kutosha katika Halmashauri zetu na kuwaboreshea mazingira ya kazi ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi na hatimaye Taifa kutimiza malengo iliyojiwekea.

Kamati yangu ingependa kuishauri Serikali kuanzisha Mifuko ya kuboresha Mazingira ya Watumishi katika Halmashauri zetu ambayo itatungiwa sheria ndogo za kuhimiza uchangiaji wa wananchi kwa lengo la kupunguza tatizo la upungufu wa watumishi kama Walimu, wauguzi na madaktari. Aidha, Mikoa iendelee kuomba vibali vya kuajiri ili kutosheleza ikama inayohitajika katika Halmashauri zetu. Vivyo hivyo, Halmashauri ziendelee kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa Watumishi waliopo kwa nia ya kuwaendeleza. Aidha, ni vema Serikali ikaangalia uwezekano wa kutoa posho ya mazingira magumu (*Hardship allowance*) kwa watumishi wa mikoa yenye mazingira magumu ya kazi.

Mheshimiwa Spika, kuboresha utekelezaji wa shughuli za kamati. Katika mwaka tunaotolea Taarifa, Kamati imefanikiwa kutembelea miradi ya maendeleo katika Halmashauri za mikoa kumi na saba (17). Utaratibu huu wa kutembelea miradi ya maendeleo baada ya kupitia vitabu vya Hesabu vya Halmashauri umeonekana kuwa na tija zaidi kwani si tu umezisukuma Halmashauri katika kukamilisha miradi iliyotelekezwa kwa muda mrefu kwa kuogopa kuwa Kamati ingebaini matumizi mabaya ya fedha na uzembe katika utendaji na hivyo kuwachukulia hatua mbalimbali wahusika, bali pia umeisaidia Kamati kujiridhisha na kile kinacholetewa kwenye taarifa za fedha kama kimetekelezwa na ni kwa kiwango gani ili iweze kutoa ushauri unaofaa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa kwa kiasi kikubwa Halmashauri nyingi sasa zinapata hati safi. Lakini Kutokana na niliyoyaeleza awali kuwa Hati safi haina maana ya kuwa hakuna ubadhirifu wala wizi wa mali ya umma, bali inasaidia mwenye mali kupata uwezo wa kugundua zaidi ubadhirifu na matumizi mabaya ya fedha zake, Kamati inashauri kuwa mfumo wa utekelezaji wa kazi zake uendelee kujikita katika kutembelea miradi ya maendeleo kama ilivyofanya katika kipindi cha mwaka tunaotolea taarifa, ili Kamati ipate fursa kubwa ya kujiridhisha na yale yaliyoandikwa kwenye vitabu vya Hesabu vya Halmashauri.

Aidha, nia ya Kamati ya kuwashirikisha Waheshimiwa Madiwani wa Kamati za Fedha kwenye ukaguzi wa miradi, baada ya muda itawajengea Waheshimwa Madiwani uwezo wa kusimamia na kukagua miradi kikamilifu na pindi hatua hiyo ikifikiwa, hakutakuwa na lazima tena wa Kamati kuzunguka nchi nzima kwa lengo la kukagua miradi. Ni imani ya Kamati kuwa ushauri huu utapokelewa na Bunge lako Tukufu na Kamati itaendelea kuwezeshwa katika utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi ili

kuhakikisha kuwa fedha zinazotolewa na Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo zinatumika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha Taarifa ya Kamati, naomba tena nitumie fursa hii kukushukuru na kukupongeza kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Shughuli za Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa kipindi kilichomalizika.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, naomba kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuona umuhimu wa kuondoa ubadhirifu wa fedha za Umma na kusisitiza kuwa kilimo ndio uti wa mgongo katika juhudi za kujiondoa katika utegemezi wa kiuchumi na kupunguza umaskini katika Taifa. Napenda kuunga mkono juhudi hizi kwa kusema kwamba tukiweza kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma na kuweka jitihada zetu za makusudi katika kukuza kilimo, Taifa letu litajikwamua kwenye umaskini na kuondoka kwenye hali ya kutegemea misaada toka kwa Wafadhili.

Mheshimiwa Spika, aidha kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati yangu, napenda kutoa shukurani za pekee kwa Mheshimiwa Mizengo Pinda, Waziri Mkuu na Mheshimiwa Celina Kombani, Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Katibu Mkuu, TAMISEMI, Bibi. Maimuna Tarishi, kwa jinsi wanavyothamini sana shughuli zinazofanywa na Kamati yangu na kwa jinsi wanavyojitahidi kuboresha Mfuko wa Serikali za Mitaa kwa lengo kuleta maendeleo endelevu kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza sana Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yangu ambao uliwateua kwa mujibu wa Kanuni ya 113(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2007, kwa ushirikiano wao na kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kipindi chote cha mwaka mmoja. Aidha, niseme kwamba ni jambo la kushukuru sana kuwa na Wajumbe wenye moyo wa kujitolea usio na kikomo, ushirikiano wa dhati na uadilifu wa kuigwa kama waliouonyesha wajumbe wa Kamati hii. Hivyo basi, Kwa heshima naomba kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dr. Willibrod P. Slaa, Mwenyekiti; Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Halima O. Kimbau, Mjumbe; Mheshimiwa Dr. Juma A. Ngasongwa, Mjumbe; Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama, Mjumbe; Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, Mjumbe; Mheshimiwa Samueli M. Chitalilo, Mjumbe; Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, Mjumbe; Mheshimiwa Mwanne S. Mchemba, Mjumbe; Mheshimiwa Riziki S. Lulida, Mjumbe; Mheshimiwa Ernest G. Mabina, Mjumbe; Mheshimiwa Eng. Laus O. Mhina, Mjumbe; Mheshimiwa Dunstan D. Mkapa, Mjumbe; Mheshimiwa Idd M. Azzan, Mjumbe; Mheshimiwa Bernadeta K. Mushashu, Mjumbe; Mheshimiwa Eng. Benito W. Malangalila, Mjumbe; Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mjumbe; Mheshimiwa Zabein M. Mhita, Mjumbe na Mheshimiwa Ahmed A. Salum, Mjumbe.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii imeniomba nifikishe salaam rasmi zao kwako na hasa kukuomba utakapopata nafasi wanakaa ufike siku moja uone kazi inayofanywa na Kamati hii mara nyingi huanza saa tatu mpaka saa sita usiku kwa sababu kupitia kila ukurasa kubaini haya ambayo tumeyasema. Tunakuomba siku moja ukipata nafasi uweze kufika.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru Wenyeviti, Wakurugenzi pamoja na Watendaji wa Halmashauri ambao ndio wenye jukumu la kuhakikisha Halmashauri zetu zinawajibika kikamilifu kwa wananchi katika kuwaletea maendeleo yaliyokusudiwa. Kimsingi, hawa ndio wanaoziendesha Halmashauri zetu na kwa maendeleo madogo ambayo yamepatikana hatuna budi kuwashukuru na kuwapa moyo wa kuendeleza jitihadi za makusudi za kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma, jitihada ambazo hatimaye zitaleta maendeleo endelevu katika Halmashauri zetu na kupunguza umaskini katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, Ndugu Ludovick S.L. Utouh na Watendaji wake, kwa umahiri wao katika kufanya ukaguzi wa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa na pia katika kutolea ufafanuzi Taarifa za kaguzi hizo pindi zinapojadiliwa wakati wa vikao vya Kamati. Aidha, shukurani za dhati nazitoa kwa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (*NAO*) kwa kuiwezesha Kamati yangu kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo katika Halmashauri za Mikoa yote 21 kwa mwaka unaohusika na ukaguzi. Lakini pia nawashukuru Maafisa Waandamizi kutoka Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Hazina hususan Bibi Batuli Kilo, Bibi. Raheli Ntiga na Ndugu Andrew Mzikila, Ofisi ya Waziri Mkuu-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), hususan Ndugu L.W Kabuje na Ndugu Mbilinyi, ambao walishirikiana ipasavyo na Kamati katika kutoa ufafanuzi na mchango wa kitaalam katika masuala mbalimbali. Aidha, niwapongeze sana kwa juhudi na kujitolea kwao kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa shughuli za Kamati.

Mwisho kabisa, Mheshimiwa Spika, niwashukuru na kuwapongeza Ndugu Mathew Kileo pamoja na Ndugu James Warburg, Makatibu wa Kamati yetu, chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge, Dr. Thomas D. Kashilillah, kwa ushirikiano wao na kwa kazi nzuri ya kuandaa, kuratibu na kuihudumia Kamati hasa katika kutoa ushauri wa kitaalam juu ya namna ya kuendesha shughuli za Kamati yetu kwa kufuata misingi ya Kanuni zilizowekwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. (Makofi)

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Slaa ahsante sana. tumepokea taarifa, sasa hoja ya tatu ni ile ya Hesabu za Mashirika ya Umma ambayo inawasilishwa na Mwenyekiti Mheshimiwa Kabwe Zitto. Kabla hujaongea nilitaka kuwakumbusheni maana yake mmeonekana kama baadhi yenu hamjazingatia hilo. Kanuni ya 62 (1) (C) inasema hivi

nanukuu. *"Mwenyekiti anayewasilisha maoni ya Kamati atayawasilisha* Kwa muda *usiozidi dakika 30."* Kwa hiyo kama mlijiandaa kwa saa moja basi mlikuwa mmeghafilika. Basi tuendelee sasa.

**MHE. KABWE Z. ZITTO - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma kwa mujibu wa Kanuni ya 114(15) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007).

Mheshimiwa Spika, naomba taarifa yote hii kama jinsi ambavyo imeandikwa ndiyo itokee kwenye *Hansard* pamoja na yale nitakayokuwa nimeongezea kutokana na suala hilo hilo la muda ambalo wenzangu wamelielezea.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, pamoja na masuala mengine, maoni na mapendekezo ya Kamati juu ya Hesabu, ufanisi wa Mashirika ya Umma na utekelezwaji wa Sera ya Ubinafsishaji nchini. Maoni na Mapendekezo haya ni kufuatia Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Mashirika ya Umma nchini kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Juni, 2008.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Majukumu ya Kamati yameainishwa katika Sehemu ya Tatu ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007 chini ya Kanuni ya 115, kifungu cha 13 katika Fasili Ndogo (a) hadi (e) kuwa ni:-

(a) Kushughulikia taarifa za kila mwaka za hesabu zilizokaguliwa za mashirika ya umma;

(b) Kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za Mashirika ya Umma yaliyoainishwa katika taarifa za kila mwaka za Mashirika hayo na kutoa mapendekezo na ushauri wa namna ya kuyaondoa matatizo hayo;

(c) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati hiyo ili kuondoa matatizo hayo;

(d) Kutathmini ufanisi wa Mashirika ya Umma; na

(e) Kufuatilia utekelezwaji wa Sera ya Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu njia au mbinu zilizotumiwa na Kamati kufanya kazi. Kamati ilitumia mbinu mbalimbali ili kutekeleza wajibu wake, zikiwemo:-

(i) Semina za mafunzo kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Msajili wa Hazina. Lengo la semina hizi lilikuwa ni kupata taaluma ya jinsi ya kusoma na kutafsiri taarifa mbalimbali za ukaguzi wa hesabu za Mashirika.

(ii) Kujadili na kuchambua taarifa za hesabu zilizokaguliwa za Mashirika mbalimbali kwa kuwaita Maafisa Masuuli (Wenyeviti wa Bodi na Wakurugenzi

Watendaji Wakuu wa Mashirika hayo ili wajibu hoja na kutoa maelezo mbalimbali kwenye Kamati).

(iii) Kufanya ziara. Kwa mfano:-

· Ziara za kujiridhisha na thamani na uwepo wa miradi (*expenditure tracking site visits*) kwa Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro, Shirika la Hifadhi za Taifa (*TANAPA*), Chuo Kikuu cha Dodoma, Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Jiji la Mwanza na Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Shinyanga- Kahama.

· Ziara za kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Ubinafsishaji katika Kiwanda cha Sukari cha Kilombero na Kiwanda cha Saruji cha Mbeya.

(iv) Kukutana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Wakuu wa Mifuko ya Hifadhi za Jamii nchini, Uongozi wa *TANESCO*, *TPDC* na Msajili wa HAZINA kwa ajili ya kikao cha mashauriano ambacho Kamati iliitisha kwa ajili ya kujadiliana uwezekano wa Mifuko ya Hifadhi za Jamii nchini kuwekeza katika miradi ya uzalishaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vitendea kazi vya Kamati. Katika kutekeleza majukumu yake Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma hutumia nyenzo zifuatazo:-

(i) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 kama ilivyofanyiwa marekebisho mara kwa mara na hasa kuhusu mamlaka ya Bunge na Kamati zake.

(ii) Kanuni za Bunge (Toleo la Mwaka 2007).

(iii) Bajeti ya Mwaka ya Kamati.

(iv) Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (kwa Mwaka ulioishia 30 Juni, 2007).

(v) Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2001 pamoja na marekebisho yake, Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2001 na Sheria iliyoanzisha kila Shirika husika.

(vi) Taarifa za Msajili wa Hazina kama Mhisa Mkuu kwa niaba ya Serikali katika mashirika yote ambapo Serikali imewekeza.

(vii) Taarifa za mahesabu za kila Shirika kwa Mwaka wa Fedha unaojadiliwa ikiambatanishwa na majibu ya hoja za Ukaguzi kutoka katika Manejimenti ya kila Shirika lililojadiliwa.

(viii) Taarifa za kitafiti kutoka maeneo mbalimbali juu ya mambo yanayogusa majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, ufuatiliaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika taarifa ya kamati ya mwaka 2007/2008. Katika kutekeleza majukumu yake kwa kipindi cha Mwaka 2009/2010, Kamati iliweza kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa Serikalini kupitia Taarifa yake ya Mwaka wa 2007/2008 iliyosomwa hapa Bungeni. Ufuatiliaji ulibaini kwamba zipo hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Kamati ambazo hazikujibiwa kikamilifu hivyo kuifanya Kamati ione kwamba upo uwezekano mkubwa matatizo hayo yakaendelea kuwa sugu kiasi cha kuendelea kuathiri ufanisi wa mashirika ya umma. Kwa mfano:-

(i) Suala la Taasisi mpya zilizokuwa kwenye orodha ya Msajili wa Hazina na suala hili ni suala la kampuni ya Buhemba *Goldmine* (MEREMETA), *TanGold* ambayo imekuwa ikizua mijadala mikali sana ndani na nje ya Bunge. Kamati iliiomba Serikali iweze kufuatilia na kutoa taarifa rasmi juu ya suala hili, lakini Serikali haikujibu chochote katika suala hili. Mnamo tarehe 8 Juni, 2009 Kamati ilimwandikia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili aweze kufanya ukaguzi wa taasisi hii mpya ambayo ilikuwa imetokea katika taarifa ya Msajili wa Hazina kama mitaji ya umma. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali akawa amewaandikia Hazina na Hazina mpaka leo hawajatoa ushirikiano kwa maana ya Serikali haijatoa ushirikiano kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusiana na suala hilo la Meremeta.

Mheshimiwa Spika, suala ambalo Kamati ilitaka ni kwamba mpaka tunapotoa taarifa mwaka jana, kampuni ya *TanGold* ilikuwa na akiba ya Dola za Marekani milioni 10 katika akaunti zake na vile vile kulikuwa na Mgodi wa Buhemba ambao Kamati ilikuwa inapendekeza Mgodi huu likabidhiwe Shirika la *STAMICO* pamoja na fedha hizo ili angalau tuweze kuiwezesha *STAMICO* kuweza kufanya kazi zake.

(ii) Kamati iliitaka Serikali kutoa idadi kamili ya mashirika yaliyopo ambayo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anapaswa kuyakagua. Lengo la Kamati katika hili ilikuwa ni kuwa na uelewa sahihi juu ya idadi ya mashirika na kiasi cha mitaji ya umma iliyowekezwa katika mashirika hayo. Kamati ililenga kuihamasisha Serikali kuwa na daftari la kudumu la idadi ya mashirika na mitaji inayowekezwa. Daftari hilo lingekuwa linahuishwa kwa nyakati tofauti. Serikali haikutoa majibu yoyote katika hili. Hata hivyo, Kamati bado inahitaji majibu ya hoja hizi.

(iii) Katika Mwaka wa Fedha ulioishia 30 Juni, 2007, Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mashirika ya Umma imeonekana kuwa uwekezaji katika baadhi ya mashirika uliondolewa katika orodha ya Msajili wa Hazina katika mazingira ya kutatanisha na bila maelezo ya kuridhisha. Mashirika husika na hisa za Serikali zilizoondolewa ni pamoja na:-

- *Tanzania Tea Authority Lupembe Branch (30%)*
- *Morogoro Shoe Company (30%)*
- *Moro Tanneries (45%)*
- *Industrial Promotion Services (30%)*

- *Tanzania Electrical Goods Manufacturer (30%)*
- *Kilombero Sugar Company (25%)*

Serikali haijajibu kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, ijapokuwa Taarifa ya Serikali haikuzungumzia lolote juu ya suala hili, Kamati inashtushwa na taarifa ya kwamba mali za Serikali zinaweza kuondolewa kwenye orodha ya Msajili wa Hazina kirahisi namna hii na hivyo kupelekea kupoteza kwa mali hizi.

Ushauri wa Kamati katika hili ni kwamba hati za hisa za serikali katika mashirika haya zirudishwe kwenye kumbukumbu za Serikali na pale ambapo kuna mabadiliko yoyote kuhusiana na umiliki huo mabadiliko hayo yatolewe maelezo. Sanjali na hilo, ni ushauri wa Kamati kwamba pale ambapo ubia unafanya faida, ni vizuri Serikali iangalie uwezekano wa kuuza hisa zake katika Soko la Mitaji la Dar es Salaam (*DSE*) ili kumilikisha uchumi kwa wananchi wengi zaidi na kuimarisha uwazi katika uendeshaji wa makampuni hayo.

(iv) Kamati ilishauri juu ya muundo mpya wa kuligawanya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (*TPDC*) katika Mashirika makubwa mawili tofauti; moja la kushughulikia vibali vya uchimbaji gesi na lingine la uwekezaji na kufanya biashara. Serikali haikutoa majibu yoyote juu ya ushauri huu wa Kamati. Hata hivyo, Kamati itapenda kupata majibu ya Serikali juu ya ushauri huu.

(v) Kamati ilitaka maelezo juu ya malipo ya kodi ya Makampuni (*Corporate Tax*) kati ya *TPDC* na *Pan African Energy Tanzania Limited)* ambayo imewekeza katika gesi ya Songosongo na Bomba la Mafuta la kutoka Songosongo mpaka Dar es salaam, baada ya kubaini kuwa Serikali inapoteza mapato makubwa ambayo ilistahili kulipwa. Kwa sababu kwa mujibu wa mkataba kati ya *TPDC* na *Pan-African Energy*, kampuni hii hailipi *corporation tax*. Ni vema Serikali ikaijibu hoja hii pia ili kuweza kuhakikisha kwamba Serikali haipotezi rasilimali zake.

(vi) Kamati ilitoa ushauri juu ya kuundwa kwa chombo cha Muungano (Mamlaka ya Mafuta na Gesi Tanzania ili kusimamia sekta hii kwa sababu kama tulivyoeleza hapo mwanzo kwamba kwa mujibu wa Katiba, suala la mafuta na gesi ni suala la Muungano, lakini shirika ambalo linasimamia suala hili siyo shirika la Muungano (*TPDC*). Kwa hiyo, tulikuwa tumetaka Serikali iweze kuondoa hiyo *abnormality* ili kuhakikisha kwamba tunaimarisha Muungano wetu. Serikali haijatoa majibu kabisa katika suala hili.

(vii) Kuhusiana na suala hili utata uliopo katika ubinafsishaji wa Shamba la Kapunga (eneo lililobinafsishwa ni pamoja na Kijiji cha Kapunga), Kamati iliitaka Serikali kutoa kauli yake endapo ni kweli na ni halali kwamba Kijiji hicho cha Kapunga ni sehemu ya eneo lililobinafsishwa. Jana katika majibu ya nyongeza Waziri wa Kilimo na Chakula alielezea, lakini inaonyesha kwamba Waziri wa Kilimo na Chakula halielewi vizuri suala la Kapunga kwa sababu maelezo aliyoyatoa ni tofauti kabisa na hali halisi

ambayo iko pale Kapunga. Kwa hiyo, tunataka Serikali iwezwe kutoa maelezo ya kina na kutatua tatizo hili la Kapunga ili wananchi wale waendelee kuwepo na kijiji chao.

(viii) Kamati iliitaka Serikali kutoa maelezo kwa nini imechukua muda mrefu kukamilisha zoezi la Ufilisi na ubinafsishaji wa shamba la Bassotu. Serikali haikujibu chochote juu ya suala hili. Hivyo, Kamati inafikiri kwamba ni vema Serikali ikalitolea maelezo jambo hili. Shamba hili lina madeni ya kiasi cha shilingi milioni 650 lakini kwa maelezo ya Serikali ubinafsishaji wake bado upo kwenye mchakato kwa zaidi ya miaka kumi sasa.

Mheshimiwa Spika, mpaka ninapotoa taarifa hii na kwa mujibu wa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Serikali imewekeza jumla ya shilingi trilioni 6.1 katika mashirika ya umma hapa nchini kama jinsi ambavyo mtakavyoona katika taarifa ambayo nimeitoa na kama jinsi ambavyo tunaeleza mara zote, mitaji hii ya Serikali katika mashirika ya umma zaidi ya 164 ni sawasawa na asilimia 30 ya Pato la Taifa *(Gross Domestic Product)*. Kwa hiyo, ni uwekezaji mkubwa sana ambao unapaswa kuangalia kwa makini sana.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa faida na hasara kwa mashirika ya umma. Yapo mashirika ya umma ambayo yalianzishwa kwa ajili ya kufanya biashara na hatimaye kupata faida na mengine yalianzishwa kwa ajili ya kutoa huduma bila kutarajia kupata faida. Hata hivyo, kwa mujibu wa mtazamo wa kifungu cha 33 cha Sheria ya Fedha za Umma Na. 6 ya mwaka 2001, suala la thamani ya fedha *(value for money)* linajitokeza na hivyo kufanya matarajio ya umma kuongezeka katika kuona mashirika mengi yakipata faida na mengine kudhibiti sana gharama za uendeshaji na hatimaye kubaki na ziada.

Mheshimiwa Spika, kama ratiba ya Bunge ingekuwa imebakia kama jinsi ilivyokuwa kabla ya kurekebishwa, tulikuwa tumealika mashirika matano ambayo yamefanya vizuri zaidi katika suala la faida *(profitability)*. Kwa taarifa tu ya Bunge naomba niyataje mashirika hayo kwa kazi nzuri sana ambayo imefanywa na Maafisa wetu wa Bunge, Maafisa wa *Treasury Registrar* na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Shirika la kwanza mpaka mwezi Juni au Desemba 2008 ambalo lilifanya vizuri sana kwenye *profitability* ni shirika la *TANESCO* ambalo liliweza kupunguza hasara kutoka shilingi bilioni 67 mpaka shilingi bilioni 21 ambayo ilikuwa ni ufanisi wa zaidi ya shilingi bilioni 45.

Mheshimiwa Spika, ni kwa masikitiko makubwa sana kwamba katika hesabu zinazoishia Disemba 2009, Shirika la *TANESCO* limerudi kwenye hasara ya bilioni 48. Kwa hiyo, yale mafanikio yote ambayo yalikuwa yamefanyika mpaka 2008 yameharibika.

Mheshimiwa Spika, shirika la pili ni la *NSSF* ambalo mwaka 2006/2007 lilipata ziada ya bilioni 119.8, 2007/2008 likapata ziada ya bilioni 148 na hiyo ni nyongeza ya bilioni 29. Shirika la tatu ni *PPF* ambalo mwaka 2006/2007 lilipata ziada ya bilioni 52,

mwaka 2007/2008 lilipata ziada ya bilioni 74 na tofauti ni bilioni 21. *TCRA* walipata bilioni 3.4 mwaka 2006/2007, mwaka 2007/2008 bilioni tisa na tofauti ni bilioni 5.6 na shirika la tano ni *Tanzania Ports Authority* ambalo mwaka 2006/2007 lilipata ziada ya bilioni 22.5, mwaka 2007/2008 bilioni 26.3 ambayo ni tofauti ya bilioni 3.7.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Bunge na kwa niaba ya Bunge lako Tukufu, napenda kutoa pongezi za dhati kabisa na kuyataka hayo mashirika matano wafanye vizuri zaidi ili na mengine pia yaweze kuyaiga ili kuhakikisha kwamba mali za umma zinatumika vizuri.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya uchambuzi wa Kamati juu ya mitaji na ukaguzi katika mashirika ya umma kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2008. Uchambuzi wa Mitaji ya Umma na hisa za Serikali katika Uwekezaji: Mheshimiwa Spika, Uchambuzi uliofanyika katika uwekezaji wa mitaji katika mashirika na Taasisi nyingine kwa kipindi cha mwaka 2007/2008 umebaini kuwa Serikali inamiliki Mashirika 153 kwa asilimia mia moja (100%) yenye jumla ya mtaji wa takriban Shilingi trilioni 4.2 ambao ni sawa na asilimia 82.6% ya mtaji wote uliowekezwa na Serikali katika Mashirika ya Umma. Pia Serikali inamiliki Mashirika matano (5) kwa asilimia kati ya hamsini na moja hadi tisini na tisa (51-99%) kwa mwaka 2007/2008 yenye jumla ya mtaji wa Shilingi bilioni 439.4 ambayo ni sawa na 8.5% ya mtaji wote uliowekezwa na Serikali katika Mashirika ya umma.

Vile vile, Serikali inamiliki Mashirika manne (4) kwa asilimia hamsini (50%) kwa kipindi cha mwaka 2007/2008 ambayo ni *TIPPER, TAZARA, BP (T) LIMITED na Chinese Tanzania Shipping Company Limited* ambayo yana jumla ya mtaji wa Shilingi bilioni 169.6 sawa na 3.3% ya mtaji wote uliowekezwa na Serikali katika Mashirika ya umma. Hata hivyo umiliki huu wa 50:50 wa hisa unatoa ugumu juu ya namna ya usimamizi wa mashirika haya kama vile namna ya ukaguzi wa hesabu kwa kuwa hayaangukii katika maelekezo ya Sheria ya Fedha za Umma moja kwa moja ya kuwa yakaguliwe na *CAG* kutokana na umiliki huo wa hisa.

Katika mwaka huo wa 2007/2008, Serikali imekuwa na uwekezaji wa kati ya 20% hadi 49% katika mashirika ishirini na saba (27) yenye jumla ya mtaji wa Shilingi bilioni 281.9 ambayo ni sawa na 5.5% ya jumla ya mtaji wote ambao Serikali imewekeza katika mashirika.

Vile vile umiliki wa Serikali katika mashirika manne (4) kwa kipindi cha mwaka 2007/08 kwa 1% hadi 19% yenye jumla ya mtaji wa Shilingi bilioni 3.1 ambayo ni sawa na 0.1% ya jumla ya mtaji uliowekezwa na Serikali katika Mashirika.

Mheshimiwa Spika, gawio ambalo Serikali inapata kutoka katika uwekezaji wake. Lengo la Serikali kuwekeza mitaji ya umma katika mashirika ni kuhakikisha kwamba wananchi wanaendelea kupata huduma stahiki. Hata hivyo, lengo lingine ni kupata faida

kwa njia ya gawio (*dividends*). Kwa mtazamo wa Kamati, kiasi cha gawio ambalo Serikali imekuwa ikipata kutokana na uwekezaji wake katika mashirika ya umma siyo cha kuridhisha sana ikilinganishwa na kiasi cha mtaji unaowekezwa. Bila shaka gawio hilo huathiriwa sana na kutokuwepo kwa uhakika wa faida halisi inayopatikana kutoka katika mashirika ambayo Serikali inamiliki hisa kadhaa kwa njia ya ubia.

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu hizo za asilimia 0.4% kuwa ndiyo jumla ya gawio kwa miaka miwili kwa mtaji wa zaidi ya Trilioni tano, ni dhahiri kwamba Serikali haipati matokeo yanayoridhisha kutokana na uwekezaji wake katika mashirika. Hivyo, ni wakati muafaka hoja hii ya uwekezaji wa Serikali ikajadiliwa kwa kina na Bunge lako na kuainisha matatizo yaliyopo na kupendekeza njia muafaka za kuyatatua kwa haraka iwezekanavyo ili kuongeza tija katika eneo hili la uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hii, Kamati inaona ni vyema Serikali iyasimamie mashirika kupunguza matumizi yake yasiyo ya lazima ili kuweza kuongeza uwezo katika kutimiza malengo ya uanzishwaji wake.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilifanya tathmini ya mali zilizopo kwenye mashirika *(assets)* na kuweza kuangalia ukubwa wa mashirika kutokana na mali ambazo mashirika hayo yanamiliki. Kwa ufanisi wa utendaji kazi kwa tofauti za ukubwa shirika la kwanza ambalo limeongeza sana mali linazomiliki ni Shirika la *National Housing Corporation* kutoka shilingi bilioni 213 mpaka bilioni 852 ambayo ni sawa na tofauti ya bilioni 639. Shirika la pili ni *TANESCO* kutoka *1.5 trillion* mpaka *1.7 trillion*, tofauti ya bilioni 208. Mali ambazo shirika la *TANESCO* linazo ni zaidi ya pato la Taifa la Burundi. Kwa hiyo, ni mali nyingi sana katika shirika hilo.

Mheshimiwa Spika, *National Social Security Fund* nyongeza ya bilioni 157 na *Parastatal Pensions Fund* nyongeza ya bilioni 108. Mamlaka ya Bandari (*TPA*) nyongeza yake ni bilioni 167. Kwa hiyo, hiyo ndiyo taarifa kuhusiana na mali ambazo mashirika yetu yanazo.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha Uzingatiaji wa Maoni ya Ukaguzi. Sababu kubwa ya kuwa na wakaguzi wa hesabu wa ndani na wa nje ni kuziwezesha taasisi mbalimbali kupata maoni yao kuhusu tathmini ya mifumo na utendaji wake ili kuweza kuboresha zaidi utendaji na tija ya taasisi hizo. Hivyo, haitarajiwi kwa taasisi kuendelea kuwa na tatizo ambalo uboreshaji wake umekwisha shauriwa na wakaguzi wa hesabu.

Hata hivyo, kumekuwapo na taasisi sugu za umma zilizoendelea kupata hati yenye shaka kwa zaidi ya mwaka mmoja mfululizo zikiwemo Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Jiji la Dar es salaam (*DAWASCO*), Kampuni ya miundombinu ya Maji ya Dar es Salaam (*DAWASA*), kampuni ya Bima ya Taifa na nyingine. Taasisi hizi na nyingine ambazo hazionyeshi mwenendo mzuri katika ushughulikiaji wa hoja za ukaguzi zinahitaji kupewa msukumo wa kipekee na Serikali ili kuhakikisha kuwa zinatekeleza kikamilifu malengo ya uanzishwaji wake.

Hata hivyo, zipo taasisi nyingine nyingi za umma ambazo zimeonyesha kiwango kizuri cha uzingatiaji maoni ya wakaguzi wa hesabu na maagizo ya Kamati ya Hesabu za

Mashirika ya Umma na hivyo kupunguza kwa kiwango kikubwa cha hoja za ukaguzi na hatimaye kupata hati safi ya hesabu zake zikiwemo mamlaka za udhibiti, taasisi za elimu ya juu ambazo kwa kipindi cha takribani miaka mitatu kuanzia 2006/2007 hadi 2008/2009 zimekuwa zikipata hati safi ya ukaguzi wa hesabu.

Mheshimiwa Spika, imebainika kwamba ufanisi wa mashirika huathiriwa na sababu tatu kubwa:-

- Mikakati hafifu ya Mashirika yenyewe katika kutekeleza majukumu yake.

- Mwenendo ama maamuzi ya Serikali Kuu juu ya Mashirika hayo (kwa mfano maelekezo ya Serikali kwa *TANAPA* kulipia gharama za matangazo ya utalii kwa kituo cha *CNN* wakati *TANAPA* hawakuhusika kabisa na mikataba ya matangazo hayo).

- Mashirika kukaa kwa muda mrefu bila Bodi za Wadhamini kwa mfano, hadi tarehe 30 machi 2010 Mashirika yafuatayo hayakuwa na Bodi za wadhamini hivyo kuyapunguzia uwezo wa kufanya kazi ipasavyo. *NIP*, *TCU*, Taasisi ya Ustawi wa jamii, Bodi ya Tumbaku Tanzania, Bodi ya Utalii Tanzania na kadhalika, Mashirika kuwa chini ya watu wanaokaimu madaraka kwa muda mrefu na kadhalika).

- Tatu ni athari zinazotokana na mabadiliko mbalimbali katika mazingira ya dunia kwa ujumla (mfano, Mdororo wa Uchumi Duniani).

Mheshimiwa Spika, matatizo sugu yaliyoanishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa Hesabu za Mashirika ya Umma zinazoishia Juni 30, 2008. Ukurasa wa 99 wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali kwa Mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2008 umeweka wazi mambo yanayochangia kurudisha nyuma utendaji wa Mashirika ya umma na taasisi zinginezo nchini kuwa ni pamoja na urasimu katika kutoa miongozo na ushauri katika mashirika husika, uongozi sio imara katika mashirika hayo, mapungufu katika mipango kazi ya mashirika, mapungufu katika kuzingatia taratibu za manunuzi na utunzaji wa vifaa vya Mashirika hayo.

Hata hivyo, ulegelege katika kutekeleza Sheria na Kanuni zinazotawala mwenendo wa mashirika na taasisi za umma nchini limekuwa ndiyo tatizo sugu linaloshusha kwa kiasi kikubwa nidhamu ya matumizi ya fedha na mali za umma katika Mashirika ya Umma. Hapa niyataje kwa uchache baadhi ya matatizo haya:-

(1) Mashirika ya Umma kutokuwa na mipango ya manunuzi kwa mwaka (*Annual Procurement Plan)* na Vitengo vya Manunuzi *(Procurement Management Unit).*

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa mambo yanayotumia kiasi kikubwa cha fedha za umma ni suala la manunuzi. Hivyo likitumiwa vibaya laweza kuwa chanzo kikubwa cha umasikini wa nchi yetu na chanzo kikubwa cha sifa mbaya ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika mashirika na Serikali kwa ujumla. Ni ushauri wa Kamati kwamba Sheria na taratibu zote za manunuzi zinapaswa kuzingatiwa. Mifano michache ya manunuzi holela ni pamoja na:-

(i) Manunuzi ya matangazo ya utalii (*USD* 800,000) yaliyofanywa na *TANAPA* kwa *CNN* na Jambo *Publication Limited* katika Mwaka wa Fedha wa 2007/2008, hayakuonesha utaratibu ambao utahakikisha matangazo yanatolewa kwa muda uliowekwa na kwa ubora unaokubalika ili shirika lipate thamani ya fedha inayolipwa.

(ii) Kiasi cha Manunuzi ya jumla ya bilioni 1.178 yaliyofanywa na Shirika la Utangazaji la Taifa (*TBC*) hayakuidhinishwa na Bodi ya Wadhamini ya Shirika hilo.

(iii) Kiasi cha zaidi ya Shilingi Milioni 130 zilitumiwa na Chuo cha Uhasibu cha Arusha kununua vifaa vya hosteli na Ofisi bila kuwepo kwenye mpango wa manunuzi wa mwaka wa Shirika hilo na manunuzi hayakutangazwa kwenye tangazo la manunuzi kama inavyotakiwa na Kanuni za Manunuzi za Mwaka 2005.

(2) Mashirika kutorejesha makato ya Kisheria ya watumishi wao kwenye vyombo vinavyostahili.

Kwa mujibu wa Kanuni za Fedha, masurufu yanapaswa kurejeshwa ndani ya siku 14 mara baada ya mhusika kurudi kutoka katika maeneo ambayo masurufu hayo yalienda kutumika. Hata hivyo, kwenye mashirika mbalimbali mathalani, Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*), Halmashauri ya Biashara ya Nje (*BET*), Shirika la Posta (*TPC*) na Hospitali ya Taifa Muhimbili (*MNH*) Kanuni hii haikuzingatiwa kwani mashirika tajwa yalishindwa kurejesha makato ya kisheria yenye jumla ya Shilingi bilioni 29.3. Madhara ya kutorejesha makato hayo yanaleta tozo kubwa ambazo mashirika husika yanatozwa kama adhabu ya kutotimiza sharti hilo la kisheria.

(3) Mashirika na Taasisi kukosa mitaji ya kujiendesha na hata mengine yenye fedha kutokuwa na miongozo ya fedha na uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, Mashirika ya Umma yana matatizo makubwa sana ya mitaji ya kuwekeza (*recapitalization*). Kukosekana kwa mtaji kunaathiri mashirika ya Umma kuendeshwa kwa ufanisi. Mashirika yaliyoathiriwa zaidi na tatizo hili ni pamoja na, Shirika la Maendeleo la Taifa (*NDC*), Shirika la Umeme Nchini (*TANESCO*) Mamlaka zote za Maji Nchini, Shirika la Bima la Taifa (*NIC*), Halmashari ya Biashara ya Nje (*BET*), Shirika la Ndege la Taifa (*ATCL*) na Shirika la Mafuta (*TPDC*) yanafanya kazi kwa kusuasua kwa sababu ya kuwa na kiasi kidogo cha mtaji.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili bado linaendelea. Hivyo, Kamati inashauri Serikali iangalie uwezekano wa kuyaongezea mashirika hayo mitaji ili yaweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Hata hivyo, ipo haja ya Bunge kujiridhisha na sababu za kupungua kwa mitaji ya Mashirika hayo.

(4) Mashirika mengi kutokuwa na hati miliki na Bima za mali:-

Mheshimiwa Spika, yapo Mashirika na Taasisi mbalimbali za Umma (kwa mfano, Bodi ya Sukari Nchini (kitalu Na.45 kilichopo barabara ya Agha Khan Mjini Dar es Salaam, Nyumba 6 katika kitalu Na.303 na nyumba za makazi zilizopo Makambako mjini Iringa); Kampuni ya Ranchi za Taifa kutokuwa na hati miliki kwa ranchi za Ruvu, Kongwa, Mabale na kadhalika na kuwa na hati miliki za ranchi ya Misenyi na Kitengile zisizokuwa na jina la Kampuni ya *NARCO*; Shirika la Reli Tanzania (Kitalu Na. 228 kilichopo Kurasini Dar es Salaam, Vitalu viwili vilivyopo ofisi ya *DCE* Mjini Dodoma na Klabu ya Shirika la Reli iliyopo barabara ya Uluguru mjini Tabora), Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Singida (Magari ya Mamlaka yenye thamani ya 43.1 Milioni na Majengo yenye thamani ya shilingi 150.9 Milioni hayakusajiliwa kwa jina la Mamlaka) na Taasisi ya Utafiti na Maendeleo ya Viwanda- *TIRDO* (Kitalu Na.1408). Taasisi hizo kwa muda wa miaka mingi hazijakidhi matakwa ya kisheria ya kuwa na Hati miliki za mali zao hususan ardhi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuliwekea suala hili mkakati maalum katika muda maalum kwa ajili ya kuhakikisha kuwa hati miliki hizo zinapatikana ili mwakani Bunge lisiendelee kusikiliza tena wimbo huu.

(5) Serikali kuwa miongoni mwa wadaiwa sugu katika huduma zinazotolewa na Mashirika ya Umma.

Uchunguzi wa Kamati katika jumla ya madeni, idadi na aina za wadaiwa unaonesha kwamba miongoni mwa wadaiwa wakubwa ni Serikali kupitia Wizara zake. Miongoni mwa mashirika yanayoathiriwa zaidi ni pamoja na Mamlaka za Maji Safi na Maji Taka nchini (Mfano ni Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Jijini Mwanza ambapo hadi kufikia Februari 2010 Madeni ya ankara za maji kwa Taasisi za Serikali yalifikia Jumla ya Shilingi milioni 360 , Shirika la Magazeti ya Taifa (*TSN*) na Shirika la Usambazaji na Ugawaji wa Umeme nchini (*TANESCO*) na Bohari ya Madawa Nchini (*MSD*) ambao takwimu zinaonesha kwamba mpaka sasa madai ya aina mbalimbali ambayo Serikali inadaiwa na *MSD* yamefikia zaidi ya shilingi bilioni 30. Kutozilipa taasisi hizi madai yao kwa wakati na kwa kiasi kinachostahili kunaathiri utekelezaji wa Mipango ya kila mwaka ya taasisi hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina imani kwamba Waheshimiwa Wbunge kama wananchi wengine mmewahi kupata adha inayotokana na ufinyu wa mitaji katika mashirika haya. Hivyo michango yenu itasaidia sana katika eneo hili.

(6) Kuendelea kuwepo kwa mashirika ya umma ambayo yanafanya kazi lakini hayapo kwenye orodha ya Msajili wa Hazina, kwa mfano; Morogoro *Leather Goods*, Kitara *Holding Ground* na Kampuni ya Maji Songwe.

(7) Baadhi ya Mashirika kufanya malipo kwa wazabuni kabla ya kupata huduma.

Katika mwaka wa fedha wa taarifa hii, yapo baadhi ya Mashirika ya umma kama vile *TANAPA*, *TPA*, na *MWAUWASA* yalifanya malipo ya jumla ya shilingi 146,024,582 kwa wazabuni mbalimbali kabla ya kupata huduma kutoka kwa wazabuni hao.

Kwa kuzingatia Kanuni ya 122(1) chini ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2005, Kamati ingependa kuagiza kuwa utaratibu huo usije ukarudia tena katika taarifa za hesabu zitakazofuata.

Mheshimiwa Spika, mafanikio, pongezi, maoni na mapendekezo ya Kamati juu ya yote yaliyojadiliwa. Katika kujadili taarifa za hesabu zilizokaguliwa za Mashirika ya Umma, Kamati imebaini kuwa yapo mafanikio na changamoto mbalimbali ambazo Mashirika hayo yanakabiliana nazo. Kwa mfano, suala la upungufu wa mitaji ya kutosha kutekeleza mipango ya kila mwaka ya Mashirika, kutoeleweka vema kwa kiasi cha hisa za Serikali ambacho kinamruhusu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kulikagua Shirika, kuwepo maelekezo ya Serikali yanayoathiri utekelezaji wa mipango mkakati ya mashirika, kutofautiana kwa kiasi kikubwa kwa viwango vya posho zinazolipwa na mashirika, kuchelewa kuundwa kwa Bodi za Wadhamini/Wakurugenzi wa baadhi ya Mashirika na baadhi ya Watendaji katika nafasi muhimu za Mashirika kukaimu kwa muda mrefu.

Ni katika mazingira ya changamoto hizi ambapo Kamati inapenda kutoa ushauri wake kwa ajili ya maboresho katika ufanisi wa Mashirika hayo.

Mheshimiwa Spika, mafanikio katika utendaji wa Kamati. Kabla ya kutoa maoni yetu juu ya mambo yaliyotajwa hapo juu, ni vema nikatoa maelezo machache juu ya mafanikio ambayo Kamati imeyapata tokea kuanzishwa kwake japokuwa ufinyu wa muda na bajeti ya kila mwaka zimekuwa changamoto na vikwazo katika ufanisi wake:-

(i) Utendaji kazi wa Kamati umeweza kuyakumbusha Mashirika kuhusu uwepo wa uangalizi (*oversight*) wa Bunge katika nidhamu ya matumizi ya fedha na raslimali za umma. Hali hii ni tofauti na nidhamu ya matumizi ya fedha na mali za umma iliyokuwepo katika mashirika kabla ya Kamati hii kuundwa.

(ii) Kwa kushirikiana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Msajili wa Hazina na wadau mbalimbali wa Maendeleo, Kamati imeweza kuandaa Makongamano kadhaa ya kujadili mwenendo wa mashirika kiutendaji kwa lengo la kutambua matatizo yanayoyakabili na kupendekeza kwa Serikali namna bora ya kutatua matatizo hayo. Makongamano hayo ni pamoja na Kongamano la Ufanisi wa Mashirika yanayoshughulikia masuala ya Miundombinu (*TPA*, *DAWASCO*, *TPDC*, *TANROADS* na *ATCL*) ambalo lilifanyika Januari 24, 2009 na Kongamano la Taasisi za Fedha nchini.

(iii) Maagizo ya Kamati yamelisaidia Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*) kutambua thamani halisi ya mali zake kutoka bilioni 213, waliokuwa wanaijua mwaka 2007/2008 mpaka bilioni 852.9 kwa hali halisi ya soko la sasa. Maana yake ni kwamba laiti *NHC* wangeamua kuuza mali zao zote nchini kwa mwaka wa fedha wa 2007/2008, pasipokuwepo Kamati hii, wangeziuza zote kwa thamani ya shilingi bilioni 213 lakini

wakifanya hivyo sasa baada ya Kamati kuamuru Shirika lithaminishe upya mali zake, mali hizo zikiuzwa kwa sasa zina thamani ya Shilingi bilioni 852.9.

(iv) Kamati imeyashawishi Mashirika ya Hifadhi za Jamii nchini kuwekeza katika miradi mbalimbali ya uzalishaji wa umeme nchini. Majadiliano bado yanaendelea miongoni mwa Mashirika na *TANESCO*.

(v) Maagizo ya Kamati yamechangia kwa kiasi kikubwa kuitoa *TANESCO* kutoka katika mazingira ya kujiendesha kwa hasara. Mwaka wa 2006/2007 Shirika hilo lilikuwa likiendeshwa kwa nakisi ya Shilingi bilioni 67 mpaka kufikia nakisi ya Shilingi bilioni 21 Mwaka 2007/2008.

(vi) Pamekuwepo na ongezeko la uwazi zaidi katika kuonesha taarifa za Mapato na Matumizi katika Mashirika ya umma hivyo kuongeza nidhamu ya matumizi ya fedha za umma katika mashirika hususan katika Mamlaka za Maji na Bodi za Mazao.

(vii) Kamati imehusika kikamilifu kupitia maagizo yake kwa mashirika ya umma katika kuchochea ongezeko la hati safi zinazoendana na usafi halisi katika matumizi ya fedha za umma katika mashirika (Hati Safi 80 Mwaka 2006/2007 na Hati Safi 86 kwa Mwaka 200/2008).

(viii) Kamati imechangia katika kuongeza ufanisi wa mashirika mbalimbali kama vile *Twiga Bankorp Ltd* na TIB (waliongezewa bilioni 1.8 katika Mwaka wa fedha uliopita) kwa kuyatetea Serikalini ili yaongezewe kiasi cha mitaji ya kuendeshea shughuli zake na kwa kuzingatia hayo *Twiga Bancorp* ipo mbioni kuwa Benki kamili kwa kuzingatia Sheria ya Benki Kuu.

(ix) Kamati imechangia *Despecification* ya Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*) ambalo sasa limepata mbia kutoka Afrika Kusini ambaye kwa pamoja wanajiandaa kujenga kiwanda cha kuchakata madini.

(x) Kamati imechochea kwa kiasi kikubwa kuundwa kwa Bodi za Zabuni na Vitengo vya Ukaguzi wa ndani katika mashirika kama vile *TBC, TPA, TCRA* na Mamlaka Mbalimbali za Maji Safi na Maji Taka nchini ikiwemo Mamlaka ya Jiji la Mwanza ikizingatiwa kuwa vitengo hivi vyote ni muhimu kwa ajili ya udhibiti wa ndani.

(xi) Maagizo ya Kamati yamechangia sana katika kuwahimiza baadhi ya wakopaji (Mfano, *Kagera Sugar Company*) kulipa madeni yao ikiwa ni pamoja na riba kwa Mashirika yaliyowakopesha kwa udhamini wa Serikali. Katika Taarifa ya *NSSF* kwa

Mwaka wa Fedha ulioishia Juni 30, 2008, Kagera *Sugar Company* imeweza kuirejeshea *NSSF* kiasi cha shilingi bilioni moja.

(xii) Kamati imeongeza ushirikiano miongoni mwa Kamati za Bunge kwa kushirikisha wajumbe wa Kamati zingine katika utekelezaji wa majukumu mtambuka. Kwa mfano, Mwaka 2008 *POAC* iliiialika Kamati ya Huduma za Jamii kwa ajili ya kutafuta muafaka wa ulipaji wa kiasi cha zaidi ya bilioni 50 zilizokopwa na Kampuni ya Sukari ya Kagera kutoka katika Mabenki na Mifuko ya Hifadhi za Jamii nchini, katika mwaka huo Kamati yetu iliweza kuwashirikisha wajumbe mbalimbali wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira katika kujiridhisha na uwepo wa miradi iliyotekelezwa na *TANAPA* katika hifadhi. Kamati imeweza kuzishirikisha Kamati mbalimbali za Bunge mathalan Kamati ya Fedha na Uchumi katika semina mbalimbali za kimafunzo zilizoandaliwa kwa ajili yake.

(xiii) Kamati imeweza kuonesha *oversight role* ya Bunge katika Mamlaka zote 19 za Maji Safi na Maji Taka nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaliona jambo hili kama sehemu ya mafanikio kwa sababu Bunge halikuwahi kwa namna yoyote kuzijadili taarifa za hesabu za Mamlaka hizi tangu ziundwe.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya kuipongeza Serikali. Yapo baadhi ya mambo ambayo kwa maoni ya Kamati ni vema kuipongeza na kuitia moyo Serikali yetu. Kamati inapongeza hatua zifuatazo:-

(i) Ufuatiliaji wa karibu unaofanywa na Serikali kuhakikisha mapato ya Shirika la Bandari hayapotei kizembe.

(ii) Kuondolewa (*despefication*) kwa *STAMICO* kutoka kwenye Orodha ya Mashirika yanayosubiri kubinafsishwa.

(iii) Juhudi zenye mwelekeo wa kuiimarisha zaidi Ofisi ya Msajili wa Hazina ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

(iv) Kuundwa kwa Kikosi Kazi kwa ajili ya kuchunguza matumizi ya kiasi cha zaidi ya Shilingi milioni mia sita (600,000,000 ) zinazodaiwa kuwa zimetumika kwa ajili ya kukarabati nyumba za Wakurugenzi wa *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Kamati katika maeneo mbalimbali. Pamoja na kutoa pongezi, Kamati ina ushauri juu ya mambo yafuatayo kwa lengo la kuboresha zaidi hali ya mashirika na taasisi za umma nchini katika kutoa huduma kwa Watanzania na katika kukuza uchumi wa nchi:-

Mheshimiwa Spika, Mifuko ya Hifadhi za Jamii nchini imeonesha uwezo mkubwa sana katika kuinua maendeleo ya jamii nchini. Mifano ipo mingi ikiwemo Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, ujenzi wa nyumba za Jeshi la Polisi na jengo la TAKUKURU. Ushauri wa Kamati ni kwamba Serikali inapaswa kuitia nguvu mifuko hii

kwa kukamilisha bila shaka yoyote taratibu zote zinazohusiana na kupatikana kwa mikopo hiyo. Mfano wa maeneo muhimu katika hili ni kusainiwa mapema iwezekanavyo kwa nyaraka zote za makubaliano muhimu ya upatikanaji wa mikopo hiyo na kulipa kwa wakati madeni yanayotokana na ukopaji huo. Ushauri huu unalenga pia katika kuitaka Serikali kusaini haraka iwezekanavyo *Memorandum of Understanding* zilizotumika kati yake Mifuko ya Hifadhi za jamii mathalan *the Memorandum of Understanding* kati ya Serikali na *NSSF* juu ya ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Bodi za wadhamini ndizo zenye jukumu kubwa katika kusimamia utendaji wa Mashirika ya umma ili yapate kutekeleza mipango yao kikamilifu. Kamati inaamini kwamba muda wa uhai wa Bodi hizi unaeleweka vema zaidi kisheria na kwa mujibu wa barua za uteuzi.

Mheshimiwa Spika, kutokuwepo kwa Bodi hizi kwa baadhi ya Mashirika siyo tu kwamba kunaathiri kasi ya maamuzi na utekelezwaji wa mipango mbalimbali ya mashirika hayo bali pia kunaathiri ratiba za utendaji kazi wa Kamati yetu. Kwa mfano, kwa mwaka wa taarifa hii, Kamati ilishindwa kujadili taarifa za hesabu za mashirika mbalimbali ikiwemo, Shirika la Tija la Taifa (*NIP*), Bodi ya Tumbaku Nchini, Bodi ya Utalii, Tume ya Vyuo Vikuu, Shirika la Magazeti la Taifa (*TSN*) na Taasisi ya Ustawi wa Jamii nchini kwa sababu hayakuwa na Bodi za Wadhamini. Kwa maana nyingine Kamati haina maoni yoyote juu ya hesabu za mashirika hayo.

Mheshimiwa Spika, ufanisi wa mamlaka za maji nchini. Tukiondoa Mamlaka ya Maji safi na Maji Taka ya Shinyanga- Kahama, Mamlaka za maji nchini zinafanya kazi kwa kutumia mitandao ya kizamani sana katika kusambaza maji kwa wananchi. Ni mitandao iliyochoka hivyo kusababisha kiasi kikubwa cha upotevu wa maji yanayosambazwa kwa gharama kubwa. Hivyo, ni ushauri wa Kamati kwamba Serikali ijipange katika kuhakikisha mitandao hiyo inakarabatiwa upya ili kutozitia Mamlaka hasara ya kusambaza maji kwa gharama kubwa. Njia mojawapo ya kujipanga ni kwa Serikali kudhamini mikopo kwa Mamlaka za maji ili zifanye uwekezaji mkubwa katika miundo mbinu ya maji ambayo kwa asilimia kubwa ni chakavu.

Ni ushauri wa Kamati pia kwamba ili kuleta ufanisi wa kutosha kwa Mamlaka za Maji nchini ni vema Serikali ikaangalia utaratibu wa kulipa ankara za maji kwa taasisi zake kupitia Wizara mama za taasisi husika ili kuondoa udhaifu unaoonekana dhahiri kwa taasisi za Serikali kuzembea kulipa ankara hizo.

Mheshimiwa Spika, utekelezwaji wa sera ya ubinafsishaji. Lengo la ubinafsishaji ni kuinua Taifa na watu wake. Kwa mantiki hiyo basi, Kamati inashauri Msajili wa Hazina aweke mikakati madhubuti ya kukusanya madeni kutoka kwa wawekezaji walioshindwa kutekeleza masharti ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, mifumo ya udhibiti wa fedha za umma katika Benki Kuu na mashirika mengine. Kama ambavyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amewahi kutahadharisha katika taarifa yake ya Mwaka ya Hesabu zilizokaguliwa za Mashirika ya Umma kwa Mwaka ulioishia 30 Juni, 2008, Serikali na Mashirika yake yote

yanapaswa kuwa na mikakati imara ya kutathmini vihatarishi vya usalama wao na mali zao. Vihatarishi hivyo vyaweza kuwa ni mambo ya teknolojia, siasa na mwenendo wa uchumi wa dunia. Tahadhari na ushauri huu ni muhimu zaidi kuzingatiwa hasa katika kipindi hiki ambacho wizi wa fedha katika mabenki kwa kutumia mitandao ya kompyuta umeonekana kupamba moto.

Mheshimiwa Spika, kuimarishwa kwa *RAHCO*. Kwa mujibu wa Sheria Na. 4 ya Mwaka 2002, Kampuni ya *RAHCO* ndiye mmiliki na mwendelezaji wa miundombinu ya reli nchini. Kwa maana nyingine ndiyo Kampuni inayotakiwa kuboresha na kuongeza miundombinu hiyo ili kuufanya usafiri wa reli ukidhi mahitaji ya usafiri na usafirishaji. Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kampuni hii inakabiliwa na changamoto lukuki ikiwemo ukosefu wa fedha kwa ajili ya kukamilishia mipango yake ya kila mwaka na kushindwa kulipa mishahara ya watumishi wake kwa viwango vinavyolingana na soko huria na makubaliano kati ya *TRAWU* na *TRL* ya kima cha chini cha Tshs.200,000/=. Changamoto hizi zinazoifanya *RAHCO* ishindwe kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Ushauri wa Kamati ni kwamba Serikali iiongezee *RAHCO* mtaji lakini pia iangalie vikwazo ambavyo *RAHCO* inavipata na kukwamishwa kutekeleza majukumu yake kutokana na vipengele vya Mkataba wake na Kampuni ya *RITES*.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*). Nishati ya umeme ni muhimu sana kwa maendeleo ya Mtanzania mmoja mmoja na kwa maendeleo ya Taifa zima. Hivyo ufanisi wa Shirika la Usambazaji na Ugawaji wa Umeme nchini ni muhimu sana. Kamati imebaini kuwa Shirika hili lina mipango muhimu sana ambayo ikitekelezwa ipasavyo nchi inaweza kuwa na uhakika wa umeme wa kutosha. Tatizo lililopo hapa ni ukosefu wa fedha za kutekelezea mipango hiyo.

Hata hivyo, Kamati ilibaini kwamba yapo baadhi ya mapungufu ambayo hufanywa na *TANESCO* yenyewe kiasi kwamba inajikosesha mapato kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, kuna ucheleweshaji katika kupeleka hati za madai kwa wateja wapya. Katika mwaka wa fedha uliojadiliwa katika Taarifa hii, wateja kama vile *Vodacom*, Alpha Nuhu, *Celtel limited* na Marcdonald Machange walitumiwa hati za madai baada ya miezi miwili. Matatizo mengine ni pamoja na kuchelewa kusoma mita za wateja, hati za madai kuwa pungufu kuliko umeme uliotumika (katika mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2010, Hoteli ya Kilimanjaro Kempinski ilipelekewa madai pungufu kwa shilingi milioni 13.1. Ni ushauri wa Kamati kwamba shirika linapaswa kujinasua kutoka katika uzembe wa aina hiyo.

Ushauri wa Kamati ni kwamba, ili kuiimarisha *TANESCO*, Serikali ijipange vya kutosha kuhakikisha kwamba, Shirika hili linatafutiwa fedha za kutosha kukamilisha mipango yake. Kamati inashauri mambo yafuatayo yazingatiwe katika orodha ya mipango inayopangwa ya kuiimarisha *TANESCO* katika kukamilisha mipango yake: -

Serikali itambue kwa dhati kuwa Taifa halina umeme wa kutosha. Hivyo, juhudi za makusudi zichukuliwe ikiwa ni pamoja na:-

(i) Serikali kutilia mkazo wazo la Kamati hii la kuishawishi Mifuko ya Hifadhi za Jamii nchini kuwekeza katika miradi ya uzalishaji wa umeme; na

(ii) Serikali kuzirudisha dola za Kimarekani 4,865,000 ilizoilipa Kampuni ya *M/s Dowans* kwa ajili ya kukodisha ndege maalum ya kusafirisha mashine za kusafirishia umeme kuja Dar es Salaam bila kuwa na kifungu kwenye Mkataba kinachoruhusu kilichoitaka kulipa malipo gharama hizo. Fedha hizo zikirudishwa ziongezwe kwenye mtaji wa *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu shilingi bilioni 5.9 zilizotolewa na *TANAPA* kama fidia katika hifadhi ya Ruaha. Katika juhudi za kupanua hifadhi za Taifa, Shirika la Hifadhi za Taifa lilitoa kiasi cha Shilingi bilioni 5.9 kama gharama za kuwafidia wananchi wa vijiji vitakavyohamishwa kutoka katika maeneo yatakayotambuliwa kuwa sehemu ya hifadhi kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ruaha Mkoani Mbeya. Kamati inashauri Serikali ilihakikishie Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla kama kiasi hicho cha fedha kiliwafikia walengwa.

Meshimiwa Spika, Serikali kuendelea kuwemo katika orodha ya wadaiwa sugu katika taasisi na mashirika ya umma: Katika kujadili taarifa za Hesabu za Mashirika na Taasisi mbalimbali za umma, imebainika kuwa lipo tatizo sugu la wateja wanaopata huduma mbalimbali (maji, umeme, madawa na elimu) kutolipa kwa wakati gharama za huduma wanazopata. Madhara yanayosababishwa na tabia kama hii ni kukosekana kwa mitaji ya mashirika kuendelea kutoa huduma kikamilifu kwa sababu ya kukosa fedha.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Serikali Kuu ndiyo inayoongoza kwa kuwa mdaiwa sugu katika taasisi ama mashirika ya umma yanayotoa huduma zilizoainishwa hapo juu. Kwa mfano:-

· Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2010, *MSD* imekuwa ikiidai Serikali kiasi cha Shilingi bilioni 36.7.

· Hadi kufikia tarehe 30 Februari, 2010, Mamlaka ya Maji Safi na maji Taka ya Jiji la Mwanza imekuwa ikiidai Serikali (Jeshi la Wananchi, Magereza na Jeshi la Polisi) kiasi cha Shilingi milioni 360.

· Yapo madeni kama hayo katika taasisi kama vile *TBC* na *TSN*.

Mheshimiwa Spika, hii ni mifano michache tu. Ushauri wa Kamati ni kwamba Serikali iandae utaratibu mpya utakaowezesha ankara za huduma hizi zilipwe moja kwa moja kutoka katika Wizara zinazohusika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kiasi cha bilioni 7.9 zilizotolewa na *TANESCO* katika Kampuni ya *Songas LTD.* kwa ajili ya upembuzi yakinifu katika juhudi za kuongeza

ufanisi wa usafirishaji wa gesi kutoka Songosongo mpaka Dar es salaam *TANESCO* waliingia Mkataba na Kampuni ya Songas ltd ili kuwezesha upanuzi wa mradi husika. Kulingana na Mkataba ilikubaliwa kwamba sehemu ya Mapato ambayo yangeenda *TANESCO* kutokana na utumiaji wa bomba la gesi la Songo Songo yabakie kwenye Kampuni ya SongoSongo kama gharama za kulipia kazi ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kupanua bomba hilo.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza hilo, mapato ya *TANESCO* yaliyobakizwa kwenye Kampuni ya Songosongo mpaka kufikia kipindi kilichoishia Desemba 31, 2008 yamefikia Shilingi bilioni 8.4. Hivyo kiasi kilichobakizwa kuwa kikubwa kuliko kiasi cha bilioni 7.9 ambazo ilikubaliwa awali kwamba TANESCO ingeilipa Kampuni ya Songosongo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kulipatia Bunge maelezo ya kutosha juu ya *value for money* iliyopo katika malipo hayo ya kiasi cha bilioni 7.9 kwa ajili ya kufanya upembuzi huo.

Mheshimiwa Spika, c*oncession fees* katika hifadhi za Taifa katika kujadili Taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Shirika la Hifadhi za Taifa *(TANAPA)* Kamati ilibaini kuwa upo upotevu mkubwa wa Mapato ya Shirika hilo kupitia viwango vidogo vya *Concession fees* zinazolipwa na wamiliki wa hoteli za kitalii zilizopo hifadhini. Michanganuo ilionesha kuwa mapato ya *concession fees* yanazidiwa kwa kiasi kikubwa na yale yanayotokana na Upigaji wa mahema *(Camping)* ambapo mtu mmoja hulipa USD 50 kwa siku katika Hifadhi ya Serengeti wakati *concession fees* ni wastani wa *USD7- 10* kwa mtu mmoja kwa siku. Malipo kama haya yanazalisha dhana kwamba kwa uchumi wa nchi hii, *Campsites* ni bora mara saba kuliko mahoteli ya kitalii yaliyomo kwenye hifadhi zetu.

Mheshimiwa Spika, juu ya maagizo ya Serikali katika mipango na mapato ya mashirika ya Umma Serikali kuhusu  katika tathmini ya Kamati juu ya ufanisi wa Mashirika ya Umma, imebainika kuwa Serikali kwa namna fulani inahusika na kuathiri ufanisi wa Mashirika hayo kupitia maagizo yanayotolewa bila kuzingatia Mipango Mkakati ya mashirika hayo. Kwa mfano katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2007/2008, hadi kufikia mwezi Oktoba 2007, kwa maagizo ya Wizara ya Maliasili na Utalii, *TANAPA* ilikuwa imekwisha ilipa *Cable News Network (CNN)* kiasi cha shilingi bilioni 1.07 kwa ajili ya Mkataba wa Matangazo ya utalii ambao *TANAPA* hawakuhusika. Kiasi hicho ni tofauti na Dola za Kimarekani 272, 002.45 zilizolipwa kwa kampuni ya Jambo Publications Ltd. ya Wingereza ikiwa ni ada ya kutoa huduma ya matangazo kwa muda wa miezi sitaJanuari- Juni, 2008.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni ya Kamati, utaratibu kama huu wa Serikali kuyalazimisha mashirika kutumia kiasi kikubwa cha fedha kama hiki nje na mipango ya mwaka ya Mashirika hayo unaathiri sana ufanisi wa mashirika hata kama nia ni nzuri.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji wa benki Kuu katika kampuni ya mwananchi *Gold*. Katika tarifa ya Kamati ya Mwaka ya 2008 Kamati ilishauri kuwa hisa zote za

Benki Kuu kwa kampuni ya Mwananchi *Gold* zipewe Shirika la *NDC* kama mkakati maalum wa Serikali wa kuiimarisha *NDC.*

Mheshimiwa Spika, yapo mashirika ambayo Serikali ina miliki hisa kiasi cha 50%; kwa mfano katika Makampuni kama vile *BP Tanzania Ltd., TIPPER, Chinese Tanzania Shipping Company* na *TAZARA*. Katika Mashirika kama haya na mengineyo ambayo Serikali inamiliki hisa chini ya 50% Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2001 pamoja na marekebisho yake haimpatii Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali nguvu ya kukagua taarifa za hesabu za mwaka za mashirika hayo.

Mheshimiwa Spika, Katika mazingira kama hayo, madhara yake ni kwamba Bunge linakuwa halina uhakika juu ya nidhamu ya matumizi ya fedha za umma zinazowekezwa katika mashirika ya namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Kamati ni kama ifuatavyo:

(i) Serikali ilieleze Bunge katika mazingira ambayo Serikali ina miliki 50% ya hisa kama ilivyo kwa Kampuni ya Mafuta ya *British Petrolium* (BP) ni nani kati ya wanahisa anakuwa mhisa mkuu (*Majority Share Holder).*

(ii) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali aandaliwe utaratibu utakao mwezesha kukagua taarifa za Mashirika ambayo Serikali ina miliki kiasi cha 50% ya hisa.

Mheshimiwa Spika, kuimarishwa kwa *STAMICO* kwakuwa kampuni ya Buhemba *Goldmine (MEREMETA) – TanGold* - ambayo imekuwa ikizua mijadala mikali ndani na nje ya Bunge haijulikani ilipo, ni ushauri wa Kamati kwamba *STAMICO* ipewe leseni iliyokuwa ikitumiwa na Kampuni ya Buhemba *Gold Mines* kama jitihada za kujiimarisha na kuwa na wigo mpana wa kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa spika, kuimarishwa kwa Hifadhi za wanyama,katika kujadili taarifa za Hesabu za Mashirika ya hifadhi za wanyama hapa nchini kwa maana ya *TANAPA* na *Ngorongoro Conservation Authority* Kamati ilibaini kwamba Mashirika hujiendesha kwa fedha zao yenyewe na huchangia kwa kiasi kikubwa shughuli za maendeleo ya jamii bila ya kupata aina yoyote ya ruzuku kutoka serikalini.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Mashirika haya yamekuwa yakitozwa kodi lukuki kutoka kwenye mapato yao ya kila mwaka. Katika mazingira mengine, Mashirika haya hutozwa pia kodi ya fedha yanayotoa kama michango kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya jamii katika vijiji jirani. Kwa mfano mashirika hayo hutozwa, 3% kama kodi kwa Bodi ya Utalii nchini; 10% kama mchango kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na 30% kama kodi ya mapato.

Mheshimiwa Spika, madhara ya kodi nyingi kiasi hicho juu ya Mashirika siyo tu kuteteresha utekelezwaji wa mipango Mkakati ya Mashirika hayo lakini pia ni mwelekeo wa kufilisika kwa mashirika haya.

Mheshimiwa Spika, hivyo, ushauri wa Kamati ni kwamba 10% ya kodi inayotozwa kwenda Serikalini ifutwe badala yake paundwe chombo kitakachoitwa *HIFADHI FUND* ambayo itayokuwa inashughulikia maendeleo ya hifadhi hizo na kwamba 30% ambazo Mashirika ya Hifadhi yanatozwa ihamishiwe katika kuimarisha Mfuko huo endapo utaanzishwa.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, ninayofuraha kwamba taarifa ya Kamati imeeleza namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake ya msingi na mafanikio iliyopata katika utekelezaji wa majukumu yake. Hivyo, kuridhihirishia Bunge lako umuhimu wa Kamati hii katika kusimamia ufanisi wa mashirika ya umma nchini.

Mheshimiwa Spika, hivyo ninapenda kuwa shukuru wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi kwa namna kamilifu tulioshirikiana katika kuweka mikakati mbalimbali ya uendeshaji wa Bunge na Kamati zake hususani Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako makini ambao umeniwezesha mimi kuwasilisha taarifa hii hapa Bungeni, umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake bila vikwazo kwa kutoa maelekezo thabiti pale Kamati ilipohitaji msaada wako.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba nimshukuru Mheshimiwa Estherina J. Kilasi, (Mb) Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii pamoja na Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma kwa michango yao katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati, nawashukuru sana na nimejifunza mambo mengi sana kutoka kwao juu ya maana halisi ya uongozi. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto - Mwenyekiti, Mheshimiwa Estherina J. Kilasi – Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Felister A. Bura, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Bahati A. Abeid, Mheshimiwa Mohammed G. Dewji, Mheshimiwa Vedastus M. Manyinyi, Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula, Mheshimiwa James P. Musalika, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi, Mheshimiwa Hafidh A. Tahir,Mheshimiwa Elisa D. Mollel, Mheshimiwa Zaynab M. Vulu, Mheshimiwa Mwanawetu S. Zarafi, Mheshimiwa Mwadini A. Jecha, Mheshimiwa Shally J. Raymond na Mheshimiwa Anthony M. Diallo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge - Dr. Thomas Kashilillah kwa ushauri wake kwa Kamati pale alipowiwa kufanya hivyo. Shukrani zaidi kwa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuendelea kuipangia Kamati Makatibu makini,

wepesi wa maamuzi na waliofanikiwa kuratibu na kushauri mwenendo bora wa shughuli za Kamati kwa kuzingatia miongozo ya utendaji kazi za Bunge na Kamati zake kwa kipindi cha miaka miwili na nusu ya uhai wa Kamati hii. Hawa ni Ndugu Bisile D. Mswige na Ndugu Erick Maseke.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kuishukuru Benki ya Dunia kwa programu yake inayojulikana kwa kifupi kama *PFMRP* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza ziara mbalimbali za kukagua ufanisi wa mashirika.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia Maafisa wote kutoka Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge kwa kurekodi mijadala mbalimbali ya Kamati na kwa kuchapa taarifa hii. Shukrani pia kwa Maafisa wa Polisi kutoka kitengo cha Ulinzi cha Ofisi ya Bunge kwa kufanikisha usalama katika ziara zote tulizoambatana nao. Nawashukuru watumishi wote wa Bunge walioisaidia Kamati kwa namna moja ama nyingine katika kufanikisha majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena nawashukuru wataalam kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Msajili wa Hazina na Maafisa kutoka Shirika Hodhi linaloshughulikia Madeni na Mali *(CHC)* kwa ushirikiano mkubwa waliouonyesha katika kuhakikisha Kamati hii inatekeleza majukumu yake vyema.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru Wakurugenzi mbalimbali wa Mashirika ya Umma nchini kwa uadilifu wao kila walipotakiwa kutoa maelezo, elimu na ufafanuzi wa aina mbalimbali kila walipohitajika kufanya hivyo mbele ya Kamati.

Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza na kunielewa. Nawatakieni mchakato mwema wa Uchaguzi Mkuu, 2010.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni zetu, sasa tutakaribisha mjadala juu ya taarifa zote hizo tatu na orodha niliyoipokea hapa mezani. Sasa kuna wachangiaji wanane. Kwa mpangilio ni Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Mohamed R. Abdalah, Mheshimiwa Athuman Janguo, Mheshimiwa Simbachawene na sasa hivi ameongezeka wa tisa Mheshimiwa Dr. Zainab Gama.

Lakini nadhani tunaweza tukaanza na wawili na pengine hata watatu kama wataongea kwa kifupi na kulenga kwenye mapendekezo ya taarifa hizi, kwa hiyo, kwa mpangilio huu namwita Mheshimiwa Mgana Msindai ajiandae na Mheshimiwa Wilson Masilingi atafuata.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nawapongeza Wenyeviti wote watatu kwa kazi nzuri waliyotoa na kwa kazi nzuri wanazozifanya

kwenye Kamati zote hizi tatu. Nakupongeza wewe kwa sababu mara kwa mara umekuwa unatuwezesha kufanya kazi zetu bila matatizo. Nampongeza sana *CAG*, kwa kweli amekuwa na Kamati hizi zote tatu bega kwa bega na anatoa msaada mkubwa na kuhakikisha mambo yanakwenda. Vilevile nawapongeze sana Benki ya Dunia kwa kutuwezesha na niwapongeze Wajumbe wote wa Kamati hizi hasa Kamati ya *LAAC* ambayo mimi niko ndani na nimpongeze zaidi Mwenyekiti wetu kwa kazi anazofanya bila kuchoka.

Mheshimiwa Spika, sasa nijikite kwenye Kamati yangu ya *LAAC*, na kwa taarifa mimi niko kwenye Kamati hii toka mwaka 1997. Kwa hiyo, nazifahamu Halmashauri, nafahamu mazuri wanayofanya na mabaya yote wanayofanya. Kwa kweli sasa hivi Halmashauri nyingi sana zinajitahidi kufanya kazi inavyotakiwa. Nikitoa mifano ya baadhi ya Halmashauri ndogo kabisa tena mpya ni Halmashauri ya Tandahimba, imeanza juzi lakini ukienda ukiona kazi wanayofanya ni kazi ya kutukuka na kwa mara ya kwanza tulipokwenda kukagua miradi kule, kile kitabu chao hakikuwa na dosari hata moja na ile miradi yao yote tuliyoikagua kwa kweli ilikuwa mizuri mno. Tunawapongeza na tunaomba waendelee hivyo.

Mheshimiwa Spika, tunaomba tu Halmashauri ya Masasi iwape vitu walivyotakiwa wagawane, wawape mapema iwezekenavyo Halmashauri ya Masasi inaota kigugumizi kuwagawia wenzao mali, kwa hiyo, hilo tunaomba hivyo. Halmashauri nyingine ambayo ningependa niipongeze ni Halmashuri ya Nkasi, miaka miwili iliyopita tulikwenda Nkasi kama Kamati tulibomoa madarasa zaidi ya matano, lakini safari hii tulivyokwenda wamefanya kazi ya kutukuka, wamejenga madarasa mazuri mno, wamejenga soko la Kimataifa ambalo kwa kweli mimi ninasema hakuna lililojengwa vizuri kama hilo, wamejenga *dip* na Minada ya hali ya juu sana. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwa hilo na ninawaomba waendelee na majirani waende wasome huko.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Halmashauri ya Mpanda, tuliwapa maagizo na sasa hivi miradi yao inakwenda vizuri ya barabara na hasa barabara za mjini wamefanya kazi nzuri sana. Tatizo lililpo, Mpanda mpaka leo, mji mdogo wa Mpanda bado wanatumia maji ambayo siyo safi na salama. Wanatumia maji ambayo hayawekwi dawa, kwa hiyo, tunaomba hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, nikija Halmashauri ya Mji wa Njombe niwapongeze sana. Viongozi wa pale wamepanga mipango yao mizuri na inatekelezwa vizuri sana. Kwa hiyo, ninaomba waendelee na sisi tuwape moyo wakiwepo Wabunge wa maeneo hayo na viongozi wa Serikali. Vilevile niseme Halmashauri ya Wilaya ya Urambo tulikuwa na matatizo ya maji pale, tukawaambia watengeneze na watu wote wapate maji bila kinyongo kwa kweli. Taarifa nilizonazo kazi inakwenda vizuri sana na vilevile tulikuwa kwenye kumalizia hospitali yao, imekamilika vizuri na tunaomba miradi mingine iendelee hivyo.

Mheshimiwa Spika, vilevile niipongeze Halmashauri ya Wilaya ya Iramba ninakotoka mimi, wanafanya kazi nzuri na hasa kwa sababu mimi niko huko na wanajua wakifanya vibaya mimi siko nao. Pia nizipongeze Halmashauri nyingine zote ambazo

zinajitahidi sana na tuna imani kabisa wote tutafikia lengo. Halmashauri niliyokuwa nasema ya Masasi ni ya Nanyumbu wamefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, nikiendelea Mwenyekiti wangu ameshasema mambo mengi sana, lakini mpaka sasa bado tuna tatizo na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Maeneo mengi barabara hazitengenezwi kwa kiwango kinachosikitisha zaidi, ni ujenzi wa madarasa, ujenzi wa Zahanati na Miradi mingine inayohusika nayo. Maeneo mengi hawajengi kwa *standard* inayotakiwa, maeneo mengi wanajenga kwa kulipua, Serikali inasema mfuko mmoja utoe matofali 25 mpaka 30, lakini ukienda kwenye Halmashauri nyingi unakuta tofali ni kama mchanga ukipapasa hivi yanapukutika. Kwa hiyo, tunaomba pamoja na kwamba tunahitaji hivi kwa haraka, kwa faida ya watoto wetu, lakini ninaomba tuendelee kuhimiza tusipotoshe misingi iliyowekwa na Serikali ya kutengeneza vitu vya kudumu.

Mheshimiwa Spika, hata milango Serikali inakataa kutumia *soft wood* kwenye milango au madirisha, lakini ukienda maeneo mengi wanatumia hiyo. Kwa hiyo, sisi hatuwezi kukubaliana na hilo na Kamati ilikuwa kali sana kwa mambo kama hayo. Bati Serikali imesema ni *gage* 28 lakini kuna maeneo mengi utakuta wanajenga kwa *gage* ndogo ambazo hazifai, bado upande wa ununuzi, bado tuna matatizo makubwa sana. Mimi ninarudia kuiomba Wizara ya Fedha itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kuwasomesha watu wa manunuzi na tuache kulindana. Sekta ya Manunuzi ni sekta muhimu na nyeti na zaidi robo tatu ya hela zinazokwenda kwenye Halmashauri zinatumika kwenye manunuzi.

Mheshimiwa Spika, lakini bado tumeweka watu ambao wanafanya kazi kwa mazoea, sasa mimi naomba sana Serikali, TAMISEMI waangalie hilo. Bado tuna tatizo la watumishi kukaa muda mrefu eneo moja mpaka wanaolewa na maeneo na mazingira wanakuwa wanafanya kazi kwa mazoea. Mimi ningeshauri ni heri Serikali itumie fedha kuhakikisha watu waliokaa kituo kimoja muda mrefu wanahamishwa waende kituo kingine waje watu wapya wenye nguvu na akili mpya kwa ajili ya kufanya hizo kazi. Mimi hilo ninaomba sana.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba sasa hivi bado Halmashauri zetu mapato yake hayatoshi. Mapato bado yanashikiliwa na Serikali Kuu. Sisi tunaomba Serikali irudishe mapato kwa Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunasema tunapeleka madaraka kwa umma, tutapelekaje madaraka kwa umma kama sisi Serikali ndiyo tunakaa na fedha zote na tunatoa kwa Halmashauri kama hisani ? Wao wana haki ya kupata mgao, wana haki ya kupata vyanzo vyao wenyewe wakusanye wenyewe ili waweze kujiendesha.

Mheshimiwa Spika, juzi tumepitisha mambo ambayo kwa kweli mimi naona niyaseme hapa. Mamlaka ni ya Halmashauri zetu, ni Serikali kamili ambayo inaweza kushtaki na kushtakiwa, lakini leo tumewanyang’anya nguvu ya kuajiri watumishi wake, tumerudisha hiyo nguvu kwa kikundi cha watu wachache ambao wao hawaajiri hata *messenger*, hivi kweli tunapeleka madaraka kwa umma. Serikali tunaomba mnapoamua

haya mambo muwe mnatushirikisha, kuamua bila kutushirikisha hatuendi kama inavyotakiwa. Ni kama mnataka kunyang'anya tena, mvunje Halmashauri tena zirudi kuwa chini ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naomba sana Serikali iliangalie jambo hilo upya na lirudi Bungeni tulirekebishe, tuwape mamlaka wenzetu Halmashauri, waajiri watu wao, wawajibishe watu wao kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni hili, niliseme tena. sasa hivi tubadilike sisi Wabunge, tunafanya kazi kwa Mkataba wa miaka mitano, ukimaliza miaka mitano unakwenda kuomba kazi upya kwa wapigakura wako, tuanze kuajiri kwa mkataba kwenye Halmashauri, tunaajiri watu wengine ambao hawana uwezo, lakini kwa sababu Mfanyakazi ni wa kudumu, basi hatuwezi kumwajibisha. Tubadilike na tuige kwa wenzetu wengi tu ambao wanafanya hivi na sisi tufanye hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukaguzi wa ndani, Mwenyekiti wangu amezungumza sana, bado ukaguzi wa ndani hauendi kama inavyotakiwa, bado Wakaguzi wa Ndani baadhi yao wanafanya kazi za Mkurugenzi, hawajitegemei. Kwa hapo hawezi kumwajibisha Mkurugenzi na Wakurugenzi wanachukua ile kama bahati wanawakandamiza, hawawapi uwezo wa kwenda kukagua Vijijini, hawawapi usafiri, posho na vitendea kazi vingine.

Mheshimiwa Spika, tulishasema hapa Bungeni kwamba Kitengo cha Ukaguzi kiundiwe mamlaka yake kutoka juu mpaka chini. Kwa hiyo, naomba sana haya mambo yazingatiwe.

Mheshimiwa Spika, lingine ni ununuzi wa vifaa kwa niaba ya Halmashauri. Hapa karibuni Serikali ilianza kununua magari kwa ajili ya Halmashauri. Ningeshauri kwamba Halmashauri iundiwe kitengo chake cha manunuzi na wafanye hii kazi wenyewe. Halmashauri gari zao wanakatia *insurance*, sasa unapowanunulia unawapa magari ya Serikali, hapo kwa kweli inakuwa haipendezi. *(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**SPIKA**: Aah! Kumbe ni kengele ya pili!

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Kicheko)*

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja za Wenyeviti watatu wa Kamati zetu muhimu tatu za usimamizi wa vyombo vyetu vya Serikali kwa niaba ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Janet Mbene, Mbunge aliyeteuliwa juzi na Mheshimiwa Rais na pia nimpongeze Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu, Mbunge kutoka *CUF* ambaye pia ameteuliwa na Mheshimiwa Rais.

Ninawaombea kwa sababu aliyewateua ni huyo huyo, atakuwa Rais hivi karibuni kwa kipindi cha pili. Jicho lake liwaone tena. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati kwa taarifa zao nzuri sana ambazo zimetolewa kwa kuzingatia mambo ambayo wameweza kuyaona kwa niaba yetu na wamefikisha kwetu kwa mapendekezo mahsusi. Mapendekezo ni mengi na mimi hoja zao zote naziunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali izingatie ushauri ambao umetolewa na Kamati zetu hizi muhimu za Hesabu za Serikali, Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa na Hesabu za Mashirika ya Umma. Nawapongeza Wenyeviti wote wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na mambo ya jumla kuhusu jinsi ambavyo Serikali yetu Kuu inavyosimamia mahesabu ya Serikali ya Mitaa, hayaridhishi. Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ameeleza katika taarifa yake ambayo tumeiona katika kukagua Hesabu za Mitaa, kwamba kwa hali ilivyo, kuna haja na hili pendekezo naomba lichukuliwe kwa uzito wa pekee wa kuwa na Mhasibu Mkuu kwa ajili ya Serikali za Mitaa *(Accountant General for Local Government Authorities)*. Ameeleza mkanganyiko ulioko kwenye *Public Finance Act* ambayo inaweza ikawa kikwazo cha kusimamia matumizi katika Halmashauri zetu, kwa sababu fedha nyingi zinakwenda kwenye Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza wale ambao wamesifiwa kwamba wanasimamia vizuri fedha za umma katika Halmashauri za Wilaya. Ni kweli kuna viongozi ambao ni waadilifu na wawajibikaji katika baadhi ya Halmashauri za Wilaya. Kwa Wilaya yangu, Wilaya ya Muleba, imepata sifa mbaya, hapa, imenifedhehesha. Walikwenda na taarifa za kugushi mbele ya Kamati ya Bunge, ni aibu! Ninasikitika Mheshimiwa Waziri Mkuu hayupo, lakini Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa yupo, wakati hayo yanasemwa Waziri Mkuu alikuwa ndani ya Ukumbi huu na mimi Wabunge walinitazama nikaona aibu! Mimi sio Mhasibu kule. Ndiyo maana niliwahi kuja na hoja hapa kwamba Wabunge tusiwe sehemu ya Madiwani katika kusimamia haya mambo.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa marekebisho ambayo yamefanywa katika uongozi wa Wilaya ya Muleba, nampongeza sana Waziri wa TAMISEMI na nifikishie shukrani zangu za dhati kwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Rais. Sasa Muleba mambo yanakwenda vizuri na sisi nadhani mwaka kesho wale watakaokuja na mimi nikiwemo, hatutasikia taarifa za aibu kama hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkurugenzi mpya huyu ni makini, ana heshima na ana adabu. Kwa hiyo, anafanya kazi kwa kuheshimu watu na kwa kuheshimu viongozi wenzake. Hawezi kujaribu kupeleka taarifa za kugushi. Wale waliojaribu kugushi wote wafuatiliwe na wawajibishwe bila aibu maana wametutia aibu. Hilo ni pendekezo langu la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pendekezo la pili ni la kuimarisha Kamati zetu hizi katika usimamizi, wote wamebainisha jinsi ambavyo kazi zao ni nyingi na wakati mwingine wanafanya hadi usiku, na wakati mwingine hawapumziki. Tunapoahirisha Bunge wanaendelea na kazi. Ninachopendekeza hawa wanakamati wapewe motisha zaidi ili kufanya kazi nzuri zaidi. Waongezewe watalaamu zaidi katika Ukaguzi kwa sababu mimi sikuvutiwa kwenye taarifa hizi kwamba wanakwenda kukagua pengine barabara, wanasema hawawezi kufanya tathmini kwa sababu za kiufundi. Kwa nini mmekwenda huko *in the first place!* Hakuna Mhandisi wa kuweza kutathmini barabara. Sisi ni wanasiasa, mnafika pale maskini, wanawaonesha barabara ndiyo hii, milioni pengine kumi, mnafanyeje?

Mheshimiwa Spika, Kamati zetu ziimarishwe kiufundi na kiutalaam, waende na Wahandisi hata kama jengo wanaliangalia waweze kumhoji huyo Mtalaam, kama ni Mhandisi wa Majengo, au Mhandisi wa barabara. Hivi kuna thamani ya fedha? Lakini ukiwaacha Wabunge wazunguke warudi bila kutuletea *value for money,* wakaeleza masikitiko hapa vile vile! Hatuwatendei haki wananchi ambao wametutuma kuwawakilisha katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nimeshangazwa zaidi na taarifa ambayo ameisisitiza vizuri, Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa kwamba kumbe hizi taarifa tunazosikia kwamba Halmashauri au vitabu vina hati safi, kumbe mkienda kulinganisha hati safi hiyo na hali halisi kwenye utekelezaji wa miradi unakuta ni tofauti, hiyo ni aibu.

Mheshimiwa Spika, huo mfumo uachwe mara moja kwa sababu Bunge lenyewe hili katika kusimamia hatuwezi kuwa tunapokea vitu ambavyo tuna uhakika havielezi hali halisi katika ukaguzi. Tunasema huyu vitabu vyake viliandikwa vizuri sana, lakini unakwenda kuangalia karavati haipo! Mheshimiwa ametumia maneno mazuri, amesema siyo rahisi karavati ya *concrete* kupotea hewani na kesi za namna hiyo nadhani zipo kwenye Halmashauri nyingi. Inaweza zikawa chache, lakini mimi ninavyofahamu kwenye Jimbo langu la Muleba Kusini, ililetwa taarifa tena kwenye kikao cha Chama kabisa, bahati nzuri haikuwa mbele yangu peke yangu maana yake mimi nikisema wanasema Masilingi mpinga maendeleo. Wajumbe wote wa Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi walifukuza hiyo taarifa, maana yake inazungumza kujenga jengo mahali ambapo hakuna hata tofali moja, kujenga mradi wa maji ambapo haupo kabisa, na hawa Maafisa wanaondoka na vitabu vyao wanaendelea kula mshahara maofisini!

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Waziri na Serikali nzima, huu ushauri mnaopewa na Bunge kwa niaba ya wananchi utekelezwe mara moja. Sisi hatuna chuki na mtu, mimi nitafurahi mtu akipewa onyo kali, sipendi mtu afukuzwe kwa sababu na mimi nina huruma.

Mheshimiwa Spika, mwanaume mjinga asitese mke wake na watoto na ukoo mzima, maana yake ukimfukuza huyo mmoja mjinga, unatesa ukoo mzima na marafiki. Hilo lijamaa lipe pesa, mama na watoto wale, lisipewe kazi, likae tu lijifunze kwanza halafu mlijaribu tena. Siyo kulitoa hapa mnaliweka hapa *immediately* linakwenda kuvuruga wengine. Lazima tuwe na huruma na watu ambao kwa kweli wanaathirika na

utendaji mbovu wa watendaji wezi, wabadhirifu wasio na heshima ya madaraka ambayo wamepewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiwa na huruma ya upande mmoja hatuwasaidii wananchi, na mimi nasisitiza wasifukuzwe, lakini wasipewe majukumu ya kufanya, walipwe kwa kutofanya chochote wakati tunawafundisha kwa angalau miezi sita, halafu tuwajaribu tena. Wakirudia, wateremshwe cheo, kwenye Majeshi wanafanya, sehemu nyingine wanafanya, unapokuja kwenye Serikali za Mitaa imekuwa wimbo sasa. Unasikia Wabunge wanalalamika kwamba huyu anaharibu hapa, wanampeleka kule.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Serikali niliousikia kwenye vyombo vya habari jana, siyo kwamba naupinga, kwa sababu umefanywa kwa nia njema na Serikali, mimi natoa maoni yangu binafsi. Ile ya Bagamoyo, wakati wanatangaza nilikuwa na wananchi kwenye Hoteli ninayokaa, walishangilia sana, kwamba wamefukuzwa. Wananchi wanasema sasa Serikali inaanza kufanya kazi. Mimi nikashtuka kweli kwamba hawa wanafurahia watu kupoteza kazi! Kwa hiyo, jamii huko nje inapenda tuchukue hatua na siyo kulindana.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho niseme tu, naishauri Serikali, hii kasi mnayokwenda nayo ya kuimarisha Halmashauri za Wilaya, Mamlaka ya Umma msiongeze, kwanza dhibiti hii. Huku chini hamna uwezo. Halafu kuna tafsiri potofu ya kupeleka mamlaka kwa wananchi au kwa umma. Unakuta huku chini wanadhani kupeleka mamlaka kwa umma ni kupelekwa kwenye Halmashauri ya Wilaya, kwa maana ya Baraza la Madiwani na Mkurugenzi kama Katibu wao. Siyo mamlaka ya Wananchi waliowatuma pale! Mpaka unafika hata kwenye ngazi za Vijiji. Halmashauri za Vijiji zinadhani madaraka kwa umma ni wao! Mkutano Mkuu wa Kijiji ambapo sheria inasema ndiyo mamlaka ya juu katika Kijiji, unapuuzwa! Sisi Serikali ya Kijiji tumeamua! Lete mahesabu, hawatoi! Mimi sipendi kusita kusema natofautiana na Mheshimiwa Msindai. Hawa hela tunazowapa kwa mkono hivi, wanakula hatuzioni; tuwaruhusu kukusanya wenyewe, tutaona kitu?

Mheshimiwa Spika, Serikali Kuu iendelee kukusanya kwanza na hawa watu tuwajenge kimaadili na kiuwezo. *Seriously* nasema hapa mara nyingine napenda kusema ninavyofikiri mwenyewe kwa nia njema, kwamba hawana uwezo katika Halmashauri za Wilaya, tuwajengee uwezo na tumepelekea mambo mengi kwa mfano elimu na afya na barabara.

Mheshimiwa Spika, nimemweleza Waziri wa Maji kwamba kuna ubadhirifu kwenye mradi wangu wa maji, wanasema mamlaka ya usimamizi ni wa Halmashauri, sasa unakuta eti Wizara na ndivyo tulivyoacha, zinatunga sera na kuwaelekeza, vitu huku chini vinaharibika. Mawaziri wanaohusika na sekta, wawe na namna ya kufika kwenye Halmashauri ili kuhakikisha kwamba ile sekta ambayo imepelekwa kule wanasimamia, wasikuharibie halafu useme mamlaka ya kusimamia ni huko, sisi ni sera.

Mheshimiwa Spika, napenda kulisisitiza hilo. Mimi napenda sana kupeleka madaraka kwa wananchi, lakini tuwapelekee wananchi wenyewe, siyo wawakilishi wasio na uwezo na uaminifu wa kuwakilisha wale wananchi, haitatusaidia.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ambazo zitashindwa kusimamia mambo kwa maana ya Madiwani na Watendaji zivunjwe, uchaguzi uitishwe tena na baada ya kuwasimamia na kuwalea. Dar es Salaam ilifanyika na tuliona tofauti. Wengine walichukia kwamba siyo uamuzi wa demokrasia. Sasa watu waharibu tu hii ndiyo demokrasia? Demokrasia ina usimamizi na ina misingi. Demokrasia isiyozingatia misingi ya haki, isiyozingatia uadilifu, hiyo siyo demokrasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipatia nafasi ya kuzungumza, lakini nisikae bila kusema amani tuliyonayo idumu na niwashukuru viongozi wetu wa Chama cha Mapinduzi na Rais wetu wa Zanzibar na Shariff Hamad, wametujengea heshima kwa maridhiano haya na yanajenga mazingira mazuri ya sisi kuweza kujadili mambo na kufanya kwa heshima na kuondoa kutiliana mashaka ndani na nje ya nchi ili tuharakishe maendeleo yetu na kwa hiyo, Waheshimiwa wa *CUF* watuunge mkono, wasipinge CCM, tuwe na maridhiano ya namna ya kuongoza kwa kipindi kingine, mbaki wale wale msiongezeke, wale rafiki zangu mliopo humu humu mbaki wale wale msiongezeke. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia. *(Makofi)*

**SPIKA**: Ahsante sana Mheshimiwa Wilson Masilingi. Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo moja tu hapa. Dr. Luka Siyame - Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya masuala ya UKIMWI anawaomba Wajumbe wa Kamati tatu za Huduma ya Jamii, Kamati ya Maendeleo ya Jamii na Kamati ya masuala ya UKIMWI wakutane leo saa 8.00 mchana huu, katika Ukumbi wa Pius Msekwa ili kukutana na Taasisi ya *Engender Health.* Ni muhimu kwa sababu kutakuwa na maelezo kuhusu dawa zinazotumika na tahadhari nyingine zinazohusu magonjwa.

Waheshimiwa Wabunge, shughuli zilizopangwa kwa asubuhi hii zimefikia hapo. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 leo jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa Mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja za Kamati majadiliano yanaendelea na kwa mujibu wa Spika alipokuwa ananikabidhi kiti aliniambia mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Said Amour Arfi, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Estherina J. Kilasi. Mheshimiwa Said Arfi, karibu!

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia taarifa za Kamati zilizowasilishwa leo asubuhi.

Napenda kwanza kabisa nizipongeze Kamati zote tatu kwa taarifa zao nzuri walizowasilisha na ninaamini kabisa kama zitasimamiwa vizuri zinaweza zikawa ni chachu ya kuleta mabadiliko makubwa katika utendaji kazi wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza pale walipozungumzia suala la madeni. Kamati imesikitishwa sana nami naungana nao katika masikitiko hayo na niisihi na kuiomba Serikali ambayo imetamkwa bayana kwamba ni miongoni mwa wadaiwa sugu, wajaribu kurekebisha dosari hii na hususani katika madawa. Inaelekea Serikali inadaiwa pesa nyingi na shirika letu la umma la *MSD*, matokeo yake ni athari ambazo zinawagusa wananchi wetu moja kwa moja. Kama wiki mbili zilizopita wakati tukiwa kwenye Kamati kule Dar es Salaam nilipigiwa simu kwamba katika hospitali ya Wilaya ya Mpanda hata kidonge cha *Panadol* ilikuwa huwezi kupata kwa sababu dawa hazikuwepo. Lakini hili kwa namna moja ama nyingine linaweza kuwa limechangiwa na kutokulipwa kwa madeni katika bohari ya madawa. Naiomba tena Serikali kwa unyenyekevu kabisa kwamba wajitahidi sana kuangalia suala la kulipa madeni na hususani madawa kwa sababu madawa ni mahitaji muhimu kwa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nizungumzie sasa taarifa ya Kamati ya Serikali za Mitaa. Pamoja na jitihada zinazofanywa za kuleta maboresho katika Halmashauri zetu, lakini bado niiombe Serikali iendeleze jitihada za kuwajengea uwezo Madiwani wetu. Tuna tatizo kubwa sana katika Halmashauri nyingi kutokana na uwezo wa Madiwani na inasikitisha hasa pale Madiwani wanapoingia kufanya maamuzi ambayo hayana maslahi katika maeneo yao  ya utawala.

Nikitolea mfano tukio hili ambalo tumekuwa tukilisoma katika vyombo vya habari juu ya Madiwani kuridhia kiwanja cha *Uhuru Park* pale Moshi kipewe mtu binafsi, hii inasikitisha sana na inaonesha ni kiasi gani Madiwani wetu bado wanahitaji kupata msukumo wa ziada wa kujua majukumu yao. Kwa hiyo, Serikali itengeneze *programme* za makusudi za kuwaongezea uwezo Madiwani wetu ili hata maamuzi watakayoyafanya yasiweze kuwa yanahojiwa na wananchi nje au ndani ya Halmashauri zao. Naamini kabisa mkakati ambao upo wa kuwajengea uwezo Madiwani utaendelezwa na ni vyema basi jitihada kubwa ifanyike katika eneo hilo kwa sababu Halmashauri zetu sasa hivi sio chombo tena cha wananchi bali ni chombo au ni Wakala wa Serikali Kuu, imetwishwa majukumu mengi na Serikali Kuu, kwa hiyo, wasimamizi wa fedha zote zinazopelekwa katika Halmashauri zetu ni Madiwani. Kwa hiyo, suala la kuwajengea uwezo na ufahamu Madiwani bado linabakia kuwa ni la lazima na la kipaumbele ili tuweze kupata tija ndani ya Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya maagizo ambayo yanatolewa na Kamati zetu zinapofanya ziara katika Halmashauri zetu, Kamati ya Serikali za Mitaa imefanya jitihada kubwa sana kuzungukia takribani Halmashauri zote katika nchi hii na kila mahali ambapo

wamekuta dosari ya aina moja au nyingine, wameweza kutoa maelekezo au maagizo kwa kadri walivyoona inafaa.

Lakini inasikitisha hasa pale maagizo yanayotolewa na Kamati zetu ya Bunge yanapopuuzwa na Watendaji. Nitolee mfano tu katika ziara waliyofanya Kamati ya Serikali za Mitaa katika Halmashauri ya Mji wa Mpanda mwaka jana waliagiza kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda ikamilishe majengo ya Shule ya Rungwa. Halmashauri ya Mji wa Mpanda imezaliwa kutoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda ambayo ilikuwa inasimamia miradi mingi wakati ule kabla ya mgawanyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Rungwa iko katika Halmashauri ya Mji, kulikuwa na majengo ya madarasa ambayo yalikuwa yanasimamiwa na Halmashauri ya Wilaya na baada ya mgawanyo huo Halmashauri ya Wilaya haitaki kukamilisha majengo yale kwa sababu tu sasa hayako chini ya usimamizi wao. Lakini nchi hii ni nchi yetu wote, Halmashauri hizi ni zetu wote na shule hizo ni kwa ajili ya watoto wote. Kwa hiyo, maagizo ya Kamati ya Serikali za Mitaa ya kuitaka Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda yanapaswa yaheshimike na Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda ifanye maandalizi sasa ya kukamilisha madarasa yale ili uhaba wa wanafunzi uliojitokeza uweze kupunguza kwa kiasi kikubwa. Naamini kwamba Watendaji watazingatia maagizo yanayotolewa na Kamati za Bunge ili kusiwepo na misuguano katika siku zinazofuata.

Aidha, pia niipongeze sana Kamati ya Serikali za Mitaa kwa kazi nzuri wanayofanya na hasa pale wanapotusemea katika yale matatizo yanayotugusa katika Halmashauri zetu. Namshukuru sana Mheshimiwa Mgana I. Msindai ambaye leo asubuhi ametolea mfano wa tatizo sugu ambalo tunalo katika mji wa Mpanda. Tuna tatizo la kutokuwa na maji salama, tuna maji mengi lakini maji haya sio salama na hakuna jitihada zozote zinazofanywa. Uwezo wa Halmashauri yetu ni mdogo na Serikali kuu inasaidia kwa kiwango kisichokidhi na kisichokuwa cha haraka.

Nitolee mfano kwamba mahitaji ya kujenga chujio katika kianzio cha maji pale Milala kinahitaji zaidi ya shilingi milioni 300, kujenga tanki la kuhifadhia maji, linahitaji zaidi ya shilingi milioni 150, matokeo yake ni kwamba tumepewa shilingi milioni 50 kwa ajili ya ujenzi wa hilo tanki, kwa hiyo, tutaendelea, hapo tanki litakapokamilika na wananchi wetu wataendelea kunywa maji yasiyokuwa salama na matokeo yake ni kwamba maradhi ya magonjwa yatokanayo na maji yanawazunguka wananchi na wakazi wa mji wa Mpanda na mahitaji ya tiba yanakuwa ni makubwa. Kwa hiyo, kama tutaweza kukamilisha miradi hii kwa wakati, pia tutapunguza gharama ambazo tunazitumia sasa kwa ajili ya kununua madawa na kuwatibu watu wetu. Ninaamini kabisa kwamba Serikali italiangalia suala hili na kuweza kusaidia ili kukamilisha hii miradi ambayo inagusa maisha ya wananchi na watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nadhani linahitaji kuangaliwa ni kuzijengea uwezo Halmashauri zetu kwa maana ya raslimali watu. Halmashauri nyingi zina upungufu mkubwa wa Wataalamu na watumishi katika kada nyingine mbalimbali. Kwa hiyo, Serikali ijitahidi kwa kujenga mipango madhubuti kabisa ya kuhakikisha kwamba inatusaidia katika Halmashauri zetu kuweza kupata Wataalamu wa fani mbalimbali. Tuna upungufu mkubwa wa Madaktari, Wauguzi na Walimu wa Shule za

Sekondari na Msingi. Haya yote ni mahitaji makubwa katika Halmashauri, takribani zote katika nchi yetu. Kasi ya uajiri wa watumishi ni ndogo, kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii wakati tukijadili taarifa za Kamati hizi kuiomba Serikali iangalie ni namna gani sasa itaongeza ikama ya watumishi ili kuweza kukidhi mahitaji ya Halmashauri zetu. Ni mfumo ambao umetengenezwa na Serikali Kuu ambayo inajiondosha katika usimamizi wa watumishi na kuwapeleka katika Halmashauri lakini ihakikishe hizo Halmashauri ili ziweze kuleta tija, basi ziwe na watumishi wa kutosha vinginevyo tutaendelea kubakia tunalalamika tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni namna gani sasa tunaweza kuzijengea hizi Halmashauri zetu uwezo wa kukusanya mapato. Sasa hivi Halmashauri hazina vyanzo vyao wenyewe vya mapato, wamekuwa wategemezi wa fedha zinazotoka Serikali Kuu zikiwa na maagizo tayari. Kwa maana hiyo, Halmashauri tena hazina mamlaka ya kubadilisha maelekezo na maagizo ya fedha zilizoteremshwa au zilizoletwa katika Halmashauri husika kwa sababu fedha hizo sio za kwao. Vilevile kwa sababu Halmashauri hazina vyanzo vya mapato, kwa hiyo, kila tatizo linalojitokeza katika Halmashauri linakuwa ni mzigo kwa Serikali Kuu. Kwa hiyo, Serikali Kuu sasa iangalie ni namna gani itaziwezesha hizi Halmashauri ziweze kujitegemea kuwa na vyanzo vyao vya uhakika wa mapato ili angalau adha ndogo ndogo waweze kuzipunguza wenyewe bila kuhitaji msaada kutoka kwenye Serikali Kuu.

Mathalani tuna tatizo kubwa katika miji mingi na hasa miji inayokua kwa kasi kama mji wa Mpanda kuhusu takataka, sasa hivi katika mji wa Mpanda uzalishaji wa taka ni kati ya tani 30 – 40 kila siku, uwezo wa kuziondoa takataka hizo haupo kabisa. Tuna gari moja la taka ambalo tulipewa kutoka Halmashauri ya Wilaya wakati tunagawanya mali, ni chakavu, haliwezi kufanya kazi zote na gari hilo hilo, bali linahitajiwa litoe huduma nyingine ndani ya Halmashauri. Lakini pia pesa zilizotengwa katika kitengo cha Afya Kinga hazitoshelezi kabisa na matokeo yake kunakuwa na mlundikano mkubwa wa takataka katika maeneo ya miji. Ili miji yetu iweze kuwa mizuri yenye kupendeza na kuvutia ni lazima sasa Serikali iangalie namna ya kuwekeza katika Halmashauri zetu ili ziweze kupambana na tatizo hili ambalo linakuja kwa kasi kubwa katika miji mingi ambayo inaendelea kukua.

Lakini kadhalika kutokana na uwezo mdogo wa Halmashauri zetu na kutokuwa na vyanzo vya uhakika wa mapato, mambo ambayo ni ya msingi na lazima ya huduma kwa watu wetu tunashindwa kuyatekeleza kwa sababu hatuwezi kwa upungufu wa fedha. Tunahitaji kuwafikishia mtandao wa mabomba watu wetu, lakini hatuwezi kufanya hivyo kwa sababu Halmashauri yenyewe haina fedha. Kwa hiyo, ingoje kile kitakacholetwa na Serikali Kuu ambacho tayari kinakuja na maelekezo na maagizo ambayo hamuwezi kuyabadilisha. Ni vizuri sasa ili Halmashauri hizi zionekane kwamba ni mali ya watu, maamuzi na mapendekezo yaanzie katika Halmashauri zenyewe na siyo yawe yanatoka juu kuja huku chini. Tukiweza kubadilisha mfumo wa kuwasikiliza watu badala ya kuwasikiliza Viongozi wanavyotaka nafikiri tutaleta mabadiliko makubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie tena kwa mara nyingine kuzipongeza sana Kamati hizi kwa kazi nzuri walizofanya na ninaamini kabisa kama Serikali itazingatia mapendekezo na ushauri uliokuwa umetolewa na Kamati hizi naamini kabisa mabadiliko makubwa na maisha bora kwa Watanzania yatapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Said Arfi. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na orodha ya wachangiaji na sasa naomba nimwite Mheshimiwa Estherina J. Kilasi na Mheshimiwa Ruth B. Msafiri atafuatia.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja hizi tatu za Kamati kwa maana ya Kamati ya *PAC*, *POAC* na *LAAC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kuwapongeza Wenyeviti wetu wa Kamati zote mbili kwa uwasilishaji mzuri, fasaha na ambao umeeleweka kwa kila mtu aliye humu ndani kwa sababu unapoambiwa u-*summarise* taarifa ya mwaka mzima kwa nusu saa inahitaji umahiri mkubwa na inahitaji busara za pekee. Kwa hiyo, naomba niwapongeze sna. *(Makofi)*

Niwapongeze vilevile kwa sababu tunapofanya nao kazi, mimi nina uzoefu, nimefanya nao kazi kwenye *PAC* nikiwa na Mwenyekiti anayetoka katika Kambi ya itikadi tofauti na mimi kwa maana ya Upinzani na sasa niko na Kamati nyingine. Lakini tunavyofanya kazi mambo ya itikadi tumekuwa tukiweka pembeni. Kwa hiyo, kazi na taarifa hii mlivyoiona imeletwa kwa kujali kabisa uzalendo na utaifa wa taifa letu ili kuweza kulifanya lisonge mbele. Kwa hiyo, naomba nipongeze kwa hilo na ninafikiri kwa busara za Mheshimiwa Spika watakaorudi nafikiri theluthi moja ya Wajumbe wa Kamati hii wasipotezwe, warudi kwenye hizi Kamati ili kuweza kuendeleza ule ufanisi wa kazi. *(Makofi)*

Lakini aliongea hapa Mheshimiwa Masilingi, Kamati hizi kwa kweli zinafanya kazi katika hali ngumu sana na bila msaada wa wafadhili wa *World Bank* kutusaidia. Kwa fedha tu za bajeti yetu hazisaidii sana kwa sababu Kamati hizi zinafanya kazi katika hali ngumu usiku na wakati mwingine mpaka saa kumi na mbili au saa moja usiku wanasafiri kwenda kuangalia hali halisi. Kwa hiyo, unaona *over sight committee* hizi tatu zote zingehitaji kuwa na bajeti kubwa zaidi kuliko Kamati nyingine. Kwa hiyo, hili nafikiri ni angalizo la pekee kwa nyakati zijazo. Mheshimiwa Masilingi alilisema vizuri sana hili na mimi naomba nilisemee kutokana na uzoefu ambao nimeuona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nilikuwa na mambo hasa ya kusema kama matatu hivi. La kwanza ni hili suala la mtambuka tunalosema ukaguzi wa ndani. Kwa kweli ukaguzi wa ndani kinaonekana ni kitengo ambacho bado hakijapewa kipaumbele sana katika utendaji wa kazi na nilifikiri ni kwenye Kamati yetu tu kwa sababu tunafikiri ukaguzi wa ndani ingekuwa ndiyo jicho la mkaguzi wa nje kwa maana ya *CAG* akifika kupata taarifa. Lakini inaonekana katika mashirika mengi, *Chief Internal*

*Auditor* au Mkaguzi wa ndani anawekwa tu kwa sababu ya kwamba ionekane kuna kitengo kimeanzishwa, lakini kazi zake hazionekani kufanyika kwa kadri anavyotakiwa kufanya.

Sasa nimesikia kwenye Kamati ya *PAC* na *LAAC* na wao wanalisema hili, najua tumetoka mbali, tulianza na tatizo la *CAG* kwamba awe anajitegemea, tukalimaliza na jana tumelizungumzia kwa upande wa msajili wa Hazina, nafikiri limekwenda vizuri. Kwa sasa nafikiri nafasi ya tatu ni hii ya Mkaguzi wa Ndan. Nafikiri ni mtu muhimu sana, kitengo hiki kiweze tena kutungiwa Sheria au kurekebishiwa ili kusudi kipewe meno na kufanya kazi na tatizo lake ni kwenye upande wa kuripoti maana yake unamkagua mtu ndani halafu taarifa unakwenda kumpelekea Mkurugenzi kwa maana ya Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi mbalimbali, yeye aangalie, ndiyo afanyie kazi hiyo taarifa. Kwa hiyo inaonekana ni kama unafanya kwa matakwa ya Mkuu wa Taasisi au Mkuu wa Shirika.

Nyingine ni kwa upande wa Sheria ya Manunuzi. Sheria ya Manunuzi inaonekana ina matatizo kidogo au sana tu kwa sababu imejionyesha sehemu nyingi. Aidha, unakuta shirika linaamua, halifanyi kwa wakati muafaka kwa sababu tu ya kusema hii Sheria ina matatizo fulani, lakini inawezekana hawajaielewa, lakini vilevile ina marekebisho makubwa na kwa sababu Serikali iko kwenye utaratibu wa kuibadili hii Sheria na mimi naomba kabisa niendelee kuishauri Serikali kuhakikisha kwamba hii Sheria tunaiboresha kwa sababu hapa ndipo kwenye hela nyingi, hapa ndipo kichaka hasa cha kutolea pesa kwa matumizi mengine ambayo hayatakiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa nafasi ya pekee kabisa Bunge lako jipya litakapoanza tunaamini Serikali itakuwa imetusikia ione ni jinsi gani inaleta Sheria hii ya manunuzi ili iweze kurekebishwa.

La nne, naomba nizungumzie upande wa *PSRC,* shirika la *PSRC* baada ya hapo ikaja *Consolidated Holding Cooperation,* shughuli zote ambazo zilikuwa zinafanywa na *PSRC* zimehamishiwa huko kwa maana madeni yote na uwekezaji zinasimamiwa na hii Taasisi. Sasa mimi nilitaka niseme kwa sababu ipo chini ya Kamati yangu, tulifikiri iwezeshwe zaidi kwa sababu wamepewa madeni, lakini wamepewa mashirika yaliyobinafsishwa na wamepewa hela ambayo tumewekeza mahali fulani kwenye hisa, lakini tatizo lililopo ni nani anafanya ufuatiliaji kwenye mashirika yote yaliyobinafsishwa kwa sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kama tumebinafsisha kama alivyosema Mwenyekiti wangu hapo nyuma alivyokuwa anatoa taarifa, tunabinafsisha mashirika mengi, lakini je, yanafanya kazi ile ambayo yalidhamiria kufanya? Je, ile *action plan* ambayo waliitoa kweli inatekelezwa? Sasa ni nani ambaye anatakiwa afanye kazi? Tunafikiri hii taasisi ndio inatakiwa ifanye hii kazi, kwani kuishauri Serikali iongeze nguvu kwenye hili shirika la *Consolidated Holding* kusudi tuweze kufuatilia, tujue. Kuna mashirika yaliyouzwa asilimia mia moja, ni mangapi na yapi? Je, tunahitaji kuyafuatilia? Lakini kuna mengine yalibinafsishwa kwa asilimia 50, asilimia 25 na yenyewe tupewe orodha yake yafuatiliwe tuone: Je, yanafanya kazi yake? Lakini ukiangalia viwanda vingi

ambavyo vilikuwa vimebinafsishwa, ukifuatilia kimoja baada ya kingine, havifanyi kazi ile ambayo walikuwa wamedhamiria kufanya.

Sasa ni nani wa kufuatilia jambo hili? Sisi kama Kamati yetu, tumejaribu kupitia tu kwenye taasisi mbalimbali tukaona kwa mfano tumekwenda Kilombero, tumekwenda Mbeya *Cement*, kuna uwekezaji wa Serikali umefanywa pale. Lakini kama tusingefuatilia, tusingejua ni kwa kiasi gani Serikali inalipwa. Lakini nenda kwenye *BP*, hili shirika la mafuta, ukiangalia, hivi lilibinafsishwaje? Ni nani *owner* wa *BP*? Kama Serikali ina asilimia 50 na mwekezaji ana asilimia 50, sasa nani mwenye *mandate* ya hiyo Bodi? Sasa tunafikiri vitu kama hivi ni vya kuangalia sana.

Lakini ubinafsishaji mbaya zaidi ambao umefanyika ni kwenye upande wa ardhi kwa maana ya mashamba haya mengi. Mwenyekiti amelisema vizuri sana hapa mchana. Sasa unaona tofauti, tangazo linapokuwa limetolewa na *PSRC* lilivyokuwa limetolewa na ukaja ukasoma mkataba wa mauzo unaona vitu viwili tofauti. Sasa hizi kesi zote zitaishaje? Mimi nafikiri *Consolidated Holding* kama wangepewa hii kazi waanze sasa na tutawaomba Serikali nzima kama upande wa mashamba Waziri wa Kilimo ahusishwe, Waziri wa Fedha na hata Waziri wa Ardhi kusudi ile ramani tujue kwamba ukubwa wa mashamba haya yaliyouzwa ni kiasi gani.

Mimi nilifikiri kwa mfano mashamba yaliyokuwa yanamilikiwa na kampuni la *NAFCO,* kinauza kile kilichoendelezwa, huwezi kuuza na sehemu ambayo ilikuwa haijaendelezwa. Tangazo lilikuwa wazi kabisa, sasa wamepewa *document* au wamepewa shamba hili.

Kwa mfano amesema Mwenyekiti, shamba la Kapunga, lakini hakuna mtu aliyempeleka pale akamwambia mpaka wako wa eneo ni huu. Anachojua yeye ni kuangalia amepewa sehemu hii yote, hatakiwi kwenda wapi, hatakiwi kuachia sehemu gani. Kwa hiyo, tunafikiri sasa kwa utaratibu mzuri tu Serikali ianze kufuatilia moja baada ya jingine, mashamba yale Mbozi, mashamba yale ya Arusha na mashamba ya Mbarali. Halafu katika yale mashamba, walikuwa wameweka *action plan* kwamba ndani ya miaka mitano tutakuwa tumefanya yafuatayo, ili aidha tuzalishe mara mbili au tuongeze chakula kwa kiasi fulani.

Sasa kama mtu ameshindwa, maana yake yule mtu anyang’anywe ili liweze kutangazwa na kupewa wananchi kama walivyokuwa wameomba. Kwa hili niliomba sana sana nilisemee na mfano mzuri ni hilo shamba ambalo limezungumzwa sana hapa. Shamba la Kapunga lilitangazwa kwa hekta 5500, lakini limeuzwa mkataba uliosainiwa ni zaidi ya 7500. Kuna hekta 1500 za mraba ambazo zimeuzwa, amechukua ambazo haziko kwenye mkataba.

Sasa tunafikiri kama Serikali itaingilia kati hilo, wananchi wajue sisi tunahama au ni mali ya nani? Kwa hiyo, hili nafikiri Mheshimiwa Wasira alilijibu vizuri sana jana kidogo na leo nimekutana naye, ni kazi ya kipaumbele kwamba tukimaliza hapa hili kwa maana kwamba uongozi wa Wilaya umwandikie kwa ajili ya kwenda kufanya tathmini hizo. Lakini hizi *action plan* zifuatwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni madeni ya wastaafu. Huwezi kujua unapokutana na wananchi wakienda kwa Waziri wa Fedha, hawajui waingie ofisi gani. Kesi ziko Mahakamani, tunaletewa katika Kamati yetu, malalamiko mbalimbali kwamba sisi tulipunguzwa kazini lakini hatujalipwa. Sasa hivi ni nani anaweza kuwalipa? Ni nani anaweza akawaelekeza watu hawa? Nilichokuwa naishauri Serikali, kama mashirika yamebinafsishwa, yule mtu hastahili kulipwa, ni afadhali akajibiwa wazi wazi kwa barua kwamba hustahili kulipwa au unastahili kulipwa, kuliko kila mwakati wakawa wanakwenda kupanda mabasi wanakwenda mjini kufuatilia mafao yao.

Lakini hivi ni kwanini tushindwe kulipa? Kwa mfano nina wastaafu kama 700 hivi, wastaafu kama 100 na kitu kutoka Wilaya ya Mbarali, shamba lile la Mbarali la *NAFCO* wanadai shilingi milioni 700, wameshashitaki, kesi wameshinda, wamerudi wanaambiwa tena tuna-*appeal*. Hivi Serikali uki-*appeal* kwa wananchi wako kweli inaonesha chochote kile cha kuwajali?

Mimi nilikuwa nafikiri shilingi milioni 700 hazitatugaramu sana ukiwalipa hao wastaafu wote. Wako wa Urafiki, wa Kilombero, Serikali ingepitia madai yao ikawalipa halafu tukaanza na ukurasa mpya, wangejua sana Serikali yao inawajali.

Kwa hiyo, mimi naomba kabisa nitoe msisitizo kwamba Serikali sasa ifike wakati tuangalie kila mahali ambapo wananchi wanadai, hasa wa mashirika ambayo yalishauzwa au yalibinafsishwa uone umuhimu wa kuwalipa mafao yao pale ambapo haki imetendeka.

*Ofcourse*, tunajua kwamba kuna watu wanagushi, wanafanya vyovyote, lakini nafikiri tathmini ifanyike shirika kwa shirika ili kuweza kuwalipa hawa na waone kwamba kweli Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi inawajali kama ilivyosikivu mpaka sasa. Hilo nilitaka niliseme kwamba ninaamini kabisa Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni sikivu kama ilivyokwishafanya kuwalipa walimu na sasa walimu wanaendelea kulipwa, nafikiri na hili litasikilizwa na litafanyiwa haraka iwezekanavyo. Kuna kesi za Urafiki, Kilombero *Sugar*, nafikiri Mwenyekiti ni shahidi, mwekezaji ameshawalipa asilimia yake tumebaki sisi kuwalipa.

Yaani ukifika, unafanya Mkutano unapata ki-*note*, Mheshimiwa sisi hatujalipwa; Mheshimiwa sisi hatujalipwa; lakini hii nchi ni nchi yao. Kwa nini wasilipwe ili waweze kufanya kazi zao vizuri na pia waweze kuishi maisha ambayo ni ya amani na sisi tupo ndani ya Serikali ambayo inajali watu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa ambalo nilitaka nizungumzie, kuna hii sheria ya *PPF*, kwa kweli tumekuta mawasilisho mengi, hayapelekwi kule kunakotakiwa kwenye mifuko ya maendeleo ya jamii. Kwa hiyo, wafanyakazi walishakatwa lakini haikuwasilishwa na mashirika kukosa pesa. Sasa nafikiri sasa Hazina ingepitia mashirika ambayo nafikiri makato yao hayajawasilishwa ili yaweze kuwasilishwa. Lakini nilipata changamoto ya swali moja, kuna wananchi wastaafu wana Chama chao ambapo walikuwa chini ya Mfuko wa *PPF*. Najua sheria labda itakuja baadaye, wako Mkoa wa Mbeya kama 300. Wanasema Mheshimiwa Mbunge sisi tumestahafu na tulikuwa tunakatwa *PPF*, sheria ilipokuja inasema mpaka tufikishe miaka

55 ndipo tuanze kulipwa. Mmoja akasema mimi nimepimwa afya yangu, naona hainifikishi hiyo miaka 55, hivi Serikali haiwezi kunisaidia mimi nikachukua mafao yangu mapema nikaondoka nayo na nikaweza kuyatumia sasa?

Sasa nafikiri tuliitunga wenyewe hiyo sheria, sasa ni wakati muafaka wa kuangalia kutokana na hali ya maisha ilivyo, mimi nina miaka arobaini na tano, naona hali yangu haifai, basi tuweke na hako ka-*provision* kwamba unaweza ukaomba ukapewa *pension* yako mapema iwezekanavyo ili kusudi uweze kumudu maisha kwa kipindi hicho. Hili ni la kuangalia sana na nafikiri Mwanasheria Mkuu atakapokuwa analeta mabadiliko ya sheria litasimamiwa kwa kiasi kikubwa kwa kuona kwamba tusisubiri miaka 55. Mimi naona kabisa nimepimwa, naumwa ugonjwa ambao siwezi kufika *ten years to come*, kwa nini nisilipwe? Sasa na hao na chama chao walikuwa wamepanga angalu waje wamwone Waziri waweze kutoa kilio chao kwamba *fifty percent* ya watu wetu, tunafikiri tunataka tuchukue *pension* yetu sasa hivi, tusisubiri miaka hamsini na tano. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa na hayo ya kusema, lakini naipongeza sana Kamati yangu kwa kazi nzuri ambazo wamezifanya, nimpongeze Mwenyekiti wetu wa Kamati namwombea arudi kupitia Chama kingine aweze kutufanyia kazi yetu vizuri. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kilasi ingawa umesahau kutaja jina la huyo Mwenyekiti wako wa Kamati, labda mimi nitamalizia kwa kutaja Mwenyekiti wako wa Kamati anaitwa Mheshimiwa Zitto Kabwe ili kuweka kumbukumbu iwe sahihi.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri na anayefuatia kadiri ya orodha ya Mheshimiwa Spika aliyoitaja asubuhi atafuatia Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nataka nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwenye hotuba za Kamati hizi tatu. Nawapongeza sana wale waliowakilisha hoja hizi asubuhi ya leo, nawanapongeza kwa jinsi walivyopangilia maudhui, nawapongeza kwa kazi nzuri ambayo kimsingi Kamati zote zinasimamia matumizi ya pesa za Serikali kwa maeneo mbalimbali ikiwemo Serikali kuu, Serikali za Mitaa pamoja na Mashirika. Nina hakika hayo ndio maeneo ambayo ni mazito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mmoja wa Kamati hizo tatu ambazo asubuhi ziliwasilisha hoja zao, kwa hiyo, nitapenda tu nizungumze machache ambayo yanahusu matumizi ya fedha za Umma. Kwa ujumla Kamati zote tatu zimedhibitisha kwamba matumizi ya fedha za Umma sio mazuri. Sehemu kubwa ya pesa zinazotengwa kwa ajili ya kunufaisha Watanzania hazitumiki ipasavyo. Pesa nyingi zinapotelea katika manunuzi ama zinachelewa kufika, ama zinapokuwa zimefika hazifanyi kazi inayostahili, ama basi pale zinapotokea kufikia, basi kazi inayokwenda kufanyika haifanani na ile thamani ya fedha. Haya kwa kweli ndio mambo ambayo yanatakiwa yarekebishwe sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya jitihada kubwa sana, naipongeza Serikali, waliotangulia wakaamua sasa kwamba kwa kuwa kwenye Halmashauri ndipo kazi kubwa sana inafanyika, angalau kiasi cha asilimia 25 ya bajeti kiteremshwe kwenye Halmashauri, hakijafikia kiasi hicho, lakini Serikali imefanya vizuri kiasi cha 23 kinatolewa kwa ajili ya Halmashauri. Hapo tunategemea sasa zinakwenda kutumika wapi? Zinatumika kwenye kujenga barabara zetu za vijijini, zinatumika kwenye kujenga shule zetu wakishirikiana vizuri sana na wananchi kwa sababu katika miradi hii, wananchi wa kawaida pia huwa wanachangia. Zinashiriki kuboresha mazingira ya shule yakiwemo vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, ununuzi wa madawati, vyoo vya wanafunzi pamoja na walimu na mazingira kuonekana ni mazingira yaliyo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunapofika katika suala zima la ujenzi ambapo ujenzi kwa vyovyote vile tunategemea tunapata mkandarasi ambaye ana vyeti na ambaye amethibitishwa kwamba huyu anaweza akatusaidia. Viwango vya ujenzi kwa kweli mara nyingi ni vile ambavyo ni vibovu sana, sakafu katika vile vyumba ni ile ambayo inaondoka kwa ufyagio, lakini ukienda kwenye madirisha kama kule kwetu Muleba ambapo kuna upepo mwingi, basi madirisha yale yanondoka na upepo. Sasa unakuta yale makusudio ya matumizi mazuri ya fedha hayafikiwi. Haya kwa kweli ni mambo yanasikitisha na hapo ndipo Kamati zilipowasilisha asubuhi ambapo zimethibitisha kwamba usimamizi sio mzuri. Pesa zikishafikishwa kwenye Halmashauri, hakuna usimamizi tena wa zile fedha zinafanya kazi gani kule vijijini. Kwa hiyo, hakuna anayekwenda kuangalia kwamba madarasa yamejengwa kwa kiwango, hata wakikosea, kuna mlango ukakataa ku-*fit* pale hakuna mtu anayekwenda kufuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili tulifanye kwa uzalendo, wakati mwingine Serikali inakuwa haina pesa za kulipa kila kazi inayofanywa ya ziada na mtaalamu aliyepelekwa kule.

Lakini mimi nilikuwa napendelea kusema kwamba kila kitu ambacho kipo kwenye mipango na kila Kijiji kipo chini ya Kata na kila Kata ina Mheshimiwa Diwani wake taratibu hizi zifanyike vizuri. Ufuatiliaji uwe karibu karibu. Walipokuwa wanatoa taarifa kwenye Serikali za Mitaa, wametoa mfano wa barabara ya Muleba, inatoka Kagono kwenda Kangantebe, ni barabara ninayoifahamu sana, wakasema itengenezwe kwa shilingi milioni tisa. Lakini Kamati ilishindwa kudhibitisha viwango kwa sababu ya mazingira. Sasa sisi ni wamoja ambao tuna mvua nyingi kwa mwaka, lakini kuwe na wakati maalamu wa kutengeneza barabara, kuna wakati mvua zinapopungua, lakini vile vile ni vizuri tunapokuwa katika taratibu za kutengeneza barabara wale ambao wanasimamia wajitahidi kuzitengeneza.

Kipindi cha mwaka 2000/2005 Jimbo la Muleba Kaskazini au niseme Wilaya nzima ya Muleba ni moja iliyokuwa na barabara nzuri sana, lakini mwaka 2005/2010 Wilaya ya Muleba ni moja ambayo ina barabara ambazo sasa nyingi ni hafifu. Nilipokuwa nikifuatilia suala hili nikaambiwa Mhandisi yuko pekee yake hana, Wasaidizi nisimlaumu. Sasa sijui kama Serikali inajua hili, kwa sababu tulishakubaliana kwamba tunapotengeneza barabara tusirudie tena kuzitengeneza kwa kiwango kama tunaanza upya, bali zikarabatiwe mara kwa mara kusudi zisiharibike tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini unakuta sisi tunaanza tena kutengeneza barabara kama tunaanza upya, lakini kigezo kinakuwa kwamba Mhandisi hana wasaidizi, sijui kama Serikali inalijua hili kwamba Muleba kuna Mhandisi na hana wasaidizi. Sasa pesa zinazokwenda zinarejeshwa Makao Makuu kwamba hazikutumika ama zinaachwa zitumike bila vile viwango kufikiwa ili mradi barabara imetengenezwa. Hii ni hatari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba pesa zinapopelekwa zihakikishwe kwamba na watu wanaokwenda kuzifuatilia na maana ya wataalamu, wataalamu wawepo wa kutosha. Kama wataalamu hawatoshi ni vizuri kabisa Serikali ikajitahidi kupeleka Wataalamu kwa sababu hawa ndio wasimamizi. Anayetakiwa kusimamia barabara ni mhandisi. Diwani anaweza kupita anaangalia, lakini Diwani hana ujuzi wa kufahamu barabara nzuri inakuwa vipi.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali iangalie sana. Lakini miradi inayogusa vijiji moja kwa moja tumemaliza uchaguzi wa Serikali na vitongoji, ni juzi tu mwaka jana. Hakuna mafunzo yametolewa, sijui unategemea Mwenyekiti wa Kijiji aongozeje Serikali yake kwa miaka mitano ambapo anatakiwa apokee pesa, ajenge darasa, ajenge nyumba ya mwalimu, aone barabara inatengenezwa, hivi anajua wapi?

Kuna pale ambapo ni bahati viongozi hawa ni wale ambao walikuwepo, lakini sehemu nyingine ni wapya. Sasa katika hali hii usimamizi unakuwa ni mdogo sana na unakuta Mwenyekiti hajui chochote, Kamati yake hana namna ya kuiongoza, matokeo yake sasa wanafikiri kila kazi ni ya Mbunge. Mbunge akifa, Mbunge darasa, Mbunge Choo cha wanafunzi, Mbunge mtoto; hizi ni kazi za Serikali za Vijiji ambazo zinapelekewa pesa kwenye Halmashauri za Wilaya.

Lakini Mwenyekiti hajui kwamba inakuwa vipi. Diwani wakati mwingine na yeye hafuatilii, kwa hiyo, Mwenyekiti aweze kumwuliza Diwani, Diwani aweze kuuliza kwenye *council* ambapo ndio pesa zinakuwepo. Sasa haya nilipenda yafanyike kwamba moja ya kuboresha utendaji kazi kwenye Halmashauri ni pamoja na kuhakikisha kwamba Serikali za Vijiji wameelimishwa jinsi inavyopaswa na halafu elimu hii isiwe ya mara moja, iwe ni ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna kikao cha maamuzi kikubwa sana kwenye Vijiji ni kikao kinaitwa Mkutano Mkuu wa Kijiji, ile mikutano imepewa nguvu sana ya maamuzi mazito, lakini inakuwa ni Mwenyekiti yule yule asiyeelimishwa na Serikali yake ndio asimamie. Haya ni matatizo.

Wale wataalamu ninaowaomba wawepo wengi kwenye *council*, wasaidie kujipanga kwenda kuhudhuria Mikutano Mikuu ya Vijiji ili maamuzi mazito yanayotoka yanayogusa ardhi, yanayogusa ujenzi, yanayogusa ubadhirifu wa mambo mengine waweze kusaidia na hata kuweka wazi bayana nini ambacho *council* zao zimeamua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasaidia na itapunguza sana malalamiko. Haya ninayasema pia nikiomba wasaidiwe sana wakuu wa idara, mimi sina hakika kama wakuu wa idara wa usafiri, kwa mfano wanaokwenda kusimamia ujenzi wa shule, sijui

kama wana usafiri au wanategemea watumie usafiri wao ama wa kuomba kwa Mkurugenzi.

Kwa hiyo, mpaka gari itoke kwenye *pool* ndio aweze kwenda kufanya hii kazi. Mwaka 2000 mimi nilipopata Ubunge, kulikuwa na barabara tatu tu ambazo zilikuwa chini ya *council* kwenye Jimbo langu, leo ninazo 30.

Kwa maana hiyo, huyu mhandisi ambaye alikuwa hatembei sana, sasa kama hawawezeshwi kupewa chombo atawezaje kupata kazi? Kwa sababu wakati mwingine tutawalundikia lawama, lakini lawama hizi unakuta kuna mahali ambapo pengine zinasimamia. Nilikuwa naomba mambo yote mawili yaangaliwe kusudi kuhakikisha kwamba huduma zetu zinakuwa ni nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo tumelalamikia sana ni matumizi ya thamani za Serikali. Nashukuru sana kwenye semina ambayo tulikuwa nayo muda mfupi uliopita tumeelezwa jinsi ambavyo thamani zinazotoka nje ya nchi zinasikitisha. Nchi yetu ina miti mizuri, tuna mininga, tuna sijui mivule, tuna miti sijui inaitwa nini sijui, ina majina mengi mazuri mazuri tu, lakini miti ile ni miti imara. Hata meza ile iliyobeba siwa, ni meza iliyotengenezwa Magereza, ni meza nzuri. Hii hapa hata kama hili Bunge litakaa miaka ishirini hapa, hii meza haitakuwa chochote.

Lakini meza tunazokwenda kuzinunua, vifaa tunavyokwenda kununua kutoka nje, thamani ya zile za nje ni zile zimetengenezwa kwa takataka za mbao na mavumbi ya karatasi na ikipata maji kidogo hauna kifaa kile, kikibebwa kwenda eneo lingine hakifai.

Lakini licha ya ubovu wake huo uliopo, Serikali inaathirika kwa vipi, kila mwaka tunatenga pesa za samani tena za mamilioni ya pesa. Sasa nenda kaangalie pesa zile nani anafaidika, ni mtu wa nje. Lakini tungetumia samani za nchini humu pesa zingebaki hapa nchini, watu wangekuwa na moyo wa kuboresha mazingira kwa kupanda miti lakini wanapata kipato. Ajira kwa vijana zingeongezeka na watu wengine wanaofanya kazi katika sekta hiyo, ajira ingeongezeka. Lakini ule ufundi ungeboreka zaidi.

Sasa mimi nilikuwa napenda kuiomba sana Serikali kama hii imewezekana Maliasili, sasa hivi samani zao ni za Tanzania, inawezekana Viwanda na Biashara, imewezekana tumekuta ujenzi unafanyika pale Mwanza imewezekana hospitali ya Bugando. Sasa kama hii inawezekana huko kwa nini sehemu nyingine haiwezekani? Hii iwe ni *commitment* ya Serikali kuhakikisha kwamba katika mwaka wa fedha ujao kusiwepo Wizara yoyote ya Serikali ama sekta yoyote inayokwenda kuagiza samani kutoka nje ya nchi, samani zote zitoke humu nchini. Wataalam tunao, vifaa tunavyo na miti tunayo ya kutosha. Tatizo ni kwamba iende wapi. Ndiyo maana kunakuwa na *smugling* na uvushaji ovyo wa miti yetu kwa sababu haitumiki vizuri hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo naomba niliseme ni matibabu ya wazee. Hivi kuna sababu ipi inayosema wazee watibiwe bure lakini wasio na uwezo. Hivi kama mzee amepata bahati ya kuishi zaidi ya miaka 60 sasa yeye labda aliwekeza vizuri kwa wanae na Mwenyezi Mungu akawapa uzima wakaishi. Kuna waliowekeza

wamewapoteza hawajafikisha umri huo, lakini sasa kwa hali nzuri anayoonekana nayo kwa macho ikawa ndiyo adhabu yake kwamba mzee huyu asitibiwe.

Nashauri kwamba wazee wote wenye miaka 60 na kuendelea watibiwe bure na Serikali kwenye hospitali zetu za Serikali. Haitoshi hawa wazee katika umri huo ni umri wenye magonjwa mengi. Wapewe bima, bima iwasaidie pale wanapokuta kwenye zahanati dawa ile haipo akaenda kwenye Kituo cha Afya haipo, aweze kwenda mpaka kwenye hospitali zingine za juu ambapo bima ile inaweza ikatumika. Vinginevyo itaonekana kwamba wazee wetu na tuchukulie wazee ambao tunao ni wazee waliofanya kazi enzi za ujamaa na kujitegemea, ule ulioshika nguvu, hakujiwekea kitu chochote.

Sasa inapofika leo huyu mzee amevaa suti, suti ya miaka 20 ya miaka 10 iliyopita ndiyo inakuwa kigezo cha kumfanya mzee anyimwe tiba ya Serikali ya bure kwa sababu eti ana watoto wanajiweza, ama ana shamba na mifugo. Hii tunakuwa hatukumtendea haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuishi ni Mungu anayetupa umri kuwa mrefu. Kwa hiyo, mimi nilikuwa napendekeza kwamba wazee na wenyewe watibiwe bure. Najua Serikali itasema hatutajua idadi ya wazee, tunawajua. Tumeandikisha wazee hapa kupiga kura wapo na wanaishi. Tuendelee kutafuta takwimu tunawajua, tumefanya sensa tunawajua. Wazee watibiwe bure bila ya kuwa wamebughudhiwa sana. Lakini nipende kuiomba Serikali isimamie mipango miji. Kila inapotokea tu aina kwamba sasa panataka kuonekana ni watu wanajikusanya kuanzisha kamji, naomba papimwe ili kusudi isaidie kuja kupitisha miundombinu ambayo ni muhimu kwa ajili ya maisha ya watu wanaokaa pale. Hivyo nalipongeza Jiji la Mwanza kwa kazi nzuri inazofanya na naomba Serikali iwape pesa kuhakikisha inaboresha ule mji vizuri zaidi iweze kusaidia kuwateremsha watu walioko mlimani hatua kwa hatua mpaka hatimaye ule mji uweze kukaa vizuri na wananchi wasilalamike. *(Makofi)*

Mwisho naipongeza Serikali sana kwa jinsi ambavyo imewapa Maafisa Masuuli wengi nafasi na wengi wao ni wanawake. Naipongeza sana Serikali na nasema hivyo kama mmoja wa wajumbe kwenye Kamati yetu, nawaona akinamama ni wengi ma-*RAS* wameongezeka na mafungu mengine ni wengi. Sasa naendelea kuwaomba akinamama wawe waaminifu, wawe wachapakazi ili kazi hii na majukumu haya waliyopewa yaweze kudhibitika na yaweze kufanyika vizuri, walete sifa nyingine nzuri ya ziada katika nchi yetu kwa jinsi ambavyo nao wameshirikishwa katika kufanya kazi hii ambayo ni kazi ngumu lakini inataka usimamizi na kujitolea zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niliyokuwa napenda kuyaongelea ni hayo na kwa kuwa nimeyaongelea kidogo kwa kituo naamini yameeleweka, sitayafanyia *summary.* Basi nataka nikushukuru kwa kunipa nafasi na nashukuru sana watu waliowasilisha leo na naamini Serikali yetu itayafanyia kazi haya ambayo tumeyazungumza. Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Ninaunga mkono hoja zote za Kamati zote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Ruth Msafiri. Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah na Mheshimiwa Athumani Janguo ajiandae.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii kuweza kuchangia taarifa za Kamati zote tatu za Mahesabu ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma. *(Makofi)*

Niwapongeze Wenyeviti wote kwa kutoa taarifa nzuri ambazo tunachangamoto kubwa Bunge hili kuhakikisha kwamba Serikali inakaa pahala pazuri katika matumizi ya fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa ni uwazi wa matumizi ya fedha za Serikali kwa wananchi. Hilo ni jambo la msingi kwamba wananchi wana haki ya kujua pesa zao zinatumika vipi na nishukuru kwamba Kamati zetu sasa hivi zinaweka wazi wakati wa mahojiano na Maafisa wa Serikali katika kuwaelimisha wananchi na wao kufahamu matumizi ya fedha hizi zinavyokwenda. Lakini haitoshi kwa kutoa tu taarifa katika vyombo vya habari kwa maana ya magazeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona sasa ifike pahala kama *session* hii au kikao hiki cha Bunge sasa hivi kinaonekana nchi nzima. Mwananchi kwa wakati wote akitaka kusikiliza kinachoendelea katika Bunge basi anaelewa mijadala mbalimbali ambayo inazunguzwa na inampa faida na kuelewa jinsi Bunge linavyofanya kazi. Sasa ifike pahala na hizi Kamati za Hesabu za Serikali Kuu, Serikali za Mitaa pamoja na Mashirika ya Umma kuwe na utaratibu maalum sasa kwamba vyombo vya habari viweze kushirikishwa na kutangazwa *live,* mwananchi yeyote ambaye anataka kufuatilia matumizi ya fedha za umma aweze kufahamu kwa sababu ni haki yao. Hilo mimi naona linawezekana ni kiasi tu cha vyombo vya habari kutaka kushiriki kwa pamoja ili waweze kupata taarifa nzuri. Vipindi vingi vinavyoonyeshwa kwenye *television* viko vingine vinaonyeshwa lakini siyo wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri utakumbuka kuna vyombo vya habari vingi vinaanza kupiga muziki kuanzia asubuhi, ikifika taarifa ya habari wanasita, halafu wanaendelea tena na muziki. Basi tutumie hizi nafasi nyingine wakati mzuri kwamba kutangaza mambo muhimu ambayo wananchi na wao wataweza kupata faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo kwamba tumeliona sisi kwenye Kamati zetu ni upungufu wa wataalam ambao wanaweza au hawakuweza kutosheleza zile kazi zilizokuwa zinahitajika kufanywa katika hizi sekta. Kwa mfano, Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ana wataalam ambao hawatoshi. Nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kutoa ahadi ya kuimarisha Ofisi hii. Hii itaweza kusaidia sana kuweza kudhibiti fedha za umma. Hili jambo ni la msingi kwa sababu fedha zinazopotea ukilinganisha na kuingiza fedha katika kuimarisha Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali faida yake ni kubwa ku-*invest* katika ofisi ile kuliko hasara ambayo tunaipata sasa hivi. Kwa hiyo, mimi naiomba Serikali ifanye haraka kabisa kuimarisha ofisi hii na hatimaye iweze kufanya kazi nzuri na kuweza kusimamia na kukagua pesa za umma jinsi zinavyotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini isitoshe kuna Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali hivi sasa iko chini ya Wizara ya Fedha, sawa lakini inatakiwa ijitegemee kama

inavyojitegemea sasa Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa sababu hiki ni chombo muhimu na ndiyo inasimamia fedha zote za nchi hii. Sasa kuwa chini ya Wizara au kuwa chini ya Katibu Mkuu kwa kweli ule uhuru wa kufanya kazi unakuwa siyo mzuri. Sasa ni vyema Serikali ikafikiria kuanza kuiacha Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ijitegemee yenyewe ili kuleta ufanisi katika utendaji kazi wa fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nilizungumze ni fedha ambazo kwamba zinakwenda katika Halmashauri zetu. Ni fedha nyingi na ni kwa mara ya kwanza katika hii Awamu ya Nne, viongozi kule vijijini kupokea fedha nyingi katika miradi mingi ya maendeleo. Inafika pahala wanaziona kwamba zile fedha kama hazitakwisha au kwamba sasa matatizo yote yatakuwa yamemalizika, lakini kinachotokea ni kwamba Mkurugenzi anapopata zile fedha akazipeleka kwenye Kamati ya Maendeleo kule kijijini kufuatilia ile miradi na matumizi ya fedha zile hapa ndiyo kwenye matatizo.

Sasa mimi naamini Halmashauri ina wataalam wa kutosha katika miradi mbalimbali. Lakini basi Serikali iweke utaratibu maalum na hata kama Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itatoa *circular* kuhakikisha ni jinsi gani ya kusimamia hizi fedha zinazokwenda kule vijijini, Kamati ya Miradi au Kamati ya mradi wowote pale kijijini wale viongozi wa kijiji upeo wao wa kufahamu mambo haya ni wachache sana. Utakuta yuko mtu mmoja mjanja pale basi anawaburuza anavyoona yeye inafaa. Hatimaye ile *value for money* ambayo ionekane kwamba imetumika vizuri tutakuwa kwamba baada ya muda mfupi ule mradi umekwishaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ni kupoteza fedha za Serikali ambazo tija yake ni ndogo sana na hatimaye mradi ule ukiharibika inabidi sasa Serikali itenge fedha nyingine ya kupeleka pale ili kuuimarisha ule mradi, wakati kulikuwa hakuna sababu isipokuwa zile fedha zingesimamiwa vizuri basi ule mradi ungekuwa imara na ungechukua muda mrefu ili kuweza kuwasaidia wananchi katika maeneo yao. Nitoe mfano, kwenye kijiji kimoja kule Pangani, Serikali ya Kijiji iliyopita katika Kijiji cha Mtang'o walipelekewa fedha za Serikali shilingi 7,200,000 wajenge nyumba ya mwalimu, *two in one*. Umefika wakati wa uchaguzi ile nyumba haijakamilika lakini wamenunua mbao, wamenunua mabati, wamefyatua matofali, hatimaye uchaguzi umefika, Serikali iliyopita haikurudi madarakani, baada ya kufika hii Serikali mpya hakuna makabidhiano kwa sababu kuna vifaa pale. Sasa utakuta ule mradi umesimama na ule uongozi mpya hawajui wafanye nini. Sasa inabidi Mbunge naye aingilie kati apate kujua ni kitu gani kinachoendelea, matofali yameharibika, mbao zimeharibika, bati mengine yameshaibiwa. Sasa haya ni matatizo ambayo Mkurugenzi wa Halmashauri anatakiwa aweke utaratibu mzuri ni jinsi gani ya kuweza kutumika hizi fedha na kuweka muda maalum kwamba huu mradi unatakiwa ukamilike. *(Makofi)*

Sasa na Mbunge naye kama Mbunge ambaye yupo pamoja na wananchi, hana lile rungu la kwamba kama yeye ni Serikali na kuweza kuchukua hatua kama Serikali inavyotaka kwa sababu mle kuna watendaji ambao kwamba wanakiuka taratibu na kuzitafuna zile fedha. Kwa hiyo, inabidi sasa Mbunge azungumze na *DC*, azungumze na Mkurugenzi waende *site* ili watatue yale matatizo hali ya kuwa kusingekuwa na sababu

ya kufika huko. Sasa haya ni mapungufu ambayo yapo katika fedha zinazokwenda vijijini kuhakikisha kwamba zinafanya kazi kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo la matumizi mabaya ya fedha katika Serikali. Bajeti ni kubwa na matumizi ni makubwa. Wakati ule Serikali inakusanya, wakati wa Awamu ya Pili, ilikuwa inakusanya shilingi bilioni 25 kwa mwezi. Tumepata taarifa tu kwamba wao wenyewe wanasema tungepata shilingi bilioni 80 matatizo yamekwisha. Lakini hivi sasa Serikali inakusanya zaidi ya shilingi bilioni 300, lakini matatizo hayaishi na yanaongezeka na matumizi yanazidi. Sasa tunashindwa kuelewa kama mlitegemea kwamba tungefika kiwango shilingi bilioni 200 tungeweza kusawazisha matatizo yetu. Sasa tunakusanya zaidi ya shilingi bilioni 300 lakini matumizi yanazidi na matatizo hayamaliziki. Sasa hapa tatizo la matumizi ya fedha ambayo si ya lazima.

Waheshimiwa Wabunge wengine wameshazungumza kama mifano ya kununua magari ya kifahari, lakini mimi niipongeze Wizara ya Maliasili na Utalii. Nilitembelea Wizarani pale, Wizara yao mpya. Kwa kweli samani zao zote ni za mbao za mninga au mvule. Ni mbao asili ambazo zimetumika za hapa hapa nchini.

Mimi kwa kweli nimefarijika sana kuona Wizara yenyewe ya Maliasili na Utalii wameweza kuonyesha mfano wa maliasili yetu wenyewe na kufanya samani zile kwa kitendo kwamba sasa ofisi yetu ya Wizara samani zote zitakuwa ni za mbao za asili zinazotokana na miti yetu hapa nchini. Sasa kama hilo limewekezana Wizara ya Maliasili na Utalii nina hakika Wizara nyingine inaweza ikafanya, lakini la msingi tu hapa ni kwamba yule kiongozi ambaye anatoa pesa kwa ajili ya ununuzi wa samani za Wizara au Idara mbalimbali basi kuwe na *circular* ambayo itasisitiza kwamba kuanzia sasa ni marufuku kununua samani kutoka nje na kuanzia sasa tuanze kununua samani zetu zinazotengezwa hapa nchini, hii itasaidia ajira mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Magereza, *SIDO*, makampuni mengi tu ya watu binafsi wanatengeneza samani nzuri. Hizi samani zetu ndani ya Bunge zinapendeza lakini Mungu apishilie mbali ikinyesha mvua ikiingia humu ndani, tukirudi tena katika Bunge lingine na kwamba kumenyesha mvua humu ndani hizi samani hatutazitamani tena, zitaumuka kama vile unga umetiwa hamira. Ni nzuri tu zinapendeza lakini zinatakiwa zionekane hivi hivi zisipate hali ya hewa mbaya zitaanza kuharibika. Sasa hii ni kupoteza fedha ambazo hazina sababu ya kufanya hivyo wakati tunao uwezo wa kutengeneza samani zetu na maliasili yetu ambayo itaweza kusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nilitaka kusema kwamba tutazame ni jinsi gani ya kuondoa majukumu au mgawanyo wa kuchukua majukumu katika fedha za Serikali. Nilizungumza leo asubuhi katika swali kwamba fedha za Halmashauri zinapita kwa *RAS.* Lakini *RAS* anazipeleka kwa Mkurugenzi. Fedha zile wakati wa ukaguzi, Kamati ya Hesabu ya Serikali inamwona kwamba *RAS* katika fedha zile ama hazikutumika, tunabidi tumhoji *RAS* wakati fedha zile hazikutumika katika Halmashauri. Sasa ni vyema tukaweka utaratibu kwamba majukumu ya *RAS* yajulikane na yakaguliwe na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hesabu za Halmashauri basi zikaguliwe na Kamati husika.

Tusichanganye mambo mawili wakati aliyefanya makosa labda ni Mkurugenzi tukaja kumwadhibu Katibu Tawala wa Mkoa. *(Makofi)*

Lakini vile vile kuna *tendency* ya kwamba fedha hizi zimekwenda Halmashauri japokuwa zimepita kwa *RAS, RAS* anawajibika sasa kufanya ulinganisho au *reconciliation* kuona kwamba zile cheki zilitolewa basi kila mmoja amechukua na hakuna zilizobaki. Kama mtu amepelekewa cheki na hakuchukua benki bado katika mahesabu itaonekana zile fedha hazikuchukuliwa. Lakini *RAS* hana habari, Mkurugenzi hana habari na hatimaye inakuja kwenye *audit query*. Sasa hii kidogo inaweka vitabu vyetu siyo vizuri kwa sababu ya taratibu mbalimbali. Serikali pia ilitazame hili ili kuweka mambo sawasawa na kila mmoja abebe jukumu lake kama inavyota Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa na haya machache ya kuzungumza. Nakushukuru kwa kunipa nafasi na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mheshimiwa Athumani Janguo na Mheshimiwa George Simbachawene ajiandae.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi ya kuchangia katika taarifa hizi tatu. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa na wewe kukuelekeza kuniita nichangie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze kupitia kwako Ofisi ya Spika kwa kuweka utaratibu wa kuingiza katika ratiba za Shughuli za Bunge, Taarifa za Kamati za Bunge ni kwa kupitia taarifa hizi tu ndiyo Bunge linatimiza wajibu wake wa kuisimamia Serikali, kuishauri na kuikosoa kama ilivyojitokeza leo katika taarifa hizi tatu. *(Makofi)*

Pili, ni taarifa hizi tu ambazo zinaweza kutuelekeza wapi Serikali inatekeleza vizuri, wapi kuna matatizo na nini tufanye ili kuweza kuondoa matatizo hayo tupate utekelezaji mzuri. Kwa maana hiyo basi ningependa kwa dhati kabisa nizishukuru Kamati za *PAC, LAAC* na Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma *(POAC)*, kwa taarifa nzuri. Na niwashukuru Wenyeviti watatu kwa kuziwasilisha taarifa hizi kwa ufasaha kabisa. Nasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Wenyeviti hawa watatu na Kamati zao, kwa kweli kumshukuru na kumpongeza Mkaguzi Mkuu na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa jinsi Idara yake inavyofanya kazi vizuri na kwa taarifa za mara kwa mara ambazo zinazingatia *value for money*. Ningependa kumpongeza pia kwa kuanzisha mambo ambayo yatasaidia Wabunge katika *capacity building* kwa maana ya kuandaa semina na masomo ambayo yatatuwezesha sisi kuchambua taarifa za hesabu. *(Makofi)*

Vilevile tumeelezwa hapa nadhani na Mheshimiwa John Cheyo kwamba utaandaliwa mkutano ambao utakutanisha Kamati zetu hizi tatu na Kamati kama hizo kutoka sehemu nyingine; mkutano ambao umeandaliwa Dar es Salaam siku chache

zijazo. Nafikiri ni jambo zuri kwa sababu linasaidia kuweza kubadilishana uzoefu baina ya Kamati na Kamati, baina ya Bunge na Bunge. Nashauri utaratibu huu uendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kufanya mapendekezo matatu; kwanza kwa kuwa Wabunge wote kwa aina moja au nyingine, wanahusika na mahesabu ya Serikali kwenye ngazi ya Taifa na kwenye Halmashauri, hasa tukiwa sisi ni madiwani vilevile, nashauri taratibu hizi za *capacity building* zienezwe kwa Wabunge wote. Pili ningeshauri kwamba sio tu *capacity building*, lakini ni lazima Wabunge tupewe wataalamu ambao wanaweza kutusaidia katika kuzikagua hesabu hizi na kukagua miradi hii ili wakati tunapoikosoa Serikali, tunafanya mambo haya kitaalamu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tupatiwe nyenzo; mimi sioni Serikali inashindwa nini kununua *laptops* kwa kila Mbunge hapa, siku hizi mambo yanakwenda kisayansi ili tuweze kuwa na nyenzo ambazo zitatuwezesha kufanya kazi zetu vizuri. Naamini kabisa wenzetu hawa waliopitia miradi hii, wangeongeza utaalamu zaidi kama wangekuwa na nyenzo za kisasa ambazo zingeweza kuwasaidia.

La mwisho ambalo ningependa kupendekeza katika haya ni kwamba *capacity building* isiishie Bungeni, iende na kwa Madiwani. Kwa sababu huko ndiko ambako fedha nyingi zinakokwenda na huko ndiko ilipo miradi mingi ya utekelezaji ambako tunafikiri kabisa wale wenzetu wakichambua katika hatua ya kwanza, ikifika hapa Bungeni, nafikiri uwezo wetu wa kuisimamia Serikali utaongezeka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye taarifa zote tatu suala la kukagua miradi lilitiliwa mkazo na mimi naungana na Kamati hizo kwenye suala hili. Kwa sababu unaweza ukajua tu *value for money* kama unakwenda kuona. Waingereza wanasema, *seeing is believing;* sasa kwa kupitia makaratasi tu hivi hivi, naamini kwamba hatuwezi kutoa mchango mzuri katika kuishauri Serikali, iwapo hatutaona kinachofanyika kule. Kwa maana hiyo, niishukuru Ofisi ya Bunge kwamba hatua kwa hatua imeongeza uwezo wa Kamati hizi kuweza kufika kwenye miradi, lakini inasikitisha kwamba Serikali nadhani haijaona umuhimu huu. Utakuta kama walivyosema wenzangu hapa, ukaguzi wa miradi unafanywa zaidi kwa huruma na uhisani wa wahisani wetu kutoka nje. Nafikiri wakati umefika, Serikali iweke *specific budget* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Wabunge wanafika kwenye miradi na wanaikagua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka kulizungumzia ni hili ambalo nimeshaligusa mwanzo pawe na utaratibu wa kudumu wa kubadilishana uzoefu, Kamati hizi za Bunge hili kukutana na Kamati za Mabunge mengine, iwe tumekwenda nje au waje hapa. Kwa kufanya hili, nafikiri tunaweza tukafanikiwa zaidi; nadhani kati ya wenzetu waliowasilisha taarifa zao asubuhi, mmoja alisema hivyo kwamba waliwahi kwenda Uganda na wakabadilishana uzoefu na wa kule. Mimi nafikiri hili ingebidi tulisimamie kwa ukaribu na Serikali itoe Bajeti ya kutosha ili haya yaweze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zilizojitokeza ni nyingi sana na Waheshimiwa Wabunge walionitangulia wamezielezea na mimi nafikiri kwamba hoja hizi, hasa zile kubwa kubwa za ucheleweshaji wa masurufu, malimbikizo ya madeni na unyofoaji wa

nyaraka kwenye taarifa zile waweze ili kuzirekebisha wakati tayari zimeshaenda kwa wakaguzi. Mambo haya yote yanatokana na wafanyakazi ambao hawataki kufuata sheria na taratibu. Hakuna dawa nyingine zaidi ya kutoa adhabu kwa wale ambao wanakiuka taratibu. *(Makofi)*

Mimi nadhani Serikali itakuwa imesaidia sana kama hili litashikiliwa; mfano ule uliotolewa wa Waziri Mkuu kuingilia mgogoro wa Bagamoyo unastahili kupongezwa. Sisi tunaotoka Mkoa wa Pwani na Madiwani wa Bagamoyo, wakiwemo Wabunge wenzetu wawili wa Bagamoyo, suala hili tumelipitia sana kwenye ngazi ya Wilaya mpaka kwenye ngazi ya baraza la ushauri la Mkoa. Lakini ufumbuzi ulipatikana mara tu Waziri Mkuu alipoingilia kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli napenda kuwapongeza wenzetu wa Bagamoyo, wale wawakilishi kwa maana ya Madiwani, wamelishikilia sana hili suala kiasi kwamba hata wakaweza kulianika wazi na ndiyo maana mpaka baadaye ikabidi Waziri Mkuu, apate angalau fursa ya kuingilia kati. *(Makofi)*

Sasa nafikiri ni vizuri kabisa kwamba sisi ambao tunakwenda kuangalia haya tuwe makini na Serikali isisite kuingilia kati na kutoa adhabu kwa wahusika. Bila ya kufanya hivyo, matatizo haya ya kukiuka Sheria yatakuwa yakiendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie habari ya taarifa ya Kamati ya ndugu yangu Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma. Kwa kweli kuna mambo ambayo ameyaeleza pale. Mimi yamenitatanisha.

La kwanza, Serikali kutokuwa sikivu kwa mapendekezo ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kwamba hata mapendekezo ya Kamati zetu hayajibiwi! Mimi nafikiri hili sio suala zuri, halipendezi. Wakati umefika Serikali ihakikishe kwamba mara tu wanapopata taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali wahusika kama nilivyosema, wanachukuliwa hatua. Wanapopata mapendekezo ya Bunge, wayashughulikie kikamilifu ili tuweze kukomesha utaratibu wa kukiuka sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ningejiunga na Kamati hii katika kuwapongeza viongozi na watendaji wa mifuko yetu ya maendeleo ya jamii kwa michango yao mikubwa waliyotoa. Tumeelezwa hapa leo na Mheshimiwa Kabwe Zitto, kwamba kwa muda wa miaka mitatu michango ambayo wametoa hawa wenzetu imepita, michango na misaada ambayo imetoka nje ya miaka 10. *(Makofi)*

Mimi nafikiri hili ni jambo la fahari, kwa hiyo, tuhakikishe kwamba tunawaenzi hawa wenzetu kwa njia zote na kwamba kila mahali inapowezekana tunawapongeza na Serikali ikawaunga mkono. Sasa inasikitisha kusikia kwamba eti ile mikataba kwa muda wote huu, Serikali inakataa kuithibitisha! Mimi sijui kuna nini! Kwa maana hiyo ningewaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba pendekezo lililotolewa na Mheshimiwa Kabwe Zitto, litekelezwe kwa maana ya sisi Wabunge, tuishinikize Serikali ili mikataba ile isainiwe mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, mengi yamesemwa na wenzangu, sitaki kengele nyingine inigongee. Nakushukuru, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Athumani Janguo. Tuweke tu kumbukumbu sahihi hapo unaposema si mifuko ya maendeleo ni mifuko ya hifadhi za jamii. Kwa hiyo, tuiweke tu hiyo kumbukumbu sawa na nakushukuru kwa mchango wako. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, mchangiaji anayefuata ni Mheshimiwa George Simbachawene, atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Zainab Gama na mchangiaji wangu wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwanza nishukuru kwa kunipa nafasi. Lakini kwa kipekee kabisa niwapongeze sana Wenyeviti wa Kamati zote hizi tatu zinazokagua na kuangalia hesabu za taasisi mbalimbali, kwa mfano tunayo Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, inayoongozwa na Mwenyekiti wangu, Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa. Mtu makini na mahiri kabisa katika Kamati yetu, lakini pia Mheshimiwa Kabwe Zitto na Kamati yake ya Hesabu za Mashirika ya Umma na Mheshimiwa John Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya viongozi hawa wa Kamati hizi kuwa wanatoka Kambi ya Upinzani, ni mafanikio makubwa yaliyoletwa na Bunge letu na hasa yanayopeleka kwenye kuweka Bunge letu kuwa la kisasa, lenye uwazi na kwa namna ya pekee kabisa nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote, lakini kipekee Spika Mheshimiwa Samuel Sitta, kwa kuwa *pioneer* wa kuongoza mabadiliko haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika huu mfumo wa sasa ambao tunasoma taarifa za Kamati ili Serikali iweze kuona namna tunavyofanya kazi kama Bunge na Bunge kama mhimili, ni fursa pekee na nzuri sana ambayo kwa hakika Serikali inapaswa kuona inapata faida kubwa ya kujua mambo mengi yanayotokea kwa undani. Hapa tunazungumzia suala la kukagua hesabu. Kamati hizi na hasa nikiizungumzia ya kwangu ya *LAAC*, ni Kamati ambazo tunafanya kazi kwa kujituma sana, kwa saa nyingi na tunatembea sana. Kwa hivyo tunayajua mengi na kwa hakika mimi ninahisi kwamba nilipata bahati kuwa kwenye Kamati hii kwa sababu sasa nimeifahamu Tanzania, Kata kwa Kata, Kijiji kwa Kijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo miradi mbalimbali katika Halmashauri na hapa nizungumzie kwa maana ya Kamati ya *LAAC*, kwa taarifa yake. Lakini mimi tatizo kubwa ninalolipata hapa na ambalo sijui wenzangu mnaonaje, lakini mimi nasema Sheria ya *Procurement* imeuwa nchi hii. Sheria tuliitunga kwenye Bunge, lakini sheria yetu hii ya *Procurement* kwa hakika sio sheria ambayo imetusaidia, ni sheria ambayo imetuuwa. Miradi mingi ambayo ikipitia na kufuata sheria ya *Procurement* inakuwa ni ya gharama kubwa, lakini vitu vingi vinavyonunuliwa kwa kupitia sheria ya *Procurement,* gaharama yake ni kubwa mno. Ndio maana hata kilimo kwanza, tutakwama tu kwa sababu *power tiller* ambayo unaweza kuipata kwa shilingi milioni nne Dar es Salaam, lakini ili ifike

Kibakwe na kumfikia mkulima, itafika kwa shilingi milioni tisa, sasa sheria hii ni nzuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa niishauri Serikali kwa namna inavyowezekana tufikirie namna ya kuibadilisha Sheria hii ili iweze kulingana na mazingira yetu. Tusiwe watumwa wa kuchukua vitu kwa kufuata urasimu ambao kwa hali ya uchumi wetu na hali ya mazingira yetu hauwezi ukatusaidia, tunafanya tu maisha kuwa na gharama kubwa bila sababu yoyote. Chukulia mfano wa fedha kidogo sana inayokwenda kwenye Halmashauri, ukiangalia utaratibu unaowekwa na Sheria ya *Procurement*, kazi itakayofanywa kwa kutumia *force account* inaweza ikawa ni kazi bora yenye thamani nzuri kuliko hata iliyotumia *procurement.* Lakini mfumo wenyewe wa *procurement* katika *Local Government*, ile *setup* ya Kamati zile, mimi nadhani kuna haja ya kufikiri upya, bado hautusaidii kitu chochote. Kama tulifikiri tunakwepa, basi ni kwamba hatujakwepa kitu chochote bali tuko kwenye matatizo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala lingine la ubora wa miradi katika majenzi yetu na hapa nizungumzie kwa maana ya Halmashauri. Katika Halmashauri miradi yake mingi ni ya ujenzi, na ukisikia maendeleo ya nchi hii ni ujenzi kwa maana ya kule chini tunakozungumzia *value for money* tunayoingalia ni ujenzi. Sasa ukiangalia ujenzi tunaoujenga leo, majengo ambayo tunakaa na kusema kwamba tuna majengo, tuna madarasa mangapi, tuna nini! Je, tujiulize yatadumu kwa muda gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatokana na utaratibu tu, ni kweli tunawashirikisha wananchi wetu, tunawataka na wao wawe *part and parcel* ya maendeleo ya nchi lakini unapofika kwenye mahali pa kujenga nyumba, hivi ni nani anayejenga nyumba yake kama yanavyojengwa madarasa? Je, hivi kweli tunasimamia vizuri? Je, ni nani anajenga? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiit, miradi mingi na madarasa haya yanayojengwa, nyumba za walimu, zahanati, tunatumia *local* fundi. Lakini *local* fundi huyu, awe angalau ana vigezo basi. Unapeleka kule mradi maadamu mtu tu ana kamtaji kidogo, basi anapewa kazi ya milioni 15, milioni 20, milioni 40. Shilingi milioni 40 kwa nchi yetu ni fedha nyingi, inapaswa isimamiwe kwa utaratibu mzuri. Haya basi hata kama ni katika kukatisha na kuondoa huo urasimu wa hizi *procurement,* basi huyo *local* fundi awe yuko *qualified,* anapimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hapa nilikuwa naishauri Serikali kwamba mitaani wako mafundi wana vyeti vyao. Tunao waliomaliza kwenye Vyuo vya Ufundi, hawa ni mafundi mchundo, tunao mafundi sanifu wanaotoka kwenye Vyuo vya *VETA*, basi angalau huyu *local* fundi, huyu mtu anayepewa kazi ya Halmashauri awe angalao ana mtu aliyemaliza hata *VETA;* hivi na hao nao hawapo jamani! Lakini unampa mtu kazi milioni 40, milioni 60, milioni 20, milioni hata 5, hajui hata kuchanganya simenti na mchanga. Unampa kazi ya kutengeneza madawati, mtu hajui kwamba hata ile *joint* ya mbao inaunganishwa kwa kutumia ile dawa, anapiga misumari tu! Hatuwezi kupata kitu kizuri, tutakuwa tunasema tunafanya mambo, lakini kwa hakika mimi nasema hatutaweza kubakia na kitu katika hivi vyote tunavyosema tumevifanya, baada ya miaka 20 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kuna haja ya kufanya kitu, kuna haja ya kushirikisha. Mimi nashangaa, mtu hawezi kufungua maabara mpaka awe na *lab technician,* mtu hawezi kufungua zahanati mpaka awe na mtu aliyesomea masuala hayo, hivi ni kwa nini watu wanaanza kujenga wakati hawana vyeti! Wanapewaje kazi za kujenga? Mbona sisi mafundi tupo, ni kwa nini msitushirikishe na sisi huku kwamba huyu asipewe hata kama ana mtaji, lakini pawepo na fundi mwenye cheti chake aliyesomea, ama wa *VETA* ama ana *FTC,* wapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeishauri Serikali tuone namna ya kufanya na kwa suala hili la *ALAT* wanaweza wakatusaidia wakatafuta namna ya mfumo mzuri tu, wakajadiliana na kutuletea mapendekezo ya jambo hili ikiwa ni njia ya mkato ya kutumia hasa katika miradi ya Halmashauri. Kweli katika *level* ya watu wetu, *Public Private Partnership* ni muhimu, lakini wapo watu wetu waliosoma tunaweza tukawashirikisha na tukapata majenzi mazuri kabisa, miradi mizuri, madarasa mazuri na nyumba nzuri zenye viwango kwa sababu zinafanywa na watu waliosomea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie jambo lingine na sasa nihamie kwenye Kamati ya Mashirika ya Umma. Nizungumzie tu kwamba kwa kweli hatua kubwa tumepiga katika Bunge hili na hasa katika Mashirika ya Umma ambapo Mashirika yetu haya sasa na hata sababu ya kufa kwa Mashirika yetu ya Umma ni kwamba yalikuwa ni mashirika ambayo hayana mwenyewe. Ilikuwa ni kwamba mtu ukiteuliwa ukawa *CEO* wa lile shirika, basi linakuwa ni mali yako, sana sana utaajiri ndugu zako, utaleta marafiki zako pale basi, kulikuwa kama vile hakuna mwenyewe.

Lakini niipongeze sana Serikali kwa kuleta mabadiliko ya Sheria hii na nimpongeze sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Werema, kwa kuleta mabadiliko ya Sheria hii ya kumtambua na kumpa mamlaka makubwa sana huyu Msajili wa Hazina kwamba sasa ndiye atakayeangalia hizi mali lakini pia atapitia na kuangalia miundo ya mashirika na kuangalia Bajeti zao na zile *employment scheme* zao na kila kitu. Mimi nadhani hii ni hatua nzuri na ni sheria nzuri na niipongeze sana Kamati ya *POAC* kwa kuwa nyuma ya jambo hili kwa nguvu kubwa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imani yangu hapa ni kwamba *Treasury Registreer* huyu *TR,* sasa atafanya kazi kwa niaba ya Watanzania, kuangalia mali zao, maana zilikuwa kama hazina mwenyewe. Mtu anapewa shirika analitafuna linaanza kulegalega mpaka linakufa, hamna cha kumfanya. Sasa hapa kuna mwenyewe, *Treasury Registreer* na sheria hii ni nzuri sana, atatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mashirika haya kuwa mengi lakini mpango wetu sisi wa nchi, kisera tulikubaliana kwamba tunabinafsisha mashirika ili Serikali ijiondoe kwenye mzigo wa kufanya biashara. Na mashirika haya badala ya kupungua wakati tulipoanza na mpango huu wa kubinafsisha sasa hivi Serikali sasa ina mashirika karibu 164, mashirika haya ni mengi mno. Kama kweli Serikali inataka kupunguza majukumu haya ikaenda kwenye kutoa huduma zaidi na kushughulikia masuala mengine na kukusanya kodi, mashirika haya 164 ni kwamba yameongezeka, ni mengi tufikirie

vizuri na tuone namna gani tunaweza tukapunguza jukumu hili zito. Lakini kinachonitisha hapa ni *investment* iliyopo kwenye mashirika haya, imesomwa na Mwenyekiti wa Kamati ya *POAC* hapa Mheshimiwa Kabwe Zitto, ni karibu shilingi trilioni 6, trilioni 6 ni hela nyingi sana *investment* hii ni kubwa mno lakini angalia ambavyo ilikuwa haipo *controlled* vizuri tunaamini sasa kwa kuwepo kwa *treasury registrar* inaweza ikawa *controlled*. Na *investment* kubwa ya namna hii kama tukiipunguza hata tukauza hata tukauza yakabakia mashirika ya msingi tu, Serikali inatakiwa ione mashirika ya msingi tu kama *TANESCO* mashirika ya namna hiyo ambayo ni makubwa lakini kuwa na utitiri wa vimashirika vidogo vidogo, mimi nadhani hiyo hii sio sawa tuwafikirie namna ya kuwapunguza kama tulivyokubaliana katika sera zetu kwamba tunabinafsisha mashirika kuipunguzia Serikali mzigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatizo lingine linalokuja hapa kwenye suala zima la haya mashrika ni pale ambapo Watanzania hata wao wenyewe hawayajui haya mashirika yao maana Watanzania ndiyo wenyewe sasa wanapokuwa hawayajui, mimi leo Mbunge mzima nilikuwa sijui kama *BP* ni shirika la umma lina *own* pale 50% ndiyo nimesikia leo, je, ni Watanzania wangapi wanayoyajua mashirika yao? Je, kama hawayajui maana yake sisi Wabunge ndiyo wawakilishi wao.

Mimi nadhani Kamati ya *POAC*, mimi ningependa niombe sana itafute namna ambavyo inaweza ikaongea na Serikali na kuona namna ya kuwafanya Watanzania wakayajua mashirika yao mengi yako kichini chini yamejificha ficha na hii *BP* ni moja tu lakini mengine hatuyajui mengi, na Mheshimiwa Kabwe Zitto ungechukua fursa kwa sababu hotuba yako hukuisoma yote na pengine ungetusomea yote maana mashirika 164 kwa hakika naamini wengi hatuyafahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi, kwa kuwa bado nina muda kidogo nizungumzie tu kwamba, nataka kuiuliza tu Serikali hivi hizi fedha zinazorudishwa Hazina kutoka kwenye mishahara kwenye Halmashauri ambazo ni fedha za mishahara ambao ni watumishi watoro, wanaofariki na wastaafu zinapaswa kupitia njia gani maana Halmashauri zingine zinarudisha kupitia kwa *RAS* anarudisha Hazina zingine sijui zinarudishwa moja kwa moja Hazina. Sasa mimi nadhani kungetenezwa utaratibu mmoja kihesabu inakuwa ni rahisi ku-*trace* kama zitakuwa zinajulikana zinapaswa kupitia njia ipi na Halmashauri zingine hazifahamu kwamba zinapaswa kupitia kwa *RAS*, kwa hiyo, ni mkanganyiko fulani ambao pengine unaweza kupelekea fedha nyingi zikawa zinapotea hapa katikati na hata kwa namna ya kuzi-*trace* likawa ni jambo gumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi niseme tu kwamba kwa niaba ya wananchi wa Kibakwe nina hakika katika muda ambao nimefanya kazi katika Kamati hii ya Hesabu ya Serikali za Mitaa imenisaidia ujuzi mkubwa ambao imenipelekea hata kuisaidia Halmashauri yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kibakwe niwashukuru wajumbe wa Kamati yetu kwa ushirikiano tuliokuwa tunapeana. Lakini

kipekee kabisa nimshukuru mzee wangu baba yangu Mzee Mgana Msindai amenipa uzoefu mkubwa katika Kamati hii. Mheshimiwa Msindai ni gwiji wa Kamati ya *LAAC*, anafahamu mambo mengi sana ametusaidia sana. Kipekee nimpongeze Mkurugenzi na Mwenyekiti wangu wa Halmashauri ya Mpwapwa Mheshimiwa Mkanwa, na Mbunge mwenzangu Mheshimiwa George Lubeleje kwa namna tulivyoshirikiana katika kupeleka mbele gurudumu la maendeleo ya wilaya yetu ya Mpwapwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Simbachawene sina uhakika sana maana ya tafsiri halisi ya neno gwiji kwa kiswahili, lakini niseme tu niongeze labda ni maarufu katika Kamati hiyo, sasa waswahili watatusaidia kuitafsiri vizuri hiyo tasfiri ya gwiji na maarufu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, labda kabla hatujaendelea niombe tu kwamba rai ya Mheshimiwa Simbachawene ni ya msingi, tumuombe Mheshimiwa Kabwe Zitto kwa niaba ya Kamati yake basi mnaweza mkatafuta namna ya kuorodhesha mashirika hayo na mkayasambaza kwa Wabunge ili Wabunge wawe nayo nadhani ni jambo la msingi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na mchangiaji anayefuata ni Mheshimiwa Dr. Zainab Gama kama nilivyosema na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi pia naomba nimpongeze Spika Mheshimiwa Samuel Sitta kwa utaratibu mzuri hasa alitupangia sisi Kamati ya *LAAC.* Zamani Kamati ya *LAAC* ilikuwa inakutana Dar es Salaam na Dodoma na tulikuwa haturuhusiwi kuzunguka, mambo yetu tulikuwa tunayasema kwa vitabu tulivyoletewa na ripoti lakini baada ya utaratibu huu tumekuja kugundua udhaifu sehemu nyingi na tumeweza kuutoa udhaifu huu kuzisaidia Halmashauri kwa kuiogopa hii Kamati waanze na wao kujirekebisha. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba nimshukuru sana na nimpongeze ndugu yetu, Spika wetu Mheshimiwa Samuel Sitta, lakini naomba nimshukuru Mwenyekiti wetu wa *LAAC.* Kwa kweli Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa anasoma na anajua kwa hiyo, naomba nimpongeze, samahani sana Wenyeviti wengine nampongeza huyu kwa sababu mimi ni mjumbe wa *LAAC* na nimeona utendaji wake. *(Makofi)*

Naomba nimpongeze *CAG* na wafanyakazi wake wanatupa msaada mkubwa katika maamuzi haya, nampongeza, pia Katibu wa Bunge na makatibu wake aliotuteulia katika Kamati yetu, wanatusaidia sana. *(Makofi)*

Lakini naomba niipongeze Benki ya Dunia wangekosa wao kutusaidia pesa hii Kamati isingeweza kuzunguka, naomba waendelee na moyo huo na niwapongeze wajumbe wote. Lakini niwapongeze Ma-*RAS* na Ma-*DC* waliokuwa wanakuja kutusikiliza wakati wa Kamati nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii imefanya Halmashauri kwa kweli sasa zijirekebishe na nyingi zifanye vizuri, naomba niwapongeze Halmashauri kwa kazi nzuri wanazofanya. Ombi langu tuwajengee watu wafuatao wafanyakazi, tuwajengee uwezo saa nyingine makosa wanayofanya si ya makusudi, ni uwezo mdogo kwa hiyo, naomba tuwajengee uwezo, tuweke Bajeti ya ku-*train. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia madiwani tusipowajengea uwezo watakuwa ni wale watu ambao nusu vipofu kama mimi Dr. Gama bila miwani sioni na madiwani tusipowajengea uwezo wanakuwa aina hiyo. Wanakaa na watendaji ambao ni ma-*graduate*, madiwani uwezo unakuwa mdogo hawaelewi ile *field* hata kama na yeye akiwa ni *graduate* lakini katika *field* nyingine matokeo yake madiwani wanaacha vitu vinapita lakini si kwa bahati mbaya ni kwa sababu hawaelewi eneo hili. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba madiwani kila wakati wajengewe uwezo, lakini uwezo mkubwa naomba kabisa ujengewe viongozi wetu wa ngazi za chini, Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, Serikali za Vijiji na Kamati zao kwa kweli hawaelewi hata *WDC* na kule chini hawaelewi imefikia hatua ukitizama mtitiriko wa utawala wa Serikali ni mzuri sana na huyu kiongozi wa chini kwenye mtaa na kijiji ndiyo msimamizi. Lakini mara nyingi anaendeshwa tu na watendaji hawaelewi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba uwezo mkubwa uende huko, hawa ndiyo wasimamizi kwa mfano, unamuelimisha kutengeneza Bajeti angalau sio Bajeti, kiutaalam lakini ile miradi ya muhimu viongozi hawa wakipendekezwa ikapelekwa huko juu ikarudi kesho na kesho kutwa hawawezi kurudi wakamuuliza Mbunge kwa nini kitu fulani hakipo unamuuliza wewe utamuuliza je, wewe katika Bajeti yako ulipanga kwa hiyo, mimi naomba hawa watu waelimishwe. Tuwaelimishe kuwa na jicho la kuona *audit report* na ile *audit report* inawekwa katika kila kata yaani iwekwe katika lugha nyepesi waelewe, waelimishwe jinsi ya kusimamia miradi inayokwenda kwao kwa mfano, barabara inapita kwao hawajui mkandarasi nani, hawajui ni kiasi gani, hawajui kwa kiwango gani wanaona maburudoza tu halafu wakiisha wao wanasimama wanalalamika. Kwa hiyo, waelimishwe hawa watatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba Kamati hii chonde kabisa ipangiwe pesa, naomba Serikali jitahidini hii Kamati inaisaidia Serikali kugundua yale mazuri na yale maovu, usipoingia pesa ikazunguka tukaa tu tunaishia kwenye meza tunadanganywa na mifano imeelezwa hapa na katika kitabu unakuta tumeletewa ripoti nzuri kabisa unaitizama mnawasifu, baada ya muda ndiyo inasabibishwa *special audit* labda *RAS* kaona kitu pungufu halafu unajiuliza sisi tumepitisha tukawapongeza. Kumbe ripoti iliyoletwa kwetu nyingine, sijui ripoti iliyoenda kwa mkuu wa mkoa nyingine, kwa mkuu wa wilaya nyingine sijui wenzetu wa CCM wanataka na wao waone utekelezaji wa hii imepelekwa nyingine, mwisho wa siku vurugu mechi wanakaa tu katika meza wanaandika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalau kuna maeneo machache lakini *this is a serious issue*, hela nyingi *value for money* wengine tunashindwa kuyasema tutakuwa tunachongea kwa sababu tumeshatoa ripoti. Lakini *value for money* haipo, na mimi

naomba kitengo hiki cha *CAG* cha *value for money* kisisubiri mpaka mtu akalalamike, wawe hiki kitengo nao wanafanya *audit*, watafutieni *staff* wengi wafanye, mtakuja kuona inatisha. Unakuta mahali makusanyo madogo lakini mradi ule unaokusanya makusanyo madogo nenda sehemu nyingine mradi huo huo unakusanya makusanyo makubwa lakini ukitizama unakuta hata ile *tender* ni ya wahusika. Kwa hiyo, mimi nasema *value for money*, hiki kitengo kiendelee. *(Makofi)*

Lakini naomba Madiwani wawe na uwezo wa kuajiri na kufukuza, tuwape *mandate* hii madiwani wetu wanafika wakati wanalalamika jamani kuna tatizo mtendaji na nini mtendaji yule na tunaona kabisa kuna matatizo anachukuliwa hapa anapelekwa kwingine kwa mfano lililotokea Bagamoyo, lisingetokea mtendaji yule alikuwa sehemu za Mahenge sijui kule Morogoro huko ndani ndani kisha wakamchukua wakamleta Bagamoyo alivyofika Bagamoyo yeye akakaa mezani akaandika ripoti hata miradi yenyewe haipo, ni kitu cha kushangaza unakuta mtu tumepewa kiasi hiki kwa hiyo, utekelezaji umefika *percent* hii hata hela yenyewe Hazina haijatolewa kumbe alikuwa anafanya utaratibu ili afanye ikija Hazina ale. *(Makofi)*

Mimi ningeshauri sasa hivi pia kuna matumizi mabaya mahali ambapo watendaji wanapata pesa Serikali inawapelekea pesa wanasema tuliletewa pesa mwisho, kisha ile hela wanaambiwa waweke katika akaunti fulani mara nyingi wanaweka kwenye amana halafu baadaye ile hela uwajibikaji kwa ile hela katika mwaka mwingine, wengine tumekuja kugundua zile hela wanatumia kwa masuala yao mengine, ulaji ndiyo unapotokea wafanye kama Serikali kuu hela ikibaki rudisha Hazina, watatumia kwa hiyo, mimi nilikuwa nataka. *(Makofi)*

Lakini miradi ya UKIMWI inanisikitisha, miradi ya UKIMWI mingi iliyoko mle ni posho, semina walengwa haziwafikii, tumeambiwa wahisani ndiyo wanataka hivyo naomba wahisani kama wanataka hiyo hela yao itumiwe na posho na semina tuikatae. *(Makofi)*

Naomba wafanyakazi waliokaa muda mrefu sio tu wakuu wa idara wafanyakazi wengine waliokaa muda mrefu tuwaondoe, mimi naogopa tu nikisema nitaambiwa nimechanganyikiwa, kuna wafanyakazi wamekaa muda mrefu sasa hivi Halmashauri zimekuwa zao wanawatishia hata wale wageni wanaokuja ambao wana uwezo, tunaomba muwaondoe dada yangu Mheshimiwa Celina Kombani, mimi kila siku najisifu jinsi unavyofanya kazi lakini kwenye hili waondoe na ukisikia mtu legelege na ukipata ripoti tu ya *LAAC* naomba fanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala ambalo *LAAC* imeagiza lakini watendaji wa Halmashauri huwa hawataki, sisi *LAAC* tunakaa mpaka saa nyingine saa sita usiku kutizama makabrasha yapata hivi matumizi tunaletewa mchanganuo mzuri tukashauri kila mwezi kwa sababu Kamati ya Fedha inakaa basi yale matumizi ya mwezi ule ichanganuliwe kama inavyoletwa kwenye *LAAC* ili wao watakuwa mchanganuo mdogo watasaidia madiwani waone lakini nakwambia mfano Halmashauri yangu wameniambia mie kwenye kikao kwamba mie muongo *LAAC* haikuagiza na nikawaambia basi nimuite Mwenyekiti wakagoma, yaani wanajidai na Halmashauri zote zimekaa kufanya hivyo

kwa hiyo tunakuomba dada yetu Mheshimiwa Celina Kombani hilo ni agizo tumeliomba, ushauri huo tumeomba sisi watu wa *LAAC* tunaomba uwaandikie kila mwezi wakisema tulijenga nyumba ya mwalimu waseme basi mabati kiasi gani kama ni *contractor* kiasi gani ili madiwani wetu wawe na macho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *IPSAS* tulifundishwa sisi tukaona utaratibu huu mzuri na zikatengwa baadhi ya Halmashauri pamoja na Halmashauri yangu na ikajulikana Halmashauri yangu huu mpango wa *IPSAS* uko baadhi ya wageni wamekuja kutizama kwenye Halmashauri yangu wakakuta hakuna sasa sijui tatizo ni nini atusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo kwa kweli ni dhahifu, tuwasidie makusanyo haya yaongezeke, Halmashauri nyingi makusanyo machache, mimi naomba kuna eneo linaitwa Vikawe lilipangiwa hela kuwa na mradi wa maji, hela ile ikadanganywa ikatumiwa Vikawe wakabaki pale, tumeomba mpaka sasa Vikawe bila ya maji ya bomba kutoka Ruvu Chini hawa watu wanachota maji ndoo shilingi mia tano yanayotoka Dar es Salaam, Kawe na tumeeleza sana. Lakini naomba miradi ya maendeleo dada yangu uwe na kitengo maalum cha kutizama miradi ya maendeleo mingi, samahani naita ni feki wanasema na hasa *DADPs* tunasema kilimo kwanza kwa utaratibu uliokuwepo miradi ya *DADPs* mingi inaliwa hapa nakataa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *proucuremt*, mmesema madiwani tusishiriki kwa sababu sisi washiriki na mimi nakubali, lakini Mkurugenzi ameamua kumchukua Mwenyekiti ni nani, kwa *interest* yake wajumbe ndiyo hao watendaji, watendaji hao hao ndiyo wanalalamikiwa wametengeneza tayari wamekubaliana fulani ndiyo atachukua *tender* unamkataza diwani asisimamie halafu unamwambia tia saini diwani, anatia saini kwa kitu gani asichokijua Mwenyekiti wa Halmashauri unamwambia atie saini *tender,* hilo kaliwa na watu ambao hayupo, anatia saini nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ukimuona unamwambia chukua *ten percent* na anachukua haoni hata jibu, maana yake hakuwepo mmekataa asiwepo lakini mnamwambia asaini kitu ambacho hajakisoma, *procurement* ni moja ya matatizo sheria hii.

Mimi nawaambia ndugu zangu Wabunge nikirudi mwaka 2011 mimi nitafanya *amendment* na niombe na uwezo uko na naomba wenzangu kule nyumbani mnisikie uwezo ninao, msisikie eti mtu asema mie tajiri nakuja kuwasaidia ajenge nyumba huko, atoe madawati anajidai yeye tajiri kama yeye ni tajiri atengeneze barabara kuna haja aje Bungeni hao ndiyo mafisadi hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ushauri wa *CAG* uchukuliwe. Mimi nitatoa mfano wa mafuriko yaliyotokea, *CAG* alitoa ushauri Babati, tukasema jamani tufanye nini haya masuala ya mafuriko yasitokee tukazembea. Mafuriko yaliyotokea juzi tumepoteza fedha nyingi kabisa. Kwa hiyo, mimi naona huu ushauri tunaupuuza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa Mheshimiwa Waziri mimi naomba *NSSF* ilikubali kujenga stendi kubwa Kibaha, *PPF* ilikubali kujenga nyumba 1,000

Kibaha, lakini wamesalitiwa, yale maeneo sasa hivi matajiri ndio wanapewa kwa utaratibu ambao haujulikani. Sasa jamani hatutaki maendeleo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi naomba niwashukuru wote. Naomba nishukuru Halmashauri yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Dr. Zainab Gama. Waheshimiwa Wabunge, naomba tuendelee. Nadhani ujumbe aliotoa Mheshimiwa Dr. Zainab Gama ulikuwa mzito sana hapa. Hasa ule wa mwisho.

**MHE. ISMAIL JUSSA LADHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii. Nimefurahi kidogo nilidhani kwamba lugha za kampeni haziruhusiwi katika nyumba hii, kumbe wakati mwingine huwa zinaruhusiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwanza kwa kulipongeza Bunge lako Tukufu hasa Mheshimiwa Spika, kwa mambo mawili, kwanza kuweka utaratibu huu wa kuzifanya Kamati hizi ambazo zinaangalia Hesabu za Serikali katika sekta tofauti kuwa zinaongozwa na Wabunge wa Upinzani ili kuhakikisha uwazi zaidi na uwajibikaji zaidi za walipa kodi. Lakini pia, kwa kuweka utaratibu huu wa kuzipa nafasi hizi kuwasilisha ripoti na kujadiliwa katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Baada ya pongezi hizo kwa Bunge na kwa Mheshimiwa Spika, vilevile nitumie nafasi hii kuwapongeza Wenyeviti wote watatu kwa kuwasilisha ripoti zao vizuri kabisa. Napata faraja zaidi nikiona Wabunge wa upande wa pili wanawapongeza na kuchambua mchango mkubwa unaotolewa na Wabunge wa upande wetu sisi katika kusimamia matumizi mazuri ya fedha za walipakodi ambao ndiyo waliotuleta hapa kuwalindia maslahi yao. Kwa hiyo, nadhani hiyo itakuwa changamoto kwa wananchi kuona katika uchaguzi wa mwaka huu wanaingia wengi zaidi kutoka upande huu ili tuweze kutekeleza vizuri zaidi majukumu hayo. Nilikuwa nasema kumbe kampeni zinaruhusiwa katika hali nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikija katika ripoti zenyewe naomba nianze na ile ripoti ya Kamati ya Hesabu za Serikali. Mengi yamezungumzwa sikusudii kuyarudia tena yale ambayo yamewasilishwa na Mwenyekiti mwenyewe katika ripoti yake na waliyochangia wenzangu. Lakini nilikuwa nasema kuna eneo moja nilikuwa nadhani nalo pia tuliangalie na hili zaidi ni pendekezo. *(Makofi)*

Hii ripoti iliyowasilishwa imesema kwamba imeanzia Aprili, 2009 hadi Aprili, 2010 lakini tunapoiangalia ripoti ya *CAG* ambayo iliwasilishwa mezani jana hapa unakuta kwamba kuna eneo moja hili la misamaha ya kodi. Ripoti ya *CAG* imeonyesha kwamba Serikali imepoteza takribani shilingi bilioni 752 katika mapato yake katika kutoa misamaha ya kodi. Sasa fedha hizi ni nyingi sana. Fedha hizi zingeweza kutumika kusaidia kutatua matatizo mengi sana yanayowakabili wananchi wetu. Lakini kwa sababu zimetolewa kwa misamaha ya kodi Serikali imezikosa. Sasa nadhani lile pendekezo la *CAG* Kamati hii iliangalie na Serikali kwa ujumla wake iliangalie ya kwamba kuna haja

ya Serikali kufikiria upya sera yake ya misamaha ya kodi ili kuongeza fedha hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakumbuka mwaka jana Kambi ya Upinzani wakati ilipokuwa inawasilisha Bajeti mbadala ilionyesha na nadhani hata mwaka juzi kwamba mapato ya Serikali yangeongezeka na kupunguza utegemezi wa fedha za wahisani kama tungekuwa tunaondoa maeneo kama haya ambayo yanapelekea Serikali kukosa mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo tuliangalie eneo lingine ambalo pia limetajwa na *CAG* nadhani pia Kamati inapaswa kuliangalia wameligusia kidogo katika ripoti yao. Lakini ripoti ya *CAG* imeonyesha kwamba Serikali imepoteza shilingi bilioni 632 kutokana na kukiuka Sheria ya Mikopo ya Serikali na Udhamini ya mwaka 1974 ambayo inataka udhamini wa mikopo hii usizidi asilimia 70. Lakini inaonekana mikopo imedhaminiwa mingine hata zaidi ya asilimia 100. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa nasema katika ripoti hii ya Kamati ya Hesabu za Serikali waliangalie hili nadhani kaka yangu Mheshimiwa John Cheyo watalitupia macho ili kuhakikisha kwamba fedha za Watanzania zinabaki salama na zinatumika kuwaondolea umaskini ambao umekithiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapo hapo nadhani vilevile katika kutoa changamoto kwa Kamati hii kuna haja ya kuangalia pia maeneo mengine ambapo mapato ya Serikali yanapotea. Gazeti la *The East African* la juzi lilikariri ripoti hii iliyotolewa na taasisi inayoitwa *Global Financial Integrity* ambayo ilikuwa na kichwa cha maneno *A list Financially flows from Africa hidden resources for development*. Hii imeonyesha kwamba Tanzania inaongoza katika Afrika Mashariki kwa fedha ambazo zinatoka nje kupitia njia zisizo halali. Hizi zimetajwa ni pamoja na usafirishaji wa fedha haramu, ukwepaji wa kodi, masuala ya ufisadi na mambo mengine. Jumla yake ni takribani bilioni 8.9. Hizi ni takribani shilingi trilioni 11.6. Sasa fedha hizi ni nyingi, haidhuru zimeambiwa zimepotea katika kipindi cha miongo minne yaani miaka 40 ambayo takribani yote imeongozwa na Serikali, inaongozwa na Chama kimoja haiwezi kukwepa lawana katika upotevu huu wa mapato.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nadhani Kamati ya Hesabu za Serikali inapaswa hilo nalo liangalie. Hizi fedha kama nilivyosema ni nyingi sana. Ukiangalia zingeweza ku-*cover* takribani asilimia 15 Bajeti yetu ya Serikali kwa mwaka uliopita, ni zaidi hizi ya Bajeti nzima ya Wizara ya Elimu kwa mwaka jana ambayo ilikuwa bilioni 507 ni zaidi ya bilioni nzima ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, ambayo ilikuwa ni bilioni 471, ni zaidi ya Bajeti nzima ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji ambayo ilikuwa ni bilioni 264. Ni zaidi ya Bajeti nzima ya mwaka jana ya bilioni 610 kwa Wizara ya Miundombinu ambayo ndiyo ingejenga misingi ya uchumi katika nchi yetu. Ni zaidi hata ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Chakula ambayo ilikuwa ni bilioni 227 kwa mwaka jana. Lakini zaidi hii ingeweza kuwalipia wanafunzi wetu wa Vyuo Vikuu mikopo yao ambayo walikuwa wanaihitaji ili kujisomea ambazo ni takribani bilioni 250. *(Makofi)*

Sasa uvujaji huu wa mapato hauashirii hali nzuri katika nchi yetu. Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza Kamati ya Hesabu za Serikali iangalie maeneo hayo. Leo tukisoma Gazeti la *Daily News*, Rais wetu mpendwa aliyeniteua mimi nikaingia katika Bunge hili Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete yuko Marekani na anasema kwamba Serikali inahitaji shilingi trilioni 1.6 kwa ajili ya mpango wake wa miaka mitano wa kuboresha mfumo wa elimu. Hizo zingetosheleza kununua vitabu, kujenga madarasa, kujenga maabara, kununua samani na vitu vingine vyote. Sasa fedha hizi zinazohitajika kwa miaka mitano hapa zinapotea kwa kiasi kama hiki kama hivi tunavyoelezwa katika taarifa hii ya wenzetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa nasema hili ni muhimu sana taarifa hii ikazingatia hasa katika kipindi kinachokuja. Pengine Serikali nayo itapaswa itupatie majibu huko mbele kwamba fedha hizi zinafikaje kuwa zinatoka nje kiasi hiki Watanzania wanaendelea kuwa maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Hapa nilikuwa na moja tu mimi, moja katika maelezo ambayo yametolewa hapa ni kwamba Halmashauri za Wilaya kadri zinavyokwenda zinaonekana zinategemea zaidi fedha kutoka Serikali Kuu kutokana na kutokuwa na vyanzo vyake vya mapato baada ya Serikali Kuu kujilimbikizia karibu takribani vyanzo vingi vya mapato kutoka katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa naomba na hili hasa tunapoelekea katika utayarishaji wa Bajeti inayokuja Serikali hii itazame haja ya kuachia baadhi ya vyanzo vya mapato ili Halmashauri zetu za Wilaya ziweze kujitegemea zenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama upande wa wenzetu hakuna sera hiyo tuko tayari kuwaazima kama tulivyowaazima sera nyingine kutoka upande wa upinzani ambazo zinazungumzia haja ya kuwapa Halmashauri za Wilaya na Serikali za Mitaa vyanzo vyao vya mapato kutoka katika maeneo yao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija katika ripoti inayoongozwa na Mheshimiwa Kabwe Zitto ya Mashirika ya Umma, mimi nilikuwa nataka kwanza nianze vilevile kwa kuungana na Kamati yake kuyapongeza yale mashirika matano ambayo amesema yamefanya vizuri kabisa. Pamoja na kwamba imepata misukosuko ni pamoja na *TANESCO* kama alivyotaja mwenyewe, *NSSF*, *PPF*, *TCRA* na *TPA*. Tunawapongeza sana tunayaomba yaendelee kufanya vizuri zaidi ili yaweze kutoa tija katika uchumi wa nchi yetu na pia wale wananchi ambao fedha zao zinaingia huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baada ya kuyapongeza mashirika hayo kama tulivyosema maana ya kuwa na ripoti hizi ni kusaidia kuhakikisha kwamba fedha za wananchi wetu, fedha za Tanzania zinalindwa na kuwatumikia wananchi. Sasa imesikitisha kwamba moja ya *findings* za Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma ni kugundua kwamba Serikali yenyewe ni moja katika wadaiwa sugu wa mashirika hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa nasema kuna haja basi ya Serikali kuondoa fedheha hii ya kuwa nayo inadaiwa na mashirika yetu na pengine kuchangia katika kuyafikisha katika hali mbaya na pengine hata mwisho kuyaua. Kumetolewa mfano katika ripoti hii kwamba mamlaka ya maji safi na maji taka Mwanza ilikuwa inadai Serikali katika Mkoa wa Mwanza milioni 360. Kwa hiyo, vitu kama hivyo havipaswi kuendelea. *(Makofi)*

Lakini hata lile la Bohari ya Madawa kwamba Serikali inadaiwa takribani bilioni 36.7 ambazo zimepelekea hata bohari hii pengine isiweze kutoa dawa na wananchi wetu wanapokosa dawa wanaathirika sasa. Tumekuwa tukisikia malalamiko hapa kwa Wabunge mbalimbali katika masuala kwamba vituo vya afya hazina dawa. Sasa haya yanaweza kuepukwa ikiwa Serikali itaondokana na fedheha hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho kabisa nataka kuzungumza ni lile ambalo pengine halikuguswa kwa lugha hiyo katika taarifa hii ya Kamati ya Mashirika ya Umma ni suala zima la *political interference* katika uendeshaji wa mashirika. Suala la uendeshwaji wa kiasi wa mashirika hayo ambao unapelekea mara nyingi na Serikali Kuu kuyaingilia katika utendaji wa shughuli zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mifano michache tu tunaambiwa kwamba Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* ililazimishwa na Serikali itoe fedha ili kujenga uwanja wa Mwanza wa Ndege takribani bilioni 7 bila kwamba zilikuwemo katika mpango wake hilo shirika. Lakini vilevile ikaagizwa itoe fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Msata Bagamoyo shilingi bilioni tatu ambapo tunaambiwa hata barabara yenyewe hata kujengwa haikujengwa. Sasa fedha hizi hawakuzipangia katika matumizi yao, lakini matokeo yake tunapolazimisha zipelekwe huko tunaathiri utendaji wao. Vilevile kwa mfano imetolewa katika ripoti hapa *TANAPA* inatakiwa kuilipa *CNN* kinyume na mipango yake ya awali shilingi bilioni 1.07 kwa ajili ya matangazo ya utalii ambao pengine hata tija yake haikuwa kama ilivyokuwa imefikiriwa. Kwa hiyo, nadhani haya tuache, lakini kubwa katika *politically interference* tumeliathiri shirika moja muhimu sana katika nchi yetu la *TANESCO*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANESCO* ambayo ilikuwa imeanza kupunguza upotevu wa fedha hizi na imeanza kuongeza faida kidogo katika uendeshaji wake kufikia shilingi bilioni mbili wanazokusanya imelazimu kuingia katika hasara tena kutokana na mgao wa umeme wa mwaka jana mwezi Oktoba ambao umepata hasara takribani shilingi bilioni 48. Sasa hili lingeweza kuepukwa pengine limechangiwa na kiasi kikubwa cha kule kuingilia *TANESCO* katika maamuzi yake kupeleka maamuzi ya kisiasa. Tumeiambia isinunue *Dowans* ambayo ilikuwa inagharimu shilingi bilioni 60. *(Makofi)*

Lakini leo *TANESCO* tunaifanya inunue umeme kutoka *IPTL* kwa shilingi bilioni 20 kwa mwezi kama ni *capacity energy charges* ambazo kwa mwaka ni shilingi bilioni 240 zingenunua mitambo ya *Dowans* mara nne. Sasa maamuzi kama haya ya kiasi yanaathiri utendaji wake na kuifanya kuingia katika hasara pengine hata kuja kuliulia shirika hili na vilevile kuwaweka wananchi gizani. Kwa hiyo, ili kuepuka haya nilikuwa

nadhani lile pendekezo la Mheshimiwa Kabwe Zitto lilitolewa la kuitaka Mifuko ya Hifadhi za Jamii kuangalia uwezekano wa kuwekeza katika sekta hii ili kulipa nguvu Shirika la *TANESCO* lakini pia kuongeza uzalishaji wa umeme katika nchi ili nchi yetu iweze kusonga mbele na kweli kupitia sera mbadala nchi yetu ipate maisha bora kwa wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii, kwa njia ya maandishi, kutoa maoni yangu kama ifuatavyo. Nianze kwa kuipongeza Serikali kwa jinsi inavyojitahidi kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ingawa kuna upungufu mdogo mdogo. Vile vile niwapongeze Wenyeviti wa Kamati zote kwa jinsi wanavyojitahidi kushirikiana na wajumbe wao wa Kamati kukagua mahesabu ya Kamati zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiojificha kuwa kazi ya Kamati hizi zote zimezaa matunda sana kwani Halmashauri nyingi, Mashirika mengi, Wizara na Mikoa mingi zimeanza kupata hati safi. Hii inatokana na kazi nzuri ya Kamati hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maoni kwa Kamati ya *LAAC* kama ifuatavyo:-

1. Halmashauri nyingi zinapata ruzuku ndogo kinyume na maombi sambamba na bajeti zao. Hali hii inawafanya washindwe kutekeleza majukumu yao;
2. Ziko Halmashauri ambazo bado zinatumia fedha kinyume na maelekezo ya Serikali yaani kuhamisha *account*;
3. Kuna matatizo ya watendaji hasa Wakuu wa Idara kukaa kwa muda mrefu na kusababisha kufanya kazi kwa mazoea;
4. Bado kuna wizi wa fedha za Serikali, nashauri Wakaguzi wa Ndani wasiwe chini ya Halmashauri ili waweze kuwa huru kukagua pia ukaguzi uimarishwe;
5. Bado kuna tatizo la ujenzi wa majengo ya Halmashauri kuwa chini ya kiwango, hakuna *value for money;* na
6. Elimu kwa Waheshimiwa Madiwani ni ndogo hivyo wanaburuzwa na watendaji, nashauri semina za kutosha zitolewe wakati Madiwani wanapoanza kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni kwa Kamati ya *PAC* ni kama ifuatavyo:-

1. Samani za Serikali zitengenezwe ndani ya nchi kwani samani za nje sio imara hazikai muda mrefu pia tukinunua ndani tutaongeza pato la wananchi wetu pamoja na kutunza fedha za Serikali;
2. Viongozi wa Serikali pamoja na watendaji wa Serikali kubadili samani za nyumba zao bila sababu maalum wakati mwingine ni rangi au chaguo lake, tunaifilisi Serikali, kuwe na muda maalum wa kununua fanicha pamoja na kukarabati nyumba za Serikali;
3. Matumizi mabaya ya fedha, nyingi kutumika kwa posho za safari ama semina au ziara ambazo sio za lazima;

4. Baadhi ya watendaji kuwa na ubinafsi na kutokushirikisha wenzao;
5. Matumizi mabaya ya magari ya Serikali pamoja na kununua magari ya thamani kubwa sana tofauti na uchumi wa nchi yetu yenye Watanzania maskini;
6. Watendaji baadhi kukaa kituo kimoja cha kazi kwa miaka mingi; na
7. Mali za Serikali kuuzwa bila sababu za msingi na kwa bei ya chini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni kwa Kamati ya *POAC* ni kama ifuatavyo:-

1. Yako Mashirika ambayo yamekufa, naishauri Serikali kufufua mashirika hayo kwa kutoa ruzuku;
2. Yako mashirika yenye hali mbaya, naishauri Serikali kuyaongezea mashirika hayo mitaji;
3. Yako mashirika yanayofanya kazi nzuri mfano *NSSF* kwa kujenga majengo ya Serikali bali Serikali inachelewa kufunga mkataba na kutoa *guarantee* mfano ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma;
4. Serikali kubinafsisha mashamba, viwanda kwa bei ndogo tena bila sababu za kutosha na miradi mingi ya Serikali hata hoteli za kitalii;
5. Sioni sababu kwa Wabunge kuondolewa kwenye Bodi za Taasisi za Serikali kwani Wabunge sio Serikali tena ni msaada mkubwa kwa bodi;
6. Ni vema Kamati kutembelea miradi ili kuona *value for money* hivyo Bunge litenge fedha za ziara za Kamati hizi za Fedha;
7. Mashirika baadhi kuchelewa kuunda Bodi na kuchelewesha utendaji wa mashirika hasa Mwenyekiti wa Bodi; na
8. Yako Mashirika ambayo hayajakaguliwa na *CAG* yanakuwa kama hayajulikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza *CAG*, anafanya kazi nzuri sana, amegundua upotevu wa pesa nyingi sana. Ninawapongeza watendaji ambao wanafanya kazi kwa ufanisi wa juu. Ninapongeza Serikali kwa kusimamia baadhi ya mashirika ambayo yamezalisha kwa kiwango cha juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba mchango huu usomwe na Wenyeviti wote.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema na hivyo kuweza kushiriki katika kikao cha leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazipongeza kamati zote tatu, kwa taarifa zao nzuri ambazo zikifuatwa na kutekelezwa, ufanisi mkubwa unaweza kupatikana Serikalini, katika Mashirika mbalimblai, Halmashauri za Wilaya pamoja na Taasisi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulipa madeni ni jambo muhimu sana ili huduma muhimu kama vile madawa, maji, umeme na kadhalika ziweze kupatikana kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalamu wa fani mbalimbali wanapaswa kupatikana katika Halmashauri zote hapa nchini ili kuboresha utendaji kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Madiwani wajengewe uwezo ili kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Halmashauri za Wilaya zinaonekana kupuuza maagizo yanayotolewa na Kamati za Bunge pale wanapofanya ziara katika Halmashauri na kutoa maagizo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna upotevu mkubwa wa fedha katika Taasisi mbalimbali Serikalini pamoja na Halmashuri mbalimbali kutokana na uzembe, wizi au utendaji mbovu wa watendaji katika Taasisi mbalimbali. Ni vyema Serikali ikayaangalia mambo haya kwa umakini mkubwa na kuchukuwa hatua pale ambapo inaoneka upotevu ni wa makusudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. HALIMA O. KIMBAU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza taarifa hizi zote ni nzuri na za maana sana kwetu. Napenda kuwapongeza Wenyeviti wote kwa kutusomea kwa ufasaha kabisa taarifa hizi. Mimi ni mmoja wa wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Taarifa yetu ya Kamati imesomwa lakini si vibaya nami nikaongezea haya machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wanakamati tumefaidika sana na mafunzo mbalimbali tuliyopata, tunashukuru sana wale wote waliochangia kutuwezesha. Pia tunashukuru kwa kutuwezesha kutembelea miradi kazi, hii kwa kweli imesaidia sana kutambua mazuri na mabaya ya watendaji wetu kwenye Halmashauri zetu. Ombi kwa Serikali kupitia Wizara husika kuona umuhimu wa taarifa zetu hizi lakini pia ushauri tunaotoa ufanyiwe kazi kwa haraka sana. Najua Wizara imekuwa ikijitahidi lakini haitoshi. Jamani kuna baadhi ya mambo yanayofanyika Wilayani yanakera na yanatisha. Serikali lazima ichukue hatua kali, kwa wakati na haraka. Jitihada zinafanywa na Serikali kupeleka fedha kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi, hii idara kwa kweli inahitaji tuiangalie sana, wakuu wake lazima tuwachuje tupate wenye ujuzi na pia wenye moyo. Hapa ndio mahali panapotumia fedha nyingi na kwa ajili ya maendeleo mfano madaraja, barabara, madarasa, zahanati na mengi mengine. Nasisitiza tupate watendaji wenye ujuzi na moyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo hewa, hii ni nini, kweli tumeshindwa kufuatilia jambo hili, si haki hata kidogo. Mengi tunasema tunafuatilia lakini nguvu nyingi zinatumika matokeo si mazuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tushirikiane, inawezekana kuondoa maovu.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Wenyeviti wote wa Kamati zote tatu kwa kuzisimamia Kamati na kuziendesha kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ulipaji wa magari kule Dubai na Japan, haiingi akilini ni kwa nini *TBS* wateuwe wakala wa kukagua magari huko nje kabla magari hayo hajaletwa nchini. Kwa kufanya hivyo, nchi yetu inapoteza fedha nyingi sana za kigeni ukizingatia kila gari hutozwa sio chini ya $150 kwa gari. Fedha hizi zingelipwa hapa Tanzania kwa kuweka Mkaguzi pale Bandarini Taifa lingefaidika na fedha hizi. Tunaweza kujiuliza, je, ni kiasi gai cha fedha kama Taifa tumefaidika kwa kuteua wakala kukusanya fedha huko Dubai na Japan? Nashauri mfumo huu wa kulipia *sticker* kule Japan na Dubai, usitishwe mara moja kwa faida ya nchi yetu na *TBS* itoe maelezo kama Taifa tumeshapata kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara tofauti, Mikoa, Halmashauri, pamekuwepo na malipo mengi sana hewa. Unakuta mfanyakazi alishafariki lakini mshahara ule bado unapelekwa bank, huu ni upotevu wa fedha za umma. Nashauri kabla fedha hazijatoka Hazina, majina ya wafanyakazi yapelekwe kila mwezi kutokana na wafanyakazi waliopo, ndio Hazina waingize fedha *bank* kutokana na majina hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wadaiwa sugu kama *TIOT* ambao inasemekana hawakamatiki wala mali zao haziwezi kukamatika sababu mali zao hawajaziorodhesha kwa kutumia majina yao. Kwa kuwa mwenye kampuni hii ni Mtanzania, kama ametumia majina ya mali zake kwa majina ya familia basi mali zile zikamatwe mpaka alipe deni hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuangalia *value for money* kwa ujenzi wa Shule za Kata inasikitisha ukizingatia shule zote hizi nyingi zimejengwa kwa kutumia nguvu za wananchi pamoja na Serikali lakini hakuna wanaojali shule hizo zinajengwa kwa kiwango gani. Ni vizuri kusisitiza Bodi za Shule ziwe makini katika usimamizi wa majengo hayo. Unakuta karatasi zinaonesha choo kinajengwa kwa shilingi milioni 10 lakini ukitembea shule ile unakuta malipo yalifanywa hewa na choo hakipo. Hivyo, Serikali ina wajibu wa kushirikiana na Mbunge, Diwani na Bodi ya Shule, hii itasaidia kuwa na usimamizi mzuri.

Baada ya kusema haya, nampongeza sana Mwenyekiti wa *PAC*, Mheshimiwa John M. Cheyo, kwa kazi yake nzuri na umakini wake na kwa kuiongoza Kamati hii na kukemea pale panapoonekana kuna upotevu wa fedha na kutoa maagizo kwa Serikali nini kifanyike ili kuweza kuokoa fedha hizo kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nalipongeza Bunge letu kuamua kuwa na *Oversight Committees,* ambazo ni *PAC, LAAC, POAC.* Kamati hizi zinafanya kazi nzuri sana za kuhakikisha fedha ya walipaji kodi inatumika kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mjumbe wa *PAC*, kwa uzoefu niliopata ndani ya Kamati yangu, kuna mambo kadha yanaonekana bado ni tatizo. Bado Serikali inapoteza mapato kwa kulipa wafanyakazi hewa.

Haiingia akilini Halmashauri hazifahamu watendaji walio hai na waliofariki wakati wao hushiriki katika mazishi ya wafanyakazi wenzao, hivyo hivyo kwa Wizara mbalimbali. Serikali iangalie jinsi gani itaziba mwanya huo wa kupoteza mapato yetu kwa njia hiyo ya kulipa mishahara hewa, ifanyike *research* wahusika wote wachukuliwe hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ununuzi wa magari ya thamani kubwa kwa watendaji wa Serikali imekuwa ni *fashion* kwa kila mtendaji bila kujali wadhifa wake Waziri, Naibu waziri, Wakurugenzi wa Halmashauri na wengine wengi kila mmoja kwa kiasi kikubwa wanatumia *VX –V8 (New Model)* ambapo maeneo mengine zahitajika gari aina nyingine zikiwemo *Land Cruiser Hardtop*. Ushauri wangu kwa Serikali, maoni ya Kamati ya *PAC* yazingatiwe kuwa magari yanunuliwe kulingana na *rank* au wadhifa wa viongozi, ijulikane gari aina fulani inatumiwa na kiongozi wa *rank* ipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ununuzi wa samani nje ya nchi, ushauri wa Kamati uzingatiwe ili kuongeza ajira za Watanzania, ofisi zote za Serikali zitumie samani zinazotengenezwa hapa nchini, hii itakuzaa viwanda vyetu. Ingawa jibu la Serikali ndiyo kwanza tuko kwenye soko huria lazima tuwe na *political will* katika hili na inawezekana Serikali ikitaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kutokuwa na uwiano kati ya fedha za miradi na miradi yenyewe, *no value for money*, Serikali ichukue hatua kwa watendaji wote wanaokula pesa za miradi na kutumia pesa kununua vifaa ambavyo havina sifa ya kudumu. Maeneo mengi madarasa yanajengwa kwa kutumia *cement* kidogo, mchanga mwingi na bati geji 30 badala ya 28.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi kutumia muda mrefu. Serikali imekuwa ikicheleweshа pesa za miradi matokeo yake gharama huzidi mfano barabara ya Dar-es-Salaam – Mtwara, Bwawa la Manchira Mara lililoanza kujengwa toka mwaka 1977. Miradi ikichelewa maana yake gharama ya vifaa hupanda na Wakandarasi hudai Serikali pesa ya ziada yaani *fine*. Hivyo, Serikali ione umuhimu wa kulipa pesa za miradi kwa wakati ili kuepuka mambo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itilie mkazo ukaguzi wa ndani bado ni tatizo kwani Mkaguzi wa Ndani ndiye anayeweza kuisaidia Serikali na kuielekeza na atakuwa kama *watchdog*. Vilevile atasaidia kutoa *information* sahihi kwa Mkaguzi wa Nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msisitizo mkubwa tunaotoa wajumbe wa *PAC*, ni kwamba Serikali ipunguze matumizi ya anasa, itafute vyanzo vingine vya mapato, izibe mianya yote ya wizi wa pesa ya walipa kodi. Ili kupunguza utegemezi wa wahisani ambao kwa kiasi kikubwa hawatoi/hawatimizi ahadi zao, mfano bajeti ya maendeleo ya

kilimo ya mwaka 2009-2010 ni ziadi ya kilo 130, asilimia 90 ni kutoka kwa wahisani maana yake ni kwamba wasipotoa Kilimo Kwanza, ni ndoto. Hivyo inabidii tujitegemee na tumeshaona miradi mingi iki-*fail* kwa ukosefu wa fedha baada ya wahisani kughairi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, labda tu niendelee kueleza utaratibu namna tutakavyohitimisha hoja hizi. Mmeona kwamba hoja hizi zinahusu Kamati Tatu ambazo ni Kamati tofauti. Kwa maana hiyo, wakati wa kuhitimisha itatupasa sasa tuamulie hoja moja baada ya nyingine ingawa mchango wa hoja hizo tumeutoa kwa pamoja. Lakini sasa wakati wa kuziamua hoja hizo itatupasa tuamue hoja moja baada ya nyingine. *(Makofi)*

Sasa utaratibu utakaofuata nitamuita Mwenyekiti mmoja baada ya mwingine na kila mmoja nitampa dakika 15 aweze kuweka msisitizo na kusema lolote linalohusu katika yale yaliyokwisha kujitokeza. Baada ya kufanya hivyo basi atatoa hoja ya Kamati yake. Atakapomaliza kutoa hoja na papo hapo nitalihoji Bunge kuhusu hoja hiyo na tutakuwa tumeshaiamulia na tutaendelea na Mwenyekiti anayefuata na tutamaliza na Mwenyekiti atakayefuata wa tatu katika hao wote watatu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge baada ya kutoa mwongozo huo sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa John Cheyo ili aweze sasa kuhitimisha hoja yake na baadaye atafuatiwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO - MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naomba dakika za mwanzo zisihesabiwe kwa sababu nitataja majina kwa Kamati zote tatu katika dakika zangu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Cheyo tutaomba ujitahidi kwa namna itakavyowezekana kwa sababu tayari Mheshimiwa Mwenyekiti, ametumia Kanuni namba 2 kufanya maamuzi yake hayo naomba uyazingatie. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza naomba kuwashukuru sana Wabunge wote ambao wamechangia hoja zetu tatu. Zaidi hoja nyingi zimetupongeza kwa kazi ambao imefanywa. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Kweli sasa naamini kwa fedha hakuna itikadi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ambao wametuchangia kwa kuandika ni Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah,

Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama na Mheshimiwa Ismail Jusa Ladhu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, waliochangia kwa maandishi niliyoyaona mimi ni Mheshimiwa Halima Kimbau, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya na Mheshimiwa Lucy Owenya. Tunawashukuru sana kwa michango yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda kuwa mchache ni vigumu kuweza kujibu hoja ya kila mmoja. Lakini nitapitia tu kwa haraka baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge kwa kila mmoja walizochangia. *(Makofi)*

Wa kwanza Mheshimiwa Mgana Msindai tunashukuru sana kwa pongezi zako. Tunaungana na wewe kwa jambo hili la *internal auditor* na hili pia limezungumzwa na Mheshimiwa Estherina Kilasi. Hoja zingine nitamwachia Mwenyekiti wa Kamati ya *LAAC* aweze kuhitimisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Wilson Masilingi nakushukuru kwa pongezi, tunaungana na wewe kututakia maslahi mazuri kwa Waheshimiwa Wabunge wanaoshughulikia na mambo haya ya udhibiti kwa sababu ya kazi zilizopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Said Arfi, mengi yatajibiwa na Mwenyekiti wa *LAAC*. Lakini nashukuru sana kwa pongezi. Jambo la *MSD* kwa upande wa *PAC* tunaona ni matatizo kwamba wao hawafanyi kazi ya kutosha. Lakini kwa upande wa kwako *MSD* haijalipwa. Kwa hiyo, ni mambo ambayo lazima tujaribu kuoanisha pamoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Estherina Kilasi na yeye amesisitiza jambo la *Internal Auditor*, namkushukuru sana. Pia namshukuru kwa kutupongeza kwa kazi tuliyoifanya bila kufuata itikadi ya Chama.

Mheshimiwa Ruth Msafiri, yeye alikuwemo katika Kamati yetu, nakushukuru sana, zaidi kwa kusisitiza jambo la samani za Serikali ziwe zinatokana na malighafi ya hapa hapa nchini badala ya kuagiza kutoka nje. Ametoa mfano Ofisi ya Utalii na Bugando, kama tulivyoona, wametumia samani zilizotengenezwa na miti ya hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la matibabu ya wazee kwamba yawe bure, naona Serikali imesikia juu ya jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kupima miji, tumeona mfano mzuri sana Mwanza tulivyofanya ziara, nashukuru sana kuwakumbusha hilo.

Halafu akinamama Maafisa Wahasibu wameongezeka, hii ni kweli na tunaipongeza Serikali kwa kuwaona akinamama na kuwawezesha.

Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, naye ni Mjumbe, nashukuru sana kwa kuona kazi nzuri tunayoifanya kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mahojiano, siku hizi ni kweli kanuni zetu zinaruhusu tunawahoji Maafisa Wahasibu mbele ya *TV*, ni kazi ngumu lakini wengi wamejitahidi. Tunaomba tuendelee na ikiwezekana tuwe *live* kama alivyosema ili wananchi waone jinsi fedha yao inavyotumika.

Pia, amesisitiza juu ya Serikali kuangalia matumizi yake kwa sababu ni kama vile tunajaza tu kwenye ndoo ambayo iko wazi na kwa hiyo haitoshelezi pamoja na mapato kuongezeka. Jambo la *RAS* pia tumelizungumza kwenye Kamati kwa kirefu.

Mheshimiwa Janguo, nashukuru sana kwa kutupongeza na umezungumzia juu ya *CAG*, pia umempongeza, tunashukuru. *VFM Conference*, hiyo ni mojawapo ya vitu ambavyo tutaendeleza, huu ni mwaka wa pili tunakuwa na *conference* baada ya kikao kama hiki cha Aprili, hii ni njia mojawapo ya kujenga uwezo lakini nakubaliana na wewe kuwa *capacity building* iwe kwa Wabunge wote kwa sababu kazi ya kudhibiti matumizi ya Serikali sio yetu tu katika Kamati ni ya Bunge lote. Hiyo nakubaliana naye na tumepata nyenzo nzuri na sasa hivi tumepata *laptops* kwa baadhi ya Wabunge wa Kamati hizi, zitatusaidia sana katika kufanya kazi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine naona yatajibiwa na Mheshimiwa Dr. Slaa na masuala ya Mheshimiwa Simbachawene Mwenyekiti wake atamjibu. Vile vile Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, nitamwachia Mwenyekiti wake atamjibu.

Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu, alizungumzia utaratibu wa Kamati hizi kuongozwa na Wapinzani, hii ndiyo Wazungu wanasema *best practice* katika ulimwengu wote kwa sasa hivi kwamba unaachia mambo ya *oversight* upande wa upinzani. Kwa hiyo, changamoto tuliyonayo, ni kuongeza uwezo wetu na kuweza kutoa maoni yetu bila ya kufuata itikadi yoyote ya Chama, ni jambo ambalo tumejitahidi sisi Wenyeviti kuonyesha kwamba fedha ya Serikali haina Chama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu misamaha ya kodi, labda utakapopata nafasi ya kuisoma vizuri zaidi taarifa yetu, utaona kwamba tumetumia muda mrefu kuzungumzia juu ya misamaha ya kodi katika Voti 50 na pia tumetumia muda mrefu sana kuzungumzia juu ya Serikali kuhakikisha kwamba mikopo yake inakuwa na *bond* au *sureties*. Lakini nakushukuru sana kwa pongezi zako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upotevu wa fedha kufuatana na ile *Global Financial Integrity*, hiyo naona Serikali imesikia na watafuatilia kama inavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Waheshimiwa walioniandikia, Mheshimiwa Lucy Owenya, ameleta hoja nyingine ambayo tuliihoji kwa kipindi kilichopita ambayo inayohusu ukaguzi wa magari nje kwamba tunapeleka takriban shilingi bilioni 62 nje kukagua gari kwa ajili ya kuipa *sticker* tu. Jambo hili naona limechukuliwa kwa ukubwa

zaidi na wenzetu wa *POAC* lakini sisi tunashangaa kulikoni? Jambo ni rahisi, gari yoyote inayoingia hapa nchini haiwezi ikapata *registration* bila ya kukaguliwa na ikikaguliwa, Serikali itapata mapato na *TBS* itapata mapato, ninyi kukimbilia kufanya ukaguzi Dubai kulikoni? Jambo hili tunaiachia TAKUKURU.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu malipo hewa na lenyewe ni jambo ambalo tumelizungumzia. Umeshauri kudhibiti *payroll*, natumaini Mheshimiwa Waziri wa Utumishi amekusikia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TIOT*, katika ripoti yangu pia nimeizungumzia, mtu mmoja tu shilingi bilioni sita miaka yote sasa anageuza majina hafuatiliwi, huyu ni nani, kwa nini Serikali haiwezi ikamdhibiti mtu huyu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo la shule, namwachia Mheshimiwa Dr. Slaa kuweza kuangalia mambo hayo. Mheshimiwa Halima Mdee, pongezi na mengine namwachia Mheshimiwa Dr. Slaa kuangalia.

Mheshimiwa Diana Chilolo, pongezi, nashukuru, kazi safi, ahsante sana kwa kutupongeza. Umezungumzia pia samani pia umesema watumishi wanakaa kwa muda mrefu sana, tuangalie posho ili kudhibiti matumizi.

Mheshimiwa Juma Said Omar, pongezi, tunashukuru mengine yatazungumzwa na wenzangu.

Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya na yeye yuko katika Kamati yetu, nashukuru sana kwa kutambua kazi tunayofanya, ahsante sana. Halafu umezungumzia juu ya *issue* ya wafanyakazi hewa jambo ambalo tunalikemea. Suala la magari ya fahari, hiyo ni njia mojawapo ya kuweza kudhibiti matumizi na Waziri Mkuu tunamshukuru kwa kuchukua hatua. Pia amesema samani za nje hazina maana na mengine mengi, amechangia vizuri kama unavyofanya kila wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nijikite tu kwa mambo machache, kitu ninachoomba kwa leo kwa Bunge hili ni kutuunga mkono kwa mapendekezo ambayo tumeyaweka. Hilo tu, kwamba mapendekezo yetu semeni Serikali iyaangalie, ndiyo hiyo tu na ndiyo hoja ambayo niliyonayo mimi. Tumeweka mapendekezo mengi sana katika udhibiti wa madeni, Serikali inatoa dhamana *(guarantees)* mpaka sasa karibu shilingi bilioni 563, ni kama vile hazina mwenyewe angalieni hizi fedha, tumetoa mapendekezo juu ya mambo hayo. Pia madeni ya Wanajeshi, Walimu lipeni kwa sababu msipolipa itakuwa ni gharama tena kwa bajeti inayofuata. Halafu tumezungumzia matumizi ya magari, utaratibu wa sheria ufuatwe. Vile vile tumesema uwekezaji katika sekta ya afya uongezeke, tunasema Kilimo Kwanza, Kilimo Kwanza hakuna bila ya mtu kuwa na afya njema. Uwekezaji katika Mashirika ya Majeshi, ni jambo ambalo tumegundua Mzinga na Nyumbu wana *potential* kubwa sana ambayo inahitaji kusaidiwa. Ujenzi wa nyumba za Serikali zinazojengwa na *TBA* uangaliwe upya kwa sababu kusema kweli haina tija. *Accountability* ya *RAS* iangaliwe, mikataba ya ujenzi wa barabara na yenyewe tumeona kwamba ni sehemu ambayo inahitaji kuangaliwa. Unaanza na barabara shilingi bilioni 28 unamaliza kwa shilingi bilioni 50, jambo hili lazima liangaliwe na Serikali. Mwisho

tunasema utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati hizi basi uzingatiwe na ndipo tutaweza kuhakikisha kwamba Serikali inapata ushauri mzuri wa kuweza kutumia fedha za walipa kodi vizuri, ni hayo tu.

Waheshimiwa Wabunge, naomba kabisa mkubali mapendekezo ambayo Kamati yetu imeyaleta ili tuweze kuisaidia Serikali kutumia fedha zake vizuri kwa ajili ya maisha bora kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa naangalia hoja imetolewa na naona Wajumbe wa pande zote mbili wamesimama na wameunga mkono hoja hiyo wakiwemo Wajumbe wa Kamati, lakini na wengine pia ambao sio Wajumbe wa Kamati. Baada ya hoja hiyo kutolewa na kuungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge ninaomba kulihoji Bunge kwamba sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo kwenye taarifa hiyo.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Nawapongeza sana Wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali, lakini nichukue nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote kwa jumla kwa kazi waliyoifanya na kwa taarifa yao waliyoiwasilisha hapa Mezani kwa siku hii ya leo.

*(Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo kwenye taarifa hiyo yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya hatua hiyo, nitawapeleka kwenye hoja ya pili, naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, ili naye aje kuhitimisha hoja yake na hatimaye niweze kulihoji Bunge kuhusu hoja hiyo.

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA – MWENYEKITI WA KAMATI ZA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, naomba nisirudie pongezi, shukrani na pia nisirudie kusoma majina, ameshayasoma mwenzangu. Nitakwenda kwenye mambo ya jumla lakini kabla sijakwenda kwenye mambo ya jumla kuna michango miwili ambayo ningependa itambuliwe na *Hansard* na naomba niiseme kwa sababu imekuja kwa njia ambayo sio ya kawaida. Mchango wa kwanza ni wa Mheshimiwa Celina Kombani ambaye naye ametupa wazo ambalo baadaye nitaliongelea lakini naomba iwe *recorded* kwamba ni sehemu ya mchango kwa sababu kwa kweli ameimarisha hoja yetu. Mchango wa pili ni wa Mheshimiwa Mwenyekiti mwenyewe Jenista Mhagama ambaye alikuwa anataka

kufuatilia suala ambalo tumelizungumzia kuhusu Madiwani. Kwa hiyo, naomba na mchango huo pia utambuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, niseme tu mambo machache kwanza ya jumla. La kwanza, ni hii hali la kutokuwa na siasa katika Kamati. Mimi nafikiri Bunge letu limekomaa kwa kutoingiza hisia za siasa, kuingiza ushabiki katika taratibu za kufanya mambo ya kitaalamu hasa mambo kama ya fedha ambayo kwa kweli hayana itikadi na naomba utamaduni huu mzuri uendelee. Hata huko nje tunapokwenda katika Mikutano ya Kimataifa, kwa kweli tunapongezwa tunafanyaje kazi. Tulikuwa na mfano mzuri sana, nadhani ilikuwa ni Mozambique kama sikosei, Wapinzani walikuwa wachache sana, nadhani sio Mozambique sikumbuki ile nchi dhidi ya Chama Tawala. Kwa hiyo, kila wakati hawapitishi hoja hata kama ni hoja nzuri kiasi gani kama hizi za kwetu, zinapingwa tu kwa sababu ya itikadi. Nadhani hii ni pongezi kwa Bunge la Tanzania, nawapongeza wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maisha bora kwa kila Mtanzania, kwa kweli nadhani tungeweza kuyafikia kwa kiwango kikubwa sana kama tungesimamia matumizi ya fedha ambazo zinakwenda kwenye Halmashauri. Kule ndiko ambapo tunataka matumizi haya yaweze kufanyika na yalete mabadiliko. Tukizungumza fedha zinazokwenda kwenye elimu, afya, barabara, huduma zozote zile za jamii hata kwenye maeneo mengine kama ambavyo unapeleka fedha za *Global Fund* kwa mfano maeneo ya UKIMWI na kadhalika, kwa kweli haya yanaweza kubadilisha maisha ya watu wetu. Lakini kama ukisoma kwenye taarifa yetu ukifanya *analysis* ya kitaalam, asilimia 23 ya bajeti sasa hivi ndio inayopelekwa sio asilimia 70 kama watu wengi wanavyofikiri. Sasa katika asilimia hiyo 23 ambayo inakwenda, kama asilimia 80 na hapa niseme kwamba hatujafanya *scientific analysis,* naomba Serikali ifanye *analysis* hii, asilimia 80 haiendi kwa walengwa. Hii ni hali ambayo sio nzuri na wenzetu hawaelewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwona Mheshimiwa Waziri anatingisha kichwa, kwenye Kamati tulikokwenda tuna Ma-*RAS* na kadhalika tuliwahoji tukawaambia watuambie hizi fedha zilizokwenda zina-*multiplier effect* gani kwa mtu wa chini? Kwa mfano, semina zinafanywa za *capacity building* zinawagusa watu wale wale katika ngazi ya Halmashauri na majina tunakwenda kuyadai tunakuta hata majina ni ya watu wale wale, sasa hapo hakuna *multiplier effect,* haiteremki tena chini. Kwa hiyo, *capacity building* inatakiwa ifanyike lakini iteremke pia kwa watu wa chini na wale watu waonje matokeo yak, hiki ndicho tunachosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na mashamba ya mifano kwa mfano juzi mara ya mwisho tumekwenda Mafia, kule kuna shamba la mfano, ni afadhali shamba la mwananchi wa kawaida kuliko lile ambalo tumetoa fedha ili liwe la mfano. Kwa hiyo, hawa ndiyo tunayoyasema na Serikali inatakiwa itusaidie ngazi zote iwe ni *DC, RC,* Mkurugenzi, Madiwani wasimamie hizi fedha ziweze kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania. Mimi naamini kama tukifanya hivyo, tunaweza kweli kupata maisha bora. Inatia uchungu unapopata fedha hasa za *Global Fund, Basket Fund* ambazo kwa kweli zinaelekezwa kwa wale watu ambao ni *marginalised,* watu wa hali ya chini kabisa lakini

zinatumika kwenye mambo ambayo hayawafikii wale walengwa, hilo nadhani wote tukubaliane tulisimamie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ambalo ninapenda kulisisitiza hapa ni suala ambalo kwa kweli tunapaswa kulikazia. Mwaka jana tumesema na *CAG* amelisemea na sisi tunalisema. Sheria zetu za Serikali za Mitaaa hazijahuishwa na Sheria za Serikali Kuu na sijui kwa nini katika hili tunachelewa. Tumeleta Sheria nyingi sana hapa, mimi ninaomba Serikali ifanye bidii, Serikali itambue kwamba Sheria Na.9 ya mwaka 1982 pamoja na *Local Authority Financial Memorandum* ya mwaka 1977 imepitwa na muda na inatupa taabu sana katika kusimamia fedha za *Local Authority*. Tunategemea katika taarifa itakayokuja, yeyote atakayekuwepo hatadai tena hili, ataanza kutoa taarifa sasa, Serikali imeshasikiliza na imetekelezwa angalau Muswada uwasilishwe katika hatua za awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ambalo linaleta tatizo ni suala zima la sisi kutoa taarifa. *CAG* ameshatoa taarifa, sisi tunaingia tena kuchambua taarifa ya *CAG*, tunagundua mambo hata zaidi ya yale aliyoyaona *CAG* kwa sababu *CAG* tukumbuke Waheshimiwa Wabunge anasema yeye anafanya *sample audit* maana yake hafanyi yote anachukua hapa na pale au yale yaliyokuwa mezani. Lakini pili anasema si kazi yake kutafuta wizi, si kazi yake kutafuta *fraud*, si kazi yake kutafuta matumizi mabaya ya fedha, akiyakuta, atayafanyia kazi na kuyaonyesha, lakini ni kazi ya mwenye mali yaani Halmashauri, Madiwani wenyewe na Wabunge kwa niaba ya Serikali Kuu. Sasa hili sisi Wabunge tuna nafasi ya kusaidia kwenye vitabu vya Halmashauri kwa sababu tuna uwezo mkubwa wa kuona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili hili lifanyike kuna mambo ya msingi ambayo nadhani ni muhimu na Serikali itusaidie na Mheshimiwa Kombaniameniandikia hapa na nafikiri ningelikuwa mkali zaidi kama nisingepata, sasa naomba nimpongeze kwa hatua aliyochukua. Sisi tumetoa maelekezo kwa Halmashauri zote na ameniomba tumpelekee kwa maandishi kwamba Madiwani hawawezi kusimamia fedha zinazopelekwa kule kwa sababu taarifa wanazopewa ni za jumla jumla tu. Natoa mfano hapa, ukisema darasa limejengwa kwa shilingi milioni 14 Diwani hawezi kuhoji lakini wakija mbele ya Kamati yangu wanasema tumetoa mabati 200, tumetoa misumari inchi tano, tumetoa mifuko kadhaa ya saruji, sisi ambao tuko mbali tunapewa taarifa, lakini wale walioko pale, wanaotakiwa kusimamia, hawapewi na muda ungetosha ningeeleza Madiwani kwenye Halmashauri fulani nadhani Muheza walitushambulia kwa sababu walifikiri sisi tunawaonea watu wao. Tulipokwenda kwenye *site* wakasema na sisi tulifika hapa, tulipouliza, tukatoa vitabu, wakagundua kumbe walidanganywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Muheza imekuja mara mbili mbele ya Kamati na tumewapiga tozo na tumewaambia sasa waje tena si ajabu tutakwenda kuwapelekea tena *Special Audit* nyingine, sasa haya yanafanyika. Mheshimiwa Kombani utusaidie katika hili, Madiwani ni lazima wapate *breakdown* na kama ni matumizi mabaya Wizara yako itakuwa ime-*contribute* kwa kiasi kikubwa kwa kutokuwasaidia Madiwani kuwapa *breakdown* inayowasaidia kusimamia miradi. Mheshimiwa Waziri,

naomba nikwambie, Madiwani wanataka mfumo huo wa kuwapa *details* lakini Wakurugenzi na Tume yao hawataki wala watumishi wengi katika Wizara yako na Hazina hawataki pia kwa sababu mtafunga njia za wale watu kula. Kwa hiyo, nakuomba sana katika hili tusaidie na tushirikiane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme mambo madogo yafuatayo. Kwanza, nianze na suala la Mheshimiwa Zitto, ni kweli Mheshimiwa Zitto sisi tulikwisha kuhoji katika Kamati yetu suala la shilingi bilioni 5.9 za TANAPA zilizokwenda Mkoa wa Mbeya wakati wa kuwahamisha wale wananchi, sisi tumehoji Halmashauri ya Mbarali, Halmashauri ya Mbarali imesema hili suala liko juu ya uwezo wetu, Mheshimiwa Zitto unasema liko juu ya uwezo wako *LAAC* tunahoji. Mimi nimehoji ndani ya Bunge hili na Spika alinipa nafasi, Waziri akajibu kwamba tutalifanyia kazi mpaka leo hatujasikia. Mheshimiwa Celina Kombani, tunaomba majibu utupatie mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Slaa, naomba uki-*address* Kiti.

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuomba Mhasibu Mkuu wa Serikali kwa Serikali za Mitaa, hili naomba pia tusilisemee sana sana kwa sababu Serikali inaona madhara yake. Ni kweli fedha za Serikali za Mitaa hazina mwenyewe. Sisi huwa tunapokwenda kwenye ziara, tunaenda na watu wa Hazina, TAMISEMI na watu wa Mkoani lakini wanaanza kurushiana mpira kwa sababu hakuna mtu anayewasimamia. Tunaomba suala hili liangaliwe ili tuweze kupata ufumbuzi wake, suala ni kuwa na Mhasibu Mkuu ambaye kutoka juu atawasimamia Wahasibu wote wa Serikali za Mitaa kama *ACGEN* anavyowasimamia Wahasibu katika Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Internal Auditor,* nimeshashukuru na naomba tu nilikazie, nisiendeleee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la mwisho, niseme tu kwamba kuna tatizo kubwa, watu ambao wanatajwa na *CAG* kwamba wameharibu, *special audit* tulizofanya mwaka jana nane, kuna watu wameagizwa walipe fedha ambazo waliiingizia Serikali hasara lakini pia wachukuliwe hatua, mpaka leo hawajachukuliwa hatua. Mfano wa hili ni hili ambalo limetokea hivi sasa. Niseme tu kwamba Bagamoyo tatizo lilikuwa kubwa kiasi kwamba *CAG* alikagua na amekagua kwa sababu kuna taarifa mbili za uongo zilitolewa, moja imeenda kwenye *route* ya Chama kwa maana ya utekelezaji wa Ilani ya CCM ambapo ni sahihi lakini nyingine ikapelekwa kwenye *route* ya *CAG* ambayo inakuja kwetu lakini zote mbili ni tofauti. Nampongeza sana Mkuu wa Mkoa wa Pwani na *DC* wake ambao walisimama kidete katika hili na nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sasa baada ya Waziri Mkuu kuchukua hatua wale watu hawakuondoka, wamebaki pale. Kilichotokea sasa ni wale watu kabla hawajachukuliwa hatua walipata nafasi ya kwenda kuchota na kuingiza mikono yao. Sasa naomba Serikali isichelewe kuchukua

hatua pale ambapo ubadhirifu, ufisadi na wizi unatokea kwa sasa wale watu wanaachwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Madiwani, ni suala la muhimu sana lakini pia kuna suala la maslahi yao na elimu yao. Tunaomba hili pia likaziwe sana, Madiwani sasa hivi kila siku mnaona wanalalamika hata posho zao na *gratuity* yao, naomba Serikali iwe makini. Ukitaka wafanye kazi nzuri na ukitaka wasimamie hela nyingi tunazowapelekea, mabilioni ya hela basi ni vizuri na wao pia tukawalinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuomba Bunge lako Tukufu liunge mkono maazimio na mapendekezo yetu yote kwa jinsi tulivyoyatoa na tuombe Serikali nayo iyafanyie kazi na tupate taarifa ya utekelezaji inayoingia kwa undani tofauti na ya mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na Wajumbe wa Kamati hiyo wameiunga mkono. Sasa nitawahoji kwamba Bunge sasa lipokee na kukubali taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo kwenye taarifa hiyo.

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo kwenye taarifa hiyo yalikubaliwa na Bunge)*

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge, naomba kutangaza rasmi kwamba Bunge limeafiki na kuipokea taarifa ya Kamati hiyo na kama ilivyo ada, Waheshimiwa Wabunge, nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Dr. Slaa, Mwenyekiti lakini nimpongeze sana Makamu wake Mheshimiwa Msindai pamoja na Waheshimiwa Wabunge wajumbe wa Kamati hiyo, kwa kazi nzuri waliyoifanya na ninaamini kwamba wataendelea kutoa ushirikiano wa kutosha ili kuisaidia Serikali yetu kufanya kazi vizuri katika eneo hilo la Serikali za Mitaa.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma, ninaomba nitambue uwepo wa Mheshimiwa Samuel Sitta, Mbunge wa Jimbo la Urambo Mashariki na Spika wa Bunge letu na kwa kweli wakati tunaamua hoja hizi, alihakikisha anawahi sana hii ya Serikali za Mitaa ili asikie haya mambo yanayohusu Halimashauri yake. Mheshimiwa Mbunge wa Urambo Mashariki tunakupongeza sana na tunakukaribisha sana kwenye mjadala wa leo jioni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumalizie na hoja ya Kamati ya mwisho na naomba nimwite Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma ili aje ahitimishe hoja yake.

**MHE. KABWE Z. ZITTO – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuhitimisha hoja iliyopo mbele yetu ya taarifa ya mwaka ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma na vilevile nitoe shukrani zangu za dhati kwa watu wote ambao wametupongeza kwa kazi ambayo tumeifanya na majina ya wachangiajia yote ni kama ambavyo yametajwa na Mheshimiwa John Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumza kwa ujumla lakini hoja *specific* ya Mheshimiwa Janguo kuhusiana na Serikali kutosaini mikataba na Mashirika ya Hifadhi za Jamii ambayo yamejenga Chuo Kikuu cha Dodoma. Kama jinsi nilivyoeleza kwenye taarifa yangu na Serikali iko hapa, kwa kweli si jambo zuri mpaka sasa miaka mitatu baada ya mashirika yetu haya kuwa yametekeleza wajibu wao wa kujenga Chuo Kikuu kikubwa kabisa Kusini mwa Jangwa la Sahara, kuweka *investments* kubwa kabisa kama jinsi ambavyo nimeileze, lakini Serikali bado haijasaini makubaliano na mashirika haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge ambao wanapenda, wakienda sasa hivi vile vilima vyote vilivyokuwepo eneo ambalo limejengwa Chuo Kikuu cha Dodoma, mtaona jinsi ambavyo majengo yameshamiri kwa lengo la kuwafundisha vijana wetu. Kwa hiyo, Serikali kuonesha kwamba wanakubaliana na wanapongeza zile juhudi ambazo zimefanywa pale, ni vizuri wafanye jitihada kuingia mikataba hii ili kuhakikisha kwamba fedha za wafanyakazi ziko salama kwa sababu *investment* hii imejengwa kwa fedha za wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutambua hilo, ndiyo maana Kamati yangu ilikutana na mifuko yote na hapa ningependa kuitaja kwa majina kwa sababu asubuhi sikuweza kuitaja kwa majina. Mfuko wa *Local Authorities Pension Provident Fund, NSSF, PPF* na *PSPF*. Katika Mkutano wetu tuliofanya kuhusiana na tatizo la nishati, tuligundua kwamba kuna tatizo kubwa sana la nishati na halijapatiwa ufumbuzi na hasa uzalishaji wa umeme. Tukawa tumeiita mifuko hii na kuweza kujadiliana nao kuangalia ni jinsi gani wanaweza kulitatua tatizo hili na tumekubaliana kimsingi kwamba wataanza kuwekeza katika eneo hili la umeme. Pia tuliita Shirika la *ZSSF* la Zanzibar na lilishirikiana na wenzao katika mkutano ule, kwa hiyo, nao pia ninapenda niwashukuru kwa kushiriki katika shughuli ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashirika haya ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kama tukitumia fedha zao vizuri, yanaweza yakatupeleka mahali pazuri sana. Mmeona hayo maendeleo ya Chuo Kikuu cha Dodoma lakini sasa hivi ninafahamu kwamba kuna utafutaji mkubwa sana wa mafuta na gesi Mikoa ya Kusini na kama Taifa hatuna wataalam wa kutosha katika maeneo ya mafuta na gesi. Kwa hiyo, kama tukifanikiwa vizuri kukamilisha Chuo Kikuu cha Dodoma, tukakamilisha suala la uzalishaji la umeme, huko siku za usoni tutakapoamua kujenga uwezo wa nchi na wataalam katika mambo ya mafuta na gesi, tunaweza tukaielekeza mifuko hii ikaangalia uwezekano wa kujenga hata

Chuo Kikuu kingine kule Mtwara kwa ajili ya kuwa-*train* watu wetu jinsi gani ya kuwekeza katika mambo haya ya mafuta na gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana tumepitisha Sheria ya *Treasury Registrar* ambayo inampa nguvu kama jinsi ambavyo Mheshimiwa Simbachawene amezungumza, hii ni hatua kubwa sana ya utekelezaji wa maagizo ambayo Serikali ameyafanya. Kwa sababu mwaka jana tumetoa taarifa hiyo na ndani ya kipindi cha miezi 12, Serikali imeleta Muswada na jana tumetunga Sheria ya kuweza kuipa nguvu Ofisi ya *Treasury Registrar* na kimsingi tumerejesha yale majukumu yaliyokuwa chini ya *SCOPO* ambayo yalikuwa yanaangalia Mashirika ya Umma, sasa *Treasury Registrar* atakuwa anaangalia Mashirika ya Umma bila tatizo lolote na haitakuwa tena Mawaziri wanaibuka tu na kutangaza Bodi bila kushauriana na mwenye mali ambaye ni *Treasury Registrar* anayezishika kwa niaba ya Serikali. Kwa hiyo, kazi tuliyoifanya jana kwa kweli ni nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Simbachawene, mashirika ni mengi sana, mashirika ambayo yako chini ya orodha ya *Treasury Registrar* ni 238, mashirika ambayo yanatazamwa hesabu zake na *CAG* ndiyo hayo 166 sio kama nilivyokuwa nimekufahamisha Mheshimiwa Simbachawene. Kwa hiyo, unaweza ukaona ni jinsi gani hivi sasa ambavyo mashirika ni mengi na kazi ya kuyasimamia kwa kweli inahitajika kuwa kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia ombi la Waheshimiwa Wabunge kutaka kuyafahamu mashirika haya, tutashauriana na *Treasury Registrar* kwa ajili ya kuweza kuandaa *booklet* ya masharika tuliyonayo ili kila Mbunge kabla ya Bunge hili la Kumi na Tisa halijavunjwa awe nayo na kiasi cha mtaji ambacho Serikali imeweka. Lakini pia tutafanya utaratibu wa kufanya mkutano kati ya baadhi ya mashirika, hatuwezi kuyaita yote 238 lakini tutaweza kuangalia yale ambayo tunaweza tukayaita labda kwenye Mkutano wa Bajeti kuweza kukutana na Wabunge ili waweze kuelezea shughuli zao mbalimbali ambazo wanazifanya.

Mheshimiwa Diana Chilolo, amerejea ile hoja ya Wabunge kuwa katika Bodi za Mashirika ya Umma, hiyo hoja nilizungumza sana jana. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amezungumza sana kwenye taarifa zake na ninadhani Serikali inaweza kusikia maana imesikia ushauri wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na nisingependa kuirudia tena hoja hii. Jambo la msingi tu ni kwamba tujaribu kuangalia kwa sababu kuna baadhi ya mashirika ambayo hayafanyi vizuri, unakuta shirika lipata *disclaimer audit opinion* na shirika hilo ndani yake lina Mbunge tena unakuta ni Mbunge mahiri kweli wa kuzungumza humu ndani lakini kwenye shirika kule linapata *disclaimer audit opinion* au wanapata hati chafu. Kwa hiyo, hivi vitu inabidi tuviangalie na tuweze kuona ni jinsi gani heshima ya Wabunge inabakia kuwa juu.

Mheshimiwa Jussa amezungumzia kuhusu Serikali kudaiwa na Mashirika ya Umma. Kwa kweli, napenda kusisitiza kwamba Serikali ijitahidi sana kulipa kwa sababu mashirika mengi sana ya umma yanashindwa kujiendesha kwa sababu hayana mapato yake kwa sababu Serikali inadaiwa mapato hayo. Lakini jambo la msingi zaidi ni

kuangalia jinsi gani tunatunza hizi mali zetu. Ninaomba tu Wabunge hasa Wabunge ambao wanapitapita Dar es Salaam, hivi wajiulize leo miaka kumi ile Hotel ya *Motel Agip* inaoza pale, *ten years* na sisi tupo tunafanya kazi zetu na tunawaambia wananchi kwamba tunasimamia mali zao! Hoteli ile haifanyi kazi yoyote na iko eneo zuri sana la kibiashara hakuna kazi yoyote ambayo tumeifanya, kwa hiyo, ni suala la kuangalia. Pia Hotel ya *Embassy* iko sehemu zuri sana, tuko kimya, hakuna mtu yeyote ambaye anaizungumzia vitu kama hivi. Hizi rasilimali za umma angalau zitutie uchungu na kuweza kuhakikisha kwamba tunazitunza vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala ambalo nililipeleka kwenye Kamati ya *LAAC*, suala la Mbarali. Sisi kwa upande wetu tulichosema ni kwamba *CAG* ametoa *audit query* kwa TANAPA kuhusiana na shilingi bilioni 5.9. Sisi tumefuatilia, tumekuta TANAPA wamelipa fedha zile Mbarali. Kwa hiyo tunachosema ni kwamba hii *audit query* si ya shirika letu. Shirika letu katika hili liko sawa. Sasa hili ni tatizo la *LAAC* na Kombani, wakae huko wayamalize. Shirika letu halina tatizo katika suala hili la haya malipo ambayo tumeyatoa na lingine...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, unapomu-*address* Mheshimiwa Celina Kombani, naomba umtaje kwa Cheo chake.

**MHE. KABWE Z. ZITTO – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni tatizo la Mwenyekiti wa Kamati ya *LAAC*, Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, Mbunge wa Karatu na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mheshimiwa Celina Kombani, wakae huko walimalize ili zile fedha ambazo Serikali yetu imetoa zimewafikia walengwa na zisiendelee kuwa sehemu ya *audit query*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mawili ya mwisho. Suala la kwanza ni la *political interference*. Ninaomba tu Serikali ijaribu kuwa makini kuhakikisha kwamba inapunguza hizi *political interference*. Ndugu Jussa ametoa mfano hapa na hata mwaka jana tulizungumza kwamba sisi kama nchi lazima tuwe na mashirika ambayo tunasema haya ni *National Champions,* tunajidai nayo. Wenzetu wa Kenya wana *Kenya Airways*. Niliuliza hapa mwaka jana Ethiopia na *Ethiopian Airlines* sisi tuna nini? Shirika ambalo tukiweka nguvu ya kutosha, tukiwekeza vizuri, litaweza kutamba ndani ya Tanzania na nje ya Tanzania, ni Shirika la Ugavi wa Umeme kwa sababu sisi ndiyo nchi ambayo ina-*potential* kubwa ya nishati kuliko nchi zote za Afrika Mashariki. Sasa Shirika hili lilishakuwa lina-*turn around*, mwaka 2008, *for the first time* toka limeanza limepata *operating profit* ya shilingi bilioni mbili lakini mwaka 2009 imerudi kwenye hasara ya shilingi bilioni 48. *It is very painful, extremely painful.* Kwa hiyo, tunaomba Serikali iweze kuangalia ni jinsi gani haya mashirika yetu tuyapunguzie hizo *political interference* ila tuyasimamie ili kuhakikisha kwamba fedha zao na mipango yao inaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, ni suala la uhifadhi. Nilizungumza hapa, sisi wote na mashirika mengine, tunapaswa kulipa kodi kama Sheria inavyotaka kwa sababu tukienda kwenye barabara, tunatumia barabara ambazo zimejengwa na

*TANROADS* kwa kodi, Taasisi zetu za hifadhi, Ngorongoro na TANAPA, zile barabara za ndani mle kwa ajili ya watalii wanajenga wao wenyewe kwa fedha zao na haziondolewe katika kutozwa kodi na bado mwisho wa mwaka *TRA* wanawapiga asilimia 30 ya kodi, Waziri wa Fedha anasema 10% ya *turn over* kwa ajili ya kwenda Serikalini hapo hapo tunapeleka 3% ya *turn over* kwa ajili ya *TTB*, kwa ajili ya kutangaza utalii. Tunachosema ni kwamba tunaua uhifadhi, watoto wetu hawataona hao tembo na Ngorongoro yenyewe na Serengeti. Tulichopendekeza ni kwamba tuhakikishe kwamba tunawaangalia, fedha zitumike kwa ajili ya uhifadhi na zile fedha za ziada tuzianzishie Mfuko Maalum *(Hifadhi Fund)*, uendeshwe vizuri kabisa na *professionals* wa *fund management*, wafanye kazi, wawekeze na kadhalika kiasi kwamba hatuhatarishi urithi huu ambao tumepewa na Mwenyezi Mungu. Hayo ndiyo ambayo tunayaomba Serikali iweze kuyaangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini nitakuwa nimejibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge kama ambavyo zimetolewa, hazikuwa nyingi sana na napenda kuwashukuru sana kwa pongezi zenu zote na mimi pia nitoe shukrani yangu ya dhati kwa Makamu Mwenyekiti wangu na kama mnavyofahamu mimi sasa hivi niko shule kwa hiyo muda mwingi amekuwa akiendesha vikao vya Kamati, yeye pamoja na Wajumbe wenzangu tumeenda vizuri sana. Kama nilivyoeleza mwaka jana, yeye ni zaidi ya Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Kilasi ni kama mama yangu kabisa kwa jinsi tunavyofanya naye kazi kwa pamoja. Lakini pia niwashukuru Wajumbe ambao nilichagua, maana ndiyo ripoti ya mwisho kwa Bunge hili la Tisa, niwashukuru sana Wajumbe maana wamenifanya niijue nchi yangu vizuri, kusimamia mashirika 166 si mchezo. Nimeweza kuijua nchi vizuri kwa sekta zote na Wizara zote ambazo zina mashirika ya umma. Niwashukuru sana sana kwa heshima ambayo mmenipa kwa kunichagua kuwa Mwenyekiti wenu nikiwa mara yangu ya kwanza kuingia Bungeni na nikiwa Mwenyekiti mwenye umri mdogo kuliko wote. Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa heshima hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Bunge lako Tukufu liipokee na kuipitisha taarifa ya mwaka ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma pamoja na maoni na mapendekezo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto Kabwe nikushukuru kwa kuhitimisha hoja yako kwa niaba ya Kamati na umeitoa hoja na nimeona Wajumbe wa Kamati yako wameiunga mkono na Wabunge wengine pia. Lakini nimeona aliyeongoza kwa kuunga mkono, ni Makamu Mwenyekiti wako, alisimama wa kwanza kabisa hapa ndani. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hoja hiyo kutolewa sasa nitawahoji kwamba Bunge sasa lipokee na kuikubali taarifa ya Kamati ya Hesabu ya Mashirika ya Umma pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo kwenye taarifa hiyo.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Mashirika yya Umma pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo kwenye taarifa hiyo yalikubaliwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Naomba nitangaze rasmi kwamba Bunge limepitisha mapendekezo ya Kamati hii. Basi nichukue nafasi hii kuwapongeza sana sana Wajumbe wa Kamati hiyo wakiongozwa na Mheshimiwa Zitto Kabwe; lakini pia nimpongeze Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii Mheshimiwa Estherina Kilasi lakini pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote wa Kamati hiyo kwa kazi nzuri waliyoifanya. Pia niwapongeze Wabunge wote kwa kazi yao nzuri waliyoifanya hapa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, ninakubaliana nanyi na wote waliochangia kwa kumpongeze sana Spika wetu, Mheshimiwa Samuel Sitta, kwa kazi nzuri ya mabadiliko ndani ya Bunge letu na hii ilipelekea Kanuni zetu za kufanya kazi ndani ya Bunge zituruhusu kufanya haya mambo yenye tija kwa Taifa letu. Kama mlivyoona, Kamati hizi zote zimewasilisha taarifa yake kwa mujibu wa Kanuni ya 114(15) ambayo inaonesha ulazima wa jambo hili ndani ya Bunge. Inasema:-

*"Itakuwa ni lazima kwa kila Kamati ya Kudumu ya Bunge kuwasilisha Bungeni taarifa ya mwaka ya shughuli zake kwa madhumuni ya kujadiliwa katika Mkutano wa mwisho kabla ya Mkutano wa Bajeti".*

Kwa hiyo, haya mambo tunayoyafanya, tunayafanya kwa mujibu wa Kanuni.

Lakini Kanuni ya 114(17) imeendelea kusisitiza, inasema:-

*"Spika ataweka utaratibu wa kujadili taarifa za Kamati na endapo Kamati yoyote katika kutekeleza majukumu yake, itaona kuwa kuna mambo ya utekelezaji ambayo yanahitaji kurekebishwa, inaweza kutoa taarifa maalum ya ushauri kwa Waziri mwenye dhamana juu ya mambo hayo ili Waziri aweze kuchukua hatua zinazostahili".*

Kwa hiyo, kama unaona kuna mambo mahsusi yenye tija kwa Taifa letu basi Kamati zetu zinaweza kuwasiliana na Waziri mwenye dhamana ili kuweza kuchukua hatua kwa maana ya kuleta tija ndani ya nchi yetu. Waheshimiwa Wabunge kwa kweli nawapongeza sana kwa kutekeleza Kanuni hii kwa umoja.

Nimepokea tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Spika kwamba ameshapokea taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini kwamba imeshakamilisha kazi kwa hali hiyo Muswada wa Sheria ya Madini utakuwepo katika Orodha ya Shughuli za kesho, Alhamisi tarehe 22 Aprili, 2010.

Tangazo la mwisho ambalo nimelipata ni kwamba ninaomba kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi uwepo wa kikao cha chama jioni hii

saa mbili usiku katika Ukumbi wa Pius Msekwa mara baada ya kuahirishwa kwa shughuli ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, naona shughuli zilizopangwa kwa siku hii ya leo zimekamilika na nirudie kusema kwa kweli kazi kubwa imefanyika. Kwa hiyo sina budi kuahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.45 usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 22 Aprili, 2010 Saa Tatu Asubuhi)*